# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kumi na Mbili – Tarehe 25 Aprili, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**.**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**MWENYEKITI:** Tutaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Zuena Athumani Bushiri, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 138

### Uhitaji wa Gari la Wagonjwa, Vifaa na Wataalam Hospitali ya Mabogini Moshi Vijijini

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka gari la wagonjwa, vifaa tiba na wataalam katika Hospitali ya Wilaya ya Mabogini Moshi Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 ilinunua magari 594 (*ambulance* 382 na usimamizi 212) ya kubebea wagonjwa na usimamizi wa huduma za afya katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imepokea magari mawili ya kubebea wagonjwa na kupelekwa Kituo cha Afya cha Umbwe na Himo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hospitali ya Wilaya ya Mabogini katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 imepelekewa shilingi milioni 165 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba. Aidha, vifaatiba vimeshanunuliwa na kupelekwa katika Hospitali ya Mabogini. Hospitali ya Mabogini ina jumla ya watumishi saba wanaotoa huduma katika hospitali hiyo kwa sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa, vifaatiba na kuajiri watumishi wa kada mbalimbali za afya kwa ajili ya Hospitali za Wilaya nchini ikiwemo Mabogini. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bushiri.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa kuwa Hospitali ya Mabogini haina *ambulance* kabisa na kwa kuwa wagonjwa wa rufaa inabidi watumie usafiri wa bodaboda hasa akinamama wajawazito. Je, Serikali ina mpango gani wa haraka wa kupeleka gari hili la wagonjwa ili kuwasaidia akinamama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, Hospitali ya Mabogini hii ipo kilometa 20 kutoka Mji wa Moshi ambapo ndipo kuna Hospitali ya Rufaa, lakini hakuna njia ya akinamama kuweza

kufika kwa urahisi. Hospitali hii haina jengo la mama na mtoto. Jengo la mama na mtoto ni jengo muhimu sana. Je, Serikali ina mipango gani ya haraka ya kujenga jengo la mama na mtoto hili ili lianze kutoa huduma? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Zuena Bushiri kwa swali ambalo linalenga kuboresha sekta ya afya hususan katika hii Wilaya ya Moshi Vijijini, Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza, Serikali mpaka wakati huu tayari imenunua magari ya kubebea wagonjwa *(ambulance)* 382 na kuyasambaza kote nchini. Serikali inaendelea kufanya michakato ya kupata fedha na kununua magari mengine mengi zaidi ya kutolea hii huduma ya kubeba wagonjwa *(ambulance)* kwa kutumia fedha za Serikali Kuu na kupitia mapato ya ndani ya halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu mkubwa sana wa kupeleka gari la kubebea wagonjwa katika hii Hospitali ya Mabogini. Nimhakikishie Serikali itatafuta fedha na kupeleka gari hiyo kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili ambalo amezungumzia ninadhani miundombinu ya barabara. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge miongoni mwa vipaumbele namba moja vya ujenzi wa barabara ni pamoja na ujenzi wa barabara kuelekea kwenye maeneo yanayotoa huduma za msingi ikiwemo huduma za afya. Kwa hiyo, ujenzi wa barabara kuelekea kwenye hii Hospitali ya Halmashauri ya Mabogini ni kipaumbele pia katika mikakati ya Serikali ya kuboresha miundombinu hii ya barabara. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Serikali itaweka kwenye mipango na kuhakikisha inajenga barabara hiyo, ili kuwe kuna njia nzuri ya akina mama kuweza

kufika kupata huduma, lakini wananchi wote kuweza kupata huduma katika hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la jengo la mama na mtoto, Serikali inafanya uwekezaji mkubwa sana katika eneo hili kuhakikisha kwamba, huduma za afya kwa mama na mtoto zinaimarika. Serikali inatafuta fedha kuhakikisha kwamba, inaendelea kujenga majengo haya muhimu kabisa ya mama na mtoto ambayo ni ya msingi kabisa kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya na msingi. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itafanya hivyo ili majengo haya yaweze kukamilika, yajengwe na yaweze kutoa huduma bora za afya kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Profesa Patrick Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kituo cha Afya cha Umbwe ambacho ni kituo cha afya pekee katika Tarafa ya Kibosho yenye kata sita, kina upungufu mkubwa sana wa vifaatiba. Je, Serikali ina mkakati gani wa kusaidia kituo hiki cha afya kipate vifaatiba ili wananchi waweze kupata huduma zilizotukuka? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya uwekezaji mkubwa sana katika sekta ya afya. Katika kipindi cha miaka minne ya Awamu ya Sita Serikali imetumia jumla ya Shilingi trilioni 1.29 kwa ajili ya kuimarisha huduma upande wa afya msingi. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali imeshatuma fedha nyingi katika kila halmashauri kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na vifaatiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kumwagiza *DMO*

katika hii Wilaya ya Moshi Vijijini aweze kutumia fedha alizopokea katika huu mwaka wa fedha 2024/2025 kwa ajili ya kuhakikisha ananunua vifaa na vifaatiba, kwa ajili ya kuvipeleka katika Kituo cha Afya cha Umbwe ili kiweze kuwanufaisha wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zaytun Swai, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYTUN S. SWAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini Serikali itakamilisha ahadi yake ya kupeleka gari la wagojwa katika Kituo cha Afya cha Engarenaibor Longido ambayo ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahadi za Viongozi wetu Wakuu ni kipaumbele namba moja katika utekelezaji wa mipango na majukumu ya Serikali. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali itahakikisha kwamba inapata fedha kwa ajili ya kununua gari hilo la kubebea wagonjwa na kulipeleka katika Kituo cha Afya alichokitaja Mheshimiwa Mbunge katika Wilaya ya Longido.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Nimwite sasa Mheshimiwa Shamsia Azizi Mtamba, Mbunge wa Mtwara Mjini, aulize swali lake.

Na. 139

**Fedha za Ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto Kituo cha Afya Mkunwa – Mtwara**

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatoa fedha za ujenzi wa Jengo la Mama na Mtoto katika Kituo cha Afya Mkunwa, Mtwara Vijijini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2018/2019 hadi 2024/2502 Serikali ilitoa shilingi bilioni 1.37 kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba ya Kituo cha Afya Mkunwa ambapo jengo la kuhudumia wagonjwa wa nje *(OPD)* limekamilika na linatoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali itatenga shilingi milioni 169.7 kwa ajili ya kukamilisha jengo la mama na mtoto katika Kituo cha Afya cha Mkunwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara**.**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shamsia, swali la nyongeza.

**MHE. SHAMSIA A. MTAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini siyo Mjini. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kuiishukuru sana Serikali kwa hatua iliyofikia mpaka sasa kituo chetu cha afya kilichopo katika Halmashauri yetu ya Wilaya Mkunwa kimeanza kutoa huduma kwa maana ya *OPD*, lakini bado kumekuwa na changamoto kubwa sana ya baadhi ya majengo kutokamilika hasa ikiwepo jengo la mama na mtoto. Swali la kwanza; ni lini Serikali itakamilisha jengo hilo muhimu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili; Mheshimiwa Waziri Mkuu alikuja kutembelea mwaka juzi katika Jimbo langu la Mtwara Vijijini alitembelea jengo la utawala na kituo chetu cha afya na akatoa ahadi pale ya kutuleta fedha shilingi milioni 600 kwa ajili ya umaliziaji wa jengo la mama na mtoto pamoja na majengo mengine. Je, ni lini sasa Serikali itatimiza ahadi hii? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu maswali ya Mheshimiwa Shamsia Mtamba yote mawili kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ahadi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kama nilivyotangulia kusema kwamba ahadi za viongozi wetu wakuu ni kipaumbele namba moja katika mipango na utekelezaji wa shughuli zetu za Serikali. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge tayari hiyo ahadi tumeanza kuitekeleza na ndiyo maana kwenye jibu la msingi nimetangulia kwa kusema kwamba katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali tayari tumetenga shilingi milioni 169.7 kwa ajili ya ukamilishaji wa jengo hili muhimu kabisa la mama na mtoto. Serikali itaendelea, kupitia fedha kutoka Serikali Kuu na halmashauri (Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa) kutenga fedha kwa ajili ya kuhakikisha tunaendelea kuimarisha miundombinu hii katika sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mheshimiwa Shamsia apokee *commitment* hiyo ya Serikali kwamba, tutakuja kuhakikisha tunatekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na kuimarisha na kukamilisha majengo hayo muhimu sana katika sekta ya afya kwenye Jimbo lake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Kasalali Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Wananchi wa Jimbo la Sumve katika Kituo cha Afya Nyambiti wameanza ujenzi wa jengo la upasuaji. Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kumalizia ujenzi wa jengo hilo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita katika kipindi cha miaka minne imefanya uwekezaji wa shilingi trilioni 1.29 kwa ajili ya kuboresha

upande wa afya msingi. Kwenye hiyo trilioni 1.29, vituo vya afya 345 vimejengwa pamoja na zahanati na hospitali za halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kutenga fedha kila mwaka wa bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba inaendelea kuboresha miundombinu ya vituo vya afya, zahanati na hospitali. Hata katika Jimbo lako Sumve Mheshimiwa Kasalali, Serikali itahakikisha kupitia mapato ya ndani na kupitia fedha za Serikali Kuu inafika katika kituo cha afya ulichokitaja kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kinakamilika na kinaweza kutoa huduma kwa wananchi wako.

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba, Vituo vya Afya vya Buswelu pamoja na Sangabuye ni vya muda mrefu lakini havina miundombinu ya kutosheleza. Buswelu ina *OPD* peke yake haina miundombinu mingine. Sangabuye ina *OPD* na wodi ya mama na mtoto lakini miundombinu mingine haipo. Je ni lini Serikali itakamilisha miundombinu katika vituo hivi viwili vya afya?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, dhamira ya Serikali ni kuendelea kuimarisha huduma za afya zinazotolewa katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi. Zaidi ya 75% ya watu nchini (Watanzania) wanategemea kupata huduma za afya kupitia vituo vyetu hivi vya huduma ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana utaona uwekezaji mkubwa unafanywa kuimarisha huduma za afya msingi. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Dkt. Angeline Mabula kwamba Serikali itafika kwenye hivi vituo vya afya viwili alivyovitaja kuhakikisha inakamilisha miundombinu ya msingi kwa ajili ya kutoa huduma bora ya afya kwa wananchi wako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea, tuna maswali mengi bado TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Jackson Gideon Kiswaga, Mbunge wa Kalenga, aulize swali lake.

Na. 140

**Ujenzi wa Wodi ya Wanaume Kituo cha Afya Kata ya Mgama - Kalenga**

**MHE. JACKSON G. KISWAGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa wodi ya wanaume katika Kituo cha Afya cha Kata ya Mgama? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Mgama ni miongoni mwa vituo vya afya vikongwe ambacho kilianza kutoa huduma kwa ngazi ya zahanati miaka ya 70 na kupandishwa hadhi ya kituo cha afya mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Serikali kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imetenga shilingi milioni 100 kwa ajili ya ujenzi wa wodi ya wanaume, wanawake na watoto katika Kituo cha Afya cha Mgama.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha katika bajeti kwa awamu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya vituo vya huduma za afya ikiwemo wodi katika Kituo cha Afya cha Mgama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwanza kwa kupata majibu mazuri ya Serikali na mipango ya kuendelea kujenga wodi kwenye hicho Kituo cha Mgama, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, ninavyo vituo viwili cha Magulilwa pamoja na cha Kibena ambacho Serikali imejenga tunaishukuru na sasa kimeanza kutumika kwa huduma za nje. Je, katika hivyo vituo viwili Serikali ina mpango upi sasa wa kutujengea wodi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika vituo vyetu vya afya kumekuwa na uhitaji mkubwa wa kuwa na *mortuary*. Je, ni mpango upi wa Serikali sasa kutujengea *mortuary* hata katika vituo vyetu vya afya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Jackson Kiswaga kwamba Serikali inakuja kuhakikisha inakamilisha miundombinu muhimu kabisa katika vituo hivi vya afya ambavyo amevitaja. Mathalani, Kituo cha Afya cha Magulilwa tayari kimetengewa shilingi milioni 60 kwenye mapato ya ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa majengo. Halikadhalika, kwenye Kituo cha Afya alichokitaja cha Kibena Serikali itatenga fedha na itafika kwa ajili ya kuhakikisha vituo hivi vya afya vinaweza kukamilika kuwa na miundombinu yote ya msingi ili viweze kutoa huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali wote ni mashahidi katika Bunge hili tulipitisha nyongeza ya bajeti. Nyongeza ya bajeti hiyo ikiwa inaelekea kwenda kukamilisha maboma katika sekta ya afya, shilingi bilioni 30.3. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kupitia fedha hizo, lakini kila mwaka wa bajeti tutakuwa tunaendelea kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya kwenda kukamilisha miundombinu ambayo haijakamilika kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kupitia fedha hizo, lakini kila mwaka wa bajeti tutakuwa

tunaendelea kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya kwenda kukamilisha miundombinu ambayo haijakamilika kwenye vituo vyetu vya kutolea huduma za afya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili la ujenzi wa majengo ya kuhifadhia maiti *(mortuary)*, jengo la *mortuary* ni miongoni mwa majengo ya msingi kabisa katika kituo cha afya. Serikali inavyojenga vituo hivi vya afya inazingatia kupeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa *mortuary*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali inatambua umuhimu wa kuwa na vyumba hivi vya kuhifadhia maiti na itaendelea kuwa inaleta fedha kwa ajili ya kuhakikisha kwamba majengo haya yanakamilika ili yaweze kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mashimba Ndaki, nilikuona mapema, swali la nyongeza.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wananchi wa Kata ya Zanzui wamekwisha kuanza uchangiaji wa ujenzi wa kituo cha afya cha kata hiyo, mpaka sasa wana tofali kama 3,000 hivi. Je, Serikali iko tayari kutenga fedha ili kuwasaidia kukamilisha kituo hicho cha afya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Sita imekuwa ikiendelea kuhakikisha kwamba inaendelea kuboresha huduma za afya msingi. Ili kufanya hivyo imeendelea kutenga na kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha miundombinu ya msingi katika vituo vyetu vya kutolea huduma ya afya msingi, ikiwemo vituo vya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kituo cha afya hiki ambacho Mheshimiwa Ndaki amekitaja, ninaomba nimhakikishie kwamba, Serikali itafika, ihakikishe, kupitia fedha za Serikali Kuu, lakini kupitia mapato ya ndani ya halmashauri inatoa fedha kwa ajili ya

kukamilisha miundombinu yote, ili kituo hiki kiweze kutoa huduma bora kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Tendega. *(Makofi)*

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Kata ya Lumuli na Zahanati ya Itengulinyi ambayo ipo Jimbo la Kalenga bado haijakamilika; wananchi wamejenga kwa nguvu zao. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha wanakamilisha zahanati hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba, katika Mwaka huu wa Fedha 2024/2025, Bunge lako Tukufu lilipitisha nyongeza ya bajeti ambapo katika nyongeza hiyo ya bajeti shilingi bilioni 30.38 zimetengwa sasa kwa ajili ya kuhakikisha zinaenda kukamilisha maboma katika vituo vya kutolea huduma za afya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kwa kutegemea na tathmini na hali ya uwekezaji ambao umefanyika katika ujenzi wa zahanati hii, Serikali itafika ili iweze kukamilisha majengo haya katika zahanati hii, ili sasa iweze kutoa huduma bora za afya wa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aysharose Mattembe.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Ni lini Serikali itapeleka fedha za kutosha kujenga nyumba za Waganga katika Kituo cha Afya cha Sepuka? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA, NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Mwenyekiti,

miongoni mwa majengo ambayo ni ya muhimu kabisa tunapojenga vituo vya afya ni pamoja na kutazama na kuwekeza katika nyumba za watumishi wa Kada hii ya Afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Ayshrose Mattembe kwamba, Serikali itaendelea kuhakikisha kwamba inatenga fedha pia mahsusi kabisa kwa ajili ya kuendelea kujenga nyumba hizi za watumishi wetu wa Kada ya Afya ili wawe karibu zaidi na maeneo ya kufanyia kazi na waweze kutoa huduma bora kabisa za afya kwa wananchi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Ameshasimama muda mrefu sana hapa. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri kwa Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Tunakwenda Wizara ya Viwanda na Biashara, ninamwita sasa Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 141

**Wajasiriamali Zanzibar Kunufaika na Mfumo wa Taarifa za Biashara – *TanTrade***

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS** aliuliza:-

Je, Wajasiriamali wa Zanzibar wananufaika vipi na Mfumo wa Taarifa za Biashara wa *TanTrade*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Exaud Kigahe.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania *(TanTrade)* ina Mfumo wa Taarifa za Biashara *(Tanzania Trade Portal)* ambao unatoa taarifa

za mazao na masoko yake pamoja na taarifa ya namna ya upatikanaji wa vibali na leseni mbalimbali zinazotolewa na Taasisi za Serikali zinazosimamia biashara nchini, ikiwemo Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar, Mfumo huo una jumla ya taarifa za mazao tisa, inayojumuisha taratibu sita za kuuza mazao nje ya nchi na taratibu tatu za kuingiza mazao ndani ya nchi. Mazao hayo ni karafuu, mazao ya baharini ikiwemo mwani na samaki, viungo, matunda, asali, pamoja na vyakula na madawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Machi, 2025, jumla ya wadau 426,579 ikiwemo wajasiriamali na wafanyabiashara 3,400 kutoka Zanzibar wamenufaika na taarifa za biashara kupitia mfumo huo, tovuti na taarifa ya SMS na mitandao ya kijamii. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tamima Abass.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; Serikali ina mikakati gani ya kutanua wigo wa matumizi ya mifumo hii, ili wadau wengi zaidi wapate taarifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa sasa hivi Zanzibar inakuwa kibiashara, je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea uwezo wa kupata taarifa pamoja na watendaji kupata elimu ya kutumia mifumo hii ili sasa watendaji wawe na uwezo wa kuitumia mifumo na taarifa hizi ziweze kuwafikia wananchi? Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Tamima Haji kwa ufuatiliaji mzuri, lakini pia na mchango wake mzuri katika

Sekta ya Biashara, mahsusi kwenye Taasisi yetu ya *TanTrade*, hasa katika upande wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo Maonesho ya Kimataifa ya Dar es Salaam ambayo tunafanya kila mwaka. Zaidi, sasa kule Zanzibar nako tumejenga uwanja wa maonesho ambao huo unalenga kuwasaidia Wazanzibar, waweze kutumia fursa ya maonesho na kupata taarifa zaidi kupitia uwanja ule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hiyo, tayari *TanTrade* imefungua ofisi kule Zanzibar ambapo baadhi ya watendaji wanafanya kazi kule, lakini kwa sababu taasisi ni ya ushirikiano, maana yake kuna wakati watendaji kutoka Bara wanaenda Zanzibar na wa Zanzibar wanakuja huku Bara, ili kuhakikisha wanapata ule utaalam na uwezo wa kujua namna ya kutumia *Apps* hizi, kwa maana ya *Portals* hizi. Pia kupata weledi zaidi katika kuhakikisha wanawasaidia si tu Wazanzibari, lakini Watanzaia kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tayari tumeona jambo hili Zanzibar nayo inanufaika na Taasisi yetu ya *TanTrade*, ili kuhakikisha nao wananufaika kuuza na kununua au kuingiza bidhaa kutoka nje ya nchi. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Tunakwenda Wizara ya Maji. Nimwite sasa Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni.

Na. 142

**Uchimbaji wa Visima 11 Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha uchimbaji wa visima 11 vilivyokuwa vichimbwe kwenye Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2021/2022 katika Jimbo la Chemba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Andrea Kundo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na ujenzi wa miundombinu ya utoaji huduma ya maji *(point sources)* kwa visima saba ambavyo vimechimbwa na maji kupatikana katika maeneo ya Cheku A, Sankwaleto, Manantu, Tumbakose, Mbarada, Madaha na Isusumya. Lengo ni kuendelea kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji Wilayani Chemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kupitia bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026, Serikali itakamilisha uchimbaji wa visima vingine vinne na kujenga miundombinu ya kutolea huduma kwa wananchi kwa Vijiji vya Ndoroboni, Ombiri, Majengo Mapya, na Mpendo, vilivyopo katika Wilaya ya Chemba. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; visima vya Cheku A na Manantu vimechimbwa tangu mwaka 2022, mpaka leo havijawekewa miundombinu ili viweze kuhudumia na kutoa maji. Ninataka kujua, ni lini Serikali itaweka miundombinu ili vianze kutumika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Kijiji cha Igunga kina changamoto ya maji tangu muda mrefu sana. Ninaishukuru Serikali, wiki tatu zilizopita walikuja kufanya *survey* na wakapata wapi wanaweza kuchimba maji. Ahadi yao ilikuwa ndani ya wiki mbili wangekuwa wamechimba, mpaka leo hawajatokea bado. Ninaomba kujua, ni lini sasa watakuja kuchimba maji? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu maswali ya nyongeza la Mheshimiwa Mohamed Monni, Mbunge wa Chemba, Mbunge ambaye anapambana sana kwa ajili ya kuhakikisha kwamba anamtua mama ndoo kichwani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kiu yake ni kuwaona akinamama wanapata huduma ya maji safi na salama. Pia, tunaendelea kumshukuru kwa kuendelea kushirikiana na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na akitambua kwamba Mheshimiwa Rais alinunua magari ya uchimbaji na ndiyo maana anajua kabisa kwamba hili linawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na Kijiji cha Igunga kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maji, ninaomba nitoe maelekezo kwa *RM* Mkoa wa Dodoma; magari tunayo, wapeleke mwezi Mei Chemba wakaanze kuchimba na wananchi wapate huduma ya maji safi na salama katika hilo eneo la Igunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema vilevile tukatambua kwamba, tunapotekeleza miradi hii ya maji jambo la kwanza ni kutafuta chanzo cha uhakika. Jambo la pili ni kuhakikisha kwamba maji yaliyopatikana yana ubora unaotakiwa na yana wingi unaotakiwa kulingana na eneo husika. Baada ya hapo sasa ndiyo tunatenga fedha kwa ajili ya kufanya usanifu ili tuweze kusambaza maji katika maeneo ambayo yanazunguka eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimtoe hofu katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge anaomba miundombinu ijengwe, tutajenga baada ya usanifu kukamilika na wananchi wako watapata huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge mko wengi lakini hamwezi kupata nafasi wote; kwa hiyo, watapata wachache. Tutaanza na Mheshimiwa Anatropia Theonest. *(Makofi)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa upendeleo huo. Ninataka kujua mkakati wa Serikali wa kuwapatia maji wananchi wangu wa Kata za Businde, Bugara na Kamuli, ambao wanatembea umbali mrefu na kupanda milima kwenda kuchota maji kwenye makorongo. Ni nini mkakati wa Serikali wa kuwachimbia visima kwenye maeneo hayo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba ili nitoe jibu la uhakika, ni mkoa gani na wilaya gani?

**MHE. ANATROPIA L. THEONIST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaongelea Mkoa wa Kagera, Wilaya ya Kyerwa, Jimbo la Kyerwa, Kata ya Kamuli, Businde na Bugara. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua kabisa kwamba Mheshimiwa Mbunge anaendelea kupambana akishirikiana na Wabunge wengine wa Mkoa wa Kagera, kuhakikisha wananchi wa Kyerwa, wanapata maji. Tunafahamu kabisa, Serikali kupitia kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tuna miradi mikubwa ambayo inaendelea kutekelezwa na Programu ya Visima 900 inaendelea. Vilevile, tunatambua kabisa kwamba baada ya visima hivi 900 bado kuna maeneo yatakuwa hayajafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali tunalipokea na tutahakikisha kwamba tunafanya usanifu kulingana na mahitaji ya maeneo husika ili tuwachimbie visima wananchi na wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninaangalia *list* yangu watu ambao hawajauliza kabisa, Mheshimiwa Mchungahela. *(Makofi)*

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi. Mradi wa Mbangara umekuwa ukisemwa siku nyingi kwamba utapelekewa pesa, utapelekewa pesa, mara kadhaa na nilishauliza hapa swali hili kuhusiana na mradi huu. Ni lini Serikali itahakikisha mradi huu unatengewa pesa kwa ajili ya ujenzi na utaanza lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na pia ninamshukuru sana Mheshimiwa Mchungahela. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mchungahela nilishafika jimboni kwake na tulizunguka katika maeneo yote yenye uhitaji na ninafahamu kwamba mradi huu ndiyo kiu yake kubwa. Sisi Serikali tunafahamu kabisa kwamba mradi huu ni *game changer* katika eneo la Mheshimiwa Mchungahela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba atambue kwamba, sisi tunaendelea kuwasiliana na wenzetu wa Wizara ya Fedha ili kuangalia ni kwa namna ipi tunaweza tukapata fedha za dharura, ili tukamsaidie Mheshimiwa Mchungahela kwa ajili ya mradi ambao wananchi wengi wanautarajia. Ukikamilika utaweza kuwasaidia sana kutatua changamoto zao za hapa na pale. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kuanzisha Mradi wa Maji wa Nyabehu katika Jimbo la Bunda Mjini, moja ya wanufaika wa kwanza ilikuwa wahusika wa Kata husika ya Guta. Katika ule mradi ilikuwa wajenge vituo lakini mpaka sasa hivi hakuna Vituo vya kutosha Gushigwamara, Kinyambwiga, Guta yenyewe, *Guta Centre*, Nyabehu yenyewe. Ni lini sasa watahakikisha wananchi ambao wanatoka katika maeneo ya mradi husika wanapata maji safi na salama? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninashukuru sana kwa swali zuri sana kutoka kwa Mheshimiwa Ester Bulaya. Ni suala ambalo liko kisera na sisi sera yetu ya maji kwanza kabisa ni pale ambapo tunapokipata chanzo cha maji, tunayapatia kipaumbele maeneo yanayozunguka eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili, iwapo ni mradi mkubwa ambao unaenda umbali mrefu angalau kilometa 12 kutoka kushoto kulia, lakini pia tunafahamu kabisa kwamba mradi huo ambapo Mheshimiwa Ester Bulaya amesema, ninakiri kabisa kwamba ni kweli eneo hilo lina uhitaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nilipokee kwa niaba ya Waziri wa Maji, kwamba tunaenda kulifanyia kazi na ninamwagiza *RM* upande wa Mkoa wa Mara aanze kufanya kazi haraka ili ahakikishe kwamba tunapata gharama halisi ili tuweze kupeleka huduma ya maji safi katika eneo hilo. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Maji wanakubaliana nami na wanakubali kwamba Makete ni moja kati ya Wilaya ambazo upatikanaji wa maji ni rahisi kwa sababu ni maji mserereko. Hata hivyo, Mradi wa Makusi na Mradi wa Mfumbi una miaka mitatu haujawahi kutekelezwa kwa kisingizio cha mabomba. Ni yapi maelekezo ya Serikali kwa wananchi wa Makete kuhusu kupata maji kwenye miradi hii miwili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na pia ninamshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Festo Sanga. Ni kweli kabisa kwamba amekuwa akifuatilia sana mradi huu na sisi Serikali tunakiri. Kwa Mradi wa Makusi, ni kwamba mkandarasi atarudi *site* mwezi Julai na hii inatokana na changamoto ya barabara kulingana na mvua

zinazoendelea kunyesha katika eneo hilo. Sasa, ile mitambo haiwezi kufika na kuendelea na kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu wa ujenzi, ni lazima tuangalie, unapojenga lazima ulinde unachokijenga kisiweze kuharibika. Kwa hiyo, kulingana na hali hiyo mkandarasi atarudi Julai na mradi utakamilika mwezi Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, Mradi wa Mafumbi; Mradi wa Mafumbi Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tuhakikishe kwamba kazi hii ifanyike na wananchi wako wa Makete waweze kupata huduma ya maji safi na salama. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na maswali, bado tupo Wizara ya Maji. Nimwite sasa Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea, Mbunge wa Korogwe Mjini, aulize swali lake. Simwoni kwenye eneo lake. Mheshimiwa Cecilia Paresso kwa niaba yake. *(Makofi)*

Na. 143

**Mradi wa Maji *Korogwe TC***

**MHE. CECILIA D. PARESSO K.n.y. MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA** aliuliza:-

Je, Mradi wa Maji wa Miji 28 ambao Korogwe *TC* ni mnufaika uko asilimia ngapi na utakamilika lini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Maji Miji 28 katika Wilaya ya Korogwe Mkoani Tanga. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ujenzi wa dakio *(intake)* katika Mto wa Pangani, lenye uwezo wa kuzalisha maji lita milioni 52 kwa siku, ujenzi wa miundombinu ya kutibu maji *(water treatment plant)* yenye uwezo wa kutibu maji lita milioni 51

kwa siku, ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 185, ujenzi wa matanki ya kuhifadhi maji yenye jumla ya ujazo wa lita 6,900,000, sanjari na ujenzi wa vituo viwili vya kusukuma maji *(booster stations)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu umefikia wastani wa 67.8% na unatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2025 na kunufaisha zaidi ya wananchi 868,034 waishio katika miji ya Korogwe, Handeni, Muheza pamoja na Pangani.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paresso, swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada zilizofanyika lakini hapa Mheshimiwa Mbunge, alitaka kujua ni lini kwa uhakika mradi huu utakamilika ili wananchi wa Korogwe waweze kupata maji? Hilo ni swali la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika Wilaya ya Karatu katika vijiji vya Changarawe na Endashangwet kuna visima vimechimbwa na vimetoa maji, lakini hakuna usambazaji uliofanyika. Ni lini sasa usambazaji utafanyika ili wananchi hawa waweze kupata maji? Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. Swali la kwanza ninaomba turejee katika majibu yangu ya msingi. Mradi huu utakamilika Disemba, 2025 kulingana na mkataba, lakini pia mradi huu umefikia 67.8%. Vilevile, tunatambua kwamba huu mradi ni mkubwa ambapo zaidi ya dola milioni 81 zimewekezwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kutekeleza miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Tanga pia ni zaidi ya shilingi bilioni 31.9 imetengwa kwa ajili ya *RUWASA* kuhakikisha kwamba tunaendelea kabla ya mradi mkubwa haujakamilika. Kuna miradi midogo midogo inaendelea kukamilika ili wananchi waanze kutumia maji kabla ya mradi mkubwa haujakamilika. Kwa hiyo tunaamini kabisa kwamba hili litaendelea kutibu na Korogwe

peke yake kuna *6.4 billion* ambayo tayari imepelekwa kwa ajili ya kutekeleza miradi 26. Kwa hiyo nikutoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Tanga mambo yanaenda kuwa mazuri kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa pili, suala la Karatu kama ambavyo nilisema hapo awali kwamba kuchimba kisima ni hatua moja, hatua ya pili ni kupima ubora na kupima wingi wa maji ili tufanye usanifu unaoendana na ule wingi wa maji tujue kwamba tunafanya usanifu unawafikia watu wangapi. Kwa hiyo nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, tunaendelea kufanyia kazi. Nikuhakikishie kwamba katika bajeti ya Mwaka 2025/2026 tutaingiza bajeti ya usambazaji katika maeneo ya Karatu na wananchi wako watapata huduma ya maji safi na salama. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Felista Njau.

**MHE. FELISTA D. NJAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni lini Serikali italaza mabomba kutoka Kijiji cha Mingeni, Kata ya Uru Kusini, Jimbo la Moshi Vijijini kuelekea Kisomboko kwa Maua ambapo kuna tenki kubwa na kukosekana kwa maji haya, Vijiji vya Longuo, Kariwa na vijiji vinavyozunguka vimekuwa vikikosa maji. Ninataka kujua, ni lini Serikali italaza mabomba takribani 20 ili kuweza kusambaza maji kwa wananchi hawa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua kiu ya akinamama, ninatambua pia Mheshimiwa Felista anavyojaribu kupambania akinamama. Hata hivyo, nimtoe hofu kwamba Serikali tumejipanga, miradi ya kimkakati, lakini miradi ambayo imefikia kwenye 70% mpaka 90% na kitu ndio tumeelekeza fedha zetu ziende huko ili tumalize miradi hiyo badala ya kuanza miradi mingine wakati kuna miradi imefikia katika hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wetu na ni msisitizo wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi hilo tunalipokea Mheshimiwa Mbunge na tutaenda kulifanyia kazi kwa uzito stahiki ili wananchi waweze kulaziwa mabomba na maji yaweze kuwafikia kwa ajili ya matumizi yao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Kata ya Ng'ang'ange kuna mradi wa maji ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ulikwenda katika ile Kata tangu mwaka juzi na Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti, Anna Lupembe, wakasaini mkataba, lakini mpaka leo wananchi wa Kata ya Ng'ang'ange hawajapata maji na hawana hata kisima wanaishi kwa shida na wanawake hawajatuliwa ndoo kichwani. Lini sasa ule mradi uliosaini mwaka juzi wataanza kupata maji? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea swali la Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati. Ni kweli kabisa nilienda Jimbo la Kilolo na kweli nilishuhudia utiaji saini nikiwa na Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira. Pia, Mkandarasi alifika *site* kwa ajili ya kuanza kazi, lakini kwa bahati mbaya ni kweli kabisa Mkandarasi alitoa vifaa vyake, lakini Wizara imeanza kufanya juhudi za kukaa naye na kujadiliana namna bora ya kutekeleza mradi huu ili wananchi ambao tayari kufikisha vifaa tayari tumeweka mkataba na wao na sisi hatutaki kuweka mkataba ambao haufiki mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati, tunakwenda kulifanyia kazi hili suala ili Mkandarasi aweze kupata fedha kidogo ili aweze kurejea kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mradi huu unaanza mara moja ili wananchi wake wapate huduma ya maji safi na salama.  Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Bado tunaendelea na maswali ya Wizara hii. Nimwite sasa Mheshimiwa Ally Anyigulile Jumbe Mlaghila, Mbunge wa Kyela aulize swali lake.

Na. 144

**Hatma ya Mradi wa Bonde la Mto Songwe**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza:-

Je, nini hatma ya Mradi wa Bonde la Mto Songwe?

**MWENYEKITI:** Ninaomba majibu Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Malawi kwa pamoja zinatekeleza Programu ya Maendeleo ya Bonde la Mto Songwe inayohusisha ujenzi wa Bwawa la Songwe Chini lenye thamani ya dola za Kimarekani milioni 761. Ujenzi wa Bwawa hilo unalenga kuzalisha umeme megawati 180.2, kuwezesha shughuli za kilimo cha umwagiliaji wa hekta 6,200 pamoja na kuzalisha maji kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo kwa Wilaya za Kyela na Ileje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa nchi zote mbili zipo katika mchakato wa kutafuta fedha za utekelezaji wa programu hiyo kupitia ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (*Public Private Partnership - PPP)*. Aidha, maandalizi ya kuandaa hadidu za rejea za kumwajiri Mtaalam Mshauri kwa ajili ya kufanya mapitio ya usanifu na taarifa za mazingira za miradi pamoja na kusimamia upatikanaji yanaendelea. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI :** Mheshimiwa Jumbe Ally Mlaghila.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu una umri wa miaka 22 tangu Serikali imeuanzisha, lakini pamoja na manufaa ambayo yamesemwa na Serikali, kuna

manufaa makubwa sana na manufaa yenyewe ni kwa ajili ya kuhakikisha mafuriko kwenye Mto Songwe yanazuilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuzuia mafuriko haya ni pamoja na kuhakikisha mpaka wetu kati ya Tanzania na Malawi unakuwa *stable*. Hivi sasa ninavyozungumza, Mto Songwe unatishia kuhama zaidi ya kilometa 10 kutoka Ndwanga kuja Bwawa la Matera na kuingia kwenye Mto Nsesi Kata ya Ngonga - Lugombo. Nilitaka kujua ni mashirika mangapi au kampuni ngapi mpaka sasa zimeonesha *interest* ya kuingia kwenye uwekezaji huo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili; mwaka 1969, Kampuni ya Maendeleo ya Japani *(JICA)* ilifanya upembuzi wa kuzuia mafuriko kwenye Mito ya Kiwira, Lufirio na Mbaka kwa kujenga mabwawa. Je, ni lini Serikali sasa itaanza ku-*implement* hizo *study* ambazo zilifanywa na *JICA*?

**MWENYEKITI :** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya kujibu swali la nyongeza. Ninafahamu Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila, anatamani sana kuona mradi huu unaanza kutekelezwa. Awali mradi huu tulitaka kuufanya kwa mfumo wa *EPC+F,* lakini baada ya kupitia na kujiridhisha kwamba njia hii haitakuwa sahihi, ndio maana tukaamua kuingia kwenye njia nyingine ambayo ni ya *PPP* ambayo tunaamini kabisa kwamba hii ndio njia sahihi ya kwenda kutekeleza mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile mradi huu ni lazima kwanza ufanyiwe mapitio ya usanifu kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge amesema, mradi huu ulifanyiwa usanifu miaka 22 iliyopita. Kwa kawaida kwenye miradi hii, *engineering* zote huwa zinafanyika kila baada ya miaka 10 basi usanifu huo lazima ufanyike upya tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika, yaliyoonesha *interest* mpaka sasa ni mengi ambayo kwa sasa ninaomba kwa ridhaa

yako nisiyataje, lakini ninaamini kabisa kwamba tayari wabia wengi wameonesha *interest* na tuna uhakika kabisa kwamba mradi huu utapata *support* nzuri kutoka kwa *private sector*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mabwawa, tuna mamlaka za bonde ambazo zimepewa majukumu kisheria kuratibu wingi wa maji (mafuriko) na uchache wa maji (ukame). Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba kunakuwa na *utilization* nzuri ya maji pale ambapo yanakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tutaendelea kuyajenga mabwawa haya kwa sababu tayari Mheshimiwa Rais, alinunua mitambo ya uchimbaji wa mabwawa. Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge, Serikali na Wizara yetu na maelekezo ya Mheshimiwa Waziri wetu yapo wazi kabisa kwamba kila eneo na *zone* zote tuhakikishe kwamba mabwawa yanazidi kuchimbwa ili kuweza kuteka maji na kuweza ku-*manage* maji. Lengo kubwa ni kwamba tuwe na uhakika wa kuwa na maji katika misimu yote ya nchini hapa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Nimwite Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Nkasi Kaskazini sasa aulize swali lake.

Na. 145

**Matokeo Chanya Baada ya Kupumzisha Ziwa Tanganyika**

**MHE. AIDA J. KHENANI** aliuliza:-

Je, yapi matokeo chanya baada ya kupumzisha Ziwa Tanganyika kwa miezi mitatu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa niaba yake Mheshimiwa Nibu Waziri, Alexander Mnyeti. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipumzisha shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika kwa muda wa miezi tatu, kuanzia tarehe 15 Mei hadi 15 Agosti, 2024 ikiwa ni utekelezaji wa Mkataba wa Kikanda wa Nchi Wanachama wa Mamlaka ya Ziwa Tanganyika *(Lake Tanganyika Authority-LTA)* unaolenga kuruhusu mifumo ya ikolojia kurejea, kutoa fursa kwa samaki kuzaliana, kukua na kuongezeka, hivyo kuwa na uvuvi endelevu, kuimarisha usalama wa chakula, kuongeza kipato cha wavuvi na kukuza mchango wa Sekta ya Uvuvi katika pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upumzishaji wa shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika umekuwa na matokeo chanya yakiwemo kuongezeka kwa mavuno ya Samaki kufikia tani 38,999 zenye thamani ya shilingi bilioni 324.8 katika kipindi cha miezi minne baada ya kufungua Ziwa (Septemba hadi Desemba, 2024) ikilinganishwa na mavuno ya samaki ya tani 25,113 zenye thamani ya shilingi bilioni 166.4 zilizovuliwa katika kipindi hicho mwaka 2023. Ongezeko hili ni sawa na 55.3% ya mavuno yaliyopatikana Septemba hadi Desemba, 2023 kabla ya kupumzisha Ziwa. Vilevile, thamani ya mauzo ya samaki nje kwa mwaka 2024 yameongezeka kufikia thamani ya shilingi bilioni 180.6 ikilinganishwa na thamani ya shilingi bilioni 97.03 mwaka 2023, ikiwa ni ongezeko la 86.2%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aida Khenani, swali la nyongeza.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Mheshimiwa Naibu Waziri, atakumbuka wakati wanafunga Ziwa nilimweleza hapa Bungeni kwamba, wanafunga Ziwa miezi mitatu wakati wavuvi hawa wamekata leseni ya mwaka mzima, kwa lugha nyingine walitumia mamlaka yenu kuwapa umaskini bila sababu, kwa sababu hawakuwapa pesa kipindi cha mpito. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa kuwa amesema kuna ongezeko la 55% kwa kipindi cha miezi minne na ripoti yenu wenyewe wanasema maziwa makuu yote samaki wamepungua, kwa nini kama kuna...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa swali.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna ongezeko hilo wasifunge maziwa yote makuu ili tupate ongezeko la samaki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kabla hawajafunga Ziwa walisema wataleta uvuvi mbadala kwa maana ya vizimba. Tangu mwaka jana mpaka leo hakuna kizimba hata kimoja. Serikali ina mpango gani wa kuleta uvuvi mbadala kabla ya kufunga kwa hayo mamlaka mnayotumia? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hili la kwanza kwamba sio kweli Serikali haijapeleka vizimba katika Ziwa Tanganyika. Katika Ziwa Tanganyika, tumekwishapeleka vizimba 29 hadi tunavyozungumza; kwa Mkoa wa Katavi tumepeleka vizimba viwili, Mkoa wa Sumbawanga tumepeleka vizimba viwili na Mkoa wa Kigoma tumepeleka vizimba 25, jumla ni vizimba 29 katika Ziwa Tanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine Mheshimiwa Mbunge kama ana vikundi vya wavuvi ambao wanataka vizimba tupo tayari tunaendelea kuvitengeneza na tupo tayari kupeleka katika maeneo yake ambayo anasema hayo ya Nkasi na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na kufunga maziwa yote makuu. Hili Ziwa Tanganyika lina mjumuisho wa nchi nne ambazo zilikaa na kukubaliana kulifunga kila mwaka kwa miezi mitatu. Sasa sisi Watanzania kwa mara ya kwanza tumefunga mwaka jana, wenzetu walishaanza siku nyingi na maziwa haya yanapofungwa, tija anaipata mvuvi mwenyewe wa samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Mbunge anaposema mvuvi amekata leseni ya mwaka mzima halafu anakuja kuvua miezi mitatu anapata umaskini, siyo kweli. Ziwa tunapolifunga,

tunapokuja kulifungua mazao ya samaki yanaongezeka mara dufu. Kwa hivyo yule mvuvi ambaye hajavua kwa hicho kipindi cha miezi tisa, kitendo cha kufunga lile ziwa kwa miezi mitatu, mazao wanayokuja kuvua ni zaidi ya kuvua hata kwa miaka mitatu. Kwa sababu mazao yanaongezeka mara dufu kama nilivyosema, mazalia ya samaki yanaongezeka, biashara ya samaki inaongezeka, hata ungefunga kwa miezi sita ingeongezeka zaidi na zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba zoezi la kufunga ziwa lina tija kubwa katika nchi yetu na hata nchi zinazofanya mazoezi haya yamekuwa yakileta *impact* kubwa katika wavuvi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Mbunge, tumejaribu kumuelewesha sana Mheshimiwa Mbunge juu ya kufunga Ziwa hili, lakini amekuwa mgumu sana kuelewa juu ya kufunga Ziwa Tanganyika. Hata hivyo, tunaendelea kumuelimisha kwamba, Ziwa Tanganyika lazima lifungwe ili kuongeza tija kwa wavuvi wetu ambao wamekuwa wakihangaika na samaki katika eneo hilo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ninakushukuru kwa majibu yako. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, nimwite sasa Mheshimiwa Jonas William Mbunda, Mbunge wa Mbinga Mjini aulize swali lake.

Na. 146

**Kuimarisha Utalii Nyanda za Juu Kusini**

**MHE. JONAS W. MBUNDA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuendeleza na kuimarisha Utalii Nyanda za Juu Kusini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri Khamis Hamza Khamis.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na jitihada za kukuza na kuimarisha shughuli za Utalii katika maeneo mbalimbali nchini kwa lengo la kuongeza idadi ya watalii, siku za wageni kukaa nchini na mchango wa Sekta ya Utalii katika ajira na uchumi. Mathalani, katika Mkoa wa Ruvuma Serikali inaendelea na ujenzi wa Uwanja wa Ndege Songea, uimarishwaji wa miundombinu ya Bustani ya Wanyamapori Luhira na Hifadhi ya Msitu wa Asili wa Matogoro. Aidha, Serikali imenunua boti ya kisasa kwa ajili ya shughuli za Utalii kwenye kisiwa cha Lundo katika Ziwa Nyasa yenye thamani ya shilingi milioni 200.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hayo, Serikali inaendelea kutekeleza mradi wa kuboresha usimamizi wa maliasili na kukuza Utalii Kusini unaolenga kuboresha Utalii katika Nyanda za Juu Kusini kwa kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege, malango ya kuingilia watalii kwenye Hifadhi, kujenga kituo cha utalii pamoja na kujenga kituo cha utafiti wa wanyamapori. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mbunda, swali la nyongeza.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niishukuru Serikali kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendeleza na kujenga miundombinu katika Pori la Liparamba, Tunduru na Namtumbo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwa kuwa Serikali imeanza kujenga bandari katika Ziwa Nyasa; je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuendelea kuweka miundombinu mizuri katika visiwa vilivyopo katika Ziwa Nyasa, lakini na fukwe kwa ajili ya kuvutia watalii? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mbunge kwa kazi nzuri anayoifanya, hasa katika kuchochea na kutia moto kwenye suala la utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inayo mpango kabambe wa kuhakikisha kwamba inaimarisha miundombinu katika maeneo yote hasa ya mapori ya akiba na yale mapori tengefu ili lengo na madhumuni kuanza kuvutia watalii, kuhakikisha kwamba tunatunza na tunahifadhi bioanuwai (mazingira) na zaidi kuongeza pato la Taifa. Nimwambie Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha ili lengo na madhumuni katika mapori haya kwanza itengeneze miundombinu ya barabara itakayowezesha watalii kuingia na kuzunguka, kujenga nyumba ambazo watafikia watalii kwa ajili ya kupumzika na kutengeneza vivuko na madaraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu yapo maeneo ya mapori yana mabonde na mengine ambayo yanahitajika kuvukwa, lakini zaidi kuimarisha usalama katika maeneo hayo. Nimwambie Mheshimiwa, tunaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira mazuri kwenye mapori hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo pia mpango wa kuhakikisha kwamba tunatengeneza fedha na tunatengeneza mazingira mazuri ya kuwekeza katika maeneo ya visiwa na kwenye fukwe mbalimbali ili lengo na madhumuni kutengeneza kuvutia watalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa nimwambie Mheshimiwa kwamba Serikali inaendelea kutafuta fedha ili kuhakikisha kwamba tunatengeneza mazingira mazuri ya uwekezaji katika maeneo ya visiwa na maeneo ya fukwe kwa ajili ya kukuza utalii. Tunategemea fedha aidha zitatoka Serikali Kuu au kutoka kwenye

Halmashauri kwa sababu bado kuna baadhi ya mapori yapo kwenye Halmashauri. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Yahya Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. Tunatambua sana umuhimu wa utalii katika kukuza uchumi wa nchi yetu, lakini wanyama hawa sasa imekuwa kero na wanaingia makazi ya wananchi. Mfano, leo ni siku ya tatu ndani ya Jimbo langu tembo wameondoka katika maeneo yao na kuvamia maeneo ya wananchi. Kata ya Sengenya, Kijiji cha Sengenya, Kijiji cha Naivanga, Kijiji cha Mkumbaru vimevamiwa na tembo na wananchi hawana amani kabisa. Pia Kata ya Napacho kwenye Kijiji cha Chimika wananchi wamevamiwa na wanyama hawa. Je, Serikali ipo tayari kupeleka ndege nyuki ili kuwafukuza wanyama hawa ambao sasa hivi wamekuwa kero kwa uhai wa wananchi wetu? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali inatambua changamoto ya athari inayosababishwa na Wanyama Pori hasa tembo kwa maana ya ndovu katika maeneo mbalimbali ya wananchi na *of course,* tumekuwa tukipokea malalamiko mengi ya athari za watu kuvamiwa kwenye mashamba pamoja na kupata hata athari watu wengine kupoteza maisha yao. Nimwambie tu Mheshimiwa kwamba Serikali imo kwenye mkakati na imo mbioni kuhakikisha kwamba tunakwenda kutatua na kuondosha changamoto ya tembo kuharibu makazi na siyo tembo tu hata wanyama wengine ambao kwa namna moja ama nyingine wanahatarisha makazi na wanahatarisha maisha ya wananchi. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa muda wetu wa maswali umeenda sana. Kwa hiyo, tunaenda Wizara ya Afya, nimwite sasa Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, aulize swali lake.

Na. 147

**Kuanzisha Kampuni Tanzu ya Usimamizi na Uzalishaji Dawa za Binadamu**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Je, lini Serikali itaanzisha Kampuni Tanzu ya usimamizi na uzalishaji wa dawa za binadamu nje ya *MSD?*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilianzisha Kampuni tanzu ya Usimamizi wa jukumu la Uzalishaji wa Dawa za Binadamu na Vifaa tiba inayojulikana kama *MSD Medi pharm Manufacturing Company Limited* mwezi Aprili, 2023. Lengo la uanzishaji wa kampuni hii ni kuongeza ufanisi katika kutekeleza jukumu la uzalishaji wa bidhaa za afya ikiwemo kupanua wigo wa bidhaa za kuzalisha na kuruhusu kuingia makubaliano ya ubia na wawekezaji wengine kupitia *joint venture* ili kuimarisha upatikanaji wa bidhaa muhimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kampuni hii ilipata Bodi yake ya Usimamizi mwezi Juni, 2024 na kwa sasa kampuni inaendesha viwanda vya kuzalisha bidhaa za afya, Mkoa wa Njombe na Keko Dar es Salaam pamoja na Mradi wa Viwanda vya Dawa, Zegereni Kibaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdallah Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Serikali nina maswali ya nyongeza. Swali la kwanza; kwa kuwa, pamoja na ubia *(joint venture)* zilizopo bado ufanisi ni

mdogo, tija ni ndogo. Ni asilimia nne tu ya dawa zinazotumika nchini ni asilimia nne tu huzalishwa hapa ndani. Je, Serikali haioni sasa ni wakati sahihi wa kutoa afua mbalimbali za kiuwekezaji na kikodi ili sekta binafsi iingie katika soko hili na kuzalisha dawa kwa wingi ili dawa zipatikane kwa bei nafuu? *(Makofi)*

Swali la pilli, kumekuwa na tatizo la *monopoly* kwenye soko la dawa, haswa kwenye dawa za ubingwa bobezi ni kubwa sana kiasi kwamba wananchi wengi wanashindwa kupata hiyo huduma. Serikali haioni sasa ni muda muafaka kuingiza wazabuni wengi zaidi ili kuleta ushindani na kufanya bei iwe yenye kushindana? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Shangazi, kwa maswali yake mazuri sana pia kwa ufuatiliaji wake mzuri sana kwenye mambo haya yanayohusu afya ya binadamu, lakini usimamizi wake kama Katibu wetu wa Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la kwanza ni suala la kwamba dawa sasa hivi tunazalisha ndani ya nchi asilimia nne tu. Ni kweli kwa miaka mitatu iliyopita unachokisema kilikuwa kweli, lakini ninataka nikuhakikishie kwa fursa alizozifungua Mheshimiwa Rais wetu lakini uwekezaji uliowekezwa kwa maana ya Keko, kuwekezwa kule Njombe na Kibaha sasa uzalishaji wa dawa kwenye nchi yetu ni 20%. Ninataka kuwaambia baada ya muda itaendelea kuongezeka, kwa hiyo, hicho unachosema asilimia nne ni kweli lakini kwa miaka mitatu iliyopita sasa tupo kwenye asilimia 20. Kwa hiyo, kuna *progress.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, kuhusu *monopoly* ya watu wachache kwenye masuala ya dawa na bidhaa tiba Waziri wetu Mheshimiwa Jenista Mhagama, alivyoingia ndiyo eneo la kwanza alilolishughulikia na tayari Bodi ya *TMDA* ilikaa na imeshatengeneza baadhi ya kanuni tayari na zimeanza kazi kwa ajili ya kuruhusu watu mbalimbali kusajili dawa aina moja kwa

kutokulazimisha mtu mmoja asajili dawa moja wengine wakazuiliwa. Kwa hiyo, sasa watu wanaruhusiwa kusajili dawa moja watu wengi kwa wakati mmoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Nimwite sasa Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 148

**Vigezo Vinavyotumika Kubaini Shule Kongwe**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza:-

Je, vipi vigezo vinavyotumika kubaini shule kongwe zilizofanyiwa ukarabati nchini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa niaba yake Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Juma Omari Kipanga, majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, vigezo vinavyotumika katika kubaini shule kongwe kwa ajili ya ukarabati ni pamoja na kuzingatia muda au mwaka tangu shule husika ilipojengwa, kiwango cha uchakavu na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia vigezo hivyo, Serikali inaendelea na ukarabati wa miundombinu katika shule kongwe nchini na hadi sasa tayari jumla ya shule kongwe 40 za msingi na sekondari 89 zimekarabatiwa. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, ninaomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shule ya Sekondari Seuta iliyopo Makao Makuu ya Wilaya ya Kilindi ni miongoni mwa shule kongwe nchini ambayo imeanzishwa mwaka 1948. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itapeleka fedha kidogo iliyobaki kumalizia bweni la wavulana ili azma yetu ya kufanya shule hiyo kuwa sekondari ya bweni ya kidato cha tano na sita iweze kutekelezeka? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu namba mbili; Shule ya Tanga *School* ni miongoni mwa shule kongwe ya kwanza nchini Tanzania iliyoanzisha mwaka 1895 na kwa kuwa shule hiyo imeongezewa mtaala wa amali, tunaomba sasa Serikali ifanye haraka kurekebisha karakana zilizopo ndani ya Tanga *School* ili vijana watakaomaliza pale wapate elimu stahiki ya amali. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaona la pili ni ombi, endelea.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninapenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa *Engineer* Ulenge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi kwamba ukarabati huu unategemea vigezo mbalimbali, kimojawapo kikiwa kile cha upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 tumetenga fedha kwa ajili ya umaliziaji wa mabweni 85 katika shule mbalimbali kongwe za sekondari nchini ikiwemo pamoja na shule hii aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge Shule ya Sekondari ya Seuta. Kwa hiyo, tunakwenda kufanya hivyo pesa ipo kidogo itapelekwa ili kuhakikisha bweni hili linakamilika na wanafunzi wetu wanapata maeneo mazuri ya kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo lake la pili, kuhusiana na suala la Tanga *School,* tunafahamu kwamba tumeanza utekelezaji wa mtaala mpya pamoja na sera yetu ya elimu, mtaala huu tunatekeleza vilevile kwa awamu. Kwa mwaka jana

tulianza na wale wanafunzi wa kidato cha kwanza na kidato ya sita tumeanza Julai, mwaka jana. Kwa hiyo, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge karakana zile zilizopo pale Tanga *School* pamoja na maabara sambamba na ununuaji wa vifaa vya maabara pamoja na vifaa vya karakana vyote tumeingiza katika bajeti yetu ya mwaka huu wa fedha 2024/2025 na 2025/2026 ili kuhakikisha maabara na karakana zile zinakuwa katika ubora unaohitajika ili kutengeneza vijana na wataalam tutaowahitaji nchini. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa muda wetu hauturuhusu tunaendelea na swali linalofuta. Nimwite sasa Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 149

**Mikopo ya Elimu ya Kati na Juu Kama Ruzuku kwa Watu Wenye Ulemavu**

**MHE. STELLA I. ALEX** aliuliza:

Je, ni hatua gani imefikiwa kufanya Mikopo ya Elimu ya Juu na Vyuo vya Kati kuwa ruzuku kwa watu wenye ulemavu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ya elimu ya juu inatolewa kwa wanafunzi wote wa kitanzania wenye uhitaji kwa kuzingatia Sheria iliyoianzisha Bodi ya Mikopo, Sura 178 na mwongozo wa utoaji mikopo kwa mwaka husika. Aidha, wanafunzi wenye ulemavu au wenye wazazi wenye ulemavu hupewa kipaumbele katika upangaji wa mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa masomo 2024/2025 jumla ya wanafunzi 2,398 wamenufaika na mikopo ya elimu ya juu kwa kigezo cha ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utoaji wa ruzuku kwa wanafunzi wenye ulemavu unatekelezwa kupitia ruzuku ya '*Samia Scholarship*' kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika mitihani ya kidato cha sita inayoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania *(NECTA)* katika Masomo ya Sayansi, Uhandisi na Hisabati na kudahiliwa katika programu za kipaumbele za sayansi, teknolojia, hisabati, uhandisi na tiba. Hadi sasa wanafunzi 30 wenye ulemavu wamenufaika tangu kuanzishwa kwake mwaka wa fedha 2022/2023. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Stella Ikupa, swali la nyongeza.

**MHE. STELLA I. ALEX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru lakini pia ninaomba niishukuru sana Serikali kwa jitihada kubwa zinazofanyika kwa kundi hili na ambazo zimefanyika na ambazo zinaendelea kufanyika. Pia ninaishukuru sana Serikali kwa jinsi ambavyo imekuwa ikizingatia ushauri ambao umekuwa ukitolewa ndani ya Bunge lako Tukufu kwa sababu mara kadhaa nilishauri kwamba mikopo hii izingatie wanafunzi wenye ulemavu, lakini na wazazi ambao wana ulemavu. Kwa hiyo, ninaishukuru Serikali kwamba suala hili limefanyiwa kazi na linaendelea kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa swali langu ilikuwa ni kwa wanafunzi wote wenye ulemavu ambao wanakuwa wame-*qualify* kuingia kwenye vyuo hivi vya elimu ya juu na elimu ya kati. Sasa nini kauli ya Serikali kuifanya mikopo hii kuwa ruzuku achana na wale ambao wanakuwa na ufaulu wa juu lakini wale wote ambao wanakuwa wame-*qualify* kuingia kwenye vyuo hivi na hasa ikizingatiwa kwamba ulemavu ni gharama kubwa na unahitaji fedha nyingi. Nikitolea mfano mtu ataanza kazi atahitaji kifaa kisaidizi gari, atahitaji msaidizi kwa asiyeona na yeye mwenyewe ndio anagharamika kulipa kupitia mshahara huo huo ambao unatakiwa ukatwe na Bodi ya Mikopo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Stela

Ikupa, kwa maswali yake ya nyongeza, ninaomba nijibu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, tumepokea ushauri wake na ninadhani alitoa ushauri huo mwaka jana kwamba tutoe kipaumbele kwa wenzetu wenye mahitaji maalum tumekuwa tukifanya hivyo. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Ikupa, Serikali hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeweka kipaumbele sana kwenye masuala ya *inclusive education* ikiwahusisha wenzetu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wake tumeupokea na ninaomba nimhakikishie tu katika kipindi hiki cha utekelezaji wa programu hii kama nilivyosema awali wanafunzi zaidi ya 30 wamenufaika, lakini yeye lengo lake ni kwamba mikopo hii sasa kwa upande wa walemavu itoke kuwa mikopo ende kuwa ruzuku. Kwa hiyo, ushauri huu tumeuchukua tutaenda kufanya kazi. Tunakwenda kufanya upembuzi yakinifu ili kuona namna bora Serikali inavyoweza kufanya. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea swali linalofuata. Nimwite Mheshimiwa Benaya Kapinga, Mbunge wa Mbinga Vijijini, aulize swali lake.

Na. 150

**Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Ugaidi kwa Nyuklia**

**MHE. BENAYA L. KAPINGA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajiunga na Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Kigaidi kwa kutumia Nyuklia wa Mwaka 2007?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkataba wa Kimataifa wa Kuzuia Vitendo vya Kigaidi kwa kutumia Nyuklia ni wa mwaka 2005.

Aidha, Serikali bado inaendelea na taratibu za ndani za kisheria za kuridhia Mkataba huo. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Benaya Kapinga, swali la nyongeza.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru Serikali kwa majibu lakini kama ilivyosema mkataba huu ni wa mwaka 2005 hadi sasa ni miaka zaidi ya 20 bado hatujaridhia. Swali la kwanza; je, ni hasara kiasi gani Serikali inapata kwa kutoridhia mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, kutokana na umuhimu wake Serikali ipo tayari kuharakisha mchakato wa kuridhia?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kapinga, Mbunge wa Mbinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli anayozungumza Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza mkataba umechukua muda mrefu, lakini ni hasara kiasi gani zinazopatikana. Ni kweli zipo faida nyingi za kuridhia mikataba hii kwa nchi ikiwemo sana sana kwenye masuala ya ulinzi katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni ushirikiano katika kukabiliana na vitendo vile vya kigaidi na mambo mengine. Tunafahamu mikataba hii kabla ya nchi kuridhia ni lazima nchi yenyewe kwanza ijiridhishe na masharti mbalimbali yaliyomo kwenye mikataba ile kabla ya kuridhia. Kwa hiyo, tulikuwa kwenye mchakato huo wa kuhakikisha kwamba masharti yale yote hayaendi kuibana nchi yetu kwenye hasara yoyote itakayojitokeza baadaye kabla ya kuridhia mkataba huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hicho ndicho kinachoendelea na ushauri ulioutoa Mheshimiwa Mbunge kwamba tuharakishe tumeshakamilisha *process* zote au michakato yote ilishakamilika mkataba umeshaingia mpaka Bungeni, Bunge limesharidhia. Kwa hiyo, sasa hivi tupo kwenye Kanuni tu zile za ndani za Serikali kuhakikisha kwamba mkataba huu unaridhiwa haraka iwezekanavyo. Ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Jasson Rweikiza, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. JASSON S. RWEIKIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kunipa nafasi kuuliza swali ya nyongeza. Mkataba huu ni kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu kujilinda na magaidi hasa hawa wanaotumia nyuklia. Sasa kwa kuchelewa na kusitasita kuridhia mkataba huu ina maana kwamba Serikali haijui kuwa Tanzania ina hifadhi ya madini ya *uranium* takribani tani 60,000 ambayo ni kivutio kikubwa kwa magaidi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishaeleza kwenye majibu ya swali la msingi, ni kweli anayozungumza Mheshimiwa Dkt. Rweikiza, kama nilivyoahidi kwamba Serikali tutahakikisha kwamba tunakwenda kurekebisha katika maeneo yale ambayo tuliona kwamba kuna dosari ili kuhakikisha kwamba nchi yetu inaingia kwenye mkataba huu ili tupate manufaa hayo yalikokusudiwa pamoja na haya aliyotaja Mheshimiwa Dkt. Rweikiza. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako.

Tunamaliza na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Nimwite Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi. Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 151

**Vikundi Wanufaika wa Mikopo ya Wanawake**

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI** aliuliza:-

Je, vikundi vipi vya wanawake vimenufaika na Mikopo ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii na kutengeneza ajira?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatoa mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake *(WDF),* ambapo kwa mwaka wa fedha 2022/2023 imetolewa mikopo yenye thamani ya shilingi 664,500,000 kwa vikundi 11 vya wanawake na wajasiriamali mmoja mmoja 14 hivyo kufanya jumla ya wanufaika kuwa 104 huku ajira zilizoanzishwa ni 165, (wanawake 103 na wanaume 62). Aidha, Wizara ilisimamisha utoaji wa mikopo kwa mwaka 2023/2024 ili kutathmini Mfuko. Kwa sasa Mfuko umerejesha utoaji wa mikopo kwa waombaji tangu mwezi Machi, 2025. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Maryam Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza Serikali kwa majibu yake mazuri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; Wizara ina majukumu ya kuratibu na kutoa mikopo ya wanawake wafanyabiashara ndogo nchini. Je, Serikali imedhamiria kutoa mikopo kwa makundi mangapi ya wanawake hapa nchini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Wizara inafanya tathmini ya maendeleo ya miradi ya wanawake walionufaika na mikopo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ninapenda nimpongeze Mheshimiwa Maryam kwa sababu ni mfuatiliaji mzuri wa uwezeshaji wanawake kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la mwanzo, Wizara itaendelea kutoa mikopo kadri maombi yatakavyokuja kwa sababu suala hili la mikopo ni endelevu katika kuwawezesha wanawake kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili; Wizara inafanya tathmini kupitia Maafisa wetu wa Maendeleo ya Jamii na kuona jinsi wakopaji wanavyoendesha biashara zao kutokana na masoko yanavyoendelea na ukuaji wa biashara zao. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul Yussuf Maalim, swali la nyongeza.

**MHE. ABDUL YUSSUF MAALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi imeelekeza kwa Wizara zisizokuwa za muungano kuwepo na ushirikiano. Je, ni upi mkakati wa Serikali kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na Wizara inayohusiana na jinsia kwa kule upande wa Zanzibar?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Abdul kwa kuunganisha Muungano baina ya Zanzibar na Serikali ya Muungano. Wizara ya Maendeleo ya Jamii na Wizara ya Maendeleo ya Jamii Zanzibar tunashirikiana vizuri katika kazi zetu, hasa zile za kuendeleza uchumi na tunapokwenda mataifa mbalimbali basi tunakuwa tunashirikiana kwa kazi zote ambazo tunaenda, kama Taifa, kuhakikisha Tanzania inakua kiuchumi na maendeleo kwa ujumla.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako kwa Waheshimiwa Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Sasa niweze kuwaletea wageni ambao tunao katika ukumbi wetu wa Bunge siku ya leo.

Kwanza kabisa ni wageni wa Mheshimiwa Spika na hawa ni wageni watatu ambao ni Viongozi wa Taasisi ya Nasimama na Mama Tanzania; tukianza na Mwenyekiti wa Hamasa na Usajili Taifa, Ndugu Zulfa Tonga; Ndugu George Makona, Mkuu wa Idara ya Mipango na Miradi Taifa na Ndugu James Ngole, Mjumbe wa Mkutano Mkuu Taifa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Naibu Spika, hawa ni wageni 59 ambao ni wanachama wa shirika la *Patriotic Organization* Nchi Yetu, Rais Wetu, Fahari Yetu kutoka Mikoa mbalimbali nchini Tanzania, tuwaone, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wengine waliokaa Jukwaa la Spika ni, wageni 18 wa Mheshimiwa Mhandisi Hamadi Yussuf Masauni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na hawa ni Viongozi Wakuu wa Wizara, Wenyeviti wa CCM Mikoa na Wilaya pamoja na familia yake Mheshimiwa Waziri tukianza kwa kuwataja Mheshimiwa Mhandisi Cyprian Luhemeja, Katibu Mkuu wa Wizara; Naibu Katibu Mkuu, Ndugu Christina Mndeme; Naibu Katibu Mkuu Muungano, Ndugu Abdallah Mitawi na Mwenyekiti Bodi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, Ndugu Mwanaasha Tumbo, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni Mkurugenzi Mkuu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*, Dkt. Immaculate Semesi; Mtendaji Mkuu wa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni *(NCMC)*, Prof. Eliakimu Zahabu; Msaidizi wa Makamu wa Rais Sheria, Ndugu Elisha Suku; Kaka wa Mheshimiwa Masauni, Ndugu Sadiq Masauni Yussuf; Kaka wa Mheshimiwa Masauni, Ndugu Abdulla Miraji Othuman na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Unguja, Ndugu Iddi Ali Ame. *(Makofi)*

Yupo pia Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kaskazini Pemba, Ndugu Mberwa Hamad Mberwa; Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Magharibi, Ndugu Mohamed Rajab Soud; Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Kusini Pemba, Ndugu Yussuf Ali Juma; Mwenyekiti CCM Mjini, Mkoa wa Mjini, Ndugu Taribu Ali Taribu na Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mjini, Ndugu Hamid Mbwana Said, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, watoto wake kutoka Tegeta, Jijini Dar es Salaam. Hawa ni Ndugu Faith Kiswaga na Ndugu Joshua Kiswaga, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge. Wageni wanne wa Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na Mabalozi wa Mazingira kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ummy Nderiananga, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu). Huyu ni Ndugu Shreyansh Bhupendra Bavish, Mkurugenzi wa *Cohoot Technologies PVT Limited Tanzania*. Yupo pale, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Esther Nicholaus Matiko, Mjomba wake kutoka Kata ya Turua Tarime Mjini, Mkoani Mara, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mwalimu kutoka Kishapu Mkoani Shinyanga, yupo pale.

Mgeni wa Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mchungaji kutoka Kigoma Kusini, karibu Mchungaji. *(Makofi)*

Wapo wageni 68 wa Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni. Hawa ni Wanafunzi na Walimu wa Shule ya Msingi Wilgrace kutoka Pugu, Jijini Dar es Salaam, akiwemo Nkamba Niceclara Kasalali, ambaye ni mtoto wake, karibuni sana, wapo pale.

Wapo pia wageni saba wa Mheshimiwa Shabani Hamisi Taletale, marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Tuna wageni wengine waliotembelea Bunge, kwa ajili ya mafunzo; yupo Ndugu Sada Choya kutoka Ruangwa Mkoani Lindi, karibu sana. *(Makofi)*

Tuna wanafunzi 85 na Walimu wanne wa Shule ya Msingi ya Mt. Monica kutoka Jijini Arusha, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna vile vie wanafunzi 123 na Walimu 10 wa Shule ya Msingi Ndetembia Matemu kutoka Mkoani Morogoro, wapo pale, karibuni sana kwa mafunzo. *(Makofi)*

Tunaye Ndg. Joan Mabeyo kutoka Jijini Dar es Salaam, yupo pale, karibu sana. *(Makofi)*

Mwisho kabisa kwa majina yaliyokuja sasa, tuna Mkadiriaji Majenzi wa Tanzania *Institute of Quantity Surveyors* kutoka Jijini Dar es Salaam, jina lake halikutajwa. Karibuni sana kwenye ukumbi wetu wa Bunge, kwenye kushuhudia na kujifunza yanayoendelea. *(Makofi)*

Haya ndiyo majina ambayo yamenifikia mpaka muda huu.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**MWENYEKITI:** Hoja za Serikali, nimwite sasa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa *Engineer* Hamad Yusuph Masauni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea mawasilisho ya taarifa kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Maji na Mazingira, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge, kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai na afya njema ya kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha taarifa kuhusu Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa uongozi wake mahiri na wa kipekee...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, hebu subiri kidogo. Waheshimiwa ninajua tunaongea mambo muhimu, hebu tupate utulivu kidogo ili tumsikie Mheshimiwa Waziri akisoma hotuba yake. Endelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa uongozi wake mahiri na wa kipekee katika kuleta mageuzi makubwa ya kimaendeleo kwa nchi. Hakika, katika kipindi cha

miaka minne ya uongozi wake, tumeshuhudia mafanikio ya mfano katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, katika uongozi wake, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika nyanja zote. Kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza jukumu la Kikatiba, kuwa msaidizi mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano pamoja na kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira nchini. Aidha, uongozi wake mahiri umeleta mafanikio ya kujivunia kwa Ofisi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pia pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuleta mafanikio ya kiuchumi Zanzibar pamoja na kuimarisha mshikamano na ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia, kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake inayotoa mwelekeo wa utekelezaji wa Shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026. Vilevile, ninampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda vilevile kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kuendelea kumsaidia Waziri Mkuu katika kusimamia utekelezaji wa Shughuli za Serikali. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake makini na juhudi za kipekee katika kusimamia vema Sekta ya Nishati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kwa namna ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais

wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, pamoja na Dkt. Hussen Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa CCM katika nafasi za Urais kwenye Uchaguzi Mkuu ujao utakaofanyika Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi ni mwanasiasa mzoefu mwenye uwezo mkubwa wa kiuongozi ndani ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali na Jumuiya za Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa CCM ambao leo wamewakilishwa vema hapa Bungeni na baadhi ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa maamuzi yao sahihi ya kuwapitisha kwa nguvu moja viongozi wetu wanaotarajiwa kupeperusha Bendera ya CCM katika nafasi za juu za uongozi katika nchi yetu katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Mwezi Oktoba, 2025. Kuchaguliwa kwao ni kielelezo cha ukomavu na imani kubwa waliyonayo wanachama wa CCM wote kwa viongozi hawa kutokana na uongozi wao makini na imara unaozingatia maslahi ya wananchi wote. Nitumie nafasi hii kuwaomba Watanzania wote kuendelea kuwaunga mkono, kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Steven Masatu Wasira kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Bara. Mheshimiwa Wasira ni kiongozi na mwanasiasa mzoefu, ambaye mchango wake unaendelea kuhitajika katika kuimarisha umoja na mshikamano wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ujumla waliotangulia kutoa hoja zao hapa Bungeni, ambazo zimetoa dira na mwelekeo wa utekelezaji wa Shughuli za Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Vilevile, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri

wote kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mbunge), kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na uadilifu mkubwa. Hakika katika kipindi cha uongozi wake tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, ninampongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Ninawapongeza pia Wenyeviti wote ukiwemo wewe, Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama kwa kusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru watangulizi wangu katika Awamu ya Sita, Mheshimiwa Dkt. Selemani Saidi Jafo, Waziri wa Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi chote walichohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Vilevile, napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Mawaziri wote na Wabunge kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninawaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutoa shukrani na pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga, pamoja na Makamu Wenyeviti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani, Ukanda wa Afrika. Tunaendelea kumwombea pumziko la milele. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tarehe 20 Februari 2025, nchi ilimpoteza Bi. Sifael Mushi, ambaye ni miongoni mwa walioshiriki katika tukio la kuchanganya udongo wa iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar, Tarehe 26 Aprili, 1965 wakati wa sherehe za kutimiza mwaka mmoja wa Muungano. Bi. Sifael Mushi atakumbukwa daima kwenye historia ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya salamu hizo na maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Ofisi ya Makamu wa Rais, kibajeti ina Mafungu mawili, ambayo ni Fungu 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 26; katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya shilingi bilioni 16.97 ziliidhinishwa, kwa ajili ya Fungu hilo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 15.98 ni, kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi milioni 989.21 ni, kwa ajili ya Mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu 31; kwa upande wa Fungu hili, jumla ya shilingi bilioni 45.72 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 23.81 ni, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 21.91 ni, kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fedha Zilizopokelewa na Kutumika Hadi Machi, 2025 kwa Upande wa Fungu 26. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya shilingi bilioni 12.64, fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa, kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 26, sawa na 75% ya bajeti iliyoidhinishwa. Kwa upande wa Fungu 31 jumla ya shilingi bilioni 17.77 fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa, sawa na 75% ya bajeti iliyoidhinishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, fedha za miradi ya maendeleo zilizopokelewa ni shilingi bilioni 11.72, ambayo ni sawa na 53% ya bajeti iliyoidhinishwa. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 47(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026), Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021, Sera ya Taifa ya Uchumi wa Bluu ya Mwaka 2024, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191, Ajenda ya Maendeleo ya Afrika (2063), Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030), Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032) na Miongozo na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Viongozi Wakuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kazi Zilizotekelezwa Katika Kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Nianze na masuala ya Muungano; Wabunge watakubaliana nami kuwa, amani, umoja, ushirikiano na kuheshimiana baina ya pande zote mbili za Muungano ni matunda ya Muungano wetu adhimu. Mwaka huu Muungano unatimiza miaka 61 tangu kuasisiwa kwake, ambayo ni zaidi ya nusu karne na ili kuendelea kuulinda, kuudumisha na kuimarisha Muungano wetu, hatuna budi kukumbuka tukio hili muhimu na kutathmini mafanikio makubwa yaliyopatikana kisiasa, kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuratibu masuala ya Muungano kwa mwaka 2024/2025, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipanga na kutekeleza yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuratibu vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia masuala ya Muungano. Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025 imeratibu vikao vitatu vya Kamati ya Pamoja ya Serikali mbili vilivyojadili masuala ya muungano. Vikao hivyo vilijumuisha; Kikao cha Makatibu Wakuu; Kikao cha Mawaziri; na Kikao cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika Ikulu, Dar es Salaam tarehe 4 Aprili, 2025 chini ya Mwenyekiti Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutoa elimu kwa umma kuhusu Muungano; katika kuhakikisha kuwa elimu kwa umma inatolewa, Ofisi imeanzisha kipindi mahsusi kinachorushwa katika televisheni na redio kijulikanacho kama "Hii ni Jamhuri ya Muungano ya Tanzania" kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu Muungano. Hadi sasa jumla ya vipindi 64 vya redio na televisheni vimerushwa. Aidha, elimu ya Muungano imeendelea kutolewa kwa umma kupitia maonesho ya kitaifa ikiwemo Siku ya Wakulima na Sherehe za Maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar. Vilevile, elimu ya Muungano ilitolewa kwa makundi mbalimbali ikiwemo Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Maadhimisho ya Miaka 61 ya Muungano; mwaka huu 2025, maadhimisho yanafanyika katika ngazi ya mikoa, Tanzania Bara na Zanzibar. Matukio mbalimbali yanaendelea kufanyika ikiwemo makongamano, midahalo ya Muungano katika ngazi ya mbalimbali na hivyo elimu ya Muungano inatolewa kwa upana wake. Kauli mbiu ya mwaka huu ni "Miaka 61 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Muungano Wetu ni Dhamana, Heshima na Tunu ya Taifa: Shiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025."

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza Mpango Kabambe wa Elimu ya Muungano kwa Umma ambapo viongozi mbalimbali wanashiriki katika vipindi

kuhusu Muungano vinavyorushwa na televisheni, redio na mitandao ya kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kurejesha Ligi ya Muungano, napenda kutoa taarifa kuwa mashindano hayo yameanza tarehe 24 Aprili, 2025 na fainali yake inatarajiwa itafanyika tarehe Mei Mosi, 2025. Ambayo yanashirikisha timu kutoka Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano (MAKAVAZI ya Muungano). Katika kipindi hiki, Ofisi inaendelea na maandalizi ya uanzishwaji wa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano kitakachokuwa katika Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais – Mtumba, Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuratibu masuala ya kiuchumi na kijamii - gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Serikali imeendelea kuratibu gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kila mwaka ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2025 jumla ya shilingi bilioni 49.2 zimepokelewa Zanzibar. Fedha hizo zinajumuisha shilingi bilioni 14, ikiwa ni makato ya mishahara ya Watumishi wa Zanzibar wanaofanya kazi Tanzania Bara *(PAYE)*; shilingi bilioni 21.7, gawio la misaada na mikopo nafuu ya kibajeti kutoka nje *(Government Budget Support*); na shilingi bilioni 13.5 ikiwa ni gawio kutokana na faida ya Benki Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo; Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 50 ya Zanzibar. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025 jumla ya shilingi bilioni 2.03 zimepelekwa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, ikiwemo miradi ya sekta ya elimu, afya, maji, miundombinu na nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kutokana na changamoto za sheria ya kusimamia fedha za Mfuko wa Kuchochea

Maendeleo ya Jimbo, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeanza mchakato wa mapitio ya sheria hiyo ili kuboresha usimamizi na utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na fedha za Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Februari, 2025, Ofisi pia ilitoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Zanzibar kwa lengo la kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu usimamizi na utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo. Katika semina hiyo Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujengewa uelewa kuhusu majukumu ya Taasisi za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi na programu za maendeleo zinazotekelezwa pande mbili za Muungano. Kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, miradi na programu mbalimbali zimeendelea kutekelezwa kwa pande mbili za Muungano kwa lengo la kuboresha ustawi wa kiuchumi na kijamii kwa wananchi ikiwemo Ujenzi wa Barabara za Mkoani – Chake Chake, Tunguu – Makunduchi; ujenzi wa vituo vya afya Tanzania Bara na Zanzibar, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(Tanzania Social Action Fund - TASAF III)*, miradi ya mazingira ya kuhimili mabadiliko ya tabianchi; na mradi wa ufungaji wa mitambo ya sauti baina ya waongozaji ndege na marubani katika viwanja vya ndege 12; vya Tanzania Bara 10 na Zanzibar viwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; katika kipindi hiki Ofisi imeendelea kuhimiza umuhimu wa Wizara, taasisi na Idara za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zisizo za Muungano kwa kufanya vikao vya ushirikiano kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika utekelezaji wa mambo yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano; Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji

wa masuala 22 ya Muungano yanayosimamiwa na Wizara, Idara na Taasisi za Muungano. Ambapo baadhi ya shughuli zilizofanyika ni pamoja na kudahili jumla ya wanafunzi 137,817 wa shahada ya kwanza katika vyuo 86 vya elimu ya juu nchini; ambapo kati ya wanafunzi hao, wanafunzi 4,860 walidahiliwa katika Vyuo Saba vya Elimu ya Juu, Zanzibar; ujenzi wa mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu cha Kiislam *(Pemba Islamic Teachers College)* uliogharimu kiasi cha shilingi milioni 300; na kufunga seti ya mitambo 20 ya hali ya hewa na seti ya mitambo 15 ya hali ya hewa-kilimo inayojiendesha yenyewe katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli nyingine ni uratibu wa ujenzi wa mfumo wa ubadilishanaji wa taarifa za *ZanXchange* unaosimamiwa na Mamlaka ya Vitambulisho Zanzibar na kujenga uwezo wa vijana 80 kuhusu utengenezaji wa mifumo wa laini na programu za TEHAMA kupitia taasisi ya Python Tanzania katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar *(SUZA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hifadhi na usimamizi endelevu wa mazingira; maendeleo endelevu ya Taifa letu yanachangiwa na ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na utunzaji wa mazingira. Aidha, matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo ni muhimu kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vijavyo. Hivyo, suala la usimamizi na uhifadhi wa mazingira ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Sita katika kuleta maendeleo endelevu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mikakati, miongozo na miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira pamoja na kuratibu utekelezaji wa mikataba ya kikanda na kimataifa inayohusu hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuratibu Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021. Mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili ni pamoja na; kujumuishwa kwa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika sera,

mikakati pamoja na mipango na bajeti ya Serikali; na kuimarika kwa uratibu na ushirikiano wa kisekta katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ikiwemo kuimarishwa kwa vitengo vya mazingira katika Wizara na taasisi za umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuratibu Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; kuhusu kanuni na miongozo ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Ofisi imeandaa Kanuni nne ambazo ni; Kanuni za Upatikanaji na Mgawanyo wa Faida za Rasilimali za Kijenetiki, Kanuni ya Dhamana ya Kuzingatia Masharti ya Mazingira, Kanuni za Usimamizi Jumuishi wa Ukanda wa Pwani, na Kanuni za Haki ya Fidia. Aidha, Ofisi imeratibu na kukamilisha mapitio ya kanuni tano ili kuendana na mahitaji ya sasa ya hifadhi na usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imekamilisha miongozo mitatu na mikakati miwili ya hifadhi ya mazingira ambayo ni: Mwongozo wa Kuhuisha Masuala ya Urejeshwaji wa Mazingira Kwenye Sera, Sheria, Mipango, Mikakati na Programu; Mwongozo wa Kuhuisha Masuala ya Jinsia Kwenye Urejeshaji wa Mazingira; Mwongozo wa Taifa wa Tathmini ya Athari na Ukaguzi wa Mazingira kwa Wizara za Kisekta; Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka wa mwaka 2025 - 2030; pamoja na Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Bayoanuai wa mwaka 2025 mpaka 2030.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Serikali iliwasilisha Muswada wa Marekebisho Madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 uliopitishwa na Bunge tarehe 12 Februari, 2025 na kusainiwa tarehe 4 Machi, 2025 kuwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.5 ya mwaka 2025. Masuala yaliyozingatiwa ni pamoja na; Kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi, kuanzishwa kisheria kwa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni na kuongeza jukumu la usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi kwa vitengo vya mazingira kwa Wizara za kisekta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Taarifa ya Hali ya Mazingira; Ofisi imekamilisha Taarifa ya Nne ya Hali ya Mazingira Nchini kwa

mujibu wa matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Aidha, taarifa hiyo itawasilishwa katika Bunge lako Tukufu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utoaji wa vibali vya tathmini ya mazingira kimkakati; Ofisi imetoa kibali kimoja cha Tathmini ya Mazingira Kimkakati kwa Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, miradi sita ya kimkakati iko katika hatua tofauti za taratibu za kupatiwa vibali vya tathmini ya mazingira kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mkutano Maalum wa Viongozi na Wataalam na Wadau wa Mazingira Kuhusu Mwenendo wa Hali ya Mazingira Nchini; Ofisi iliratibu Mkutano Maalum wa Viongozi, Wataalam na Wadau wa Mazingira kuhusu Mwenendo wa Hali ya Mazingira Nchini uliofanyika tarehe 9-10 Septemba, 2024 Jijini Dodoma, uliohudhuriwa na washiriki 2,541. Maazimio ya Mkutano huo yalijumuisha: Suala la hifadhi ya mazingira kupewa kipaumbele katika mipango na bajeti za wadau wote ikiwemo bajeti za Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Asasi Za Kiraia; kuweka mazingira wezeshi yatakayohakikisha gharama nafuu na upatikanaji wa teknolojia ya nishati safi ya kupikia; suala la mazingira kuwa ajenda ya kudumu katika vikao vyote vya Mamlaka za Serikali za Mitaa; kurejesha Idara ya Mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuimarisha usimamizi wa uchumi wa bluu; kuhamasisha wadau wote kushiriki na kunufaika na fursa za biashara ya kaboni; na kuboresha mbinu za utoaji elimu ya mazingira kwa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ni kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2022 mpaka 2032. Katika kipindi cha mwaka 2024/2025, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Aidha, nitumie fursa hii kuendelea kuwahimiza wadau wote kuhakikisha wanajumuisha utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wa mwaka 2022 mpaka 2032 katika sera, mikakati, mipango na bajeti zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, ni kuimarisha uratibu na utekelezaji wa masuala ya hifadhi ya usimamizi wa mazingira katika Wizara za kisekta, sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ofisi imeteua maafisa viungo 28 kwa lengo la kuimarisha uratibu, msukumo na ufuatiliaji wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira kwenye Wizara, taasisi za umma, sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hatua hii imeimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa mazingira katika sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Baadhi ya mafanikio muhimu ni pamoja na:-

(i) Kuongezeka kwa uelewa kuhusu uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;

(ii) Kubainishwa kwa fursa na changamoto za uhifadhi wa mazingira katika mikoa na kuweka mikakati ya kunufaika na fursa hizo na kukabiliana na changamoto zilizopo; na

(iii) Kuhamasisha ushiriki katika biashara ya kaboni ambapo Viongozi wa Sekretarieti za Mikoa 26, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakuu wa Taasisi za Umma 284 walijengewa uwezo kuhusu Biashara ya Kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, ni udhibiti wa taka. Ili kudhibiti usimamizi wa taka na kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo ya majiji na miji, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi, imeendelea kuboresha mifumo ya usafi wa mazingira ikiwemo ujenzi wa vituo vya kukusanya, kuhifadhi na kurejeleza taka ngumu na uboreshaji wa mifumo ya majitaka katika miji na majiji. Mathalani, Jiji la Dar es Salaam lina jumla ya viwanda/vituo vya urejelezaji taka 44 kwa aina ya plastiki, chuma chakavu, mafuta machafu, tairi chakavu, taka za kielektroniki na taka ozo ambapo jumla ya tani 12,926 za taka zimechakatwa. Uwepo wa mfumo huu umepunguza kiasi cha taka kinachopelekwa dampo na kutoa fursa za ajira na kipato kwa makampuni na vikundi vya ukusanyaji wa taka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado hali ya usafi wa miji na majiji yetu siyo ya kuridhisha. Kupitia Bunge lako Tukufu, nazielekeza sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia udhibiti wa taka na kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo yao. Aidha, natoa rai kwa wananchi na wadau wote kuendeleza utamaduni wa kufanya usafi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita, ni nishati Safi ya Kupikia. Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia wa mwaka 2024 mpaka 2034. Ofisi imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi za umma na binafsi, ambapo jumla ya taasisi 903 zimeanza kutumia nishati safi ya kupikia. Taasisi hizo ni pamoja na; Shule za msingi na sekondari, vyuo vya kati na ualimu, Magereza, Jeshi la Ulinzi, Jeshi la Kujenga Taifa, Sekta Binafsi na Taasisi za Dini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, Ofisi imefanya uhamasishaji kwa taasisi za kifedha kuwezesha wadau wa nishati safi ya kupikia ambapo kwa mwaka 2025, Benki ya *NMB* imetenga jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 100 kwa ajili ya utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa makampuni ya usambazaji wa gesi pamoja na wajasiriamali wadogo wakiwemo baba na mama lishe ili waweze kuweka miundombinu na nishati safi ya kupikia katika maeneo yao ya biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni *(NCMC),* kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani *(WFP)* imeanzisha miradi ya mfano ya biashara ya kaboni kwa shule za msingi na sekondari zinazotumia nishati safi ya kupikia ya majiko ya umeme *(pressure cookers)* kwa Mikoa ya Kigoma, Tabora na Dar es Salaam kama maeneo ya majaribio. Aidha, miradi hiyo inatarajiwa kutekelezwa katika maeneo mengine nchini na hivyo kuwezesha taasisi hizo kupata mapato yatokanayo na biashara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba kuzielekeza sekretarieti za mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia utekelezaji wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi za umma na binafsi zinazolisha watu zaidi ya 100 sambamba na kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba, ni elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Ofisi imeanzisha kipindi maalum kiitwacho "Mazingira Yetu na Tanzania Ijayo" ambapo jumla ya vipindi 67 vimeandaliwa na kurushwa kupitia *TBC* Taifa. Vipindi hivyo vilihusu matumizi ya nishati safi ya kupikia, fursa za uwekezaji katika sekta ya mazingira, biashara ya kaboni, kampeni ya upandaji miti, Maadhimisho ya Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni, uhamasishaji wa usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu. Aidha, ili kuhakikisha kuwa uhifadhi wa mazingira unakuwa endelevu, Ofisi ya Makamu wa Rais imepanga kutoa elimu ya mazingira kwa umma kuanzia ngazi za chini, hususan watoto ili kuwajengea utamaduni wa usafi na uhifadhi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane, ni Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani. Katika kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira, Ofisi imepanga kufanya maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Mazingira Duniani yatakayofanyika tarehe 5 Juni, 2025. Shughuli zilizopangwa kufanyika kuelekea kilele cha maadhimisho hayo ni pamoja na:-

(i) Kongamano la Viongozi wa Dini, usafi wa mazingira nchi nzima;

(ii) Uzinduzi wa Jukwaa Maalumu la Wadau wa Mazingira kwa ajili ya kujadili kwa pamoja changamoto na fursa katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa Tanzania Bara na Zanzibar; na

(iii) Tamasha la Vijana Kuhusu Mazingira, na Tamasha la Wadau wa Nishati Safi ya Kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, maadhimisho haya yatashirikisha ipasavyo vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ili kuhakikisha elimu ya hifadhi ya mazingira itakayotolewa wakati wa maadhimisho hayo inawafikia wananchi wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa, ni kuhusu kampeni ya kitaifa ya upandaji miti. Ofisi inaendelea kuhamasisha kampeni ya upandaji na utunzaji miti ambayo inalenga kila halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka ambapo takribani miti 224,795,501 ilipandwa katika halmashauri zote nchini, sawa na 81% ya lengo la miti 276,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mkakati huu wa kitaifa, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikihamasisha wadau mbalimbali kujihusisha na suala la kukijanisha Jiji la Dodoma. Kwa mfano Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* imekuwa ikisaidia juhudi za Serikali, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, kupitia mradi wa Jawabu la Kijani katika Jiji la Dodoma. Mradi huu umejikita katika upandaji wa miti katika eneo la pembezoni mwa barabara ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima vya maji kwa ajili ya ustawi wa miti hiyo iliyopandwa. Mwamko huu wa upandaji miti barabarani, pia umeungwa mkono na JKT Makutupora, ambapo tayari sura ya kijani katika eneo hilo imeanza kujitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai kwa wananchi, taasisi mbalimbali na sekta binafsi kuendelea kupanda na kutunza miti hasa katika kipindi hiki ambacho mvua za masika zinaendelea kunyesha. Vilevile, nizikumbushe halmashauri zote kuendelea kusimamia na kugharamia zoezi la upandaji miti. Vilevile nazikumbusha taasisi husika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu aina ya miti ya kupanda katika maeneo mbalimbali na kutoa ushauri wa namna ya kupanda miti na maua kwenye maeneo ya miji, ikiwa ni pamoja na maeneo kame na ya milima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi, ni kuratibu na kusimamia biashara ya Kaboni nchini. Mwezi Februari 2025, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ambayo yalijumuisha kuanzishwa kisheria

kwa Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni *(National Carbon Monitoring Centre – NCMC)*. Kuanzishwa kwa kituo hiki ni hatua ya kimkakati itakayowezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunufaika zaidi na biashara ya Kaboni na hivyo kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi kwa kushirikiana na *NCMC,* imeendelea kuratibu na kuimarisha usimamizi wa biashara ya Kaboni nchini ambapo jumla ya miradi 73 ya biashara ya kaboni imesajiliwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya kaboni imeanza kuleta manufaa kiasi katika baadhi ya maeneo nchini, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 45 zimelipwa na kunufaisha wananchi katika halmashauri 10 nchini kama gawio la mauzo ya viwango vya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hicho, ofisi iliratibu vikao mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kikao cha kuwajengea uwezo Makatibu Wakuu 21 kuhusu biashara ya kaboni kilichofanyika mwezi Agosti, 2024 Dodoma;

(ii) Kikao na Wawakilishi wa Kampuni 27 zinazojihusisha na biashara ya Kaboni; na

(iii) Vikao vya kimkakati vya kuimarisha usimamizi wa biashara ya Kaboni baina ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Wizara ya Fedha; Wizara ya Maliasili na Utalii; Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania *(TUCTA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Ofisi iliratibu Mkutano wa Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma uliohusisha washiriki 850 uliolenga pamoja na mambo mengine kuibua fursa ya miradi ya kimkakati ya kitaifa ya biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha kuwa biashara ya kaboni inaendeshwa kwa uwazi na fursa zilizopo zinatumika ipasavyo na kuleta tija na manufaa kwa wananchi. Serikali imeunda Kamati ya Wataalam iliyopewa majukumu ya kushauri kuhusu mikakati madhubuti ya kuimarisha usimamizi wa biashara ya kaboni; na kubaini na kutoa mapendekezo ya kushughulikia changamoto zilizopo au zinazoweza kujitokeza katika biashara ya kaboni. Kamati hiyo inajumuisha wajumbe kutoka Wizara, Idara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, na Mashirika yasiyo ya Serikali. Aidha, Kamati husika inatarajiwa kuwasilisha taarifa yake tarehe 9 Mei, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ukweli kuwa Biashara ya Kaboni ni dhana ngeni kwa wananchi walio wengi. Nitoe rai kwa umma kutumia ipasavyo Kituo cha Uratibu wa Kaboni nchini ili kupata ushauri wa kitaalam na miongozo stahiki kuhusu biashara hiyo ambayo siyo tu inachangia ukuaji wa uchumi, lakini pia uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, ninatoa rai kwa taasisi za umma na sekta binafsi zijumuishe masuala ya biashara ya kaboni katika miradi yake ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ushirika wa nchi katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi iliratibu na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kama ifuatavyo:-

(i) Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi;

(ii) Mkutano wa 16 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bioanuai;

(iii) Mkutano wa 39 wa Nchi Wanachama wa Itifaki ya *Montreal* kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni;

(iv) Mkutano wa 16 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame *(UNCCD)*;

(v) Mkutano wa 11 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi *(COP 11)*; na

(vi) Mkutano wa 12 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia mikutano hiyo, makubaliano na maazimio mbalimbali yaliyokubaliwa ambayo yatainufaisha nchi yetu katika maeneo mbalimbali ikijumuisha:-

(i) Kuanza kufanya kazi kwa Mfuko wa Kushughulikia Upotevu na Hasara zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Kuwekwa kwa utaratibu na uwazi wa kusimamia miradi ya biashara ya Kaboni inayotekelezwa baina ya nchi na nchi;

(iii) Pamoja na miradi ya upandaji miti kukubaliwa kusajiliwa katika biashara ya Kaboni;

(iv) Kupata ahadi ya Dola za Marekani milioni 784.33, ambayo ni sawa na shilingi trilioni mbili kwa ajili ya miradi ya hifadhi za mazingira na mabadiliko ya tabianchi; na

(v) Tanzania kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa kundi la Wataalam wa Afrika wa majadiliano katika Mikataba ya Umoja wa Mataifa *(Africa Group of Negotiators (AGN))*, ambapo Dkt. Richard Stanslaus Muyungi, Mjumbe Maalumu na Mshauri wa Rais wa masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya tabianchi ndiye Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza sana Dkt. Muyungi kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa *AGN*. Aidha, Mwenyekiti huyo ameanza kuetekeleza majukumu yake kuanzia tarehe 15 Machi, 2025 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Serikali itaendelea kuyafanyia kazi kikamilifu makubaliano na maazimio yote yaliyofikiwa, ikiwemo ahadi za fedha na misaada ya kiufundi ili kuhakikisha kuwa nchi inaendelea kunufaika vyema na fursa za mikataba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira; Ofisi iliratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kumi 10 kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Fukwe ili kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi zitokanazo na ongezeko la kina cha bahari;

(ii) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini;

(iii) Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania;

(iv) Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai Tanzania;

(v) Mradi wa Kuanzisha Bustani ya Kijani Katika Eneo la Swaswa Mnarani, Dodoma;

(vi) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa *Montreal* kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong’onyoa Tabaka la Ozoni;

(vii) Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma;

(viii) Mradi wa kuandaa Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kuhifadhi Bioanuai;

(ix) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Mazingira na Kuboresha Maisha ya Jamii za Wavuvi; na

(x) Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Mheshimiwa Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa miradi hiyo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:-

(i) Kuimarisha uwezo wa kitaasisi na utaalam katika hifadhi ya mazingira ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;

(ii) Kuimarika kwa utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191;

(iii) Kuwezesha uwepo wa shughuli mbadala kwa jamii zinazoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi; na

(iv) Kurejeshwa kwa ardhi iliyoharibika kutokana na uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uratibu wa uchumi wa buluu nchini; Ofisi Katika kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa shughuli za Uchumi wa Buluu, Serikali ilizindua Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 na Mkakati wa Utekelezaji wake (2024 - 2034), mwezi Juni, 2024. Kufuatia uzinduzi huo, Ofisi ya Makamu wa Rais imekasimiwa jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera hiyo ambapo miongoni mwa shughuli muhimu katika utekelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu zinajumuisha kuanzisha mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya kuratibu shughuli za uchumi wa buluu na kuandaa Mpango wa Matumizi wa Maeneo ya Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli hizo za uchumi wa Buluu, ambapo Kamati za Makatibu Wakuu na Mawaziri wa Sekta za Uchumi wa Buluu kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa shughuli husika zimeundwa na kuanza kufanya kazi. Aidha, katika kuimarisha mfumo wa

uratibu wa masuala ya uchumi wa buluu, Ofisi inaendelea kufanyia kazi masuala ya kimuundo na kisheria katika uratibu wa shughuli hizo. Vilevile katika kipindi hicho utoaji elimu kwa umma kuhusu uchumi wa buluu kupitia makongamano na mikutano mbalimbali umefanyika. Aidha, nitumie fursa hii kuwahimiza wadau wote wa uchumi wa buluu nchini kutekeleza shughuli zilizopangwa kama ilivyobainishwa katika mkakati wa utekelezaji wa sera na kutoa taarifa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu changamoto na utatuzi; pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka wa fedha 2024/2025, ofisi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo: uelewa mdogo wa jamii kuhusu masuala ya Muungano na faida zake hususani vijana. Aidha, kwa upande hifadhi na usimamizi wa mazingira bado kuna changamoto ya uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa hifadhi ya mazingira na uzingatiaji hafifu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa changamoto; katika kukabiliana na changamoto hizo, ofisi imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano na faida zake kwa jamii hususan vijana kupitia vyombo vya habari, makongamano, warsha, semina, mitandao ya kijamii na midahalo mbalimbali. Aidha, kuanzia sasa ofisi imepanga kuwa na programu mahsusi ya elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano ili kuondoa ombwe la ukosefu wa uelewa wa kutosha miongoni mwa jamii hususan vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikakati mingine iliyotekelezwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191; na kujenga uwezo kwa wataalam katika Wizara, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza kasi ya utoaji wa elimu na usimamizi wa hifadhi ya mazingira pamoja na biashara ya kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)*. Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Mipango,

Miongozo na maelekezo mbalimbali ya Serikali. Katika kipindi hicho, masuala yaliyotekelezwa yanajumuisha:

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, uzingatiaji na usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 19. Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira. Baraza limefanya kaguzi katika miradi mbalimbali ikiwemo miradi 3,278 katika maeneo mbalimbali ili kuimarisha uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 na Kanuni zake. Katika kaguzi hizo, ilibainika kuwepo kwa ongezeko la uzingatiaji wa Sheria katika maeneo yote yaliyokaguliwa. Uhamasishaji na ufuatiliaji umesababisha ongezeko la idadi ya wawekezaji wanaosajili miradi kwa ajili ya tathmini ya athari ya mazingira na kaguzi za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti wa taka hatarishi; Baraza limeendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti wa Taka Hatarishi za mwaka 2019 na Marekebisho yake ya mwaka 2020/2021. Katika kipindi hicho, Baraza lilipokea maombi 289 ya vibali vya usimamizi wa taka hatarishi, ambapo vibali 121 vilitolewa. Aidha, Baraza lilipokea maombi 82 ya uteketezaji wa taka hatarishi na kusimamia uteketezaji wa tani 5,840.6, zikiwemo dawa na vifaatiba vilivyokwisha muda wake na mabati ya *Asbestosis*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kushughulikia malalamiko ya umma kuhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Katika kipindi hicho, Baraza lilipokea na kushughulikia malalamiko 247 yaliyohusu kelele, utupaji taka ovyo, utiririshaji ovyo wa majitaka, ujenzi holela, uchimbaji usio rasmi wa mchanga na uchafuzi wa hewa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: Kutoa elimu kwa jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira; na adhabu ilitolewa pale ilipobainika kama kuna ukiukwaji wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tathmini ya athari kwa mazingira na ukaguzi wa mazingira. Miradi iliyosajiliwa. Katika hicho jumla ya miradi 1,358 ilisajiliwa katika miradi hiyo 1,113 ilisajiliwa kwa ajili ya tathmini ya athari ya mazingira na miradi 245 kwa ajili ya ukaguzi wa mazingira. Aidha, miradi 740 imeidhinishwa

na kupata vyeti ambapo 705 ni ya tathmini ya athari kwa mazingira na 35 ni miradi ya ukaguzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usajili na uratibu wa utendaji kazi wa Wataalam Elekezi wa Mazingira. Baraza lilipokea na kuchakata jumla ya maombi 106 ya usajili wa Wataalam Elekezi wa Mazingira. Katika maombi hayo, jumla ya Wataalam Elekezi wa Mazingira 49 waliidhinishwa. Vilevile, Baraza lilipokea na kuchakata maombi 81 ya vyeti vya utendaji kazi wa Wataalam Elekezi wa Mazingira. Aidha, Wataalam 55 walikidhi vigezo na kupatiwa vyeti vya utendaji kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, utekelezaji wa Ajenda ya Taifa ya Tafiti za Mazingira. Baraza lilifanya tathmini na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu masuala mbalimbali ya mazingira katika Mifumo Ikolojia ikiwemo: Maporomoko ya Mlima Kawetere na Mlima Hanang pamoja na misitu na vichaka vya Itigi vilivyoko Mkoani Singida; Mlima wa Livingstone; Maporomoko ya Ardhi Muleba; na Mafuriko Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, uratibu wa miradi inayotekelezwa na Baraza. Baraza kwa kushirikiana na wadau mbalimbali limeendelea kuratibu miradi mbalimbali ya kuhifadhi mazingira ikiwemo mradi wa kupunguza matumizi ya zebaki kwenye uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu ambapo umechangia kuleta teknolojia mbadala ya zebaki. Aidha, miradi mingine ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi wilayani Bunda; Mradi wa uvunaji maji wa kimkakati kuwezesha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwa wakazi wa vijijini kwenye sehemu kame za Wilaya za Bunda, Kongwa na Bahi, Manyoni, Igunga na Nzega na Zanzibar (Kaskazini B na Wete – Pemba), miradi hii imechangia kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi na kuwezesha jamii kuwa na shughuli mbadala za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu elimu kwa umma; Baraza limeendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, runinga, na mitandao ya kijamii. Aidha, elimu

ilitolewa kupitia maonesho, makala na magazeti, makongamano, na semina mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2025/2026. Mpango na bajeti ya Ofisi umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo: Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; Mpango Mkakati wa Ofisi (2021/2022 - 2025/2026); Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 hadi 2025/2026); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025; maagizo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Serikali; na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, kwa mwaka wa fedha 2025/2026: moja, masuala ya Muungano. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kwa masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kushughulikia Masuala ya Muungano; kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(ii) Kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano (MAKAVAZI);

(iii) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii;

(iv) Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano;

(v) Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano;

(vi) Kuandaa machapisho na kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 62 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na

(vii) Kukamilisha na kutumia Mfumo wa Kieletroniki wa Uratibu wa Taarifa za Masuala ya Muungano na yasiyo ya Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, hifadhi ya usimamizi endelevu wa mazingira. Katika kuhakikisha masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira linakuwa endelevu, ofisi imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo kwa mwaka wa fedha 2025/2026:-

(i) Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032);

(ii) Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira;

(iii) Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira;

(iv) Kuendelea kuratibu miradi ya maendeleo inayohusu hifadhi ya Mazingira;

(v) Kuendelea kuratibu Biashara ya Kaboni nchini; na

(vi) Kuendelea kuhamasisha na kuratibu matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, uratibu wa shughuli za uchumi wa buluu. Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya Mwaka 2024 na Mkakati wake (2024 – 2034), ambapo kazi zilizopangwa kutekelezwa zinajumuisha:-

(i) Kuratibu marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Uendeshaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura 388 ili

kuiwezesha taasisi hiyo kusimamia rasilimali zote za Uchumi wa Buluu zilizopo katika eneo la Ukanda wa uchumi wa bahari na Bahari Kuu na hivyo nchi kunufaika ipasavyo na rasilimali tulizonazo;

(ii) Kuratibu maandalizi ya mpango wa kushirikisha jamii katika kuimarisha usalama wa maeneo ya maji;

(iii) Kuratibu maandalizi ya Mpango wa Matumizi ya Maeneo ya Maji;

(iv) Kuratibu maandalizi ya mpango wa kuhamasisha uwekezaji wa kimkakati na jumuishi; na

(v) Kuandaa mwongozo wa kufanya utafiti jumuishi miongoni mwa sekta za uchumi wa buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, kazi nyingine zitakazotekelezwa na Ofisi; kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni pamoja na:-

(i) Kusimamia masuala ya utawala na menejimenti ya rasilimali watu;

(ii) Kuratibu maandalizi ya nyaraka mbalimbali;

(iii) Kuandaa bajeti na utekelezaji wa mipango mbalimbali;

(iv) Kuelimisha umma kuhusu majukumu, sera, mikakati na programu zinazotekelezwa na Ofisi;

(v) Kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria;

(vi) Kkufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake;

(vii) Kushauri na kusimamia masuala ya ununuzi wa huduma na bidhaa;

(viii) Kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya Fungu 26 na 31;

(ix) Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi; na

(x) Kutoa msaada wa kitaalam katika masuala ya TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano, kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bioanuai. Lengo la mradi ni kuimarisha usimamizi jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa Mfumo wa Ikolojia na jamii kwa ujumla Nchini Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Tanganyika, Sumbawanga na Mpimbwe katika Bonde la Ziwa Rukwa na Halmashauri za Wilaya ya Mbeya, Mbarali, Wanging'ombe na Iringa katika Bonde la Ruaha Mkuu. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha Shilingi bilioni 7.1 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Kujenga Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Kigoma; mradi huu ni kuboresha mifumo ikolojia itakayoongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma, Wilaya ya Kakonko; Kibondo na Kasulu, hivyo kuchangia moja kwa moja kuboresha mazingira katika maeneo husika. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi bilioni 17.0 kimetengwa kwa ajili ya shughuli za mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi katika jamii zinazozunguka Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Zanzibar. Lengo la Mradi huu ni Kupunguza athari na kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika jamii

pamoja na ikolojia katika Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Maeneo Kame ya Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa katika Misitu ya Miombo iliyopo katika Mikoa ya Tabora, Katavi na Rukwa kwa Tanzania Bara pamoja na Zanzibar. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Maandalizi ya Taarifa ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi. Mradi huu ni kwa ajili ya kuandaa taarifa ya tatu ya utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi katika mwaka wa fedha 2025/2026, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.4 kimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaifa wa Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris kuhusu mabadiliko ya tabianchi. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni Nchi Mwanachama wa Makubaliano ya Paris, ili kuwezesha utekelezaji wa makubaliano hayo ofisi iliratibu mradi kwenye lengo la kujenga uwezo wa taasisi katika utekelezaji wa makubaliano husika. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi Kutekeleza Mkataba wa *Montreal* kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; mradi unalenga kujenga uwezo wa kitaasisi kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya *Montreal* kuhusu udhibiti wa kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya *Montreal* kupitia Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa *(UNEP)*. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, shilingi milioni 433 zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Babati; katika kurejesha Ikolojia ya Ziwa Babati, Ofisi imepanga kutekeleza mradi uliolenga kukabiliana na uharibifu unaotokana na shughuli za kibinadamu katika ziwa hilo.

Katika mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi milioni 200 kimetengwa kwa ajili ya shughuli za mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Chala na Ziwa Jipe. Lengo la Mradi huu ni kuimarisha ikolojia na usimamizi endelevu wa Ziwa Chala na Ziwa Jipe. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi milioni 200 zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Kuanzisha Bustani ya Kijani katika Eneo la Swaswa Mnarani, Dodoma. Mradi huu unahusu kuanzishwa kwa Bustani ya Kijani katika eneo oevu la Swaswa Mnarani Jijini Dodoma. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kiasi cha shilingi bilioni 2.5 kimetengwa kwa ajili utekelezaji wa shughuli za mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi mingine inayotekelezwa ni: Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Mradi huu ni kwa ajili ya kuwezesha ujenzi na ukarabati wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.7 kimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendelea kuratibu tathmini ya athari ya mazingira na kusajili Wataalam Elekezi wa mazingira;

(ii) Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira;

(iii) Kufanya kaguzi za mazingira katika maeneo mbalimbali;

(iv) Kufanya tafiti mbalimbali za mazingira;

(v) Kufanya mapitio ya Ajenda ya Taifa ya Tafiti za Mazingira;

(vi) Kuratibu na kuendesha Kongamano la Sita la Sayansi kuhusu uhifadhi wa maeneo oevu; na

(vii) Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Binadamu na Hifadhi Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho na shukrani; mafanikio yaliyopatikana katika mwaka wa fedha 2024/2025 yamechangiwa na ushirikiano mzuri kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, Sekta binafsi, Taasisi za Fedha nchini, Asasi Zisizo za Kiserikali za ndani na nje ya nchi na wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na, Umoja wa Nchi za Ulaya *(EU)*, Benki ya Dunia *World Bank* Shirika la Fedha la Kimataifa *(IMF)*, Serikali ya Norway, Serikali ya Saudi Arabia, Serikali ya Sweden, Serikali ya Uingereza, Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini, Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira *(UNEP)*, Mfuko wa Mazingira wa Dunia *(GEF)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Kimataifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi *(AF)*, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*AfDB)*, Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola *(FCDO)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda *(UNIDO)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Maendeleo *(UNCDF)*, Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani *(WWF)*, Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo – *IFAD*, Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi *(GCF)*, Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula *(FAO)*, Mfuko wa Utekelezaji wa Mkataba wa *Montreal*, Mfuko wa Dunia wa *Bayoanuai (GBFF)*, Shirika la Chakula Duniani *(WFP)*, *The Good Neighbors Global Impact Foundation, Korea Investment Securities* na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani *(GIZ)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa wadau wote wa ndani ambao wamekuwa wakitoa msaada wa kitaalam na rasilimali fedha katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuimarisha hifadhi ya usimamizi wa mazingira

wadau hao wanajumuisha Taasisi za Kifedha, Sekta Binafsi, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali pamoja na Taasisi za Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, natoa shukrani za dhati kwa mabalozi wa mazingira kwa mchango wao mkubwa katika kuhamasisha jamii kuhusu hifadhi na usimamia wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutumia fursa hii kuwaomba washirika wa maendeleo na wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi katika kuimarisha Muungano wetu na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi nchini kwa maendeleo endelevu ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya shukrani hizo kwa washirika wa maendeleo, ninaomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis Chilo, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nitumie fursa hii kuwashukuru wasaidizi wangu katika utendaji kazi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wakiongozwa na Mhandishi Cyprian John Luhemeja – Katibu Mkuu; Bwana Abdallah Hassan Mitawi – Naibu Katibu Mkuu (Muungano); na Bibi Christina Solomon Mndeme – Naibu Katibu Mkuu (Mazingira); Dkt. Immaculate Sware Semesi – Mkurugenzi Mkuu wa *NEMC*; Profesa Eliakimu Zahabu, Kaimu Mtendaji Mkuu wa *NCMC;* Wakuu wa Idara na Vitengo na wafanyakazi wote kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, mwanzoni mwa mwezi Aprili, 2025, Mhandisi Mwanasha Rajab Tumbo aliteuliwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya *NEMC*. Tunampongeza Mhandisi Mwanasha na tunamtakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yake, pamoja na wajumbe wa bodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu mahususi ninaomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kuendelea kuniamini kuwatumikia kwenye nafasi ya Ubunge pamoja na kunivumilia katika kipindi chote ambacho ninakuwa nje ya Jimbo nikitekeleza majukumu mengine ya Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nimetaarifiwa kuwa hivi sasa wanaendelea kunifuatilia mubashara katika tukio hili la uwasilishaji wa bajeti kutokea kule jimboni. Hivyo, ninawashukuru sana kwa upendo mkubwa kwangu, nami ninawaahidi nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa na Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini sio kwa umuhimu, ninapenda kuishukuru familia yangu pendwa nikianza na mke wangu mpenzi Thania Ali Abdalah na watoto wetu, Riziki Hamad Masauni, Asha Hamad Masauni na Bareek Hamad Masauni kwa upendo wao unaonipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu vema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 19,946,399,000.00 kwa ajili ya matumizi ya Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na shilingi 61,917,791,000. 00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Fungu 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya kiasi kinachoombwa kwa Fungu 26, shilingi 1,066,899,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 18,879,500,000.00 ni matumizi mengineyo. Maombi ya fedha kwa Fungu 31 yanajumuisha Matumizi ya Kawaida shilingi 28,858,213,000.00, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 10,907,597,000.00 ni Mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(NEMC)* na shilingi 17,950,616,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha shilingi 4,602,000,000.00 fedha za ndani na shilingi 28,457,578,000.00 ikiwa ni fedha za nje.

**25 APRILI, 2025**

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Ofisi ambayo ni *www.vpo.go.tz.*

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS KUHUSU MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAPINGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025 NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**A. UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, baada ya Bunge lako Tukufu kupokea mawasilisho ya taarifa kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge za Utawala, Katiba na Sheria pamoja na Maji na Mazingira, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili taarifa kuhusu utekelezaji wa mpango na bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2024/25. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/26.

**2.** ***Mheshimiwa Spika***, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijalia uhai na afya njema ya kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha taarifa kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2024/25 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2025/26.

**Salamu za Pongezi**

**3.** ***Mheshimiwa* Spika,** napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu, kwa uongozi wake mahiri na wa kipekee katika kuleta mageuzi makubwa ya kimaendeleo kwa nchi. Hakika, katika kipindi cha miaka minne (04) ya uongozi wake, tumeshuhudia mafanikio ya mfano katika nyanja za kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, katika uongozi wake, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika nyanja zote. Kipekee,

napenda kumshukuru Rais kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**4.** ***Mheshimiwa* Spika,** napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kutekeleza jukumu la kikatiba kuwa msaidizi mkuu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu mambo yote ya Jamhuri ya Muungano pamoja na kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira nchini. Aidha, uongozi wake mahiri umeleta mafanikio ya kujivunia kwa Ofisi hii.

**5.** ***Mheshimiwa* Spika,** pia, natoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa **Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuleta mafanikio ya kiuchumi Zanzibar pamoja na kuimarisha mshikamano na ushirikiano baina ya pande mbili za Muungano.

**6.** ***Mheshimiwa* Spika,** nitumie fursa hii pia kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa **Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa hotuba yake inayotoa mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa kipindi cha mwaka 2025/26. Vilevile, ninampongeza kwa uongozi wake thabiti katika kusimamia shughuli za Serikali ndani na nje ya Bunge lako Tukufu.

**7.** ***Mheshimiwa* Spika,** vilevile, napenda kumshukuru Mheshimiwa **Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.)**, Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, kwa kuendelea kumsaidia Waziri Mkuu katika kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Aidha, nampongeza kwa uongozi wake makini na juhudi za kipekee katika kusimamia vema sekta ya nishati.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kwa namna ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa **Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na **Dkt. Hussen Ali Mwinyi**, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

kwa kuchaguliwa kuwa wagombea wa CCM katika nafasi za Urais kwenye Uchaguzi Mkuu ujao utakaofanyika Oktoba, 2025.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii pia kumpongeza sana Mheshimiwa **Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi**, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Balozi Dkt. Nchimbi ni mwanasiasa mzoefu mwenye uwezo mkubwa wa kiuongozi ndani ya Chama cha Mapinduzi, Serikali, na jumuiya za kimataifa.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwapongeza wajumbe wote wa Mkutano Mkuu wa CCM ambao leo wamewakilishwa vema hapa bungeni na baadhi ya Wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa maamuzi yao sahihi ya kuwapitishwa kwa nguvu moja Viongozi wetu wanao tarajiwa kupeperusha bendera ya CCM katika nafasi za juu za uongozi katika nchi yetu kupitia Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika mwezi Oktoba,2025.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuchaguliwa kwao ni kielelezo cha ukomavu na imani kubwa waliyonayo wana CCM wote kwa viongozi hawa kutokana na uongozi wao makini na imara unaozingatia maslahi ya wananchi wote. Nitumie nafasi hii kuwaomba Watanzania wote kuendelea kuwaunga mkono kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** nimpongeze Mheshimiwa **Steven Masatu Wasira** kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Bara. Mheshimiwa Wasira ni kiongozi na mwanasiasa mkongwe, ambaye mchango wake unaendelea kuhitajika katika kuimarisha umoja na mshikamano wa Taifa letu.

**13.** ***Mheshimiwa*** **Spika**, nawashukuru na kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote kwa ujumla waliotangulia kutoa hoja zao hapa Bungeni, ambazo zimetoa dira na mwelekeo wa utekelezaji wa shughuli za Serikali kwa mwaka 2025/26. Vilevile, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wote kwa kazi kubwa wanayoifanya na kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kusimamia masuala ya Muungano na Mazingira nchini.

**14.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutoa shukrani na pongezi zangu za dhati kwako wewe binafsi Mheshimiwa **Dkt.Tulia Ackson (Mb.)**, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi na uadilifu mkubwa. Hakika katika kipindi cha uongozi wako tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuisimamia na kuishauri Serikali. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.)**, Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri anayoifanya. Ninawapongeza pia **Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama (Mb.) na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.)** Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu kwa kukusaidia kuliongoza Bunge letu kwa weledi na uadilifu.

**15.** ***Mheshimiwa Spika***, ninawashukuru watangulizi wangu katika awamu ya sita, Mheshimiwa **Dkt. Selemani Saidi Jafo (Mb.),** Waziri wa Viwanda na Biashara na Mheshimiwa **Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji (Mb.),** Waziri wa Mifugo na Uvuvi kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi chote walichohudumu katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Vilevile, napenda kutoa shukrani kwa Waheshimiwa Mawaziri wote na Wabunge kwa ushirikiano mzuri wanaoutoa katika kutekeleza majukumu yangu. Aidha, ninawaahidi kuendelea kuwapa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao.

**16.** ***Mheshimiwa* Spika,** napenda kutoa shukrani na pongezi kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Mheshimiwa **Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.),** na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira, Mheshimiwa **Jackson Gedion Kiswaga (Mb.),** pamoja na Makamu Wenyeviti na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati hizo kwa kupokea, kujadili, na kupitisha Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2024/25 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais kwa mwaka 2025/26.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia kuwashukuru Mama zetu, Mama Fatma Karume, Mke wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Hayati Abeid Amani Karume kwa kukubali mwaliko wetu na kushiriki nasi leo hapa kwenye tukio hili muhimu pamoja na Mama

Maria Nyerere, Mke wa Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa kukubali mwaliko wetu kuwa pamoja nasi leo. Aidha, tunawashukuru sana Mama zetu hawa kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuwatia nguvu Marais wetu walioongoza mapambano ya ukombozi wa nchi yetu pamoja na kuasisi Muungano wetu ambao leo tunajivunia. Mwenyezi Mungu azidi kuwapa afya njema na umri mrefu wazee wetu hawa.

**Salamu za Pole**

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutumia fursa hii kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na mpendwa wetu **Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteulewa wa Shirika la Afya Duniani ukanda wa Afrika. Tunaendelea kumuombea pumziko la milele.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile tarehe 20 Februari 2025, nchi ilimpoteza **Bi. Sifael Mushi**, ambaye ni miongoni mwa walioshiriki katika tukio la kuchanganya udongo wa iliyokuwa Tanganyika na Zanzibar tarehe 26 Aprili, 1965 wakati wa sherehe za kutimiza mwaka mmoja wa Muungano. Bi. Sifael Mushi atakumbukwa daima kwenye historia ya Muungano wetu.

**20.** ***Mheshimiwa* Spika,** baada ya salamu hizo na maelezo hayo ya utangulizi, sasa ninaomba kutoa taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2024/25 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2025/26.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2024/25

### Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mwaka 2024/25

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais kibajeti ina Mafungu mawili ambayo ni Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**Fungu 26:**

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, jumla ya Shilingi 16,969,208,000.00 ziliidhinishwa kwa ajili ya Fungu 26. Kati ya fedha hizo, Shilingi 15,980,000,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na Shilingi 989,208,000.00 ni kwa ajili ya Mishahara.

**Fungu 31:**

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Fungu 31, jumla ya Shilingi 45,718,554,000.00 ziliidhinishwa. Kati ya fedha hizo Shilingi 23,810,713,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi 21,907,841,000.00 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inajumuisha Shilingi 3,899,034,000.00 kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Shilingi 5,813,516,000.00 kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Shilingi 14,098,163,000.00 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, Bajeti ya Miradi ya Maendeleo inajumuisha Shilingi 3,602,000,000.00 fedha za ndani na Shilingi 18,305,841,000.00 fedha za nje.

**Fedha zilizopokelewa na kutumika hadi Machi, 2025**

**Fungu 26**

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya Shilingi 12,642,445,000.00 fedha za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Fungu 26 sawa na asilimia 75 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi 12,110,000,000.00 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, sawa na asilimia 76 na Shilingi 532,445,000.00 ni kwa ajili ya mishahara sawa na asilimia 54 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, katika kipindi hicho jumla ya Shilingi 12,498,163,818.58 zilitumika sawa na asilimia 99 ya fedha zilizopokelewa.

**Fungu 31**

**25.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi, 2025, Fungu 31 lilipokea jumla ya Shilingi 17,768,095,508.11 fedha za Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 75 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya kiasi kilichopokelewa, Shilingi 2,790,546,090.97 ni mishahara ya Watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais sawa na asilimia 72 ya bajeti iliyoidhinishwa, Shilingi 4,138,830,915.56 ni Mishahara ya Watumishi wa NEMC sawa na asilimia 71 ya bajeti iliyoidhinishwa, na Shilingi 10,838,718,501.58 ni Matumizi Mengineyo sawa na asilimia 77 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi cha Matumizi ya Kawaida kilichopokelewa, Shilingi 16,827,481,320.63 zilitumika sawa na asilimia 95.

**26.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo jumla ya Shilingi 11,719,488,299.10 zilipokelewa sawa na asilimia 53 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya kiasi hicho fedha za ndani ni Shilingi 722,188,299.10 na fedha za nje ni Shilingi 10,997,300,000.00. Aidha, katika kipindi hicho, Shilingi 7,748,358,299.10 zilitumika ambapo Shilingi 722,188,299.10 ni fedha za ndani sawa na asilimia 100 na Shilingi 7,026,170,000.00 ni fedha za nje sawa na asilimia 64.

**27.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 47(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Taifa wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Sera ya Taifa ya uchumi wa Buluu ya mwaka 2024; Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika (2063); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030); Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032); na Miongozo na Maelekezo mbalimbali yanayotolewa na Viongozi Wakuu.

**KAZI ZILIZOTEKELEZWA KATIKA KIPINDI CHA JULAI, 2024 HADI MACHI, 2025**

**1) MASUALA YA MUUNGANO**

**28.** ***Mheshimiwa Spika***, Mtakubaliana nami kuwa, amani, umoja, ushirikiano na kuheshimiana baina ya pande zote mbili za Muungano ni matunda ya Muungano wetu adhimu. Mwaka huu Muungano unatimiza miaka 61 tangu kuasisiwa kwake ambayo ni zaidi ya nusu karne na ili kuendelea kuulinda, kuudumisha na kuimarisha Muungano wetu, hatuna budi kukumbuka tukio hili muhimu na kutathmini mafanikio makubwa yaliyopatikana kisiasa, kiuchumi na kijamii.

**29.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuratibu masuala ya Muungano kwa mwaka 2024/25, Ofisi ya Makamu wa Rais ilipanga na kutekeleza yafuatayo:

**a) Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano**

**30.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Makamu wa Rais katika kipindi cha mwaka 2024/25, imeratibu vikao vitatu (3) vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ vilivyojadili hoja nne (4) za Muungano. Vikao hivyo ni: Kikao cha Makatibu Wakuu wa SJMT na SMZ kilifanyika Ikulu, Dar es Salaam tarehe 25 Machi, 2025; Kikao cha Mawaziri wa SJMT na SMZ kilifanyika Ikulu, Dar es Salaam tarehe 25 Machi, 2025; na Kikao cha Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano kilifanyika Ikulu, Dar es Salaam tarehe 4 Aprili, 2025. Vikao hivyo viliandaliwa na Sekretarieti ya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ iliyofanya vikao vyake tarehe 27 Agosti, 2024 na tarehe 21 Februari, 2025.

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali zote mbili zina nia ya dhati na thabiti katika kuhakikisha kuwa, hoja za Muungano zilizopo kwa sasa na zitakazojitokeza zinashughulikiwa na kupatiwa ufumbuzi.



*Mhe. Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akiongoza Kikao cha 15 cha Kamati ya Pamoja ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ) ya kushughulikia Masuala ya Muungano kilichofanyika katika Ukumbi wa Jakaya Kikwete, Ikulu Jijini Dar es Salaam tarehe 04 Aprili, 2025.*

**b) Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu Muungano**

**32.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa elimu kwa umma inatolewa kwa ufasaha, Ofisi imeandaa kipindi mahsusi kinachorushwa katika Runinga na Redio kijulikanacho kama "***Hii ni Jamhuri ya Muungano ya Tanzania"*** kwa lengo la kuelimisha umma kuhusu Muungano. Kipindi hiki kinarushwa TBC na ZBC na kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Julai, 2024. Maudhui yanayorushwa yanahusu: Misingi ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; Matukio muhimu kuelekea Muungano; Wasifu wa Viongozi Wakuu waliohudumu katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Majukumu ya Taasisi za Muungano. Hadi sasa jumla ya Vipindi 64 vya Redio na Runinga vimeandaliwa na kurushwa.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, elimu ya Muungano imeendelea kutolewa kwa umma kupitia maonesho ya Kitaifa ikiwemo Siku ya Wakulima (Nanenane) na Sherehe za Maadhimisho ya Mapinduzi ya Zanzibar. Aidha, elimu ya

Muungano ilitolewa kwa makundi mbalimbali ikiwemo Waheshimiwa Wabunge.

**c) Maadhimisho ya Miaka 61 ya Muungano**

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka huu 2025, Maadhimisho yanafanyika katika ngazi ya Mikoa, Tanzania Bara na Zanzibar. Matukio mbalimbali yanaendelea kufanyika ikiwemo makongamano/midahalo ya Muungano katika ngazi ya Mikoa na Wilaya na hivyo elimu ya Muungano inatolewa kwa upana wake. Kauli Mbiu ya Mwaka huu ni "***Miaka 61 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania: Muungano Wetu ni Dhamana, Heshima na Tunu ya Taifa: Shiriki Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025".*** Aidha, Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza Mpango Kabambe wa Elimu ya Muungano kwa Umma ambapo Viongozi mbalimbali wanashiriki katika vipindi kuhusu Muungano vinavyorushwa katika runinga, redio na mitandao ya kijamii.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kurejesha Ligi ya Muungano, napenda kutoa taarifa kuwa mashindano hayo yameanza tarehe 24 Aprili, 2025 na fainali itafanyika tarehe 01 Mei, 2025. Mashindano hayo yanashirikisha Timu nane (8), nne (04) kutoka Tanzania Bara na nne (04) kutoka Zanzibar na yanafanyika katika Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

**d) Kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano (MAKAVAZI ya Muungano)**

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi hiki, Ofisi inaendelea na maandalizi ya uanzishwaji wa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano (**MAKAVAZI ya Muungano**) kitakachokuwa katika Jengo la OMR – Mtumba, Dodoma**.** Kazi zilizofanyika zinajumuisha: Kikao cha wataalamu na kuandaa Mpango Kazi; kuandaa michoro na mgawanyo wa vyumba na kuidhinishwa na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka na Idara ya Makumbusho ya Taifa kwa mujibu wa Sheria; kukusanya Nyaraka zinazohusu masuala ya Muungano ambazo ni Vitabu, Magazeti, picha, Hati (Instruments), Video, sauti na maandiko (Thesis) kutoka katika

Shirika la Utangazji la Taifa (TBC), Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali, Shirika la Magazeti, Makumbusho ya Taifa la Tanzania, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Uhuru Publication na Habari Maelezo.

**e) Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii**

**i. Gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuratibu gawio kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kila mwaka ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2025 jumla ya shilingi bilioni 49.2 zimepokelewa Zanzibar. Fedha hizi zinajumuisha shilingi bilioni 14.00 ikiwa ni makato ya mishahara ya watumishi wa Zanzibar wanaofanya kazi Tanzania Bara (PAYE); shilingi bilioni 21.7 gawio la misaada na mikopo nafuu ya kibajeti kutoka nje *(Government Budget Support - GBS)*; na Shilingi bilioni 13.5 ikiwa ni gawio kutokana na faida ya Benki Kuu.

**ii. Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Zanzibar**

**38.** ***Mheshimiwa Spika;*** Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa miradi ya kipaumbele na ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa kwa fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo kwa Majimbo 50 ya Zanzibar, ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2025 jumla ya shilingi bilioni 2 zimepelekwa Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Miradi inayotekelezwa ni pamoja na miradi ya sekta za elimu, afya, maji, miundombinu na nishati. Aidha, kutokana na changamoto za sheria ya kusimamia fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI imeanza mchakato wa mapitio ya sheria hiyo ili kuboresha usimamizi na utekelezaji wa miradi inayotekelezwa na fedha za Mfuko wa Jimbo.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, tarehe 28 Februari, 2025, Ofisi ilitoa semina kwa Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Zanzibar kwa lengo la

kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu usimamizi na utekelezaji wa miradi inayotekelezwa kwa Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo. Katika semina hiyo Waheshimiwa Wabunge walipata fursa ya kujengewa uelewa kuhusu majukumu ya Taasisi za Muungano. Napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Ofisi itaendelea kutoa Semina kuhusu masuala mbalimbali ya Muungano mara kwa mara ili kujenga uelewa mpana wa masuala ya Muungano.



*Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kutoka Zanzibar wakishiriki Semina Kuhusu Usimamizi wa Fedha za Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo na Taasisi za Muungano iliyofanyika Zanzibar, tarehe 28 Februari, 2025.*

**f) Miradi na Programu za Maendeleo zinazotekelezwa pande mbili za Muungano**

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, miradi na programu mbalimbali zimeendelea kutekelezwa pande mbili za Muungano kwa lengo la kuboresha ustawi wa kiuchumi na kijamii kwa wananchi ikiwemo: Ujenzi wa Barabara za Mkoani - Chake Chake, Tunguu – Makunduchi; Ujenzi wa Vituo vya Afya Tanzania Bara na Zanzibar ikiwemo Kituo cha afya Kiuyu Minungwini, Kituo cha Afya Kizimkazi na Hospitali ya Rufaa Binguni; Programu ya Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP); Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki (BEVAC); na Miradi ya ujenzi wa

nyumba za Polisi ikiwemo Pemba, Mfikiwa, Finya Kaskazini na Mazizini, Unguja.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** miradi na programu nyingine ni pamoja na: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tanzania Social Action Fund - TASAF III; Miradi ya Mazingira (Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame Nchini (LDSF), Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini (EBARR), Ujenzi wa Kuta kati Ufukwe wa Sipwese, Pemba, Kujenga Uhimilivu wa Jamii na Mifumo – Ikolojia katika Maeneo ya Misitu ya Miombo na Maeneo Kame Zanzibar (IAP), Mradi wa kuwezesha Uhimilivu katika Visiwa Vidogo vidogo vya Bahari ya Hindi kwa Zanzibar n.k); Mradi wa Huduma za Maendeleo ya Biashara na Uongezaji wa Tija Katika Uzalishaji *(KAIZEN);* Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (TANIPAC); na Mradi wa Ufungaji wa mitambo ya sauti baina ya waongozaji ndege na marubani katika viwanja vya ndege 12 vya Tanzania Bara (10) na Zanzibar (2).

**g) Mfumo wa Kielektroniki wa Uratibu wa Taarifa za Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Uratibu wa Taarifa za Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano (UNUMMiS) ambao utasaidia kurahisisha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano kwa ajili ya kurahisisha utendaji kazi. Kwa sasa mfumo upo katika hatua za majaribio ili kuona kama unakidhi mahitaji ya watumiaji.

**h) Kuratibu ushirikiano katika masuala yasiyo ya Muungano kati ya SJMT na SMZ**

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hiki, Ofisi imeendelea kuhimiza umuhimu wa Wizara/Taasisi na Idara za SJMT na SMZ zisizo za Muungano kufanya vikao vya ushirikiano. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025 vikao tisa (9) vimefanyika. Lengo la vikao vya ushirikiano ni kubadilishana uzoefu, Sera, Sheria na utaalamu, katika utekelezaji wa mambo yasiyo ya Muungano.

## i) Kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano

**44.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano yanayosimamiwa na Wizara, Idara na Taasisi za Muungano. Tarehe 19 hadi 24 Februari, 2025 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ilifanya ziara Zanzibar na kutembelea Taasisi tano (5) za Muungano ambazo ni Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA); Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU); Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS); Tume ya Pamoja ya Fedha (JFC); na Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa. Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo. Aidha, Kamati ilielekeza Taasisi hizo kujenga Ofisi za kudumu Zanzibar.



*Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Mhe. Florent Kyombo akizungumza wakati wa ziara Kamati hiyo ya kutembelea Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar, tarehe 19 Februari, 2025.*

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi za Muungano zinaendelea kutekeleza majukumu yake pande zote mbili za Muungano ambapo katika kipindi hicho, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) ilidahili jumla ya wanafunzi 137,817 wa Shahada ya kwanza katika Vyuo 86 vya Elimu ya Juu nchini ambapo kati ya wanafunzi hao, 4,860 walidahiliwa katika Vyuo saba (7) vya Elimu ya Juu, Zanzibar; Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) iliwezesha ujenzi wa mabweni

mawili katika Chuo cha Ualimu cha Kiislam (*Pemba Islamic Teachers College*) uliogharimu kiasi cha shilingi milioni 300; na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) ilifunga seti ya mitambo 20 ya hali ya hewa na seti ya mitambo 15 ya hali ya hewa - kilimo inayojiendesha yenyewe katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na Zanzibar.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafanikio mengine ni Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) iliratibu ujenzi wa mfumo wa ubadilishanaji taarifa za ZanXchange unaosimamiwa na Mamlaka ya Utambulisho Zanzibar na kujenga uwezo wa vijana 80 kuhusu utengenezaji wa mifumo laini na Programu za TEHAMA kupitia Taasisi ya Python Tanzania katika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA).

## 2) HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** maendeleo endelevu ya Taifa letu yanachangiwa na ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na utunzaji wa Mazingira. Aidha, matumizi endelevu ya rasilimali zilizopo ni muhimu kwa maslahi ya vizazi vya sasa na vijavyo. Hivyo, suala la usimamizi na uhifadhi wa mazingira ni kipaumbele cha Serikali ya Awamu ya Sita katika kuleta maendeleo endelevu nchini. Pamoja na jitihada zinazoendelea kufanyika na mafanikio yaliyopatikana katika eneo hili, uharibifu wa mazingira nchini umeendelea kuathiri ustawi wa hali ya maisha na ukuaji wa uchumi nchini kutokana na changamoto zilizopo. Changamoto hizo ni pamoja na: upotevu wa makazi ya wanyamapori na bayoanuai; Ukataji ovyo wa miti na uharibifu wa misitu unaochangiwa na utegemezi wa matumizi ya nishati ya kuni na mkaa; Uchafuzi wa mazingira; Uharibifu wa vyanzo vya maji, mifumo ikolojia ya ukanda wa pwani na bahari; Kuenea kwa viumbe vamizi; na Athari za mabadiliko ya tabianchi. Kwa kiasi kikubwa uharibifu wa mazingira unatokana na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu zinazofanyika katika maeneo mbalimbali nchini.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini na mabadiliko ya tabianchi, Serikali imeendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Sera,

Sheria, Mikakati, Miongozo na Miradi mbalimbali ya hifadhi na usimamizi wa mazingira pamoja na kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Hifadhi ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Hivyo, kwa mwaka 2024/25, Ofisi kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetekeleza yafuatayo:-

**a) Kuratibu Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021 ambapo mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho ni pamoja na: Kujumuishwa kwa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi katika sera, mikakati pamoja na mipango na bajeti ya Serikali; na Kuimarika kwa uratibu na ushirikiano wa kisekta katika utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ikiwemo kuimarishwa kwa Vitengo vya Mazingira katika Wizara na Taasisi za Umma.

**b) Kuratibu Utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

**i) Kanuni na Miongozo ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imeandaa Kanuni nne (4) ambazo ni: Kanuni za Upatikanaji na Mgawanyo wa Faida za Rasilimali za Kijenetiki, Tangazo la Serikali Na. 387/2024; Kanuni za Dhamana ya Kuzingatia Masharti ya Mazingira, Tangazo la Serikali Na. 388/2024; Kanuni za Usimamizi Jumuishi wa Ukanda wa Pwani, Tangazo la Serikali Na. 384/2024; na Kanuni za Haki ya Fidia, Tangazo la Serikali Na. 385/2024. Aidha, Ofisi imeratibu na kukamilisha mapitio ya Kanuni tano (5) ili kuendana na mahitaji ya sasa ya hifadhi na usimamizi wa mazingira. Kanuni hizo ni: Kanuni za Ada na Tozo, Tangazo la Serikali Na. 588/2024; Kanuni za Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi, Tangazo la Serikali Na. 957/2024; Kanuni za Dhamana ya Kuzingatia Masharti ya Mazingira, Tangazo la Serikali Na. 189/2025; Kanuni za Usimamizi Jumuishi wa Ukanda wa Pwani,

Tangazo la Serikali Na. 188/2025; Kanuni za Upatikanaji na Mgawanyo wa Faida za Rasimali za Kijenetiki, Tangazo la Serikali Na. 187/2025.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi inaendelea kukamilisha Kanuni tatu (3) ambazo ni: Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Kemikali zinazodumu kwenye mazingira kwa muda mrefu; Katazo la Matumizi ya Kuni na Mkaa kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100 kwa siku; Kanuni za Usimamizi wa Maeneo Lindwa na Nyeti; na Kanuni ya Udhibiti wa Taka Ngumu ya mwaka 2009 ambayo imefanyiwa mapitio ili iendane na matakwa ya sasa.

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Ofisi imekamilisha Miongozo mitatu (3) na mikakati miwili (2) ya hifadhi ya Mazingira ambayo ni: Mwongozo wa Kuhuisha Masuala ya Urejeshwaji wa Mazingira Kwenye Sera, Sheria, Mipango, Mikakati na Programu; Mwongozo wa Kuhuisha Masuala ya Jinsia Kwenye Urejeshaji wa Mazingira; Mwongozo wa Taifa wa Tathmini ya Athari na Ukaguzi wa Mazingira kwa Wizara za Kisekta; Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Taka (2025-2030); na Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Bayoanuai (2025-2030).

**ii) Mapitio ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Serikali iliwasilisha muswada wa marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 uliopitishwa na Bunge tarehe 12 Februari, 2025 na kusainiwa tarehe 4 Machi, 2025 kuwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na.5 ya mwaka 2025. Masuala yaliyozingatiwa ni pamoja na: Kuanzishwa kwa Kamati ya Kitaifa ya Usimamizi wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi; Kuanzishwa kisheria Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni; na Kuongeza jukumu la usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi kwa vitengo vya mazingira kwa Wizara za Kisekta.

**Taarifa ya Hali ya Mazingira**

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imekamilisha Taarifa ya Nne ya Hali ya Mazingira Nchini kwa

mujibu wa matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Aidha, taarifa hiyo itawasilishwa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Sheria.

**iv) Utoaji wa Vibali vya Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK)**

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imetoa kibali kimoja (1) cha Tathmini ya Mazingira Kimkakati (TMK) kwa Mradi wa Mabasi Yaendayo Kasi katika Jiji la Dar es Salaam *(Transit Oriented Development (TOD) in Dar es Salaam City)*. Aidha, miradi sita (6) ya kimkakati iko katika hatua tofauti za taratibu za kupatiwa vibali vya TMK. Miradi hiyo ni pamoja na Uanzishwaji na Uendelezaji wa Vizimba vya Samaki Ziwa Victoria; Bonde la Mto Msimbazi; Kongani ya Viwanda Kibaha; Uchimbaji wa Madini ya Urani Mto Mkuju; Mpango Kabambe wa Mji wa Kibaha; na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi katika Wilaya ya Simanjiro.

**v) Mkutano Maalum wa Wadau wa Mazingira Kuhusu Mwenendo wa Hali ya Mazingira Nchini**

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu Mkutano Maalum wa Viongozi na Wataalam na Wadau wa Mazingira Kuhusu Mwenendo wa Hali ya Mazingira Nchini uliofanyika tarehe 9 - 10 Septemba, 2024, Dodoma, uliohudhuriwa na Washiriki 2,541. Lengo la Mkutano huo lilikuwa kujadili hali ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi nchini pamoja na ushiriki wa jamii na taasisi katika masuala ya Biashara ya Kaboni. Maazimio ya Mkutano huo yalijumuisha: Suala la hifadhi ya mazingira kupewa kipaumbele katika mipango na bajeti za wadau wote ikiwemo bajeti za Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia; Kuweka mazingira wezeshi yatakayohakikisha gharama nafuu na upatikanaji wa teknolojia ya nishati safi ya kupikia; Suala la Mazingira kuwa ajenda ya kudumu katika vikao vyote vya Mamlaka za Serikali za Mitaa; kurejesha Idara ya Mazingira katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; Kuimarisha usimamizi wa uchumi wa buluu; Kuhamasisha wadau wote kushiriki na kunufaika na fursa za biashara ya kaboni; na Kuboresha mbinu za utoaji elimu ya mazingira kwa umma.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe.Dkt. Philip Isdor Mpango akiwapongeza Wanafunzi wa Shule ya Msingi Mnadani ya Jijini Dodoma mara baada ya kuimba wimbo wa kuhamasisha utunzaji mazingira katika Mkutano Maalum wa Viongozi, Wataalamu na Wadau wa Mazingira kuhusu Mwenendo wa Hali ya Mazingira Nchini tarehe 09 Septemba, 2024.*

**c) Kuratibu Utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032)**

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira ambapo jumla ya maandiko dhana ya miradi kumi na sita (16) yameandaliwa. Aidha, maandiko dhana ya miradi sita (6) kati ya kumi na sita (16) yenye thamani ya shilingi bilioni 96.2 yamewasilishwa kwenye Sekretarieti za Mifuko ya Kimataifa na kupata idhini ya kuandaa maandiko kamili ya miradi. Miradi hiyo ni: Uhifadhi mazingira na kuongeza uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Bonde la Mto Wami na Ruvu; Hifadhi ya eneo la Ardhi-oevu ya Malagarasi-Moyowosi; Kuongeza uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi kwa jamii za wakulima na wafugaji; Matumizi endelevu ya ardhi na ustawi wa jamii katika maeneo kame na njia za uhamaji wa

mifugo; Kuwezesha Jamii zinazozunguka hifadhi za Serengeti na Ngorongoro kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia mifumo ya kiikolojia; na Kuhimili mabadiliko ya Tabianchi katika jamii zinazozunguka misitu ya Miombo katika mikoa ya Tabora, Katavi na Rukwa kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

**58.** ***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Mazingira katika Wizara za Kisekta umehusisha shughuli zifuatazo: kufanya Tathmini ya Matumizi ya Fedha za Umma *(Public Expenditure Review - PER)* katika masuala ya lishe, jinsia na mazingira; Kuanzisha mchakato wa uanzishwaji wa Kitengo cha Fedha za Mabadiliko ya Tabianchi katika Wizara ya Fedha kwa lengo la kuimarisha upatikanaji na uratibu wa fedha za mabadiliko ya tabianchi kwa vyanzo vya ndani na nje ya nchi; na Kuandaliwa kwa Mpango-Kazi wa Mazingira wa Sekta ya Uchukuzi (2025-2030).

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuendelea kuwahimiza wadau wote kuhakikisha wanajumuisha utekelezaji wa Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira 2022 – 2032 katika sera, mikakati, mipango na bajeti zao.

**d) Kuimarisha uratibu na utekelezaji wa masuala ya Hifadhi ya Usimamizi wa Mazingira katika Wizara za kisekta, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa**

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imeteua Maafisa Viungo 28 kwa lengo la kuimarisha uratibu, msukumo na ufuatiliaji wa shughuli za hifadhi na usimamizi wa mazingira kwenye Wizara, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hatua hii imeimarisha ufuatiliaji na usimamizi wa mazingira katika Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Baadhi ya mafanikio muhimu ni pamoja na: Kuongezeka kwa uelewa kuhusu uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira; kubainishwa kwa fursa na changamoto za uhifadhi wa mazingira katika mikoa na kuweka mikakati ya kunufaika na fursa hizo na kukabiliana na changamoto zilizopo; kuhamasisha ushiriki katika biashara ya

kaboni ambapo viongozi wa Sekretarieti za Mikoa 26, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wakuu wa Taasisi za Umma 284 walijengewa uwezo kuhusu Biashara ya Kaboni. Aidha, baadhi ya Halmashauri zimeanza kutenga maeneo ya Misitu na taratibu nyingine za usajili zinaendelea kwa ajili ya kuingizwa katika Biashara ya Kaboni zikiwemo: Halmashauri za Wilaya za Busekelo (Msitu wa hekta 684.8); Pangani (Msitu wa Mikoko wenye Hekta 3,750); Sumbawanga (Msitu wa Lyampa lya Mfipa wenye Hekta 8,870); na Iringa (misitu yenye jumla ya Hekta 20,577.23).

### e) Udhibiti wa taka

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kudhibiti usimamizi wa taka na kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo ya majiji na miji, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi, imeendelea kuboresha mifumo ya usafi wa mazingira ikiwemo ujenzi wa vituo vya kukusanya, kuhifadhi na kurejeleza taka ngumu na uboreshaji wa mifumo ya majitaka katika miji na majiji. Mathalani, Jiji la Dar es Salaam lina jumla ya viwanda/vituo vya urejelezaji 44 vya taka aina ya plastiki, chuma chakavu, mafuta machafu, tairi chakavu, taka za kielektroniki na taka ozo ambapo jumla ya tani 12,926 za taka zimechakatwa. Uwepo wa mfumo huu umepunguza kiasi cha taka kinachopelekwa dampo; na kutoa fursa za ajira na kipato kwa makampuni na vikundi vya ukusanyaji wa taka.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** bado hali ya usafi wa miji na majiji yetu siyo ya kuridhisha. Kupitia Bunge lako Tukufu, nazielekeza Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia udhibiti wa taka na kuimarisha usafi wa mazingira katika maeneo yao. Aidha, natoa rai kwa wananchi na wadau wote kuendeleza utamaduni wa kufanya usafi katika maeneo yao.

### f) Nishati Safi ya Kupikia

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Makamu wa Rais imeendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (20242034). Ofisi imefanya ufuatiliaji wa utekelezaji

wa matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa taasisi za umma na binafsi, ambapo jumla ya Taasisi 903 zimeanza kutumia nishati safi ya kupikia. Taasisi hizo ni pamoja na: Shule za Msingi na Sekondari; Vyuo vya Kati na Ualimu; Magereza; Jeshi la Ulinzi; Jeshi la Kujenga Taifa; Sekta Binafsi na Taasisi za Dini.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Ofisi imefanya uhamasishaji kwa Taasisi za kifedha kuwezesha wadau wa nishati safi ya kupikia ambapo kwa mwaka 2025, Benki ya NMB imetenga jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 100kwa ajili ya utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa makampuni ya usambazaji wa gesi pamoja na wajasiriamali wadogo wakiwemo Baba na Mama lishe ili waweze kuweka miundombinu ya nishati safi ya kupikia katika maeneo yao ya biashara.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (NCMC), kwa kushirikiana na Shirika la Chakula Duniani (WFP) imeanzisha miradi ya mfano ya biashara ya kaboni kwa shule za msingi na sekondari zinazotumia nishati safi ya kupikia ya majiko ya umeme (pressure cookers) kwa mikoa ya Kigoma, Tabora na Dar es Salaam kama maeneo ya majaribio. Aidha, miradi hiyo inatarajiwa kutekelezwa katika maeneo mengine nchini na hivyo kuwezesha taasisi hizo kupata mapato yatokanayo na biashara hiyo.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu naomba kuzielekeza Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kusimamia utekelezaji wa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa Taasisi za Umma na Binafsi zinazolisha watu zaidi ya 100 sambamba na kuendelea kutoa elimu kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa jamii.

## g) Elimu kwa Umma Kuhusu Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imeendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi na usimamizi wa mazingira kupitia vyombo vya habari,

makongamano, semina, warsha na maonesho ya kitaifa na kimataifa. Aidha, Ofisi imeanzisha kipindi maalumu kiitwacho ***"Mazingira Yetu na Tanzania Ijayo"*** ambapo jumla ya vipindi 67 ikiwemo vipindi 36 vya runinga vilirushwa kupitia TBC1, Channel Ten na Azam TV; na Vipindi 31 vimeandaliwa na kurushwa kupitia Redio ya TBC Taifa. Vipindi hivyo vilihusu Matumizi ya nishati Safi ya kupikia, Fursa za Uwekezaji katika Sekta ya Mazingira, Biashara ya Kaboni, Kampeni ya Upandaji Miti, Maadhimisho ya Siku ya Hifadhi ya Tabaka la Ozoni, Uhamasishaji wa Usafi wa Mazingira; na Udhibiti wa Taka Ngumu. Aidha, ili kuhakikisha kuwa uhifadhi wa mazingira unakuwa endelevu, Ofisi ya Makamu wa Rais imepanga kutoa elimu ya mazingira kwa umma kuanzia ngazi za chini hususan watoto ili kuwajengea utamaduni wa usafi na uhifadhi wa mazingira.

**h) Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani**

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu uhifadhi na usimamizi wa mazingira, Ofisi imepanga kufanya maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Mazingira Duniani yatakayofanyika tarehe 05 Juni, 2025. Shughuli zilizopangwa kufanyika kuelekea kilele cha maadhimisho hayo ni pamoja na: Kongamano la Viongozi wa Dini; Usafi wa Mazingira nchi nzima; Uzinduzi wa Jukwaa Maalumu la Wadau wa Mazingira kwa ajili ya kujadili kwa pamoja changamoto na fursa katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira kwa Tanzania Bara na Zanzibar; Tamasha la Vijana Kuhusu Mazingira; na Tamasha la Wadau wa Nishati Safi ya Kupikia. Vilevile, maadhimisho haya yatashirikisha ipasavyo vyombo vya habari na mitandao ya kijamii ili kuhakikisha elimu ya hifadhi ya mazingira itakayotolewa wakati wa maadhimisho hayo inawafikia wananchi wengi.

**i) Kampeni ya Kitaifa ya Upandaji miti**

***69. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuhamasisha Kampeni ya upandaji na utunzaji miti ambayo inalenga kila Halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka ambapo takribani miti 224,795,501 ilipandwa katika Halmashauri zote nchini, sawa na asilimia 81 ya lengo la miti 276,000,000.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mkakati huu wa kitaifa, Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikihamasisha wadau mbalimbali kujihusisha na suala la kukijanisha Jiji la Dodoma. Kwa mfano Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imekuwa ikisaidia juhudi za Serikali, katika kukabiliana na Athari za mabadiliko ya Tabianchi, kupitia mradi wa Jawabu la Kijani (*Green Solutions Project*), unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), katika Jiji la Dodoma. Mradi huu umejikita katika upandaji wa miti katika eneo la pembezoni mwa barabara (*Green belt roads*) ikiwa ni pamoja na uchimbaji wa visima vya maji kwa ajili ya ustawi wa miti inayopandwa. Mwamko huo wa upandaji miti barabarani, pia umeungwa mkono na JKT Makutupora, ambapo tayari sura ya kijani katika eneo hilo imeanza kujitokeza.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa wananchi, taasisi mbalimbali na sekta binafsi kuendelea kupanda na kuitunza miti hasa katika kipindi hiki ambacho mvua za masika zinaendelea kunyesha. Vilevile, nizikumbushe Halmashauri zote kuendelea kusimamia na kuhamasisha zoezi la upandaji miti. Aidha, katika kuendeleza kampeni ya kukijanisha Dodoma jumla ya miti 1,238,628 ilipandwa katika Mkoa wa Dodoma na bustani za kijani kumi na mbili (12) zimeanzishwa.

**72.** ***Mheshimiwa Spika**,* pamoja na hili naendelea kusisitiza umuhimu wa upandaji wa miti katika Barabara zetu pamoja na uanzishwaji na uendelezaji wa bustani za Kijani katika Jiji letu la Dodoma, ili kupunguza hali ya ukame. Bustani hizi pamoja na kuwa na umuhimu kwa upande wa mazingira zitasaidia ajira kwa vijana wetu na pia kusaidia kukuza utalii wa ndani ya nchi. Hivyo, natoa rai kwa wadau mbalimbali wa maendeleo kuunga mkono jitihada hizi. Vilevile, nizikumbushe Taasisi husika kutoa elimu kwa wananchi kuhusu aina ya miti ya kupanda katika maeneo mbalimbali na kutoa ushauri wa namna ya kupanda miti na maua kwenye maeneo ya miji, ikiwa ni pamoja na maeneo kame na ya milima.

## j) Kuratibu na Kusimamia Biashara ya Kaboni nchini

**73.** ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Februari 2025, Bunge lako Tukufu lilipitisha Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 ambayo yalijumuisha kuanzishwa kisheria Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni (*National Carbon Monitoring Centre* – NCMC). Kuanzishwa kwa Kituo hiki ni hatua ya kimkakati itakayowezesha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kunufaika zaidi na biashara ya Kaboni na hivyo kuongeza pato la taifa.

**74.** ***Mheshimiwa Spika***, Ofisi kwa kushirikiana na NCMC, imeendelea kuratibu na kuimarisha usimamizi wa Biashara ya Kaboni nchini ambapo jumla ya Miradi 73 ya Biashara ya Kaboni imesajiliwa na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Biashara ya kaboni imeanza kuleta manufaa kiasi katika baadhi ya maeneo nchini ambapo kiasi cha Shilingi bilioni 45 zimelipwa na kunufaisha wananchi katika Halmashauri kumi (10) nchini kama gawio la mauzo ya viwango vya kaboni.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Ofisi iliratibu vikao mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Kikao cha kuwajengea uwezo Makatibu Wakuu 21 kuhusu biashara ya kaboni kilichofanyika mwezi Agosti, 2024 Dodoma; Kikao na Wawakilishi wa Makampuni 27 yanayojihusisha na biashara ya Kaboni; Vikao vya kimkakati vya kuimarisha usimamizi wa biashara ya Kaboni baina ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Wizara ya Fedha; Wizara ya Maliasili na Utalii; Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; na Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi Tanzania (TUCTA). Aidha, Ofisi iliratibu Mkutano wa Wakuu wa Taasisi na Mashirika ya Umma uliohusisha washiriki 850 uliolenga pamoja na mambo mengine kuibua fursa ya miradi ya kimkakati ya kitaifa ya biashara ya kaboni.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kuwa biashara ya kaboni inaendeshwa kwa uwazi na fursa zilizopo zinatumika ipasavyo na kuleta tija na manufaa kwa wananchi, Serikali imeunda Kamati ya Wataalamu iliyopewa majukumu ya kushauri

kuhusu mikakati madhubuti ya kuimarisha usimamizi wa biashara ya kaboni; na kubaini na kutoa mapendekezo ya kushughulikia changamoto zilizopo au zinazoweza kujitokeza katika biashara ya kaboni. Kamati hiyo inajumuisha wajumbe kutoka Ofisi ya Rais - TAMISEMI; Ofisi ya Makamu wa Rais; Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais – Zanzibar; Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; Wizara zenye dhamana ya: Fedha; Mambo ya Nje; Viwanda na Biashara; Mambo ya Ndani ya Nchi; Ardhi; Kilimo; Madini; Mifugo na Uvuvi; Nishati; Uchukuzi; na Maliasili na Utalii. Wajumbe wengine ni kutoka: Benki Kuu ya Tanzania; Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA); Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS); Chuo Kikuu cha Dodoma; Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana; Soko la Bidhaa (TMX); Wawakilishi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGOs); na Sekta Binafsi. Aidha, Kamati husika inatarajiwa kuwasilisha taarifa yake tarehe 09 Mei, 2025.

**78.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kubadilishana uzoefu kuhusu biashara ya kaboni, wataalam kutoka nchi ya Malawi walifanya ziara ya mafunzo nchini kwa lengo la kupata uzoefu kuhusu uratibu na usimamizi wa biashara ya kaboni. Aidha, Viongozi na wataalamu mbalimbali kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais na NCMC walishiriki ziara ya mafunzo kuhusu usimamizi wa biashara ya kaboni nchini Ghana na Korea ya Kusini. Vile vile, Wataalamu 167 kutoka Wizara na Taasisi za umma walijengewa uwezo kuhusu masuala ya biashara ya Kaboni.

**79.** ***Mheshimiwa Spika***, kutokana na ukweli kuwa Biashara ya Kaboni ni dhana ngeni kwa wananchi walio wengi, nitoe rai kwa umma kutumia ipasavyo Kituo cha Uratibu wa Kaboni nchini ili kupata ushauri wa kitaalamu na miongozo stahiki kuhusu biashara hiyo ambayo siyo tu inachangia ukuaji wa uchumi lakini pia uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, natoa rai kwa taasisi za umma na sekta binafsi zijumuishe masuala ya biashara ya kaboni katika miradi yake ya maendeleo.

**k) Ushiriki wa Nchi Katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi iliratibu na kushiriki katika mikutano mbalimbali ya Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kama ifuatavyo:-

**i) Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi**

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika jijini Baku, Azerbaijan tarehe 11 hadi 22 Novemba, 2024. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa **Dkt. Philip Isdor Mpango**, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akifungua Mkutano wa Nishati Safi ya Kupikia ulioandaliwa na Tanzania kwa kushirikiana na Umoja wa Afrika (AU) pamoja na Tume ya Nishati Afrika (AFREC) Pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) jijini Baku, Azerbaijan.*

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** makubaliano yaliyofikiwa katika Mkutano huo na yenye maslahi kwa Taifa ni pamoja na: Kuanza kufanya kazi kwa Mfuko wa Kushughulikia Upotevu na Hasara zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi; Kuwekwa kwa utaratibu wa wazi wa kusimamia miradi ya biashara ya Kaboni inayotekelezwa baina ya nchi na nchi pamoja na miradi ya upandaji miti kukubaliwa kusajiliwa katika biashara ya Kaboni; Kuongeza muda wa utekelezaji wa Mpango-kazi wa Lima kuhusu kuhuisha masuala ya Jinsia kwenye Mabadiliko ya Tabianchi kwa miaka 10 (2025-2035); na Nchi wanachama kuwasilisha Awamu ya Tatu ya Michango ya Taifa ya Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi (NDC. 3.0).

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika mkutano wa COP29 umekuwa na tija na mafanikio kwa Taifa ambapo pamoja na mambo mengine Tanzania imefanikiwa kupata ahadi ya Dola za Marekani milioni 782.2 sawa na takriban Shilingi trilioni 1.944 kwa ajili ya miradi ya hifadhi ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Katika kufuatilia ahadi zilizotolewa katika COP29, hadi Machi, 2025 kiasi cha Dola za Marekani Milioni 463.31 zipo katika hatua mbalimbali za upatikanaji kwa ajili ya kuwezesha kuanza kwa utekelezaji wa miradi.



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Philip Mpango akiteta na Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Duniani (GCA) Prof. Patrick Verkooijen, pembezoni mwa Mkutano wa 29 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi (COP-29) jijini Baku, Azerbaijan.*

**84.** ***Mheshimiwa Spika****,* Majadiliano katika Mkataba wa Umoja wa Mataifa huendeshwa kupitia makundi mbalimbali ya Watalamu likiwemo Kundi la Nchi za Afrika. Katika mwaka 2024/25 Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Nchi za Afrika ambapo Dkt. Richard Stanslaus Muyungi, Mjumbe Maalum na Mshauri wa Rais wa masuala ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi ndiye Mwenyekiti wa Kundi la Wataalamu wa Afrika (AGN). Tunampongeza sana Dkt. Muyungi kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa AGN. Aidha, mwenyekiti huyo ameanza kuetekeleza majukumu yake kuanzia tarehe 15 Machi 2025 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hii mara ya Kwanza kwa Jamhuri ya Muungano kuwa mwenyekiti wa kundi hili. Aidha, majukumu ya nafasi hiyo ya Uenyekiti ni pamoja na: Kuongoza Majadiliano ya Kitaalam katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa; Kuratibu maandalizi na kuwasilisha Msimamo wa nchi za Afrika katika Majadiliano ya Mikutano ya Kikanda na Kimataifa; Kusimamia Agenda ya Nishati safi ya Kupikia ikiwemo upatikanaji wa fedha za kutekeleza Programu ya Nishati Safi ya Kupikia

ambayo inaongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**ii) Mkutano wa 16 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bayoanuai**

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wa 16 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bayoanuai uliofanyika mjini Cali, Colombia tarehe 21 Oktoba hadi 01 Novemba, 2024. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maazimio ya Mkutano huo ni pamoja na: Kuanzishwa kwa Mfuko Maalumu wa Kusimamia Masuala ya Mgawanyo wa Faida zitokanazo na Rasilimali za Kijenetiki; Kuongeza ushirikiano na kujenga uelewa na ujuzi wa jamii juu ya athari za viumbe vamizi kwa bayoanuai na ikolojia; Kukamilisha na kuwasilisha Mkakati wa Taifa wa Kuhifadhi Bayoanuai; na Kuandaa Mpangokazi wa hatua za kujenga uwezo kwa Itifaki ya Cartagena, kwa kuzingatia na kutumia rasilimali zilizotengwa kwa ajili ya kusaidia utekelezaji wa Itifaki.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ushiriki wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano huo ulikuwa na tija ambapo ilitolewa ahadi ya Dola za Marekani milioni 2.13 sawa na takribani Shilingi bilioni 6.2 kwa ajili ya miradi ya kuhifadhi bayoanuai.

**iii) Mkutano wa 39 wa Nchi Wanachama wa Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 39 wa Nchi Wanachama wa Itifaki ya Montreal uliofanyika jijini Bangkok, Thailand kuanzia tarehe 27 Oktoba hadi 1 Novemba, 2024. Makubaliano ya Mkutano huo ni pamoja na: Nchi wanachama kuimarisha uwezo wa taasisi zinazosimamia utekelezaji wa Itifaki ya Montreal; Kukamilisha

uridhiaji wa Marekebisho ya Sheria na Mipango ya Utekelezaji wa Marekebisho ya Kigali kuhusu kupunguza uzalishaji na matumizi ya kemikali jamii ya Haidroflorokaboni; na Kuandaa maandiko ya miradi kuhusu uhaulishaji wa teknolojia mbadala. Katika kutekeleza maazimio ya Mkutano huo, Serikali kupitia OMR imeandaa andiko la mradi wa kujenga uwezo wa kitaifa kuhusu utekelezaji wa Itifaki ya Montreal ambalo limewasilishwa katika Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP) mwezi Februari, 2025 kwa ajili ya kupata fedha na kuanza utekelezaiji.

### iv) Mkutano wa 16 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (UNCCD)

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa Tanzania katika Mkutano wa 16 wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kupambana na Kuenea kwa Jangwa uliofanyika Riyadh, Saudi Arabia kuanzia tarehe 2 hadi 13 Disemba 2024. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maazimio yatokanayo na Mkutano huu ni pamoja na: Nchi Wanachama kuweka Mikakati maalumu ya kukabiliana na changamoto za kuenea kwa hali ya jangwa na ukame; na Kukamilisha Mipango Kazi ya Kitaifa kwa ajili ya kukabiliana na kuenea kwa jangwa na ukame. Katika utekelezaji wa maazimio hayo, Tanzania imeandaa Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na kuenea kwa hali ya jangwa na ukame.

### v) Mkutano wa Kumi na Moja wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi (COP 11)

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa nchi katika Mkutano wa Kumi na Moja wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Nairobi (COP 11) uliofanyika Madagascar kuanzia tarehe 20 - 22 Agosti, 2024. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji (Mb.), aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira). Katika Mkutano huo, Tanzania

ilichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Sekretarieti ya Mkataba kwa kipindi cha miaka miwili (2) na kuwa mwenyeji wa Mkutano wa 12 wa Nchi Wanachama wa Mkataba utakaofanyika mwaka 2026.

**vi) Mkutano wa 12 wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde La Ziwa Tanganyika**

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi iliratibu ushiriki wa nchi katika Mkutano wa Kumi na Mbili wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika uliofanyika tarehe 8-12 Disemba, 2024 Kinshasa, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis (Mb.), Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Maazimio yatokanayo na Mkutano huo ni pamoja na: Kukamilisha mchakato wa kuridhiwa kwa Itifaki ya Ufugaji wa Samaki chini ya Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Bonde la Ziwa Tanganyika; Kuendeleza utekelezaji wa Chata ya Masuala ya Uvuvi kwa kufunga shughuli za uvuvi katika Ziwa kwa Miezi Mitatu kila mwaka; na Kuanza mchakato wa kumpata Mkurugenzi Mtendaji wa Sekretarieti ya Mamlaka ya Bonde la Ziwa Tanganyika.

**l) Utekelezaji wa Miradi ya Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira**

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi iliratibu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kumi (10) kama ifuatavyo:

**i) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Fukwe ili kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi zitokanazo na ongezeko la kina cha Bahari**

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la Mradi huu ni kuzuia maji ya bahari kujaa na kuathiri maeneo ya makazi na kilimo katika fukwe za Sipwese (Pemba) na Mikindani (Mtwara). Mradi huu

unatekelezwa kwa fedha za ndani ambapo kwa kipindi cha mwaka 2024/25 kiasi cha shilingi milioni 293.8 kilipokelewa na kutumika ambapo utekelezaji wa mradi umefikia wastani wa asilimia 79.

**ii) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini – EBARR**

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imeendelea kutekeleza Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa Kutumia Mifumo Ikolojia Vijijini katika Halmashauri za Wilaya za Kaskazini A – Unguja, Kishapu, Mpwapwa, Mvomero na Simanjiro ambapo hadi mwezi Machi, 2025, kiasi cha shilingi milioni 820 zimepokelewa na kutumika kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi ikijumuisha: Ujenzi wa kisima kirefu na Mfereji Mkuu wa Skimu ya Umwagiliaji; ujenzi wa Ghala la Kuhifadhi Nafaka; na urejeshaji wa hekta 9,000 za ardhi iliyoharibika.

**iii) Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania**

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza shughuli za mradi kwa mwaka 2024/25, kiasi cha shilingi milioni 406.2 zimepokelewa na kutumika katika maeneo ya mradi katika Halmashauri za Mkalama, Nzega, Kondoa, Magu na Kaskazini-A.

**iv) Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai Tanzania**

**98.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2024/25, kiasi cha shilingi bilioni 6.2 kilipokelewa na kuetekeleza shughuli zilizopangwa katika Halmashauri za Iringa, Mbarali, Wanging'ombe, Mbeya, Tanganyika, Mpimbwe na Sumbawanga. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: kuanzisha vitalu 11 vya miche vyenye jumla ya miche 2,654,224; kuandaliwa kwa mipango ya usimamizi wa misitu yenye jumla ya hekta 50,848.64 kwa ajili ya kuwezesha kuingia katika biashara ya kaboni; na ujenzi wa majengo ya viwanda vidogo vya kuongeza thamani ya mazao ya alizeti, asali, maziwa na mpunga.

**v) Mradi wa Kuanzisha Bustani ya Kijani Katika Eneo la Swaswa Mnarani, Dodoma**

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa fedha 2024/25, Ofisi imeanza utekelezaji wa Mradi wa Kuboresha eneo la Bwawa la Swaswa jijini Dodoma. Mradi huu unalenga kuboresha ikolojia ya Bwawa la Swaswa, kuhimili athari za mazingira na kupendezesha jiji la Dodoma. Hadi kufikia Machi, 2025, fedha za ndani kiasi cha shilingi milioni 205.2 kilipokelewa. Katika kipindi hicho shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na usanifu wa kina kuhusu miundombinu ya Barabara, majengo, bwawa, viwanja vya michezo, na bustani umefanyika katika eneo la mradi.

**vi) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2025, kiasi cha shilingi milioni 230 kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi ambapo shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Kufanya mafunzo kwa Mawakala wa Forodha 103 waliopo katika mipaka ya Tunduma, Holili, Horohoro na Bandari ya Tanga kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa kemikali na vifaa vyenye kemikali zinazomong'onyoa tabaka la ozoni; Kufanya mafunzo kwa Mafundi mchundo 82 wa viyoyozi na majokofu wa Mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma kuhusu mbinu bora za kuhudumia vifaa husika; ununuzi wa vitambuzi vya gesi kwa ajili ya kuwezesha kutambua kemikali zinazodhibitiwa chini ya Itifaki Montreal; na Ununuzi wa mashine za kunasa na kurejeleza gesi chakavu za Majokofu na Viyoyozi.

**vii) Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma**

**101.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, Ofisi kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Shirika la Wakimbizi Duniani (UNHCR), Sekretarieti ya Mkoa wa Kigoma, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Wakala wa

Huduma za Misitu Tanzania (TFS) imeanza kutekeleza Mradi wa Kujenga Ustahimilivu wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi Mkoani Kigoma. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi *(Green Climate FundGCF)* kupitia Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP). Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (05) katika Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Kibondo na Kakonko. Lengo la mradi huu ni kuboresha mifumo ya kiikolojia itakayoongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma na hivyo kuchangia kuboresha mazingira. Hadi Machi, 2025, kiasi cha shilingi bilioni 1.5 kilipokelewa. Shughuli zilizoanza kutekelezwa zinajumuisha: Kufanya tathmini ya awali ya migogoro inayoweza kujitokeza katika utekelezaji wa Mradi *(Conflict sensitivity assessment)*; na Tathmini ya taarifa za awali za eneo la Mradi *(Baseline Assessment)*. Katika kipindi cha Machi hadi Juni, 2025, shughuli zilizopangwa kutekelezwa zinajumuisha: Kupanga matumizi ya ardhi kwa vijiji; Kuwezesha upandaji wa miti na uhifadhi wa misitu; Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji; na kujenga miundombinu ya kudhibiti mmomonyoko wa ardhi.

**viii) Mradi wa kuandaa Mkakati na Mpango Kazi wa Taifa wa Kuhifadhi Bayoanuai**

**102.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2024/25, Ofisi imetekeleza Mradi wa kuandaa Mkakati na Mpango-Kazi wa Taifa wa Kuhifadhi Bayoanuai (2025-2030). Lengo la mradi huu ni kuandaa Mpango-kazi wa Taifa utakaowezesha utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Hifadhi ya Bayoanuai. Hadi kufikia Machi, 2025, kiasi cha shilingi milioni 526.3 kilipokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi zilizopangwa.

**ix) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa Mazingira na Kuboresha Maisha ya Jamii za Wavuvi**

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Ofisi imetekeleza Mradi huu katika Halmashauri ya Mkinga, Tanga. Lengo la Mradi ni kuimarisha maisha ya jamii za Pwani kwa kuzingatia matumizi endelevu ya rasilimali za Bahari na uhifadhi

wa mazingira. Hadi kufikia Machi, 2025 kiasi cha Shilingi milioni 120 kimepokelewa na kutekeleza shughuli zilizopangwa ikijumuisha uandaaji wa Mpango wa Matumizi Endelevu ya Maeneo ya Bahari.

**Miradi Mingine Iliyotekelezwa**

i) **Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kutekeleza mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais. Kwa mwaka 2024/25, mradi ulitengewa kiasi cha shilingi Milioni 700 ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2025 kiasi cha Shilingi milioni 223.1 kimetumika katika ukarabati wa Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli II (Dar es Salaam) sawa na asilimia 32 ya bajeti iliyoidhinishwa. Aidha, shughuli za utekelezaji wa mradi zinategemewa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2025.

**3) URATIBU WA UCHUMI WA BULUU NCHINI**

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi Katika kuimarisha uratibu wa utekelezaji wa shughuli za Uchumi wa Buluu nchini, Serikali ilizindua Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 na Mkakati wa Utekelezaji wake (2024 - 2034), mwezi Juni, 2024. Kufuatia uzinduzi huo, OMR imekasimiwa jukumu la kuratibu utekelezaji wa Sera hiyo ambapo miongoni mwa shughuli muhimu katika utekelezaji zinajumuisha kuanzisha mfumo wa kitaasisi kwa ajili ya kuratibu shughuli za uchumi wa buluu nchini, kuandaa Mpango wa Matumizi wa Maeneo ya Maji, kuratibu uwekezaji wa kimkakati na fungamanishi katika matumizi ya rasilimali za Uchumi wa Buluu na kuwezesha uwepo wa utafiti na ujuzi katika matumizi ya rasilimali za Uchumi wa Buluu nchini.

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa shughuli hizo ambapo Kamati za Makatibu Wakuu na Mawaziri wa Sekta za Uchumi wa Buluu kwa ajili ya kusimamia utekelezaji wa shughuli husika zimeundwa na kuanza kufanya kazi. Kamati husika ziliidhinisha Mpango kazi wa utekelezaji wa Sera

kwa 2024/25 na 2025/26 katika vikao vyake vya vilivyofanyika mwezi Februari, 2025.

Aidha, katika kuimarisha mfumo wa uratibu wa masuala ya uchumi wa buluu, Ofisi inaendelea kufanyia kazi masuala ya kimuundo na kisheria katika uratibu wa shughuli hizo. Vilevile, katika kipindi hicho utoaji elimu kwa umma kuhusu uchumi wa buluu kupitia makongamano na mikutano mbalimbali umefanyika. Aidha, nitumie fursa hii kuwahimiza Wadau wote wa Uchumi wa Buluu nchini kutekeleza shughuli zilizopangwa kama ilivyobainishwa katika Mpango kazi wa utekelezaji wa Mkakati wa Sera na kutoa taarifa Ofisi ya Makamu wa Rais kwa wakati.

**4) MASUALA MENGINE YALIYOTEKELEZWA**

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizotekelezwa na Ofisi kwa kipindi cha mwaka 2024/25 ni pamoja na: Kuandaa taarifa za utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya uchaguzi wa mwaka 2020 kwa kipindi cha kuanzia Novemba, 2020 hadi Agosti, 2024; Kuandaa Mpango na Bajeti ya Ofisi na taarifa za utekelezaji wa mipango mbalimbali; Kuendelea kusimamia masuala ya utawala na usimamizi wa rasilimali watu ikiwemo utoaji wa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa watumishi; Kuwezesha ununuzi wa vitendea kazi na huduma kwa ajili ya matumizi ya Ofisi; Kuandaa na kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA; Kuandaa taarifa za hesabu za fungu 26 na 31; na kufanya Ufuatiliaji na Tathimini ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi.

**CHANGAMOTO NA UTATUZI**

**Changamoto**

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwa mwaka 2024/25 Ofisi inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo: Uelewa mdogo wa jamii kuhusu Masuala ya Muungano na faida zake hususan vijana. Aidha, kwa upande hifadhi na usimamizi wa Mazingira bado kuna changamoto ya uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa

hifadhi ya mazingira na uzingatiaji hafifu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake.

**Utatuzi wa Changamoto**

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto hizo, Ofisi imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano na faida zake kwa jamii hususani vijana kupitia vyombo vya habari, makongamano, warsha, semina, na mitandao ya kijamii. Aidha, kuanzia sasa Ofisi imepanga kuwa na programu mahsusi ya elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano ili kuondoa ombwe la ukosefu wa uelewa wa kutosha miongoni mwa jamii hususan vijana. Mikakati mingine iliyotekelezwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; na kujenga uwezo kwa wataalamu katika Wizara,Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuongeza kasi ya utoaji wa elimu na usimamizi wa hifadhi ya mazingira na biashara ya kaboni.

**5) BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)**

**110.** ***Mheshimiwa Spika***, Katika kipindi cha mwaka 2024/25, Baraza limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Mipango, Miongozo na maelekezo mbalimbali ya Serikali. Katika kipindi hicho, masuala yaliyotekelezwa yanajumuisha:

**a) Uzingatiaji na Usimamizi wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191**

**i) Ukaguzi na Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira**

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Baraza limefanya kaguzi katika miradi 3,278 inayojumuisha viwanda, migodi (yakiwemo machimbo ya mchanga na kokoto), mabomba ya mafuta, mitambo ya gesi na mafuta na nishati ya

umeme, maghala ya kemikali na taka zenye madhara, vituo vya mafuta, masoko, madampo, machinjio ya wanyama, kumbi za starehe na nyumba za ibada, hoteli, hifadhi ya vyanzo vya maji, mashamba, mifumo ya maji taka, Taasisi za elimu na afya, maghala ya kuhifadhi kemikali na taka hatarishi, majengo ya biashara na makazi pamoja na miradi mingine ya maendeleo nchini ili kuimarisha uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 na Kanuni zake.

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kaguzi hizo, ilibainika kuwepo kwa ongezeko la uzingatiaji wa Sheria katika maeneo yote yaliyokaguliwa. Hii imetokana na utoaji elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu uhifadhi wa mazingira na uzingatiaji wa Sheria, uwekaji mifumo thabiti ya kuhifadhi taka ngumu, kuboresha mifumo ya kutibu majitaka na udhibiti wa hewa chafu. Uhamasishaji na ufuatiliaji umesababisha ongezeko la idadi ya wawekezaji wanaosajili miradi kwa ajili ya TAM na kaguzi za mazingira.



*Wajumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wakiwa katika ziara ya kukagua Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) unavyozingatia utunzaji mazingira Chongoleani mkoani Tanga tarehe 20 Januari, 2025.*

### ii) Udhibiti wa Taka Hatarishi

**113. *Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kusimamia utekelezaji wa Kanuni za Udhibiti wa Taka Hatarishi za mwaka 2019 na Marekebisho yake ya mwaka 2021. Katika kipindi hicho, Baraza lilipokea maombi 289 ya vibali vya usimamizi wa taka hatarishi, ambapo vibali 121 vilitolewa. Aidha, Baraza lilipokea maombi 82 ya uteketezaji wa taka hatarishi na kusimamia uteketezaji wa tani 5,840.6, zikiwemo dawa na vifaa tiba vilivyokwisha muda wake na mabati ya *Asbestosi.*

**114. *Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu natoa rai kwa Wafanyabiashara wa Taka Hatarishi kuzingatia Sheria, Kanuni, miongozo na taratibu zilizopo ili kuepusha migogoro na kuimarisha udhibiti wa taka hatarishi na hivyo kulinda mazingira.

### iii) Kushughulikia Malalamiko ya Umma Kuhusu Uchafuzi na Uharibifu wa Mazingira

**115. *Mheshimiwa Spika*,** Baraza limeendelea kushughulikia malalamiko ya wananchi kuhusu uchafuzi na uharibifu wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025, Baraza lilipokea na kushughulikia malalamiko 247 yaliyohusu kelele, utupaji taka ovyo, utiririshaji ovyo wa majitaka, ujenzi holela, uchimbaji usio rasmi wa mchanga na uchafuzi wa hewa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na: kutoa elimu kwa jamii kuhusu uhifadhi wa mazingira hali iliyosababisha kupungua kwa malalamiko na muitikio chanya wa jamii; na adhabu ilitolewa pale ilipobainika kuna ukiukwaji wa sheria.

## b) Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Ukaguzi wa Mazingira

### i) Miradi Iliyosajiliwa

**116. *Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Baraza limesimamia usajili wa miradi ya maendeleo kwa ajili ya kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na Ukaguzi wa Mazingira. Katika kipindi hicho, jumla ya Miradi 1,358 ilisajiliwa. Kati

ya miradi hiyo 1,113 ilisajiliwa kwa ajili ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na miradi 245 kwa ajili ya Ukaguzi wa Mazingira. Aidha, miradi 740 imeidhinishwa na kupata vyeti ambapo 705 ni ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) na 35 ni miradi ya ukaguzi wa mazingira.

**ii) Usajili na Uratibu wa Utendaji Kazi wa Wataalam Elekezi wa Mazingira**

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kusajili na kutoa vyeti vya utendaji kazi kwa Wataalam Elekezi wa Mazingira. Hadi kufikia mwezi Machi, 2025, Baraza lilipokea na kuchakata jumla ya maombi 106 ya usajili wa Wataalam Elekezi wa Mazingira (Binafsi 104 na Kampuni 2). Katika maombi hayo, jumla ya Wataalam Elekezi wa Mazingira 49 waliidhinishwa. Vilevile, Baraza lilipokea na kuchakata maombi 81 ya vyeti vya utendaji kazi wa Wataalam Elekezi wa Mazingira. Aidha, Wataalam 55 walikidhi vigezo na kupatiwa vyeti vya utendaji kazi *(Practicing Certificate)*.

**c) Utekelezaji wa Ajenda ya Taifa ya Tafiti za Mazingira (Tafiti na Tathmini)**

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kutekeleza Ajenda ya Taifa ya Utafiti wa Mazingira (NERA) yenye lengo la kutoa mwelekeo wa kitaifa kwa wadau wa kufanya tafiti za mazingira ili kuwawezesha kuandaa programu, miradi na shughuli mbalimbali za kitafiti kwa kuzingatia maeneo ya kipaumbele ya Kitaifa yaliyomo kwenye ajenda.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kipindi cha mwaka 2024/25, Baraza lilifanya tathmini kuhusu masuala mbalimbali ya mazingira katika mifumo ikolojia ikiwemo: maporomoko ya Mlima Kawetere na Mlima Hanang pamoja na misitu/vichaka vya Itigi vilivyoko mkoani Singida. Vile vile, Baraza lilifanya tathmini ya mazingira katika Mlima Livingstone. Tathmini hizi ni hatua muhimu kwa uhifadhi endelevu wa rasilimali za milima husika.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, Baraza limefanya tathmini na kutoa ripoti zenye ushauri kuhusu

uharibifu wa mazingira. Tathmini hizo zilihusu maporomoko ya ardhi Muleba, kuvuja kwa bomba la mafuta TAZAMA Chalinze, moto katika maghala ya sulphur Vingunguti, kumwagika kwa sulphur Chalinze, na athari za mafuriko Rufiji.

**d) Uratibu wa Miradi Inayotekelezwa na Baraza**

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kuratibu miradi mbalimbali ya kuhifadhi mazingira ikiwemo mradi wa kupunguza matumizi ya zebaki kwenye uchimbaji mdogo wa madini ya dhahabu. Vilevile, Baraza linasimamia utekelezaji wa miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ambapo miradi hii inatekelezwa na wadau mbalimbali nchini ikiwemo Mradi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi wilayani Bunda; Mradi wa uvunaji maji wa kimkakati kuwezesha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi kwa wakazi wa vijijini kwenye sehemu kame za Wilaya za Bunda, Kongwa na Bahi, Manyoni, Igunga na Nzega na Zanzibar (Kaskazini B na Wete – Pemba); Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa Wakazi wa Pwani ya Zanzibar; na Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Jamii za Wakulima na Wafugaji Wilayani Kongwa.

**e) Elimu kwa Umma**

**122.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limeendelea kutoa elimu kuhusu masuala ya mazingira kwa kushiriki katika Maonesho ikiwemo maonesho ya Sabasaba (Dar es Salaam); Nanenane (Dodoma); Tamasha la Mafia; Maonesho ya Biashara Dubai; na Maonesho ya Anwani za Makazi (Dodoma). Vilevile, Baraza lilitoa elimu kuhusiana na masuala ya Mazingira kwa kutumia mabango makubwa 6; vipeperushi 7,500; mabango madogo 992; vishikizo 500 vya funguo; fulana 300; mashati 150; kalenda 600 na shajara 600 zenye jumbe mbalimbali za mazingira zilitolewa kwa wadau wa Mazingira.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** Baraza limefanikiwa kutoa elimu ya Mazingira kupitia programu tisini na mbili (92) za uhamasishaji kupitia redio za jamii na kitaifa, vipindi Thelathini na Nne (34) vya runinga; makala maalum kumi (10); habari arobaini na tano (45)

zilizorushwa kwenye Runinga; na taarifa za magazeti mia mbili hamsini na nne (254) zilizochapishwa katika magazeti mbalimbali kuhusu uhifadhi wa mazingira.

**f) Changamoto zilizojitokeza na utatuzi**

**124.** ***Mheshimiwa Spika***, Pamoja na jitihada ambazo zinafanywa na Baraza katika kukuza uelewa wa masuala ya mazingira, bado kumekuwa na uelewa mdogo wa Sheria ya Mazingira na Kanuni zake kwa wawekezaji, wataalamu elekezi na jamii kwa ujumla. Aidha, Baraza limeendelea kutumia vyombo vya habari ili kuhakikisha elimu ya mazingira inawafikia wananchi ipasavyo kupitia vipindi vya Runinga, Redio, magazeti, vibango (posters), katuni na mitandao ya kijamii.

**C. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26**

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mpango na bajeti ya Ofisi umezingatia miongozo mbalimbali ikiwemo; Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/26; Mpango Mkakati wa Ofisi (2021/22 - 2025/26); Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2021/22 hadi 2025/26); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020-2025; maagizo mbalimbali ya Viongozi wa Serikali; na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.

**SHUGHULI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA NA OFISI KWA MWAKA 2025/26**

**1) MASUALA YA MUUNGANO**

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26 Ofisi itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuratibu masuala ya Muungano na kuimarisha ushirikiano kwa masuala yasiyo ya Muungano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SJMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuratibu Vikao vya Kamati ya Pamoja ya SJMT na SMZ ya Kushughulikia Masuala ya Muungano; Kuratibu

utekelezaji wa masuala 22 ya Muungano kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Kuanzisha Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano (MAKAVAZI); Kuratibu Masuala ya Kiuchumi na Kijamii; Kuratibu masuala yasiyo ya Muungano; Kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya Muungano; Kuandaa machapisho na kushiriki katika Maadhimisho ya Miaka 62 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar; na Kukamilisha na kutumia Mfumo wa Kieletroniki wa Uratibu wa Taarifa za Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano.

**2) HIFADHI NA USIMAMIZI ENDELEVU WA MAZINGIRA**

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha suala la hifadhi na usimamizi wa mazingira linakuwa endelevu, Ofisi imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo kwa mwaka 2025/26: Kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021, Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191; Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 - 2032); Kutoa elimu kwa umma kuhusu hifadhi ya mazingira; Kuendelea kuratibu utekelezaji wa Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayohusu hifadhi na usimamizi wa mazingira; Kuendelea kuratibu miradi ya maendeleo inayohusu hifadhi ya Mazingira; Kuendelea kuratibu biashara ya kaboni nchini; na Kuendelea kuhamasisha na kuratibu matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa Taasisi zinazolisha watu zaidi ya 100.

**3) URATIBU WA SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU**

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ofisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu ya mwaka 2024 na Mkakati wake (2024 – 2034). Ambapo kazi zilizopangwa kutekelezwa zinajumuisha: Kuratibu marekebisho ya Sheria ya Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu, Sura 388 ili kuiwezesha taasisi hiyo kusimamia rasilimali zote za Uchumi wa Buluu zilizopo katika eneo la Ukanda Maalumu wa Uchumi wa Bahari na Bahari Kuu na hivyo nchi kunufaika ipasavyo na rasilimali tulizonazo; Kuratibu maandalizi ya Mpango wa kushirikisha jamii katika kuimarisha usalama wa maeneo ya maji; Kuratibu maandalizi ya Mpango wa Matumizi ya Maeneo ya Maji;

Kuratibu maandalizi ya Mpango wa kuhamasisha uwekezaji wa kimkakati na jumuishi; na Kuandaa mwongozo wa kufanya utafiti jumuishi miongoni mwa sekta za uchumi wa buluu.

## 4) KAZI NYINGINE ZITAKAZOTEKELEZWA NA OFISI

**129.** ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zilizopangwa kutekelezwa na Ofisi kwa mwaka 2025/26 ni pamoja na: Kusimamia masuala ya Utawala na Menejimenti ya Rasilimaliwatu; Kuratibu maandalizi ya maandiko na nyaraka mbalimbali za Ofisi; Kuandaa Mpango na Bajeti ya Ofisi na taarifa za utekelezaji wa mipango mbalimbali; Kuelimisha umma kuhusu majukumu, Sera, mikakati na programu zinazotekelezwa na Ofisi; Kutoa huduma ya ushauri wa masuala ya kisheria; Kufanya kaguzi za fedha zilizopokelewa na matumizi yake; Kushauri na kusimamia masuala ya ununuzi wa huduma na bidhaa; Kuandaa taarifa za mapato na matumizi ya Fungu 26 na 31; Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa majukumu ya Ofisi; na Kutoa msaada wa kitaalamu katika masuala ya TEHAMA.

## 5) KURATIBU UTEKELEZAJI WA MIRADI YA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

**130.** ***Mheshimiwa Spika***, Kwa mwaka 2025/26, Ofisi itaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya hifadhi na usimamizi wa mazingira kama ifuatavyo:

### a) Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo kuu la mradi ni kuimarisha usimamizi jumuishi wa mazingira na urejeshwaji wa ardhi iliyoharibiwa ili kujenga uhimilivu wa mifumo-ikolojia na jamii kwa ujumla nchini Tanzania. Mradi huu unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Tanganyika, Sumbawanga na Mpimbwe katika bonde la Ziwa Rukwa na Halmashauri za Wilaya ya Mbeya, Mbarali, Wanging'ombe na Iringa katika bonde la Ruaha Mkuu. Kwa mwaka 2025/26 kiasi cha Shilingi bilioni 7.1 zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za

mradi ikiwa ni pamoja na: Ujenzi wa malambo; Kufanya tathmini ya matokeo ya kampeni za uhamasishaji katika maeneo ya mradi; na Kufanya mafunzo kuhusu urejeshaji wa mazingira na hifadhi ya bayoanuai; na kurejesha ardhi iliyoharibika katika maeneo ya mradi.

**b) Mradi wa kujenga Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Kigoma**

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuboresha mifumo ikolojia itakayoongeza ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma na hivyo kuchangia moja kwa moja kuboresha mazingira katika eneo husika. Katika mwaka 2025/26 kiasi cha shilingi bilioni 17.0 kimetengwa kwa ajili ya shughuli za mradi ikiwemo: Ukarabati wa bwawa moja la uvunaji maji katika Halmashauri ya Kakonko; Kujenga mifereji ya uvunaji maji na kuhamasisha matumizi ya mbinu bora za umwagiliaji; Kuwezesha uandaaji wa Mipango ya matumizi ya ardhi katika vijiji kumi na mbili (12) vinavyozunguka kambi za wakimbizi katika maeneo ya mradi; Kuwezesha upandaji wa miti hekari elfu kumi na mbili (12,000); na Kukuza teknolojia za kisasa na mbinu za usimamizi ili kuimarisha uwezo wa wakulima katika kilimo kinachostahimili mabadiliko ya tabianchi.

**c) Mradi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi Katika Jamii zinazozunguka Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Zanzibar**

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la Mradi huu ni Kupunguza athari na kuimarisha uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika jamii pamoja na ikolojia katika Misitu ya Miombo Tanzania Bara na Maeneo Kame ya Zanzibar. Mradi huu unatekelezwa katika misitu ya Miombo iliyopo katika mikoa ya Tabora, Katavi na Rukwa kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Katika mwaka 2025/26 kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ikiwa ni pamoja na: Kufanya utafiti wa mahitaji ya uvunaji wa maji na teknolojia za kisasa za umwagiliaji; Kutoa mafunzo na kuwezesha upatikanaji wa teknolojia za usindikaji kwa wajasiriamali wa kati na wadogo; Kuwezesha ununuzi wa mizinga

ya nyuki ya kisasa; Kujenga vituo vya ukusanyaji wa asali; na Kununua vifaa na pembejeo kwa ajili ya mashamba darasa.

**d) Mradi wa Maandalizi ya Taarifa ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkataba wa Mabadiliko ya Tabianchi**

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni Kuandaa Taarifa ya Tatu ya Utekelezaji wa Mkataba wa Umoja wa Mataifa kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi. Katika mwaka 2025/26, kiasi cha shilingi bilioni 1.4 kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuandaa taarifa ya uzalishaji wa gesijoto nchini; na utekelezaji wa Mkataba husika.

**e) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaifa wa Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi**

**135.** ***Mheshimiwa Spika***, Lengo la mradi huu ni Kujenga Uwezo wa Taasisi katika Utekelezaji wa Makubaliano ya Paris. Katika mwaka 2025/26 kiasi cha shilingi bilioni 1.2 kimetengwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli za mradi ikiwemo: Kutoa elimu kwa wadau kuhusu ukusanyaji wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi; Kuweka mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za mabadiliko ya tabianchi; na Kutoa mafunzo kuhusu ufuatiliaji wa Mchango wa taifa wa kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi.

**f) Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kitaasisi Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni**

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la Mradi ni kujenga uwezo wa Kitaasisi kuwezesha utekelezaji wa Itifaki ya Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni. Mradi huu unafadhiliwa na Mfuko wa Utekelezaji wa Itifaki ya Montreal kupitia Shirika la Mazingira la Umoja wa Mataifa (UNEP). Katika mwaka 2025/26, Shilingi milioni 433 zimetengwa kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa Mafundi mchundo 250 wa viyoyozi na majokofu kuhusu mbinu bora za kuhudumia vifaa hivyo bila kuathiri Tabaka la hewa ya Ozoni; Kutoa mafunzo kwa mawakala wa forodha

500 kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa gesi zinazodhibitiwa chini ya Itifaki; Kununua mashine za kunasa na kurejeleza gesi chakavu za Majokofu na Viyoyozi; Kufanya mafunzo kwa maafisa forodha na wasimamizi wa Sheria 200 kuhusu kuhusu udhibiti wa uingizaji nchini wa gesi zinazodhibitiwa chini ya Itifaki; na Kutoa mafunzo kwa maafisa ugavi na ununuzi 120 wa Wizara na Taasisi kuhusu matakwa ya Itifaki ya Montreal.

**g) Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Babati**

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kurejesha ikolojia ya ziwa Babati lililoathiriwa kutokana na shughuli za kibinadamu. Katika mwaka 2025/26 kiasi cha shilingi milioni 200 kimetengwa kwa ajili ya Kupanda miti ili kuzuia mmomonyoko wa udongo; Kubaini na kuweka mipaka ya kudumu katika ziwa; Kuandaa Mpango wa Usimamizi wa Matumizi wa rasilimali za Maji; na Kutoa mafunzo kuhusu udhibiti wa magugu maji kwa jamii zinazozunguka eneo la ziwa na Kubainisha njia mbadala za kujikimu kwa jamii zinazozunguka maeneo ya ziwa.

**h) Mradi wa Usimamizi na Uhifadhi wa Ikolojia ya Ziwa Chala na Ziwa Jipe**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuimarisha ikolojia na usimamizi endelevu wa Ziwa Chala na Ziwa Jipe. Katika mwaka 2025/26 kiasi cha shilingi milioni 200 kimetengwa kwa ajili ya Kubainisha njia mbadala za kujikimu kwa jamii zinazozunguka katika maeneo ya ziwa; Kuhamasisha mbinu za asili zinazotumika kuondoa magugu maji katika Ziwa Chala na Ziwa Jipe; Kufanya mapitio ya sheria ndogo zinazosimamia Ziwa Chala na Ziwa Jipe; na Kukuza uelewa wa jamii kuhusu usimamizi endelevu wa Ziwa Chala na Ziwa Jipe.

***Mradi wa Kuanzisha Bustani ya Kijani Katika Eneo la Swaswa Mnarani, Dodoma***

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Lengo la mradi huu ni kuanzisha eneo lenye mandhari ya kijani na mazingira safi katika eneo oevu

la Swaswa Mnarani Jijini Dodoma ambapo kwa mwaka 2025/26 kiasi cha shilingi bilioni 2.5 kimetengwa kwa ajili ya Kufanya maboresho na kujenga mifereji mipya maji ya mvua na kujenga bwawa la kuhifadhi maji ya mvua eneo la Swaswa.

**Miradi Mingine Itakayotekelezwa**

**(i) Mradi wa Ujenzi na ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais**

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** lengo la mradi huu ni kuwezesha shughuli za ujenzi na ukarabati wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais. Kwa mwaka 2025/26 kiasi cha shilingi bilioni 1.7 kimetengwa kwa ajili ya kazi hii.

**6) BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26 Baraza litaendelea kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura 191 kwa kutekeleza shughuli zifuatazo: Kuendelea kutekeleza Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Kutekeleza Mkakati wa Taifa wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia (2024 – 2034) ili kupunguza uharibifu wa mazingira; Kuendelea kuratibu mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira na kusajili Wataalam Elekezi wa Mazingira; Kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya hifadhi na usimamizi wa mazingira; Kufanya kaguzi za mazingira katika maeneo mbalimbali ili kulinda na kutunza mazingira; Kufanya tafiti mbalimbali za mazingira; Kufanya mapitio ya Ajenda ya Taifa ya Tafiti za Mazingira (NERA, 2017/2022); Kuratibu na kuendesha Kongamano la Sita la Sayansi kuhusu uhifadhi wa maeneo oevu; Kuratibu utekelezaji wa Programu ya Binadamu na Hifadhi Hai kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Sayansi na Elimu (UNESCO); na Kuratibu shughuli za masuala ya maeneo nyeti na lindwa.

**D. HITIMISHO NA SHUKRANI**

**143.** ***Mheshimiwa Spika***, Mafanikio yaliyopatikana katika mwaka 2024/25 yamechangiwa na ushirikiano mzuri kutoka kwa

Washirika wa Maendeleo, Sekta binafsi, Taasisi za Fedha nchini, Asasi Zisizo za Kiserikali za ndani na nje ya nchi; na Wadau mbalimbali. Washirika wa Maendeleo ikiwa ni pamoja na: Umoja wa Nchi za Ulaya (EU); Benki ya Dunia (WB); Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF); Serikali ya Norway; Serikali ya Saudi Arabia; Serikali ya Sweden; Serikali ya Uingereza; Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao hapa nchini; Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP); Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP); Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF); Mfuko wa Kimataifa wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi (AF); Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Shirika la Maendeleo la Jumuiya ya Madola (FCDO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO); Shirika la Umoja wa Mataifa la Mitaji na Maendeleo (UNCDF); Shirika la Uhifadhi wa Mazingira Duniani (WWF); Mfuko wa Kimataifa wa Kuendeleza Kilimo - IFAD; Mfuko wa Mabadiliko ya Tabianchi (GCF); Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO); Mfuko wa Utekelezaji wa Mkataba wa Montreal; Mfuko wa Dunia wa Bayoanuai (GBFF); Shirika la Chakula Duniani (WFP); The Good Neighbours Global Impact Foundation; Korea Investment Securities; na Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Ujerumani (GIZ).

***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia fursa hii kuwaomba Washirika wa Maendeleo na Wadau wengine kuendelea kushirikiana na Ofisi katika kuimarisha Muungano wetu na usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi nchini kwa maendeleo endelevu.

**144.** ***Mheshimiwa*** **Spika,** Baada ya shukrani hizo kwa washirika wa maendeleo, ninaomba sasa nichukue nafasi hii kumshukuru **Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis (Chilo) (Mb.)**, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), kwa ushirikiano na msaada mkubwa anaonipa katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

**145.** ***Mheshimiwa*** **Spika,** Vilevile, nitumie fursa hii kuwashukuru wasaidizi wangu katika utendaji kazi wa Ofisi ya Makamu wa Rais wakiongozwa na *Mhandisi* Cyprian John Luhemeja, Katibu Mkuu; Bw. Abdallah Hassan Mitawi, Naibu

Katibu Mkuu (Muungano); na Bibi Christina Solomon Mndeme, Naibu Katibu Mkuu (Mazingira); Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mkurugenzi Mkuu (NEMC); Prof. Eliakimu Zahabu, Kaimu Mtendaji Mkuu (NCMC); Wakuu wa Idara na Vitengo; na Wafanyakazi wote kwa mchango wao katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi. Aidha, mwanzoni mwa mwezi Aprili, 2025, Mhandisi Mwanasha Rajab Tumbo aliteuliwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NEMC. Tunampongeza Mhandisi Mwanasha na tunamtakia kila la kheri katika utekelezaji wa majukumu yake, pamoja na wajumbe wa bodi.

**146.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa umuhimu mahususi naomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Kikwajuni kwa kuendelea kuniamini kuwatumikia kwenye nafasi ya Ubunge pamoja na kunivumilia katika kipindi chote ambacho ninakuwa nje ya Jimbo nikitekeleza majukumu mengine ya Kitaifa. Aidha, nimetaarifiwa kuwa hivi sasa wanaendelea kunifuatilia mubashara katika tukio hili la uwasilishaji wa bajeti kutokea kule jimboni. Hivyo, ninawashukuru sana kwa upendo mkubwa kwangu, na mimi ninawaahidi nitaendelea kuwatumikia kwa uadilifu mkubwa na Mwenyezi Mungu awabariki sana.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mwisho lakini sio kwa umuhimu napenda kuishukuru familia yangu pendwa nikianza na Mke Wangu Kipenzi Thania Ali Abulla na Watoto wetu, Riziki Hamad Masauni, Asha Hamad Masauni na Bareek Hamad Masauni kwa upendo wao unaonipa nguvu ya kutekeleza majukumu yangu vema.

## MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2025/26

**148.** ***Mheshimiwa* Spika,** ninaomba Bunge lako tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 19,946,399,000.00** kwa ajili ya matumizi ya Fungu 26 (Ofisi binafsi ya Makamu wa Rais) na Shilingi **61,917,791,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa Fungu 31. Kati ya kiasi kinachoombwa kwa Fungu 26, **Shilingi**

**1,066,899,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi **18,879,500,000.00** ni Matumizi mengineyo.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** maombi ya fedha kwa Fungu 31 yanajumuisha Matumizi ya Kawaida **Shilingi 28,858,213,000.00** ambapo kati ya fedha hizo Shilingi **10,907,597,000.00** ni Mishahara ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na **Shilingi 17,950,616,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Shilingi 4,602,000,000.00** fedha za ndani na **Shilingi 28,457,578,000.00** ikiwa ni fedha za nje.

**HITIMISHO**

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukukrani zangu za kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Aidha, Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Ofisi ambayo ni www.vpo.go.tz.

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa lamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Hoja imetolewa na hoja imeungwa mkono. Nimuite sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria kwa niaba yake Mheshimiwa Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU TA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge. Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu

Makadirio na Mapato ya matumizi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2024, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi masharti yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya kwanza, inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(b) Sehemu ya pili, inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;

(c) Sehemu ya tatu, inahusu uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(d) Sehemu ya nne, inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

(e) Sehemu ya tano, ni hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2024. Kifungu

cha 6(2)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu mawili ambayo ni, Fungu 26 - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais, na Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi na tathmini; matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu matatu yaliyochambuliwa kama ifuatavyo:-

(a) Mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya Kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; na

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na. 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais. Mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 16,969,208,000.00, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 989.20 ni Mishahara na shilingi bilioni 13.490 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 11.29 sawa na 66.6% ya bajeti iliyoidhinishwa ambapo kati ya fedha hizo shilingi milioni

473,715,000.00 ilikuwa ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 10.82 kwa ajili ya matumizi Mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Fungu Na. 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano). Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 14.84 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 14.14 ikiwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 3,000,000,000 ilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 14 ilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha shilingi bilioni 700,000,000.00 sawa na 4.2% ilitengwa kwa ajili ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ilipokea jumla ya shilingi bilioni 8.31kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na 58.8% ya bajeti iliyoidhinishwa na shilingi milioni 122.08 sawa na 17.4% ilipokelewa kwa ajili ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira ni kama inavyoonekana katika jedwali namba moja na jedwali namba mbili yaliyopo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni wa kuridhisha, kama inavyoonekana katika jedwali namba moja, isipokuwa katika fedha za miradi ya maendeleo ambapo Kamati ilielezwa kwamba sababu ya upungufu wa upatikanaji wa fedha za ndani za maendeleo umetokana na Mkandarasi kutowasilisha hati za malipo kwa Serikali ili Hazina iweze kutoa fedha za kumlipa Mkandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Kamati ilielezwa kwamba mkandarasi ameshawasilisha Serikalini hati ya pili ya malipo na hivyo hadi mwisho wa mwezi huu Serikali kupitia Mfuko Mkuu wa Hazina itakuwa imeshamlipa na hivyo kumwezesha kuendelea na kazi zilizobaki katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na mazingira

kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 700,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika Jedwali namba tatu lililopo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo inayosimamiwa na Wizara na kubaini yafuatayo: Ujenzi wa Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais, Mradi Namba 6309.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa ujenzi na ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais Luthuli Jijini Dar es Salaam na Mtumba Jijini Dodoma umekamilika kwa asilimia kubwa ambapo hadi kufika Februari, 2025 Wizara imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(a) Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais katika Mji wa Serikali Mtumba ambapo mpaka kufikia Februari mwaka 2025 hatua ya iliyofikiwa katika ujenzi huo ni 85%; na

(b) Ukarabati wa Majengo ya Ofisi ya Makamu wa Rais Luthuli Dar es Salaam Wizara inaendelea na ujenzi wa eneo la kuegeshea magari, ujenzi wa mfumo wa maji safi na maji taka, ujenzi wa *lift* na uwekaji mifumo ya umeme na hadi kufikia Februari mwaka 2025 Ujenzi ulikua umekamilika kwa 69%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha sehemu kubwa na kuisisitiza kutekeleza sehemu ya miradi iliyobakia kama walivyotengewa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Matumizi ya kawaida, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 38.10 ikiwa ni fedha za matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.76 ni mishahara na shilingi bilioni 35.33 ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika jedwali Na.4 lililopo kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika mwaka wa fedha 2025/2026 imeongezeka kwa 18.36% ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha wa 2024/2025. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili limechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zitumike vizuri, na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Serikali ihakikishe kwamba imewasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya maendeleo; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 1.7 ambazo ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo wa ujenzi na ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2025/2026, imeongezeka kwa shilingi bilioni moja sawa na ongezeko la 41% ikilinganishwa na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Kamati ilielezwa kwamba ongezeko hili la bajeti limechangiwa na ongezeko la bei za bidhaa za ujenzi kama inavyooneshwa kwenye Jedwali Na.5 lililopo kwenye taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi yake kwa kutumia fedha za ndani pekee bila kutegemea fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Maoni ya Jumla; kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo:-

(i) Serikali kushindwa kupeleka bajeti iliyoidhinishwa kwa wakati kwa Wizara huweza kuchangia kupunguza kasi na ufanisi wa utendaji kazi wa ofisi hii; na

(ii) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kwa wakati, kunapelekea miradi ya maendeleo kutokukamilika kwa wakati na hivyo kuchelewesha utoaji huduma kwa wananchi waliokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mahususi fungu kwa fungu; Fungu 31- Ofisi ya Makamu wa Rais: -

(i) Serikali ihakikishe kwamba inatoa fedha za maendeleo na matumizi mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, taasisi na idara zilizoko chini yake kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi;

(ii) Serikali ifanye tathmini ya utekelezaji na mafanikio ya miradi ya maendeleo inayohusu Muungano; na

(iii) Serikali ihakikishe kwamba inasimamia kikamilifu mchakato wa kuanzishwa kwa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (MAKAVAZI).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ninapenda kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Ninapenda kuwashukuru Wajumbe wa

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao yote yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi ya Bunge kama yalivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Hamad Masauni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano wao ambao wametupatia kwa wakati wote wa kuandaa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara, pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano wanaoipatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo Mhandisi Cyprian John Luhemeja, Naibu Katibu Mkuu Muungano Ndugu Abdallah Hassan Mitawi, na Naibu Katibu Mkuu Mazingira Bi. Christine Solomon Mndeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, lakini sio kwa umuhimu, ninapenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee ninawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kwa kiasi kikubwa na kwa weledi mkubwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuwashukuru Wanajimbo wa Muleba, wapigakura wangu, Jimbo la Muleba Kusini na Wilaya ya Muleba kwa ujumla wake kwa upendo wao. Ni kwa upendo huo, ninasimama hapa mbele yako. Ninaomba waendelee kuniamini kwa kipindi kingine ili niendelee kuwatumikia kama Mbunge wao kwa maendeleo ya Jimbo la Muleba Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais,

Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 UTANGULIZI**

**1.1. Maelezo ya Awali**

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2024, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi masharti yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Bunge, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla kuonesha msingi na Muundo wa taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

b) Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa Upatikanaji wa

fedha za bajeti, utekelezaji wa miradi ya Maendeleo na Uzingatiaji wa Ushauri na maoni ya Kamati;

c) Sehemu ya Tatu inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

d) Sehemu ya Nne inahusu majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

**1.2. Msingi wa Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Kamati kufanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2024. Kifungu cha 6(2)(b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

**1.3 Mawanda ya Uchambuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu mawili (2) ambayo ni:-

a) **Fungu 26** - Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais; na

b) **Fungu 31** - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHIMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira. Kwa sababu hiyo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, naomba kubainisha mambo makuu matatu yaliyochambuliwa kama ifuatavyo; -

(a) Mwenendo wa Upatikanaji wa fedha za Bajeti ya Matumizi ya kawaida na Bajeti ya Maendeleo;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira; na

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge.

### 2.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Bajeti

#### 2.2.1 Fungu Na. 26 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 16,969,208,000.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 989,208,000.00** ni Mishahara na **Sh. 13,480,000,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Februari, 2025 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 11,293,715,000.00 sawa na asilimia 66.6 ya bajeti iliyoidhinishwa** ambapo kati ya fedha hizo **Sh. 473, 715,000.00** kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 10,820,000,000.00** kwa ajili ya matumizi Mengineyo (OC).

### 2.2.2 Fungu Na. 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 14,840,447,100.00**, kati ya fedha hizo **Sh. 14,140,447,100.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ambapo **Sh. 3,003,975,000.00** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara na **Sh. 11,136,472,100.00** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo, Aidha **Sh. 700,000,000.00** sawa na **asilimia 4.2** ilitengwa kwa ajili ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ilipokea jumla ya **Sh. 8,317,310,318.29** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida ambayo ni sawa na **asilimia 58.8** ya bajeti iliyoidhinishwa na **Sh. 122,082,517.71** sawa na **asilimia 17.4** zilipokelewa kwa ajili ya Maendeleo.

Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1 na Jedwali Na. 2.**

**JEDWALI NA. 1: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 26**– Ofisi binafsi ya Mkamu wa Rais | 16,969,208,000.00 | 11,293,715,000.0 | 75 |
| **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | 14,840,447,100.00 | 8,317,310,318.29 | 58.8 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **JUMLA KUU** | **31,109,655,100.00** | **19,611,025,318.29** | **63.03** |

*Chanzo: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Uratibu na Usanifu wa Kamati.*

**JEDWALI NA. 2: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2024/2025**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 26** – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais | 00 | 00 | 00 |
| **Fungu 31**– Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | 700,000,000.00 | 122,082,517.71 | 17.4 |
| **JUMLA KUU** | **700,000,000.00** | **122,082,517.71** | **17.4** |

*Chanzo: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kwa ujumla, mwenendo wa upatikanaji wa fedha katika Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira ni wa kuridhisha, kama inavyoonekana katika jedwali namba 1, isipokuwa katika fedha za miradi ya maendeleo ambapo kamati ilielezwa kwamba sababu ya upungufu wa upatikanaji wa fedha za ndani za maendeleo umetokana na Mkandarasi kutowasilisha Hati za malipo kwa Serikali ili Hazina iweze kutoa fedha za kumlipa Mkandarasi.

**Mheshimiwa Spika**, Aidha Kamati ilielezwa kwamba mkandarasi ameshawasilisha Serikalini Hati ya pili ya malipo na Hivyo hadi mwisho wa mwezi huu Serikali kupitia mfuko mkuu wa Hazina itakuwa umeshamlipa na Hivyo kumuwezesha kuendelea na kazi zilizobaki katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara hii.

### 2.3 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 iliidhinishiwa jumla ya **Sh 700,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika **Jedwali Na. 3**

**JEDWALI NA. 3: Miradi ya Maendeleo iliyotengewa Fedha 2024/2025**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2024/2025 |
|---|---|---|
| **Fungu 26** – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais | | 00 |
| **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | **NA. 6309**-Ujenzi wa ukarabati wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais | 700,000,000.00 |
| **JUMLA KUU** | | **700,000,000.00** |

*Chanzo: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua utekelezaji wa bajeti ya miradi ya Maendeleo inayosimamiwa na Wizara na kubaini yafuatayo

#### 2.3.1 Ujenzi wa Ukarabati wa Ofisi na Makazi ya Makamu wa Rais (Namba ya Mradi 6309)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu wa ujenzi na ukarabati wa ofisi na makazi ya Makamu wa Rais Luthuli jijini Dar es Salaam na Mtumba jijini Dodoma umekamilika kwa asilimia kubwa ambapo hadi kufika Februari 2025 Wizara Imetekeleza shughuli zifuatazo

i. Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais katika Mji wa Serikali Mtumba ambapo mpaka kufikia Februari mwaka 2025 hatua ya iliyofikiwa katika ujenzi huo ni asilimia 85.

ii. Ukarabati wa Majengo ya Ofisi ya Makamu wa RaisLuthuli-II – Dar es salaam Wizara inaendelea na ujenzi wa eneo la kuegeshea magari, ujenzi wa mfumo wa maji safi na maji taka, ujenzi wa lift na uwekaji mifumo ya umeme na hadi kufikia Februari mwaka 2025 Ujenzi ulikua umekamilika kwa **asilimia 69**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha sehemu kubwa na kuisisitiza kutekeleza sehemu miradi iliyobakia kama walivyotengewa fedha.

### 2.4 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa Uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ilitoa maoni, ushauri na mapendekezo mbalimbali ili kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hiyo. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba kwa sehemu kubwa Serikali imezingatia maoni na ushauri wa Kamati.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

### 3.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 38,106,589,000.00** ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo **Sh. 2,766,899,000.00** ni mishahara, **Sh. 35,339,690,000.00** ni matumizi mengineyo, kama ambavyo imechanganuliwa katika **Jedwali Na. 4.**

**JEDWALI NA. 4: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2025/2026**

| FUNGU | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU | JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA |
|---|---|---|---|---|
| **Fungu 26** – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais | 1,066,899,000.00 | 18,879,500,000.00 | 00 | 19,946,399,000.00 |
| **Fungu 31** – Ofisi Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | 3,115,273,000.00 | 13,344,917,000.00 | 00 | 16,460,190,000.00 |
| **JUMLA KUU** | **4,182,172,000.00** | **32,224,417,000.00** | **00** | **36,406,589,000.00** |

*Chanzo: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira na Uratibu na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **asilimia 14.5** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili limechangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa.

Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zitumike vizuri, na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, na Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria.

### 3.2 Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh.1, 700,000,000.00** ambazo ni fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa maendeleo ya Ujenzi wa ukarabati wa ofisi na makazi ya Makamu wa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Sh. 1,000,000,000.00** sawa na ongezeko la **asilimia 58.8** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha, Kamati ilielezwa kwamba ongezeko hilo la bajeti limechangiwa na Ongezeko la mahitaji ya ukarabati na kupanda kwa bei za malighafi za ujenzi. **Jedwali Na. 5** limechanganua.

**JEDWALI NA. 5: Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| FUNGU | NAMBA NA JINA LA MRADI | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | |
|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 26** – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais | | 00 | 00 |
| **Fungu 31** – Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira | **NA. 6309-** Ujenzi wa ukarabati wa Ofisi na makazi ya Makamu wa Rais | 1,700,000,000.00 | 00 |
| **Jumla Ndogo** | | **1,700,000,000.00** | **00** |
| **JUMLA KUU** | | **1,700,000,000.00** | |

*Chanzo: Randama za Ofisi ya Makamu wa Rais Muuungano na Mazingira na Usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi yake kwa kutumia fedha za ndani pekee bila kutegemea fedha za nje.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kwa kuzingatia majadiliano ya kina kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kwa mafungu yote kama ifuatavyo: -

(i) Serikali kushindwa kupeleka Bajeti iliyoidhinishwa kwa wakati kwa Wizara huweza kuchangia kupunguza kasi na ufanisi wa utendaji kazi wa ofisi hii.

(ii) Kutokutolewa kwa fedha za maendeleo kwa wakati, kunapelekea Miradi ya Maendeleo kutokukamilika kwa wakati na hivyo kuchelewesha utoaji huduma kwa wananchi waliokusudiwa.

**4.2 Ushauri Mahususi Fungu kwa Fungu**

**4.2.1 Fungu 31: Ofisi ya Makamu wa Rais**

i. Serikali ihakikishe kwamba inatoa Fedha za Maendeleo na Matumizi Mengineyo ili kuwezesha Wizara hii, taasisi na idara zilizoko chini yake kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kwa ufanisi.

ii. Serikali ifanye tathmini ya utekelezaji na mafanikio wa miradi ya maendeleo inayohusu Muungano.

iii. Serikali ihakikishe kwamba inasimamia kikamilifu mchakato wa kuanzishwa kwa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar (MAKAVAZI).

**SEHEMU YA TANO**

**5.0 HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika**, Napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi ya Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.
7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Suma Ikenda Fyandomo, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Seif Khamis Said Gulamali, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Aziza Seylum Ally, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.
21. Mhe. Joseph Anania Tadayo, Mb.
22. Mhe. Dkt. Oscar Ishengoma Kikoyo, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza na kumshukuru Mhe. Hamad Masauni Mb, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira na Mhe. Khamis Hamza Khamis Mb, Naibu Waziri wa Nchi, Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiutoa kwa Kamati wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Ninaomba pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara, pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo

Mhandisi Cyprian John Luhemeja, Naibu Katibu Mkuu Muungano Ndg. Abdallah Hassan Mitawi na Naibu Katibu Mkuu Mazingira Bi. Christine Solomon Mndeme.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Ildephonce Leonard kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, kiupekee nawashukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**

25 Aprili, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Oscar Kikoyo. Sasa nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Maji na Mazingira, kwa niaba yake atawakilishwa na Mheshimiwa Asya Sharif Omar. *(Makofi)*

**MHE. ASYA SHARIF OMAR K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na uhai na hatimaye kuweza kukutana siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba taarifa hii yote iingie kwenye Kumbukumbu ya Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo:-

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyoweza kufanya kazi;

(ii) Sehemu ya Pili inabainisha Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Kamati ilizingatia Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februali, 2023 na kufanya Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2024/2025 katika Kamati kwenye maeneo yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Hali ya Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina;

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025. kwa

mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilitoa ushauri katika maeneo 10. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu ya ushauri imefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri uliotekelezwa kwa sehemu ni mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ili kuendana na Sera ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira ya mwaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala hili ninaomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba, katika Mkutano wa 18, Bunge lilifanya marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 ambapo Waziri aliahidi kuwasilisha Miswada yenye marekebisho makubwa yatakayoongeza ufanisi katika usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Waziri alilieleza Bunge na ameendelea kuihakikishia Kamati kuwa Miswada ya Marekebisho hayo itawasilishwa wakati wa Mkutano wa 19 wa Bunge. Hivyo ni matumaini ya Kamati kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira itatekeleza ahadi ya kuwasilisha Miswada miwili inayohusu uchumi wa buluu na uundwaji wa Mamlaka ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira Nchini *(NEMA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa ushauri wa Kamati unaoendelea kutekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira ni kuendelea kutoa elimu kuhusu uhifadhi wa Mazingira kwa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara zote ushauri unapotolewa Bungeni unalenga kuboresha shughuli za umma kwa maslahi ya wananchi. Hivyo, kuzingatiwa kwa ushauri huo kunatimiza azma ya kuboresha ustawi wa wananchi. Aidha, kwa kuchelewa kuzingatia ushauri, hatari yake ni kutoboresha shughuli za Umma kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo; Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi miwili kati ya miradi

16 ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi miwili iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati ni kama hii ifuatayo:-

(i) Urejeshwaji endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika; na

(ii) Mradi wa kurejesha ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo yanapatikana katika ukurasa wa sita wa Taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni ya Kamati; Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea na utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na wigo wa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kama vile mradi wa Bwawa la Sigiri na josho la mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Kutoridhishwa huku kunatokana na Kamati kuwa na matarajio makubwa kuwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira itaratibu miradi mfano ya kugusa wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Upatikanaji wa fedha ni hatua muhimu katika utekelezaji wa bajeti. Aidha, uzoefu wa kiwango cha fedha kinachopatikana kwa mwaka mmoja ni muhimu katika uamuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka unaofuata. Kwa mantiki hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi yanaonesha mambo yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ya upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida; Hadi mwezi Februari, 2025, upatikanaji wa fedha za matumizi ya Kawaida kutoka Hazina ulikuwa ni shilingi 680,826,000,000 sawa na 76.1% kwa mishahara ya Idara ya

Mazingira, shilingi 3,662,047,000 sawa na 63% kwa mishahara ya *NEMC* na shilingi 2,902,364,000 sawa na 98% kwa shughuli za uendeshaji *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa shughuli za Idara ya Mazingira na *NEMC* ulifikia shilingi 7,245,237,780, sawa na 75% ya kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili hiyo. Mwenendo huo unaashiria utekelezaji mzuri wa bajeti uliotarajiwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa fedha za matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hali ya upatikanaji wa fedha za miradi ya maendeleo. Matokeo ya uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi yanaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Kwa ujumla Kamati imebaini, ucheleweshaji wa fedha za miradi ya maendeleo na utolewaji mdogo wa fedha za ndani. Kwa mfano, hadi Februari 2025, fedha za ndani zilizotolewa ni shilingi bilioni 499 sawa na 17% tu ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili hiyo;

(ii) Fedha za nje kwa ajili ya miradi ya mazingira zimepatikana shilingi 9,940,230,000 sawa na 54% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Kiwango cha upatikanaji wa fedha kimepungua kwa 10% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2023/2024 ambapo hadi mwezi Februari, 2024 kiwango kilichopokelewa kilikuwa shilingi 9,710,000,000 sawa na 64% ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge;

(iii) Baadhi ya miradi haikupokea fedha kabisa kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mfano, Mradi wa Mfano wa kujenga Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Kigoma haukupokea fedha kabisa; na

(iv) Jumla ya fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya mazingira hadi Februari, 2025 ni shilingi 10,439,230,000 sawa na 49% ambayo ni ndogo ikilinganishwa na 66.6% iliyopaswa kufikiwa kwa kipindi kama hicho. Hali hiyo ni dalili ya wazi kwamba upo uwezekano wa miradi

mingi ya mazingira kutokamilika kama ilivyokusudiwa kufikia Juni, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla mtiririko wa fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo hauridhishi. Aidha, upatikanaji wa fedha za ndani ni mdogo zaidi hali inayoashiria uwepo wa msukumo mdogo wa kifedha katika utekelezaji wa miradi ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo wa fedha. Umakini zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya mishahara kwa Idara ya Mazingira *(NEMC)* na uendeshaji wa shughuli zinazohusu masuala ya mazingira *(OC)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa maeneo hayo unafanyika kwa kuzingatia ahadi iliyotolewa kwa wananchi kwenye Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 - 2025. Ahadi hiyo ilihusu kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani kwa kuzingatia kipaumbele katika kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira imetengewa jumla ya shilingi 31,359,578,000 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 2,902,000,000 ni fedha za ndani na shilingi 28,457,578,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Maendeleo katika mwaka wa fedha 2025/2026, imeongezeka kwa shilingi 10,151,737,000

sawa na 47.9% ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha unaoishia 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa:-

(i) Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kwa 47.9% ikilinganishwa na Bajeti ya mwaka wa fedha unaoishia;

(ii) Bajeti ya fedha za nje imeongezeka kwa shilingi 10,151,737,000 sawa na 55.5% huku Bajeti ya ndani haikuongezeka ikilinganishwa na fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(iii) Upangaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 haujazingatia ipasavyo hali ya upatikanaji wa fedha unaotokana na mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Maendeleo kwa Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itatoa fedha hizo kama zilivyopangwa na kwa wakati ili kutekeleza mpango kazi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi ya kawaida; kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi 12,395,023,000 ikiwa ni fedha kwa ajili ya matumizi ya mawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi 1,117,037,000 ni fedha za mishahara kwa Idara ya Mazingira, shilingi 6,675,287,000 ni fedha za mishahara kwa *NEMC* na shilingi 4,605,696,000 ni fedha inayoombwa kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi unaonesha kuwa bajeti ya matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2024/2025 imeongezeka kwa 28.2% ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaoisha ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi

9,670,266,000. Kamati imebaini kwamba, miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko hili ni kuongezeka kwa nafasi za ajira kwa watumishi katika sekta ya mazingira ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya sekta hiyo.

Mheshmiwa Mwenyekiti, jumla ya fedha inayoombwa na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni shilingi 43,757,601,000. Kiasi hiki ni sawa na ongezeko la 41.7% ya bajeti ya ofisi hiyo iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya Taifa na bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia ulinganisho huo, Kamati ilibaini kuwa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira ni asilimia 0.08 ya bajeti yote ya Taifa. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia 0.02. Matokeo hayo kwa ujumla yanatoa taswira ya namna Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira inavyojipanga kusimamia mazingira. Aidha, Kamati ina maoni kuwa utekelezaji wa mipango ya Serikali kuhusu masuala ya mazingira uendelee kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati; lengo kuu la taarifa hii ni kubainisha maoni na ushauri wa Kamati ili kuwezesha majadiliano ya Bunge. Kamati inaamini kuwa maelezo yaliyotolewa ndani ya taarifa hii yatakuwa na msaada muhimu kwa Bunge. Pamoja na majadiliano kuhusu hoja hii, upo umuhimu wa kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa katika taarifa hii kwa lengo la kuboresha shughuli zinazohusu usimamizi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira – Fungu 31 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naomba kubainisha maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Fedha zinazotengwa kutekeleza baadhi ya miradi ya maendeleo hazitoshi na hazikidhi dhamira ya Serikali ya

kuwa na miradi ya kielelezo kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, hususani katika mapambano dhidi ya Mabadiliko ya tabianchi;

(b) Utolewaji mdogo wa fedha za ndani kwa miradi ya maendeleo hauoneshi msukumo wa kutosha wa Serikali katika Sekta ya Mazingira na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa miradi;

(c) Kutosomana kwa mifumo ya kiutendaji na uratibu hafifu katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo unasababisha miradi hiyo kutotekelezwa ipasavyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa;

(d) Manufaa ya biashara ya kaboni ni kichocheo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na;

(e) Marekebisho makubwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 yataongeza hamasa katika usimamizi na uhifadhi wa mazingira nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati; Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(a) Serikali itenge fedha za kutosha katika utekelezaji wa miradi mahsusi ya maendeleo ili kutanua wigo katika utekelezaji wa miradi hiyo na kunufaisha wananchi wengi zaidi;

(b) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge inatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu ili kufanikisha mipango iliyowekwa katika usimamizi wa mazingira;

(c) Ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi hususan ya ufugaji Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira:

(i) Ihakikishe kabla ya kutekeleza miradi, tafiti zinafanyika ili kubaini iwapo mradi utafikia malengo yaliyotarajiwa;

(ii) Ishirikishe Wizara za kisekta katika kutekeleza miradi mahsusi ili kubaini maeneo sahihi yanayohitaji kunufaika zaidi kwa miradi hiyo;

(iii) Ishiriki ipasavyo katika hatua zote za utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kama ilivyokusudiwa; na

(iv) Ifanye ufuatiliaji wa karibu kwa kila hatua ya miradi

(d) Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iendelee kuhamasisha vijiji vingi zaidi kujihusisha na biashara ya kaboni ili manufaa yatakayopatikana katika biashara hiyo yawe chachu katika maendeleo ya vijiji husika; na

(e) Kwa dhamira ya ulinzi, uhifadhi bora wa mazingira na udhibiti wa mabadiliko ya tabianchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira iharakishe mchakato wa kufanya marekebisho makubwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kuwasilisha Miswada ya marekebisho hayo Bungeni wakati wa Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge kama ilivyoahidi wakati wa Mkutano wa Kumi na Nane wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako madhubuti. Kamati yangu inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunakuombea afya njema, maisha marefu na mafaniko katika utekelezaji wa majukumu yako. Aidha, ninamshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa moyo wa dhati kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Majina Mazingira kwa kuniamini mimi Asya Sharif Omar, Mbunge wa Viti Maalum wa Chama Cha Mapinduzi kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba, kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kwa niaba yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa katika taarifa ya Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninaomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Hamad Yussuf Masauni, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa ushirikiano katika uwasilishaji Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu, Mhandisi Cyprian Luhemeja kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, naomba nimshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Baraka Leonard, kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa

Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRAKUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS – MAZINGIRA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118(9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, Muundo wa Taarifa hii umezingatia masharti ya Kanuni ya 142 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023. Kwa msingi huo, Taarifa ninayoiwasilisha imegawanyika katika sehemu kuu tatu zifuatazo: -

(i) Sehemu ya Kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi na Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyofanya kazi;

(ii) Sehemu ya Pili inabainisha Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025

na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(iii) Sehemu ya Tatu inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Kazi ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Msingi wa Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira ni kwa mujibu wa Kifungu cha 6 (6) (b) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, Toleo la Februari, 2023. Vifungu hivyo vinaipa Kamati jukumu la kufanya uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, imeweka masharti yanayoitaka Kamati kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha unaoisha. Aidha, Masharti ya Kanuni ya 118 (4) ya Kanuni za Bunge, yanaitaka Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa Mwaka wa fedha 2024/2025 ili kulinganisha na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** Madhumuni ya Taarifa hii ni kuliwezesha Bunge kujadili Hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira aliyoiwasilisha mapema leo hii. Ili kuliwezesha Bunge kufanya kazi hiyo inavyostahili, Taarifa hii inabainisha uchambuzi katika maeneo yafuatayo:-

(i) Hatua iliyofikiwa katika uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(iii) Hali ya Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2025;
(iv) Hatua iliyofikiwa katika Utekelezaji wa mipango iliyowekwa kwa Mwaka wa fedha 2024/2025; na

(v) Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Njia iliyotumika kufanya uchambuzi inajumuisha kulinganisha hali ilivyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Njia ya ukokotoaji wa asilimia imetumika kubaini hatua inayofikiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha na kujiridhisha na uwezekano wa mipango inayolengwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa kutumia uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

**2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2024/2025**

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilijikita katika maeneo Makuu Matatu yafuatayo: -

(i) Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025;

(ii) Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo iliyoidhinishiwa fedha kwa mwaka wa fedha 2024/2025, na;

(iii) Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika**, kwa urahisi wa ufuatiliaji na uamuzi wa kibunge, naomba kubainisha matokeo ya uchambuzi kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri uliotolewa na Kamati kwa mwaka wa fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, wakati majadiliano ya Hotuba ya Bajeti ya OMRM kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, iliyosomwa tarehe 23 Aprili 2024, Kamati ilitoa Ushauri katika maeneo Kumi. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sehemu ya ushauri imefanyiwa kazi na sehemu nyingine utekelezaji unaendelea.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa Ushauri uliotekelezwa kwa sehemu ni Mchakato wa kuifanyia Marekebisho Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ili kuendana na Sera ya Taifa ya usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2021.

**Mheshimiwa Spika,** katika suala hili naomba kulikumbusha Bunge lako Tukufu kwamba, katika Mkutano wa 18, Bunge lilifanya marekebisho madogo ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 ambapo Waziri aliahidi kuwasilisha Miswada yenye marekebisho makubwa yatakayoongeza ufanisi katika usimamizi wa Mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Waziri alilieleza Bunge, na ameendelea kuihakikishia Kamati kuwa Miswada ya Marekebisho hayo itawasilishwa wakati wa Mkutano wa 19 wa Bunge. Hivyo ni matumaini ya Kamati kwamba OMRM itatekeleza ahadi ya kuwasilisha Miswada miwili itakayohusu Uchumi wa buluu na uundwaji wa mamlaka ya uhifadhi na usimamizi wa Mazingira nchini (NEMA).

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa ushauri wa Kamati unaoendelea kutekelezwa ni OMRM kuendelea kutoa elimu kuhusu uhifadhi wa Mazingira kwa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** mara zote ushauri unaotolewa Bungeni unalenga kuboresha shughuli za umma kwa maslahi ya Wananchi. Hivyo, kuzingatiwa kwa ushauri huo kunatimiza azma ya kuboresha ustawi wa Wananchi. Aidha, kwa kuchelewa

kuzingatia ushauri, hatari yake ni kutoboresha shughuli za umma kwa wakati.

### 2.2.2 Hali ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Bunge kuidhinisha Bajeti kwa ajili ya gharama za utekelezaji wa miradi ya maendeleo, Kamati ilipaswa kujiridhisha na utekelezaji wa miradi hiyo katika sekta ya mazingira. Hivyo, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kwa kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi miwili kati ya miradi kumi na sita ya Maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** miradi miwili iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati ni: -

(i) Urejeshwaji endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika; na

(ii) Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania - *Reversing Land Degradation Trends and Increasing Food Security in Degraded Ecosystems of Semi-Arid Areas of Tanzania (LDFS).*

#### (a) Mradi wa Urejeshwaji Endelevu wa Mazingira na Hifadhi ya Bayoanuai Tanzania (SLR - Project)

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Tanganyika ni miongoni mwa Halmashauri saba zinazotekeleza mradi huu. Halmashauri zingine ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mbarali, Wanging’ombe, Iringa, Sumbawanga na Mpimbwe ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kiasi cha Shilingi **6,216,803,345** kiliidhinishwa katika utekelezaji wa Mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mradi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika unaendelea ambapo kiasi cha **Shilingi**

**257,244,749.5** kilipokelewa. Aidha, shughuli zilizotekelezwa kwa fedha hizo ni pamoja na kuwezesha mashamba darasa ya malisho, uwezeshaji wa mizinga na vifaa vya ufugaji wa nyuki, ufugaji wa ng'ombe wa Maziwa, uhifadhi wa misitu na ujenzi wa Majiko banifu.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara yake ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika, Kamati ilitembelea miradi mitatu inayotekelezwa na OMRM katika Kijiji cha Kapanga ambayo ni –

(i) Mradi wa Shamba darasa la Malisho;

(ii) Mradi wa Josho, Banio na Birika la Mifugo; na

(iii) Mradi wa kikundi cha ufugaji wa ng'ombe wa Maziwa.

**(i) Mradi wa Shamba darasa la Malisho**

**Mheshimiwa Spika,** Shamba darasa lililotembelewa na Kamati lina ukubwa wa ekari 2.5 likiwa na aina tatu za malisho ambazo ni jamii ya majani (*chloris gayana*), mabingo bingo na malisho ya milukina (Leucaena *leococephala*).

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulitengewa fedha kiasi cha Shilingi **2,724,037.53** ambapo Lengo la mradi ni kuwawezesha wafugaji kuelewa umuhimu wa kuwa na malisho bora ya mifugo yanayopunguza hali ya uharibifu wa mazingira ambao husababishwa na mambo mbalimbali ikiwemo ufugaji wa kuhamahama. Hivyo, mradi umewezesha wanakijiji kupata mbegu na kuanzisha malisho yao ili kupunguza utegemezi wa malisho kwenye misitu ya hifadhi.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya Kamati kwa Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira kutanua wigo wa utekelezaji wa mradi huu ili kuwezesha wananchi wa maeneo mengi ya jamii za kifugaji kuzifunza njia sahihi za uendelezaji wa malisho hali itakayoimarisha shughuli za ufugaji na ustawi wa Mazingira.

**(ii) Mradi wa Josho, Banio na Birika la Mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulianzishwa kwa lengo la kuwa na miundombinu wezeshi kwa mifugo kupata huduma bora na rafiki kwa shughuli za ufugaji endelevu ili kuongeza tija katika shughuli za uhifadhi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu umegharimu shilingi **71,100,000** ambapo shilingi **27,000,000** zilitokana na mapato ya biashara ya hewa ukaa. Utekelezaji wa mradi huu **umefikia asilimia 90** ambapo wafugaji katika kijiji cha Kapanga na vijiji jirani wameanza kunufaika.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa mradi huu umelenga kunufaisha wafugaji katika maeneo unapotekelezwa. Hata hivyo, hali ya utekelezaji wa mradi hairidhishi kutokana na mapungufu mbalimbali yaliyobainishwa na Kamati. Mapungufu hayo ni pamoja na:

(i). Kukosekana kwa Maji katika josho na birika hali inayolazimu wafugaji wenyewe kujaza maji hayo ili kunusuru afya za mifugo yao;

(ii). Kukosekana kwa usimamizi sahihi wa fedha zinazotokana na malipo kwa matumizi ya josho; na

(iii). Kukosekana kwa mifumo ya utoaji wa maji kwenye josho baada ya kutumika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Halmashauri ya Tanganyika kwa kuchukua hatua za haraka kutatua baadhi ya changamoto zilizobainishwa ikiwemo suala la usimamizi wa fedha zinazotokana na malipo ya josho.

(iv). **Mradi wa kikundi cha ufugaji wa ng'ombe wa Maziwa.**

**Mheshimiwa Spika,** Kikundi kinachotekeleza mradi huu kimesajiliwa na Halmashauri ya Tanganyika na kina wanachama 24 wenye lengo la kujiendeleza kiuchumi kupitia ufugaji wa

ng'ombe wa maziwa. Aidha, Mradi umekiwezesha kikundi kwa jumla ya Shilingi **5,760,656** kwa ajili ya uchangiaji wa ujenzi wa banda, ununuzi wa ng'ombe wawili wa maziwa, ununuzi wa dawa na virutubisho.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada za OMRM katika kuhamasisha mapambano dhidi ya mabadiliko ya tabianchi. Hata hivyo, Kamati inaona umuhimu kwa OMRM kuandaa Mkakati wa kuwa na Miradi Mikubwa ya Mifano itakayoshirikisha Sekta mahsusi ambayo itakuwa kielelezo kwa Sekta hizo kujifunza na kuhamasika kuongeza jitihada sahihi katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo huathiri sekta mtambuka.

**b). Mradi wa Kurejesha Ardhi iliyoharibika na kuongeza Usalama wa Chakula katika maeneo kame ya Tanzania - *Reversing Land Degradation Trends and Increasing Food Security in Degraded Ecosystems of Semi-Arid Areas of Tanzania (LDFS)*.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ni miongoni mwa miradi inayotekelezwa chini ya OMRM kupitia ufadhili wa Mfuko wa Dunia wa Mazingira na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo kwa dhumuni la kurejesha na kustawisha Mifumo ya kiikolojia ili kusaidia ongezeko la hali ya uzalishaji wa chakula nchini. Mradi huu unatekelezwa katika maeneo ya Halmashauri za Wilaya za Kondoa (Dodoma), Mkalama (Singida), Nzega (Tabora), Magu (Mwanza) na Micheweni (Kaskazini Pemba).

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilitenga bajeti ya **Shilingi 405,768,416** ili kuwezesha pamoja na masuala mengine kuendelea kwa ujenzi wa –

(i). Malambo mawili (2) na ukarabati wa lambo moja (1), mabirika matatu (3) ya kunyweshea mifugo na majosho mawili (2) katika Halmashauri ya Magu;

(ii) Malambo matatu (3), bwawa moja (1), mabirika manne (4) ya kunyweshea mifugo na majosho mawili (2) katika Halmashauri ya Nzega; na

(iii). Mabwawa matatu (3) na lambo moja (1), mabirika manne (4) ya kunyweshea mifugo na majosho manne (4) katika Halmashauri ya Mkalama.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara ya Kamati Mkoani Tabora, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi wa OMRM katika Halmashauri ya Nzega ikihusisha ujenzi wa Bwawa la Maji, josho la mifugo pamoja na Kiwanda cha Asali.

**Mheshimiwa Spika,** itakumbukwa kwamba katika ziara za kukagua miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha **2023/2024**, Kamati ilitembelea mradi huu na kutoa maoni na ushauri kuhusu utekelezaji bora wa Mradi. Hivyo, katika ziara hii pamoja na kukagua utekelezaji bajeti ya Mwaka 2024/2025, Kamati iliweza kubaini jinsi ambavyo ushauri wake umezingatiwa.

**(i) Mradi wa Maji katika Kijiji cha Sigiri**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa na OMRM kwa kushirikiana na RUWASA kwa ufadhili wa *international Fund for Agricultural Development* – IFAD. Utekelezaji wa mradi ulianza tarehe 17/09/2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 29.04.2025 kwa gharama ya **shilingi 259,583,795.96**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia mwezi Machi, 2025 shughuli zilizotekelezwa katika Mradi huu ni pamoja na uchimbaji wa mitaro umbali wa mita 1300, ulazaji na uunganishaji wa mabomba, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 150,000 ambao umefikia asilimia 65, ununuzi na ufungaji wa pampu na sola zake, ujenzi wa nyumba ya mitambo, uzio na ununuzi wa pampu nne. Kwa ujumla utekelezaji wa Mradi huu umefikia **asilimia 84.67** ukiwa umegharimu kiasi cha **shilingi 87,612,286.** Aidha, kukamilika kwake kunatarajiwa kunufaisha wananchi wapatao **5,623** katika Vijiji vya Bulambuka, Lyamalagwa na Bulende.

**(ii). Mradi wa bwawa na birika la kunyweshea mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Mradi huu ulianza tarehe 06/03/2024 na ulikamilika tarehe 30/09/2024 kwa Bajeti ya **Shilingi 540,004,740.00** ambapo hadi kukamilika kwake mradi umegharimu kiasi cha **Shilingi 490,913,338.00** ambapo mkandarasi amelipwa kiasi cha **Sh.476,287,922.13.**

**Mheshimiwa Spika,** katika ujenzi wa bwawa kwa Kijiji cha Sigiri kazi zilizofanyika zinahusisha –

(a) Uchimbaji wa eneo la kukusanyia maji ya bwawa;

(b) Ujenzi wa tuta lenye urefu wa mita 250;

(c) Ujenzi wa utoro wa maji (spillway) wenye upana wa mita 31;

(d) Ujenzi wa chemba za kuingizia na kutolea maji; na

(e) Birika la kunyweshea mifugo lenye urefu mita 18.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatarajiwa kuwezesha wakazi wa maeneo yanayozunguka Bwawa kupata maji kwa matumizi mbalimbali ikiwemo Kilimo na Mifugo. Aidha, Mradi utawanufaisha wakazi wapatao 4,306 waishio katika maeneo yanayozunguka mradi.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi huu, Kamati inaona bado kuna mambo mbalimbali yanayopaswa kuzingatiwa kabla ya kukabidhiwa kwa mradi huo kwa wananchi. Mambo hayo ni Pamoja na

(a) Kuelimisha wananchi kuhusu matumizi sahihi ya bwawa; na

(b) Ujenzi wa kingo za bwawa na Upandaji wa Majani stahimilivu pembezoni mwa bwawa ili kuzuia mmomonyoko wa ardhi ambao umeanza kujitokeza.

**(iii) Ujenzi wa Josho la Kuogeshea Mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulitengewa kiasi cha **Shilingi 45,000,000.00** ambapo hadi kukamilika kwake, mradi umegharimu **Shilingi 43,038,440.90.** Mkataba wa utekelezaji wa mradi ulisainiwa tarehe 25/09/2024 na Mkandarasi alikamilisha mradi huo kwa wakati. Mradi unatarajiwa kusaidia uogeshaji wa mifugo ambayo ni ng'ombe takribani **7,532,** mbuzi **3,218,** kondoo **830** na punda **436** iliyopo Kata ya Sigiri na maeneo jirani.

**(iv) Mradi wa Nyuki**

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ulitembelewa katika mwaka wa fedha **2023/2024** na unatekelezwa kwa vikundi ambapo vimeundwa vikundi sita (6) vya ufugaji wa nyuki kutoka katika Vijiji vya Sigiri, Bulambuka, Lyamalagwa, Bulende na Iboja katika Halmashauri ya Wilaya ya Nzega vyenye wanachama 153 ambao wamepata mafunzo ya ufugaji nyuki na kuwezeshwa kuongeza thamani ya mazao hayo.

**Mheshimiwa Spika,** tangu mwaka 2023 hadi sasa, Mradi umeongeza idadi ya mizinga 300 na kuwa na jumla ya Mizinga 1,372 ili kuwezesha vikundi hivyo kuongeza uzalishaji wa zao la asali. Mathalani, msimu wa mwaka 2023/2024 vikundi viliweza kuzalisha jumla ya lita 480 za asali ambapo kiasi cha shilingi 1,881,000 kilipatikana, kadhalika msimu wa mwaka 2024/2025 vikundi vimezalisha lita 895 za asali na kupata kiasi cha fedha cha shilingi 5,066,000/=.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya manufaa hayo machache kwa wanavikundi, mradi umekumbwa na changamoto mbalimbali Ikiwemo:

(i) Hali ya Ukame ambayo imesababisha uzalishaji mdogo wa asali;

(ii) Kushamiri kwa Wadudu shambulizi kwa nyuki kama vile simba wa nyuki na sisimizi; na

(iii) Ufuatiliaji mdogo wa ukaguzi wa mizinga kwa wanavikundi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea na utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na wigo wa utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kama vile mradi wa bwawa la Sigiri na josho la mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Kutoridhishwa huku kunatokana na Kamati kuwa na matarajio makubwa kuwa OMRM itaratibu miradi ya mfano yenye kugusa wananchi wengi zaidi.

### 2.2.3 Upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji wa fedha ni hatua muhimu katika utekelezaji wa Bajeti. Aidha, uzoefu wa kiwango cha fedha kinachopatikana kwa mwaka mmoja ni muhimu katika uamuzi wa makadirio ya matumizi kwa mwaka unaofuata. Kwa mantiki hiyo, Kamati ilifanya uchambuzi wa hali ya upatikanaji wa fedha kwa bajeti ya mwaka 2024/2025. Naomba kulijulisha Bunge kuwa matokeo ya uchambuzi yameonesha mambo yafuatayo: -

#### (a) Hali ya upatikanaji wa fedha za Matumizi ya Kawaida

(i). Hadi mwezi Februari, 2025, upatikanaji wa fedha za matumizi ya Kawaida kutoka Hazina ulikuwa ni **Shilingi 680,826,000** sawa na **asilimia 76.1** kwa mishahara ya Idara ya Mazingira, **shilingi 3,662,047,702.68** sawa na **asilimia 63** kwa mishahara ya NEMC na **Shilingi 2,902,364,078.30** sawa na **asilimia 98** kwa shughuli za uendeshaji (OC). Mchanganuo zaidi unaonekana kwenye kielelezo Na. 1

**Kielelezo Na. 1: Uwiano wa Kiasi cha Fedha za Mishahara kilichotengwa na kiasi kilichopokelewa hadi februari, 2025**

| FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA ZILIZOPOKELEWA HADI FEBRUARI 2025 | | | |
|---|---|---|---|
| **Matumizi** | **Fedha iliyotengwa 2024/25** | **Fedha zilizopokelewa** | **% ya Fedha iliyopokelewa** |
| **Mishahara Idara ya Mazingira** | 895,059,000.00 | 680,826,000.00 | 76.1 |
| **Mishahara NEMC** | 5,813,516,000.00 | 3,662,047,702.68 | 63 |
| **OC** | 2,961,690,900.00 | 2,902,364,078.30 | 98 |
| **Jumla** | **9,670,265,900.00** | **7,245,237,780.98** | **75** |

***Chanzo: Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 31***

(ii). Kwa ujumla upatikanaji wa fedha za uendeshaji wa shughuli za Idara ya Mazingira na NEMC ulifikia shilingi **7,245,237,780.98** sawa na **asilimia 75** ya kiasi kilichoidhinishwa kwa ajili hiyo. Mwenendo huo unaashiria utekelezaji mzuri wa Bajeti uliotarajiwa kwa mwaka wa fedha **2024/2025** kwa fedha za matumizi ya kawaida.

### 2.2.4 Hali ya upatikanaji wa fedha za Miradi ya maendeleo

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa hali ya utekelezaji wa miradi yanaonesha mambo yafuatayo: -

(i) Ucheleweshaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo na utolewaji mdogo wa fedha za ndani. Kwa mfano hadi Februari 2025, Fedha za ndani zilizotolewa ni **Shilingi 499,000,000.00** sawa na **asilimia 17** tu ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo;

(ii) Fedha za nje kwa ajili ya Miradi ya Mazingira zimepatikana **shilingi 9,940,230,000** sawa na **asilimia 54** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kiwango hicho kimepungua kwa **asilimia 10** ililinganishwa na mwaka wa fedha

2023/2024 ambapo hadi mwezi Februari, 2024 kiwango kilichopokelewa kilikuwa ni **asilimia 64**. Baadhi ya miradi haikupokea fedha kabisa kama ilivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mfano, Mradi wa Mfano wa kujenga Ustahimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Kigoma.

(iii) Jumla ya fedha iliyopatikana kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Mazingira hadi Februari, 2025 ni **Shilingi 10,439,230,000.00** sawa na **asilimia 49** ambayo ni ndogo ikilingashwa na **asilimia 66.6** iliyopaswa kufikiwa kwa kipindi kama hicho. Hali hiyo ni dalili ya wazi kwamba upo uwezekano wa Miradi mingi ya mazingira kutokamilika kama ilivyokusudiwa kufikia Juni, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Mtiririko wa Fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo hauridhishi. Aidha, Upatikanaji wa fedha za ndani ni mdogo zaidi hali inayoashiria uwepo wa msukumo mdogo wa kifedha katika utekelezaji wa miradi ya mazingira.

**2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, ulifanyika kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka huo wa fedha. Umakini zaidi uliwekwa katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya kugharimia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo;

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Mishahara kwa Idara ya Mazingira na NEMC na uendeshaji wa shughuli zinazohusu masuala ya mazingira (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa maeneo hayo unafanyika kwa kuzingatia ahadi iliyotolewa kwa Wananchi kwenye Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 20202025.

Ahadi hiyo ilihusu Kukuza uchumi wa kisasa, fungamanishi, jumuishi na shindani kwa kuzingatia kipaumbele katika Kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira na uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

### 2.3.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 OMRM, imetengewa jumla ya Shilingi **31,359,578,000.00** kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, Shilingi **2,902,000,000** ni fedha za ndani, na Shilingi **28,457,578,000.00** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 imeongezeka kwa **Shilingi 10,151,737,000** sawa na **asilimia 47.9** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha kama inavyoonekana kwenye **Kielelezo Na. 2.**

**Kielelezo Na. 2: Ulinganisho wa Bajeti ya Fedha za Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026**

| ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Aina ya Matumizi** | **BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025** | **BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** | **Ongezeko** | **Asilimia ya Ongezeko** |
| **Fedha za ndani** | 2,902,000,000 | 2,902,000,000 | 00 | **00** |
| **Fedha za nje** | 18,305,841,000 | 28,457,578,000 | 10,151,737,000 | **55.5** |
| **Jumla** | **21,207,841,000** | **31,359,578,000** | **10,151,737,000** | **47.9** |

***Chanzo: Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 31***

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati unaonesha kuwa:-

(a) Bajeti ya Maendeleo imeongezeka kwa **asilimia 47.9** ikilinganishwa na Bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha;

(b) Bajeti ya Fedha za Nje imeongezeka kwa **shilingi 10,151,737,000** sawa na **asilimia 55.5** huku Bajeti ya ndani haikuongeza ikilinganishwa na fedha za Maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa Mwaka wa fedha 2024/2025; na

(c) Upangaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 haujazingatia ipasavyo hali ya upatikanaji wa fedha unaotokana na mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuona umuhimu wa kuongeza bajeti ya Maendeleo kwa OMRM. Ni matarajio ya Kamati kwamba Serikali itatoa fedha hizo kama zilivyopangwa na kwa wakati ili kutekeleza mpango kazi wake.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira inaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya Shilingi 12,398,023,000 ikiwa ni Fedha kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, Shilingi 1,117,037,000.00 ni fedha za Mishahara kwa Idara ya Mazingira, Shilingi 6,675,287,000 ni fedha za Mishahara kwa NEMC na Shilingi 4,605,699,000 ni fedha inayoombwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo.

**Kielelezo Na. 3: Ulinganisho wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2024 na 2025/2026**

| ULINGANISHO WA BAJETI YA MATUMIZI YA KAWAIDA FUNGU 31 KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA 2025/2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **AINA YA MATUMIZI** | **2024/2025** | **2025/2026** | **ONGEZEKO** | **ASILIMIA YA ONGEZEKO** |
| **Mishahara Idara ya Mazingira** | 895,059,000 | 1,117,037,000.00 | 221,978,000 | **24.8** |
| **Mishahara NEMC** | 5,813,516,000 | 6,675,287,000 | 861,771,000 | **14.8** |
| **OC** | 2,961,691,000 | 4,605,699,000 | 1,644,008,000 | **55.5** |
| **Jumla** | **9,670,266,000** | **12,398,023,000** | **2,727,757,000** | **28.2** |

***Chanzo. Randama ya Bajeti 2025/2026 Fungu 31***

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi katika kielelezo Na. 3 unaonesha kuwa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 imeongezeka kwa **asilimia 28.2** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa **Shilingi 9,670,266,000**. Kamati imebaini kwamba, miongoni mwa sababu zilizopelekea ongezeko hili ni kuongezeka kwa nafasi za ajira kwa Watumishi katika Sekta ya Mazingira ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Sekta hiyo.

### 2.2.3 Ulinganisho wa bajeti ya Taifa na bajeti ya OMRM

**Mheshmiwa Spika,** jumla ya fedha inayoombwa na OMRM kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni Shilingi **43,757,601,000.** Kiasi hiki ni sawa na Ongezeko la **asilimia 41.7** ya Bajeti ya Ofisi hiyo iliyoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya Taifa na Bajeti ya OMRM kwa mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia ulinganisho huo, Kamati ilibaini kuwa bajeti ya OMRM ni asilimia **0.08** ya bajeti yote ya Taifa. Hii ni sawa na ongezeko la asilimia **0.02** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo hayo kwa ujumla yanatoa taswira ya namna Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira inavyojipanga kusimamia mazingira. Aidha, Kamati ina maoni kuwa utekelezaji wa Mipango ya Serikali kuhusu masuala ya mazingira uendelee kupewa kipaumbele.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la Taarifa hii ni kubainisha maoni na ushauri wa Kamati ili kuwezesha majadiliano ya Bunge. Kamati inaamini kuwa maelezo yaliyotolewa ndani ya Taarifa hii yatakuwa na msaada muhimu kwa Bunge. Pamoja na majadiliano kuhusu hoja hii, upo umuhimu wa kuzingatia maoni na ushauri unaotolewa katika Taarifa hii kwa lengo la kuboresha shughuli zinazohusu usimamizi wa mazingira.

### 3.2 Maoni ya Kamati

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Uchambuzi wa kina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya OMRM –Fungu 31 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026, naomba kubainisha Maoni ya Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Fedha zinazotengwa kutekeleza baadhi ya miradi ya Maendeleo hazitoshi na hazikidhi dhamira ya Serikali ya kuwa na Miradi ya Kielelezo kupitia OMRMM hususan katika mapambano dhidi ya Mabadiliko ya tabianchi;

(b) Utolewaji mdogo wa fedha za ndani kwa Miradi ya Maendeleo hauoneshi msukumo wa kutosha wa Serikali katika Sekta ya Mazingira na hivyo kuchelewesha utekelezaji wa Miradi;

(c) Kutosomana kwa Mifumo ya Kiutendaji na uratibu hafifu katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo unasababisha miradi hiyo kutotekelezwa ipasavyo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa;

(d) Manufaa ya biashara ya Kaboni ni kichocheo katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo;na

(e) Marekebisho makubwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 yataongeza hamasa katika usimamizi na uhifadhi wa Mazingira Nchini.

### 3.3 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inashauri mambo yafuatayo: -

(a) Serikali itenge fedha za kutosha katika utekelezaji wa Miradi Mahsusi ya Maendeleo ili kutanua wigo katika utekelezaji wa miradi hiyo na kunufaisha wananchi wengi zaidi;

(b) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge inatolewa kwa wakati na kwa ukamilifu ili kufanikisha mipango iliyowekwa katika usimamizi wa mazingira;

(c) Ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa miradi hususan ya ufugaji OMRM-

(i) Ihakikishe kabla ya kutekeleza miradi, tafiti zinafanyika ili kubaini iwapo mradi utafikia malengo yaliyotarajiwa;

(ii) Ishirikishe Wizara za kisekta katika kutekeleza miradi mahsusi ili kubaini maeneo sahihi 0yanayohitaji kunufaika zaidi kwa miradi hiyo;

(iii) Ishiriki ipasavyo katika hatua zote za utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha miradi inatekelezwa kama ilivyokusudiwa; na

(iv) Ifanye ufuatiliaji wa karibu kwa kila hatua ya miradi

(d) OMRM iendelee kuhamasisha Vijiji vingi zaidi kujihusisha na biashara ya kaboni ili manufaa yatakayopatikana katika biashara hiyo yawe chachu katika maendeleo ya Vijiji husika; na

(e) Kwa dhamira ya ulinzi, uhifadhi bora wa mazingira na udhibiti wa mabadiliko ya tabianchi, OMRM iharakishe mchakato wa kufanya Marekebisho Makubwa katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na kuwasilisha Miswada ya marekebisho hayo Bungeni wakati wa Mkutano huu wa 19 wa Bunge kama ilivyoahidi wakati wa Mkutano wa 18 wa Bunge.

**3.4 Hitimisho**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Kamati kwa mara nyingine napenda kukupongeza tena kwa uongozi wako madhubuti. Kamati yangu inakuahidi ushirikiano wa hali ya juu na tunakuombea afya njema, Maisha marefu na mafaniko katika utekelezaji wa majukumu yako. Aidha, namshukuru na kumpongeza Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia katika kuliwezesha Bunge kutekeleza wajibu wake wa kuisimamia na kuishauri Serikali kwa ustadi wa hali ya juu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa moyo wa dhati kabisa napenda kumshukuru Mheshimiwa Jackson Kiswaga (Mb), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Majina Mazingira kwa kuniamini na kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya maoni ya Kamati kwa niaba yake.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingie kwenye kumbukumbu za Taarifa

Rasmi za Bunge kama yalivyo wasilishwa katika taarifa hii; nayo ni kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Jackson Gedion Kiswaga, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Anna Richard. Lupembe, Mb - **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Asya Sharif Omar, - **Mjumbe**
4. Mhe. Mohammed Jumah Soud, Mb - **Mjumbe**
5. Mhe. Prof. Shukrani Elisha Manya, Mb- **Mjumbe**
6. Mhe. Juma Usonge Hamad, Mb - **Mjumbe**
7. Mhe. Haji Makame Mlenge, Mb - **Mjumbe**
8. Mhe. Asya Mwadini Mohammed, Mb- **Mjumbe**
9. Mhe. Kavejuru Eliadory Felix, Mb - **Mjumbe**
10. Mhe. Regina Ndege Qwaray, Mb - **Mjumbe**
11. Mhe. Agnes Elias Hokororo, Mb - **Mjumbe**
12. Mhe. Eng. Stella Martin Manyanya, Mb- **Mjumbe**
13. Mhe. Keneth Nollo, Mb - **Mjumbe**
14. Mhe. Suleiman Omar Mohamed, Mb - **Mjumbe**
15. Mhe. Ritta Kabati Enespher, Mb - **Mjumbe**
16. Mhe. Balozi Dkt. Bashiru A. Kakurwa, Mb - **Mjumbe**
17. Mhe. Charles Mwijage, Mb - **Mjumbe**
18. Mhe. Deo Kasenyanda Sanga, Mb - **Mjumbe**
19. Mhe. Emmanuel Peter Cherehani, Mb- **Mjumbe**
20. Mhe. Robert Chacha Maboto, Mb - **Mjumbe**
21. Mhe. Kasalali Emmanuel Mageni, Mb- **Mjumbe**

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza **Mhe. Hamad Yussuf Masauni** (Mb), Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira na **Mhe. Khamis Hamza Khamis** (Mb), Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa ushirikiano katika uwasilishaji Makadirio ya Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Makamu wa Rais pamoja na taasisi zake wakiongozwa na Katibu Mkuu Mhandisi Cyprian Luhemeja kwa ushirikiano walioipatia Kamati katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho kabisa lakini si kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Baraka Leonard, kwa umakini na weledi katika kuratibu shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake bila kukwama.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Jackson G. Kiswaga, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAJI NA MAZINGIRA**
25 Aprili, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Asya Sharif Omar kwa kusoma hii taarifa ya Kamati vizuri sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunakwenda kwenye hatua ya pili hatua nyingine ya uchangiaji na yule Mwenyekiti aliyesifiwa ndiyo ataanza kutuongoza uchangiaji. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninamwita sasa Mheshimiwa Jackson Gedion Kiswaga atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, ajiandae.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi leo ili niwe mchangiaji wa kwanza kwenye hoja iliyoko mezani, hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, hoja muhimu sana, hoja nyeti inayohusu masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kabisa kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu

mpendwa kabisa, mwanamazingira namba moja, mtu anayependa mazingira. Tunamshukuru kwa sababu tumeona dhamira yake ya kweli ya kutaka kuyaboresha mazingira ya Tanzania, kwanza kwa nafasi pia aliyopewa kuwa kinara wa Afrika kwenye masuala ya nishati safi ya kupikia, lakini na zile hamasa ambazo ameendelea kuzitoa mara kwa mara kuhakikisha kwamba Taifa letu linabaki kuwa salama katika eneo la mazingira. Niwaombe tu Watanzania wenzangu tuendelee kumuunga mkono Mheshimiwa Rais kwenye ajenda ya mazingira ya kuhakikisha kwamba Taifa hili linaendelea kudumu na kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Waziri, *Engineer* Masauni pamoja na Watendaji wote walio chini yake sitataja mmoja mmoja kwa maslahi ya muda ni Waziri mgeni kwenye Wizara hii, sasa ameshaanza kuzoea, lakini tumeona ushirikiano wake na Kamati ni mzuri na tunaelewana katika kila jambo ambalo tunalipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mwenyekiti mpya wa Bodi ya *NEMC,* Mhandishi Mwanasha Tumbo, mimi kama Jackson Kiswaga na Mwenyekiti wa Kamati hii ninamwamini sana kwa maana kwa kipindi cha miaka miwili na zaidi nimefanya naye kazi kwa karibu, nimeshirikiana naye, kwa kweli ni mtu rahimu anayejua kazi yake, anayeipenda kazi yake na ninaamini hicho kiti alichopewa na Mheshimiwa Rais atakitendea kazi vizuri. Pamoja na wajumbe ambao watamsaidia kwenye hiyo bodi ikiwa ni pamoja na mpigakura wangu Wakili Msomi Ndugu yangu Alex Mgongola tunatoka Jimbo la Kalenga, mimi na yeye tuliachiana jimbo sasa ninajua huku atatumia hiyo nafasi kunishauri vizuri zaidi namna ya kuisimamia pia Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajielekeza kwenye upande wa mazingira. Kamati hii imegawanyika sehemu mbili kwa maana iko Kamati inayoangalia Muungano na ninaangalia masuala ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukianza kuzungumzia mabadiliko ya tabianchi. Mabaliko ya tabianchi ni jambo halisi, mabaliko ya tabianchi ni janga la dunia na kwa kweli sisi kama Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mazingira tunaona kwamba mabadiliko ya tabianchi ni janga la dunia na hivyo ni suala la usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijasema ni Idara ya Usalama wa Taifa ila ninasema ni suala la usalama wa Taifa kwa sababu madhara yake yanayopelekea watu kupoteza maisha ambayo tunaona katika nchi nyingine, sisi tumeona tuipe hadhi Idara ya Mazingira kama hili suala ni la usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tunasema hivyo nitawatolea mfano, mwaka jana wakati nimehudhuria mkutano mmoja kwenye wakala wa kimataifa wa nishati jadidifu pale Abu Dhabi nikaona dada mmoja analia kutoka Chad, namna gani mabadiliko ya tabianchi yalivyoathiri nchi yake na mimi baadaye nikajipa muda kwenda kwenye mitandao kuona nini kimeendelea. Nikagundua kwamba kutokana na mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira katika nchi yake miji mingi ya nchi ile joto limekuwa juu sana nikawa naangalia kwa mfano Faya-Largeau nikaona joto limefika 51%, nikaangalia pale N'Djamena nikaona nyuzi joto zimefika 50%, nikaangalia pale Moundou nikaona joto limefikia 46%, nilivyoambiwa watu wamepoteza maisha, watu wamekufa kwa wingi sikuona jambo la ajabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye taarifa kuanzia mwezi wa Saba mpaka sasa wanasema zaidi ya watu 576 wamekufa kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi ambayo yamesababisha joto sana kuongezeka, mafuriko na mambo mengine, pia mifugo zaidi ya 72,000 imekufa na watu zaidi ya milioni 1.9 wametawanyika kwa sababu ya mambo haya yanayohusiana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nilikuwa nasoma taarifa moja *BBC,* nikaona kichwa cha habari kinasema *a river died over night in Zambia after acidic waste spill at the Chinese owned mine*. Kwamba mtu umekufa kwa usiku mmoja kwa sababu ya

mtiririko wa maji machafu ambayo yametokana na kampuni moja inaitwa *Sinometals* ambayo imetiririsha maji machafu yakaenda kwenye Mto Kafue na mto huo umekufa baada ya kuonekana samaki wengi walikuwa wamekufa pembezoni ya mto huo na inaonekana madhara yake yatakwenda kwa muda mrefu na yataweza kuathiri watu wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninavyojielekeza kutoa ushauri sisi kama Kamati tunatamani sana suala la mazingira, kwa hii mifano miwili ambayo imetolewa kwamba lichukuliwe kwamba ni suala muhimu lenye maslahi makubwa ya kitaifa, lenye maslahi makubwa ya umma. Ndiyo maana ushauri wetu umekuwa yakijielekeza kwamba kuundwa kwa hiki chombo cha mamlaka ya usimamizi wa mazingira ambacho Mheshimiwa Waziri ameridhia kwamba kitaundwa. Kamati tutaendelea kusisitiza kwamba jambo hilo litokee kwa sababu haya mambo ambayo yametokea Zambia ni kwa sababu pengine ya usimamizi mdogo ambao hauleti ukaguzi wa mara kwa mara kwenye migodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia katika nchi yetu migodi mingi sana inazaliwa kila siku, hawa wenzetu ambao wametajwa hapa walisema *Chinese owned company,* wanaingia kwa wingi sana na wanapewa kuchimba maeneo mengi, sasa tusipokuwa na usimamizi madhubuti nchi hii tutaingia kwenye matatizo ambayo baadaye tutakwenda kuangamiza maisha ya watu ndiyo maana tumesema suala la mazingira, tumelipa hadhi ya usalama wa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisikia taarifa inayohusiana na mazingira siku hizi na mimi ninaonekana kama nimekuwa mwanamazingira huwa natetemeka kidogo. Siku moja kwenye *ITV* nikaona pale Chunya inaonekana wananchi wanalalamika kwamba kuna uchimbaji unaendelea kwenye mto, lakini pia *NEMC* walitoa maagizo ambayo inaonekana hayakuzingatiwa. Ndiyo maana tutasema kwamba tunataka chombo hiki kiwe na mamlaka makubwa kiwe na meno ili kwamba masuala ya mazingira yasichukuliwe mchezo mchezo kwenye nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Mwenyezi Mungu katika kuumba Dunia alisema iwe nuru ikawa nuru. Maana yake sisi tutaendelea kutamka mpaka iwe, mpaka itakavyokuwa. Sasa leo nitakuwa tu na ushauri mdogo kwenye mambo ya mazingira, lakini kabla sijaingia kwenye ushauri niipongeze Wizara, kwa miradi mingi ambayo wanaitekeleza miradi mbalimbali ya kimazingira. Hata kwenye Jimbo langu kule la Kalenga wamegusa kidogo, kwa maana wamejenga vitalu nyumba pale, wamepeleka ng'ombe wa maziwa, wameboresha skimu, wameweka shamba darasa, hii ni miradi ambayo wanaifanya nchi nzima, ni *initiative* nzuri sana ninawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu sasa ni *initiatives* hizi nzuri, ni ubunifu mzuri, lakini tunataka uwe nguzo kwa jamii, kwamba ukimpelekea mtu ng'ombe basi angalau uanzie watano hivi kwenye kikundi. Ukiweka shamba darasa, angalau kashamba kawe kakubwakubwa ambako tunaweza kuanza kusema matokeo yake ni haya, ambayo tunaweza kuyaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwenye ushauri, nitashauri sawasawa na Mwongozo wa Katiba hii. Katiba hii katika Ibara ya 63(2) kinasema, "Sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambacho kitakuwa na Madaraka kwa niaba ya wananchi kusimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Sheria. Kwa hiyo, mambo tunayofanya hapa, hata kama ni ushauri mdogo, tunafanya kwa mujibu wa Katiba. Ushauri huu ni vizuri ukawa unazingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nikianza kwenye suala la *carbon*. Kwanza nimpongeze sana Profesa Dhahabu Eliakimu anafanya kazi nzuri na mimi hivi karibuni nilimtumia watu wangu pale na baadaye nikawa ninafuatilia matokeo ni namna gani walipokelewa na nini; wakanipa *feedback* wamepokelewa vizuri na wameelekezwa. Kwa hiyo, ninafurahi kwamba, tuna watu ambao ni makini, wanafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye eneo hili ni kwamba, sisi kwenye kituo cha *carbon* tuwe na kanzidata ya maeneo ambayo tunaweza kuwaelekeza wawekezaji kwenda kuwekeza. Mwekezaji akija nchini, akisema anataka kuwekeza katika eneo la *carbon,* kituo kiwe na maeneo ambayo kimeyaainisha. Kwa nini ninasema hivyo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2012 nilihudhuria kikao kimoja cha *USAID,* alikuja Mkuu wa *USAID* Duniani, Rajiv Shah, pale katika ubalozi wa Marekani walikuwa wanatoa fedha, kwa ajili ya kuendeleza wakulima katika ushoroba wa Kusini, *(SAGOT) Southern Agriculture Growth Corridor.* Sasa akawa analalamika kwamba wanatoa fedha, lakini hawapati maeneo. Sasa tuna changamoto ya maeneo katika nchi hii, wawekezaji wengi wakija hawapati maeneo, sisi twende tukawekeze katika maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwenye ushauri, ninaomba tuone ni namna gani tunaweza tukaweka tozo kidogo kwenye viwanda kwa sababu, viwanda vinazalisha joto. Zile tozo kidogo ziende kusimamia masuala yanayohusu mazingira, lakini ninaona kengele imenisimamisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mengi, nitamwandikia Waziri, lakini la mwisho kwenye fedha zile za mazingira za wafadhili ambazo tunazipata tuone ni namna gani tunaweza kuzipeleka kuchimba visima kwenye shule kwa sababu, tunasema soma na mti, panda mti, ili yale maji yanayopatikana pale yaweze kuleta usafi, lakini iwe kupanda miti na kutunza mazingira. Zaidi ya yote ninaendelea tena kumshukuru Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri na Wizara yake yote kwa mambo mazuri waliyofanya, kwa ajili ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiswaga ahsante sana. Sasa nimwite Mheshimiwa Ali Hassan Omar King.

**MHE. ALI HASSAN OMAR KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia siku ya leo kusimama hapa tukiwa wazima, ili kuweza kuzungumza mambo yenye maslahi kwa Tanzania yetu na kwa upande wangu mimi kuzungumzia Muungano wetu. Mara nyingi sana katika jambo la Muungano watakaokuwa wanazungumzia hoja za Muungano au labda changamoto ni wale ambao ni wadogo na ndiyo maana siyo wengi, kati ya Wabunge wa Tanzania Bara, kuwasikia wanazungumzia changamoto za Muungano, lakini wale wa kutoka Zanzibar mara nyingi utawasikia ndiyo wanazungumzia changamoto na hiyo ni *nature*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mmoja Mtume Daudi aliendewa na watu wawili, wakishtakiana. Mmoja alisema, *innahadha akhii lahu tis un wa tis unna naja Waliya najatun Wahida faa kaala fil liha wa'azani filkitab*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimwendea watu wawili, mmoja anamlalamikia mwenzake kwamba, mimi nina kondoo mmoja, mwenzangu ana kondoo 99, ameniambia tuchanganye na amenishinda kwa hoja. Kwa maana hiyo, lazima wale wachache ndiyo watakuwa wanaongea changamoto, ila kwa upande wangu, leo sitoongelea changamoto, nitaongelea fursa ambazo zipo katika Muungano badala ya changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaungana, Zanzibar *geographical area* yake ilikuwa ni ileile, 2,654 *square kilometers* na Tanzania Bara ilikuwa ni 945,000, haijaongezeka. Ile kule Zanzibar inaliwa na maji inapungua, lakini *population* ya Zanzibar wakati ule ni 312,000 na *population* ya Tanzania Bara ni milioni 12. Sasa ninachotaka kuzungumza ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *population* ya Zanzibar ni 1,800,000 na *population* ya Tanzania Bara ni takribani milioni 60 au tunaweza tukasema ni milioni 59 *point something*. Maana yangu ni kwamba, katika Muungano huu wazee wetu walivyokaa walizungumzia mambo yenye maslahi katika muundo au Muungano huu. Katika mambo hayo ambayo walisema vizingatiwe vitu vitatu, ninataja viwili katika hivyo vitatu na hii

nimenukuu kutokana na mjadala wa kongamano la juzi ambalo alikuwepo Dkt. Mwakyembe akieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimoja ni kwamba, *autonomy* ya Zanzibar iendelee kuwepo, lakini cha pili ni waangalie *geographical and demographical factors* ambazo zipo kwenye *demographical* na kwenye *population*. Sasa hivi *population growth rate* ya Zanzibar ni 3.8% ina maana kwamba, tukitoka sasa hivi milioni 1,800,000 baada ya miaka 10 tunakwenda milioni mbili, kwa maana hiyo *square meter* ambazo atakuwa anakaa Mzanzibari mmoja zitazidi kupungua. Kwa hiyo, fursa ya ardhi ya Zanzibar, kwa ajili ya uchumi itakuwa imepungua kutokana na ardhi na makazi yatakavyoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikizungumza hivi, wale walioishi Mjini Zanzibar wanajua, mashamba yalianza Mwanakwerekwe kwenda mbele, unakuta vijiji ni vichache, lakini sasa hivi mashamba yako huko mbele. Ulikuwa ukifika kwa Mzee wetu Thabit Kombo, Mwenyezi Mungu amrehemu, ndiyo nyumba ya mwisho. Kutoka Mwanakwerekwe kote kule ilikuwa ni ardhi ya kilimo na tunajua wapi kuna mikarafuu, wapi kuna matufaa, wapi kuna mipera. Sasa ile ardhi inasogea mbele huko. Ina maana kwamba, ardhi ya Zanzibar inaenda kwisha. Maana yangu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliposema kwamba, kuzingatia *autonomy* ya Zanzibar, hasa kiuchumi, nina maana tukienda katika eneo la Bahari Kuu. Ndiyo maana nikasema tuzungumzie fursa ya kiuchumi ya Zanzibar kwenye Bahari kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali ianze kufanya utafiti kuiangalia Zanzibar sasa kwa kuwa, ardhi itakuwa kiuchumi imekaliwa. Ina maana, maeneo ya Bahari kuu Zanzibar yaweze kupewa fursa kiuchumi, ili yaweze kujiendeleza, kwa ajili ya uvuvi kwa sababu, tutakuwa huku hakuna tena fursa hiyo ya kukaa katika ardhi na kufanya maendeleo na uchumi katika ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha pili ni kwamba, Zanzibar ilianzisha jambo linaitwa Bandari Huru, lilishindikana kwa sababu, tuli-*harmonize tax*. *Tax* za pamoja zilishindikana ku-*operate*

bandari huru. Ni wakati sasa tuangalie fursa hii, kwa ajili ya *autonomy* ya Zanzibar asiombeombe sana kuangalia kwamba, kufanya awe na bandari kuu kwa kuangalia au kwa kufanya *de-harmonization* ya zile *tax* ambazo tunahisi, hizi zinaweza zikazuia *autonomy* ya Zanzibar katika uchumi na kujiendesha yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ni, Zanzibar inajitahidi kujenga bandari, lakini kama ikianzisha fursa ya *trans treatment,* meli kubwa zikaleta mizigo Zanzibar, halafu meli ndogondogo zikaja zikabeba mzigo pale, zikasambaza katika nchi nyingine pia, biashara hiyo Zanzibar inaweza ikatusaidia kwa sababu, tutakuwa tumekosa ardhi. Kwa hiyo, ninaishauri Serikali kuhusu hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna jambo jingine ambalo nilikuwa ninataka niliseme. Mheshimiwa Waziri alizungumza katika Ukurasa wa 23 na 24, pale alitaja gawio *(dividend)* ambalo linapokewa kutoka *BOT* ni 4.5%. Pia, kumezungumziwa *GBS,* nayo ni 4.5%; mimi ninajiuliza *logic* ya 4.5% kwa sababu, mchango wa Zanzibar katika kuanzisha Benki Kuu ni 20%. *Why* kwenye manufaa anapata 4.5%?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusijaribu kuangalia kile kinachostahili kwa sababu, mtu ukiwa kama ni *shareholder* wa kitu, kama ulichangia 20% na manufaa unapata kwa 20%. Ninaiomba Serikali ijaribu kuangalia katika eneo hili, ili kutafiti, kuweza kuona kwamba, hii 4.5% haijawa *arrived* kutokana na *shareholding* katika kuanzisha hii benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine nikija katika *GBS (General Budget Support),* ambayo tunapata tunasema kwamba, ni mikopo na misaada ya kibajeti, ambayo inakuja. Ukiangalia *documents* zote za Serikali katika Wizara ya Fedha, ukitazama kwamba, *finance gape* ndiyo tunaenda kukopa na kuomba msaada, lakini inapofikiwa hiyo *finance gap,* wakishapata huo msaada, ambao *base* ni *finance gap,* ukifika huku Zanzibar anapata 4.5%. Kwa nini, hatuitazami na *finance gap* ya Zanzibar? Kwamba, Zanzibar ameshindwa kwenye *gap* hili hapa na lile likaunganishwa pale?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kile kitakachopatikana ni kutokana na *finance gap*. Kama *base* ya kuombea mkopo na msaada ni *finance gap,* kwa nini tusichukue ile *finance gap* tunakuja katika 4.5%? Kwa hiyo, ninashauri tujaribu kuli-*review* hili kwa sababu, lina fursa. Kama tunatengeneza *document* zetu kwa kuangalia *finance gape, why* tunarudi katika *4.5%?* Kwamba, hiki ndicho kigezo chenyewe kilichopo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, ninakuja katika Mfuko wa Jimbo. Kuna kitu ambacho hata mimi nilitaka kususia Mfuko wa Jimbo kwa sababu, sote tulipigwa *flat*. Wewe unaongezwa sita na wewe sita, hakuna hesabu za kufanya hata ukapatikana ule Mfuko wa Jimbo? Yaani kila mmoja alichoongezewa ni sawa na jimbo la mwenzake!

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu humu tukikaa, tukisema jimbo fulani linapewa shilingi milioni 500, huwezi kusikia jimbo la Zanzibar kwamba, litapewa shilingi milioni 500 kwa barabara, wala huwezi kusikia kwamba, litapewa shilingi milioni 500 au 200 kwa maji, unapewa uleule Mfuko wa Jimbo. Basi katika huu Mfuko wa Jimbo, kwa ajili ya Zanzibar tungejaribu kuangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna siku nilizungumza na Waziri, pesa ambazo tuliongezewa ilikuwa ni sawasawa na *Turhani*. *Turhani* ni nazi ambazo ukishahesabiwa 100 unapewa mbili, zinachukuliwa zozote, unaambiwa haya na hizo mbili. Kwa hiyo, Mfuko wa Jimbo kuongezewa kama nazi za *turhani*, hiki kitu siyo kizuri. Tujaribu kuangalia fursa wanazopata Wabunge wenzetu wa Tanzania Bara, leo kila mmoja anakwenda zake anajisemea, kwa ajili ya maendeleo. Mbunge wa Zanzibar ni Mwakilishi tu kuzungumza kero za Muungano, kama ninavyozungumza mimi, lakini kimaendeleo bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujaribu kuangalia. Yule Mbunge kule Zanzibar anafanya nini jimboni? Kwa sababu, ipo hiyo *factor* kwamba, ni kuangalia. Kwa mfano, kwenye chama nyote mnapimwa kwa ufanisi. Unaendaje kumpima mtu ufanisi kwa shilingi milioni 24? Anafanya ufanisi gani? Bila shaka atakuwa

anatoa fedha zake za mfukoni ambazo ndizo zimfanye yeye kwamba, amefanya, kwa sababu, unatazamwa utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapohapo, hiyo shilingi milioni 24 unapewa, lakini pia na ukaguzi bado unakuja. Ninajaribu kuangalia muungano, sioni kama kuna changamoto, ila kwenye muungano kuna fursa na ili twende vizuri tujaribu kuziangalia hizi fursa, lakini kubwa tuangalie ardhi ya Zanzibar, sasa hivi inaenda kutoweka kwa hiyo, vitu gani tutumie kiuchumi. Kiuchumi, ile *autonomy* waliyoiona wazee wetu kwamba, ibakie katika kuangalia sura ipi ya Muungano na *shape* ipi, iwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tujaribu kuangalia, hili ni jambo muhimu, ninaishauri Wizara ikae na wataalam. Sisi Wabunge kazi yetu tunasema ni kushauri, lakini kitaalam tukaangalie fursa zipi tunaweza tukaibakisha Zanzibar ikawa na *autonomy* yake kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Omar King, ahsante sana.

Waheshimiwa Wabunge tuna wageni ambao wameingia baada ya kuanza majadiliano au uchangiaji:-

Nina wageni 30 wa Mheshimiwa Spika. Hawa ni Wanafunzi wa Chuo cha Maendeleo ya Uongozi wa Elimu *(ADEM),* Kampasi ya Mbeya, tuwaone, karibuni sana.

Wapo vilevile wageni wa Waheshimiwa Wabunge; tuna wageni 120 wa Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Hawa ni Wakurugenzi wa Wizara pamoja na Wakuu wa Idara mbalimbali, kuna Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM Taifa *(NEC)* kutoka mikoa mbalimbali nchini na kuna wapigakura wake kutoka Wilaya za Mjini Amani Zanzibar, wakiongozwa na Madiwani wa Jimbo la Kikwajuni, Mheshimiwa Mbarouk Said

Hanga na Mheshimiwa Ibrahim Hamisi Ngassa. Wako pale. *(Makofi)*

Tuna wageni tisa wa Mheshimiwa Antony Peter Mavunde, Waziri wa Madini, ambao ni Wasanii wa Muziki wa Bongo Fleva kutoka Dar es Salaam, tuwaone mlipo. Kazi yenu inathaminiwa sana, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni 26 wa Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama, Mwenyekiti wa Bunge. Hawa ni Wadau wa Jukwaa la Sera kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania, wako pale, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 35 wa Mheshimiwa Dkt. Thea Medard Ntara, ambao ni wanachama wa *Empowerment Bridge Initiative* kutoka Mjini Dodoma, wako pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna mgeni wa Mheshimiwa Anatropia Theonest, huyu ni Ndugu Emmanuel Likuda, Mkurugenzi wa *Geo Plant Tanzania,* mwandaaji wa tuzo za mazingira; hebu tumwone, yuko pale. Karibu sana.

Waheshimiwa Wabunge, tuna wageni 30 wa Wabunge waliotutembelea, kwa ajili ya mafunzo; hawa ni Wanamichezo wa Kunduchi *Veterans Sports Club* kutoka Dar es Salaam, ambao watacheza mechi ya kirafiki na Timu ya Mpira wa Miguu ya Bunge, kesho tarehe 26 *April,* 2025, Mjini Dodoma, tuwaone. Wajiandae kufungwa, karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Wanachama 12 wa Shirika la Wanautalii Tanzania kutoka Jijini Dar es Salaam, wako pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tuna Walimu 13 wa Shule ya Sekondari Lwahira kutoka Kidatu, Mkoani Morogoro, wako pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaendelea na uchangiaji. Sasa ninamwita Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, atafuatiwa na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad na Mheshimiwa Ally Juma Mohammed ajiandae.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuwa mchangiaji. Awali ya yote nitumie fursa hii kuwashukuru sana Marais wetu kwa kuwa vinara wakubwa wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Ujenzi wa miundombinu yetu hii mikubwa tunayojenga, kwa wakati tulionao, inahitaji kuzingatia sana athari za mabadiliko ya tabianchi na mazingira yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza hivi kwa sababu, wakati mwingine tuna uwezo wa kwenda kujenga barabara za vumbi katika maeneo hatarishi. Barabara zile wakati mvua inaponyesha mara moja, barabara za vumbi na kokoto zinasombwa na maji ya mvua, kitu ambacho kinakuwa ni kazi mara mbili, lakini katika hili kwa dhati ya moyo wangu ninamshukuru sana Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakapokwenda Zanzibar, kule kwenye maeneo korofi, katika ujenzi wa miundombinu ya barabara maeneo ambayo ikinyesha mvua yalikuwa hayapitiki, sasa hivi ukienda sehemu zote zile zimejengwa madaraja, ambayo yatakuwa yanaruhusu maji ya mvua kupita na harakati za kiuchumi kuruhusiwa kufanyika wakati wa jua na wakati wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ukienda sehemu zote zile zimejengwa madaraja ambayo yatakuwa yanaruhusu maji ya mvua kupita na harakati za kiuchumi kuruhusiwa kufanyika wakati wa jua na wakati wa mvua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbuka jimboni kwangu Nungwi kule tangu nazaliwa mpaka miaka ya hivi karibuni, miaka mitatu hii, barabara zetu, licha ya kwamba jimbo lile linategemewa kwa kiasi kikubwa kutokana na harakati za uchumi wa bluu, lakini asilimia kubwa ya barabara za wakati ule zilizokuwepo ni barabara zilizokuwa zimejengwa kwa vumbi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Rais msikivu na anaelewa umuhimu na athari za mabadiliko ya tabia nchi, 90% ya barabara za Jimbo la Nungwi zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Imefanyika hivi tu ili kuweza kuruhusu harakati za kiuchumi zifanyike hata wakati wa jua na wakati wa mvua, nashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niseme kitu kimoja. Kwa kawaida mwanadamu ana tabia ya kuishi kwa mazoea lakini mazoea ya kimazingira hayajawahi kumzoea mwanadamu, na ndiyo maana tunasema ni vizuri binadamu tuishi kulingana na mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuondoka hapa tulipo na kutufikisha pale tunapohitajika, chombo pekee ambacho kinaweza kutuvusha ni elimu sahihi juu ya mazingira na mabadiliko ya mazingira yenyewe. Hizi tabia za kwenda kulima kwa kuanza kuandaa shamba kwa kuchoma moto misitu, kwa wakati huu siyo kitu kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi tabia za kwenda kulima katika maeneo ya milima na baadaye mvua zinaponyesha kunatokea maporomoko ya udongo na kuondoa ule uoto wa asili, siyo kitu kizuri. Hizi tabia za kuvua kwa kutumia uvuvi usiofuata sheria, kiukweli kabisa siyo kitu kizuri. Pia hizi tabia za kwenda kukata miamba ya mawe kwa ajili ya ujenzi siyo kitu kizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi zote nilizozisema ndizo harakati halisi za kiuchumi za wananchi wetu wenye kipato cha chini zinazowapatia kipato chao cha kuendeleza harakati za maisha. Tutakapoweza kuzizuia hizi, ni vizuri tukatafuta mbadala wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, njia pekee itakayotusababisha tufikie malengo ni lazima Wizara iandae utaratibu maalum na endelevu wa kuwapatia elimu na kuwaelimisha wananchi juu ya matumizi mabaya ya rasilimali hizi zilizotuzunguka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumejaaliwa kuwa na vyanzo vingi mno vya mapato hususan kupitia Uchumi wa Bluu. Imejaliwa kuwa na mito mingi, tumejaliwa kuwa na maziwa mengi, tumejaliwa kuwa na Bahari; lakini uvuvi wetu tunaoutumia umekuwa ukituondolea manufaa ambayo tulitarajiwa kuyapata

kwa sababu uvuvi huu siyo rasmi na hivyo umesababisha kuharibika kwa masalia mengi ya samaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunavyozungumza inaonekana wazi kwamba, mabadiliko ya tabianchi yameweza kuathiri hadi usalama wa chakula. Kama tungekuwa na utaratibu mzuri wa kuhifadhi na kutunza mazingira yetu ya bahari, basi hata kama tusingepata mavuno mazuri kwenye kilimo tungeweza kupata mavuno mazuri na uvuvi pia na maisha baadaye yakaendelea mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imebadilisha sheria za mazingira na kuweka sheria za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, ni jambo zuri. Vilevile Serikali sasa hivi imeweka sheria za namna bora ya kukabiliana na kusimamia biashara ya kaboni, na kuna baadhi ya halmashauri tayari zimeshaanza kunufaika na miradi hiyo, vilevile ni jambo zuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo bado Serikali haijakamilisha mchakato wa sheria ya kubadilisha au itakayokwenda kusimamia mahususi kuhusiana na Uchumi wa Bluu, na ndiko ambako athari kubwa za mabadiliko ya tabia nchi zinatokea katika yale maeneo yaliyopitiwa na hizi fukwe. Kitendo cha kuendelea kuchelewesha hizi sheria kinasababisha au kinatusababishia sisi wananchi kuendelea kushindwa kudhibiti na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi hususan katika maeneo yaliyopitiwa na hizi biashara za utalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, mimi ningesisitiza vitu viwili lazima tuvizingatie. Kwanza, usimamizi na udhibiti wa mazingira; pili, uhifadhi wa mazingira yenyewe. Tunapozungumzia suala la usimamizi na udhibiti, hapa ni vizuri sana tukawa makini na biashara ya chuma chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya chuma chakavu sasa hivi imeanza kuingilia miundombinu yetu tuliyoijenga kwa gharama kubwa mno. Miezi michache iliyopita; na katika hili Serikali lazima niishukuru sana na niipongeze, kwani kulikuwa na

utaratibu wa baadhi ya wananchi kuvamia miundombinu yetu ya *SGR* lakini kwa sasa hivi tayari wameshaweza kudhibitiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kipindi hapa Mheshimiwa Naibu Waziri alikuja akazungumza kwa masikitiko makubwa, kwamba baadhi ya wananchi wasiolitakia mema Taifa hili wamekuwa na utaratibu wa kuchukua waya na kuharibu zile transfoma. Sisi tunafanya utaratibu wa kuongeza kasi ya umeme, lakini Watanzania wenzetu wanahujumu miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati lengo la biashara ya chuma chakavu ni kukitoa chuma chakavu katika mazingira na kukileta katika biashara yenye tija kiuchumi, sasa badala ya kutumika utaratibu ule wa kuhifadhi mazingira sasa hivi imekuwa ikitumika kama ni sehemu ya kuharibu miundombinu yetu tuliyokuwanayo.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha.

**MHE. SIMAI HASSAN SADIKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, nimwite Mheshimiwa Juma Usonge Hamad.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii nami niweze kusimama na pia kuwa miongoni mwa wale wachangiaji wa Wizara hii ya Muungano na Mazingira. Kipekee namshukuru sana na pia nimponge Mheshimiwa Waziri Hamad Masauni kwa uwasilishaji mzuri wa taarifa yake pamoja na Kamati zote zile mbili ambazo leo zimewasilisha taarifa hapa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe historia ndogo fupi sana ya namna gani Mheshimiwa Rais ndani ya miaka hii minne tangu ashike kijiti alivyoibadilisha nchi yetu ya Tanzania kwenye maono na fikra.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alipoingia madarakani, wengi walishangaa kwamba huyu mama ataweza kweli? Lakini amefanya mambo pasi na kufikiria kama huyu anaweza akafanya zaidi ya vile ambavyo watu wanavyomfikiria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Rais, hususan kwenye masuala ya uimarishaji miundombinu ya barabara pamoja na reli. Tunafahamu Mheshimiwa Rais aliposhika nchi hii kuna miradi mingi ya kielelezo ambayo mtangulizi wake aliiacha; Mheshimiwa Rais hakuiacha na badala yake akaiendeleza na amemaliza na ameendelea zaidi katika kuyafanya makubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Rais amekuta vipo baadhi ya viwanja vya ndege havijamaliziwa. Mheshimiwa Rais naye alipambana binafsi kuhakikisha kwamba viwanja vya ndege vyote vinakamilika na anaongeza vingine vya ziada zaidi pamoja na ununuzi wa ndege za kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunampongeza sana Mheshimiwa Rais, kwani amepambana sana vya kutosha kuhakikisha kwamba nchi hii inasonga mbele hususan kwenye huduma za afya. Tumeshuhudia hospitali nyingi, vituo vya afya kila kijiji, kila kata, kila mkoa na kila maeneo Mheshimiwa Rais ameweka alama. Pia tumeshuhudia Mheshimiwa Rais ujenzi wa madarasa kila kata, kila kijiji Mheshimiwa Rais amehakikisha ameweka darasa ili kumkomboa mtoto wa Kitanzania asitembee masafa marefu aweze kupata elimu. Hayo yote ni maono thabiti ya Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha kwamba nchi hii inasonga mbele, na kwamba inasonga mbele kimaendeleo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa kuwa msikivu na pia kwa kuwa mama ambaye anajali; anaposhauriwa anakubali kushaurika. Miaka ya nyuma tumeshuhudia Wizara kutokutengewa fedha, fedha nyingi zinategemewa kutoka kwa wadau na wahisani mbalimbali. Mheshimiwa Rais mwaka huu tumeshuhudia kwa mara ya kwanza Wizara hii ya Muungano inatengewa fedha za ndani, tena ni

nyingi kuliko hata hizo fedha fedha za nje ambazo tulizitegemea miaka yote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Rais, kwenye maeneo haya tayari Wizara hii imeshaonesha miradi gani itakayotekelezwa ukilinganisha na kipindi cha nyuma. Maoni yangu, kama Kamati iivyoshauri hapa, fedha zinazotengwa kwa ajili ya hii miradi kweli hazitoshi, lakini naomba sana Wizara kupitia Mheshimiwa Masauni, namfahamu ni msikivu, na ni Waziri ambaye ni mchapakazi mzuri; fedha hazitoshi, lakini tuhakikishe kabisa miradi tunayokwenda kuitekeleza ni lazima iwe na tija, pia iwe na dira na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia miradi mingi ambayo imetekelezwa, hususan hii ya mazingira, inakuwa ni midogo midogo sana. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, fedha hizi ambazo tayari tunazitenga, za ndani kabisa, twende tuhakikishe kabisa kwamba tunatengeneza miradi mikubwa yenye tija pia itakayoleta manufaa kwa Taifa kiuchumi na zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye maoni yangu ya pili. Utoaji wa fedha unakuwa ni mdogo sana. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, fedha tunapozitoa kwa ajili ya kutekeleza miradi, basi ziende kwa ajili ya kunufaisha hususan wananchi ambao tayari wako kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, miezi ya nyuma hivi iliyopita tulitembelea miradi tofauti tofauti kwenye maeneo mbalimbali. Tumeona kuna miradi midogo midogo kiasi kwamba utashangaa kwamba ni kwa nini fedha nyingi zinaelekezwa huku, lakini tunafanya miradi midogo midogo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, tunapokwenda kutekeleza miradi hii, hata kama ni fedha ndogo, lakini tutengeneze mradi ambao utaleta tija, na utaweza kusaidia wananchi kiujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, kwa kuwa Wizara hii ni Wizara ya Muungano, na fedha hizi hizi pia zinategemewa kwa upande wa pili wa Zanzibar, miradi mingi inayoibuliwa Zanzibar nashangaa sijui hata hii baadhi ya miradi inakuwa inatoka wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwamba miradi inayoibuliwa Zanzibar ni lazima tuiangalie kwa upande mwingine wa kipekee zaidi. Ipo baadhi ya miradi inayoibuliwa hapa, inazungumzwa. Kwa mfano, kama mabadiliko ya tabianchi, Zanzibar ni kisiwa na hivyo ni lazima kiangaliwe kwa upekee wake; na fedha zinapoenda, lazima zielekezwe kwenye maeneo hususan yanayoharibika na mabadiliko ya tabianchi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juma muda wako umeisha.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie sekunde moja.

**MWENYEKITI:** Haya, hitimisha.

**MHE. JUMA USONGE HAMAD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri tukimaliza bajeti hii hebu apite pale Chaani, kuna kijiji changu kinaitwa Ketwa, twende akakiangalie. Kila zikinyesha mvua miaka yote, mabadiliko ya tabianchi yanakwenda kuathiri na wananchi wanahama kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hoja, nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nimwite Mheshimiwa Ali Juma Mohamed.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nami napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia kufika siku ya leo na pia kunipa fursa hii ya kuweza kutoa

mchango wangu katika Bajeti hii muhimu ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanza, napenda niwapongeze Marais wetu, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mama yetu Samia Suluhu Hassan na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Nawapongeza kwa sababu wamesimama kidete katika kulinda na kuhifadhi Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kesho tarehe 26 tukijaliwa Muungano wetu unatimiza miaka 61 tangu uasisiwe. Pia napenda nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu ya Rais, Muungano na Mazingira kaka yangu Hamad Yussuf Masauni kwa namna bora anavyosimamia Wizara hii muhimu katika Taifa letu, Wizara ambayo inahusiana na masuala ya Muungano pamoja na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Naibu Waziri wa Wizara hii ndugu yangu Khamis Hamza Khamis kwa namna bora na umahiri wake anaposimama Bungeni hapa, anapojibu maswali ya Wabunge na kutatua shida mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu tangu awe kwenye Wizara hii, tumeona mabadiliko makubwa kuhusiana na mambo mbalimbali hususan changamoto zile ambazo tulikuwa tukiziona kupitia Wizara hii muhimu ya Muungano. Kazi hii nzuri ambayo anaifanya Mheshimiwa Waziri nafikiri hata ndugu zetu wa Jimbo la Kikwajuni watafikiria vizuri zaidi namna gani waweze kumwongezea tena fursa ya kuweza kuliongoza tena Jimbo la Kikwajuni akiwa kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda nipongeze vyombo vyetu vya ulinzi na usalama. Licha ya kuwa na majukumu mbalimbali ya ulinzi, pia vimesimama kidete katika kulinda Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze mchango wangu kwa kuipongeza Serikali kwa namna ambavyo sasa tunaona kuna ushirikiano mzuri kati ya taasisi zile za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na taasisi za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi siyo kirefu sana tuliwahi kutoa ushauri kupitia Wizara ya Mambo ya Ndani, na kama Mheshimiwa Waziri atakumbuka, wakati huo alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani; tulitoa ushauri baada ya kupata malalamiko kupitia Jeshi letu la Zimamoto na Uokozi kuwa na uhaba wa wataalam wa masuala ya uzamiaji na uokoaji katika matukio mbalimbali ambayo yanatokea kwenye maji, kwa maana ya bahari pamoja na maziwa yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoa ushauri kuwa Serikali badala ya kutumia gharama kubwa kwenda kuwapeleka maafisa wetu hapa na pengine nje ya nchi; Kwa kule Zanzibar huwa kuna kikosi maalum kinaitwa KMKM, ni wabobezi katika masuala haya ya uokozi na uzamiaji katika masuala ya maji na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri huu ulipokelewa vizuri na Jeshi la Zimamoto na Uokozi, lilipeleka vijana wake kule Zanzibar kwa kuweza kupata mafunzo na wakahitimu na hivi sasa jeshi letu limeongeza idadi kubwa ya wataalam wanaoweza kufanya kazi zao hasa panapotokea majanga katika maeneo ya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa jambo hili kwa sababu limeendelea kuonesha ushauri ambao unatolewa na Waheshimiwa Wabunge unapokelewa na unafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, niendelee kuipongeza Serikali, kwani hivi sasa tumeshuhudia mara kwa mara kila panapotokea fursa za ajira, tumeona ule uwiano wa nafasi za ajira katika taasisi za Muungano umekuwa ukiimarika. Zinapotokea ajira, basi huwa zinaangalia maeneo yote mawili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli hili limekuwa likifurahiwa sana na vijana wetu kwa sababu fursa za ajira zimekuwa zikitoka, lakini zinapatikana kwa vijana wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa hiyo, niwapongeze Serikali kwa namna ya usimamizi huu mzuri ambao unatenda haki kwa pande zote mbili za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar ulipoanza, ulianza katika namna tofauti tofauti. Historia inatuonesha kuwa Muungano huu ulianzishwa pia kwa kupitia vyama vyetu vya michezo. Kulikuwa kuna matukio mbalimbali ya michezo ndiyo iliyosababisha viongozi wetu kukutana na hatimaye kufanyika kwa Mapinduzi ya Zanzibar na pia kupatikana kwa Uhuru wa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali, jana tarehe 24 Serikali imerejesha tena lile jambo ambalo tulikuwa tukilisema sana hapa Bungeni la historia ya kuanzishwa kwa ligi hii ya Muungano. Jana ilianza na hili tunalifurahia…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Muda wako umekwisha, hebu hitimisha.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishukuru Serikali kwa ajili ya kulisimamia hilo. Kwa kumalizia, fursa hizi ambazo zimepatikana katika michezo, zimekuwa zikiwahamasisha vijana wetu kuweza kuona vipaji vyao mbalimbali vya michezo na Muungano huu umesaidia sana vijana wetu. Ukiangalia kwa Zanzibar, sasa hivi kuna vijana ambao wanafanyia kazi zao Tanzania Bara hususan katika suala la soka. Naomba niwataje wachache ambao wananufaika na ajira …

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa.

**MHE. ALI JUMA MOHAMED:** …wa kwanza ni Feisal Salim (Fei Toto) wa pili Sajenti Ibrahim (Bacca); wa tatu, Mudathir Yahya Abbas wa nne ni Shekhan na Makame Laurian na Hilika. Hawa wote ni vijana wa Zanzibar, lakini hivi sasa wanapata ajira na wanaendesha maisha yao huku Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Shaurimoyo, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, mchangiaji wetu wa mwisho kwa mchana huu atakuwa Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa hii nafasi. Awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Makamu Rais kwa namna ambavyo Wizara inayohusika na Ofisi yake imewasilisha vizuri bajeti yetu na imeonesha namna ambavyo nchi yetu bado ni imara na tumejipanga kuendelea kuwahudumia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza kaka yangu Waziri, Mheshimiwa Masauni kwa namna ambavyo ameingia kwenye Wizara hii na kuonesha namna ya kuongoza. Mheshimiwa Waziri, Wizara imetulia, kazi zinaenda, hongera sana na timu yako Wizarani, Naibu Waziri Chilo, Katibu Mkuu, na Wakurugenzi waliopo Wizarani kwako. Kweli mimi nikiwa Mbunge, lakini Mjumbe wa Kamati hii ambayo wewe unakuja kuwasilisha kwetu, naona kazi inafanyika vizuri sana, hongera sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nijielekeze kwenye ushauri kwa sababu ya muda. Kuna jambo hapa tumekuwa tukilizungumza kwenye Kamati, na Bungeni hapa tuliwahi kushauri na wazungumzaji wa mwanzo wamesema kwamba upo umuhimu mkubwa wa Mamlaka inayosimamia mazingira (Baraza la Mazingira la Taifa - *NEMC),* kupewa mamlaka kamili, yaani kuwa *NEMA*. Tulishauri kwenye Kamati na tulishauri tulipopata nafasi ya kuchangia hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize kwamba kama nchi yetu kweli inataka kwenda mbele kwenye suala hili la mazingira na kama tunataka tuyasimamie kweli mazingira ili yaendelee kutulinda na kutubeba kama nchi, tunayo sababu ya msingi kuipa mamlaka kamili Baraza la Mazingira ili liwe na meno, liweze kusimamia vizuri mazingira yetu na liweze kuwa na uwezo wa kufanya maamuzi yasiyoingiliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri niliwahi kutoa mfano hapa wa namna ambavyo Baraza letu la Mazingira linakutana na changamoto mbalimbali kutokana na kukosa meno ya kusimamia. Tulitoa mfano wa namna ambavyo miji yetu sasa imegeuka kuwa sehemu ya uchafuzi wa mazingira kwenye suala la kelele, kwenye suala la baa ambazo zinafunguliwa kila kukicha bila kufuata sheria, kwenye suala la *club* zinazokesha usiku katikati ya majumba ya watu. Jambo hili limekuwa ni kero kubwa sana kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania huko hawalali, hawapati muda wa kufanya kazi zao vizuri. Hata hivyo, Baraza letu la Mazingira limekuwa likitambua hili, linakwenda kusimamia sheria, kuzuia na kuzifunga baa mbalimbali zisizofuata sheria, lakini mwisho wa siku kwa sababu halina meno, maamuzi yake yamekuwa yakitenguliwa na Wakuu wa Wilaya, au Wakuu wa Mikoa. Kwa hiyo, mwisho wa siku limekua sasa ni kama Baraza tu la maigizo hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna umuhimu sana na niwasisitize Wizara suala la kuifanya *NEMC* kuwa mamlaka kamili lipewe kipaumbele katika mambo yenu makubwa na ya muhimu kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo naliona, nadhani kuna namna fulani hii Wizara ya Mazingira tunaichukulia kwa urahisi, lakini ni Wizara nyeti sana. Kwanza inashughulika na Muungano wa nchi yetu; ili nchi yetu iwepo lazima Muungano uwepo, lakini pia wanahusika na mazingira, mazingira ni uhai. Vitu vyote vinavyotuzunguka ni mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ziara ambazo mimi nimetembea kama Mjumbe wa Kamati kuangalia miradi mbalimbali ambayo inasimamiwa na Wizara ya Mazingira, ambacho nimekiona na wenzangu wamekisema, kuna namna fulani ya uzito wa kutoa pesa kwenye miradi ya Mazingira. Kuna namna fulani ya kuona kwamba mazingira kama vile ni kitu cha ziada sana, siyo kitu cha msingi, lakini kwa uhalisia ni kwamba mazingira ndiyo uhai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naweza nikatoa mfano, Mwanza kuna dampo limejengwa kwa gharama kubwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kama sikosei. Pesa nyingi zimewekwa pale na lile dampo nia yake ni kufanya Mwanza iwe safi, takataka zinazozalishwa Mwanza zipate sehemu ya kwenda, na ni dampo la kisasa. Lakini kwa sababu suala la kutunza mazingira tunalichukulia poa, lile dampo sasa hivi naona limeshakuwa soko la machinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani ina maana zile pesa ambazo Serikali ilitumia kujenga lile dampo ili kutunza mazingira Mwanza iwe safi, siyo jambo la muhimu sana; hawawezi kupelekwa machinga kwenye hospitali, hawawezi kupelekwa machinga sehemu nyingine, wangepeleka hata wakaweka wao soko la machinga kwenye Ofisi ya Mkurugenzi, lakini wakaona wakaweke kwenye dampo kwa sababu wanafikiri suala la usafi, suala la takataka za mjini siyo la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazingira ni uhai. Madampo tunayahitaji. Nadhani sisi sote tu mashahidi Dar es Salaam ni Mji wa mfano ambao uzoaji taka bado haujafikia viwango vinavyostahili. Ukiizunguka Dar es Salaam; mimi naishi maeneo ya Pugu, utakutana na malori yanayobeba uchafu, hayana taa, ni machafu, yaani lile lori lililobeba uchafu ni chafu kuliko uchafu wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, malori yanayobeba uchafu yananuka, yaani ukikutana nalo kwenye foleni likawa mbele yako kama gari haina *AC* au mko kwenye daladala ni mateso

makubwa. Kwa hiyo, hii ni ishara mbaya kwetu kwamba suala la mazingira tunalichukulia poa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mamlaka zetu za Serikali za Mitaa zinatakiwa zihakikishe magari yanayobeba takataka mijini yanakuwa na viwango maalumu. Siyo magari ambayo yanasababisha ajali, magari ambayo hayana taa, magari ambayo hayana breki, magari ambayo yanaharibika kila siku na yanasababisha ajali nyingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani tunazo sababu za kulifanya suala la mazingira kuwa suala la kipaumbele likichagizwa na vitu vidogo vidogo kama usafi wa miji, usimamizi wa uchafuzi wa mazingira na mwisho wa siku kuhakikisha anayesimamia shughuli hizi, ambaye ni Baraza la Mazingira kwa sasa anapandishwa hadhi kuwa Mamlaka kamili inayosimamia mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tumefika mwisho wa kipindi hiki cha uchangiaji, lakini bado tuna wachangiaji ambao watachangia baadaye mchana baada ya kusitisha Shughuli za Bunge, tutakaporudi watakaoanza ni Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na baada ya hapo atafuata Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said.

Waheshimiwa Wabunge, Kiti kimepata taarifa kutoka kwa Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba yupo safarini kikazi na wakati yeye hayupo na wakati Naibu Waziri Mkuu hayupo, aliyekabidhiwa Kiti cha kuwa Mkuu wa Shughuli za Serikali ndani ya Bunge ni Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, nasitisha Shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

**25 APRILI, 2025**

*(Saa 07.10 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mheshimiwa (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, (Muungano na Mazingira) kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano yetu. Tutaanza na Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SAADA MONSOUR HUSSEIN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami leo niweze kuchangia hii Bajeti ya Muungano na Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu wa leo kwenye sekta hii ya Muungano na Mazingira, napenda sana kumshukuru Mwenyezi Mungu. Pili, nampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuulinda Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano wetu umeendelea kuwa imara na kinara zaidi na unang'ara. Umoja na utuliuvu umeimarika kote Zanzibar na Tanzania Bara. Nampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan na Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuudumisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa ajenda ya nishati safi ya kupikia nchini Tanzania, Bara la Afrika na Dunia nzima. Juhudi za Mheshimiwa Samia kuhimiza katika nishati safi ya kupikia ni kielelezo cha juhudi kubwa ya kulinda na kutunza mazingira. Ajenda ya nishati safi ya kupikia ni muhimu katika kuokoa ukataji holela wa misitu katika matumizi ya mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupitia Wizara hii, naomba kushauri Serikali kubuni sera madhubuti juu ya matumizi ya nishati safi ya kupikia ili kuwezesha akina mama na familia nyingi kutumia nishati safi ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tena kushauri Serikali iwasaidie akina mama wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kupata nishati safi ya kupikia kama vile mkaa, na gesi kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kule Zanzibar Mkoa wangu wa Kaskazini Unguja, hasa maeneo ya Kiwengwa, Nungwi, Pwani Mchangani, Bumbwini, Tumbatu na maeneo mengine akina mama wanateseka sana na matumizi ya kupikia kuni na mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naomba kupitia Bunge hili hasa wanawake wote wa Tanzania kuendelea kumuunga mkono Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika juhudi kubwa za kulinda mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2024 nilisimama hapa kuchangia wananchi wa Tanzania wanavyoteseka pale bandarini kwa ajili ya kupita na zawadi zao. Mwaka huu nasema naipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanya kazi kubwa na nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ramadhani ya mwaka huu wananchi wetu wamekuja kuchukua nguo zao za sikukuu madukani, hawajabughudhiwa, na Watanzania Bara wamekwenda Zanzibar waliochukua zawadi hawajabughudhiwa.

Pale bandarini sasa hivi pako vizuri. Nawapongeza sana Serikali na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuulinda Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, nilimtaja Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix ajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi jioni hii ya leo. Kwanza kabisa nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu na timu yote ya Wizara hii katika juhudi zao mbalimbali za kuhakikisha nchi yetu inakua kimaendeleo na kimazingira na yote katika kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu napenda kuchukua fursa hii adhimu kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, kwa kubeba ajenda ya uhamasishaji wa matumizi ya nishati safi na salama ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Tanzania zaidi ya hekta 469 za misitu zinatekekea kila mwaka, ikiwemo huduma mbalimbali pamoja na matumizi mbalimbali ya kibinadamu. Naipongeza Serikali kwa juhudi mbalimbali inazochukua katika upandaji miti katika maeneo yetu ya nchi ya Tanzania. Pia, nasisitiza kuilea ile miti, ili iweze kukua na kutoa faida kwa vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wanapenda sana, na sasa hivi wamehamasika sana kutumia hii nishati safi, lakini naendelea kuishauri Serikali iendelee kuona namna bora zaidi ambayo wananchi watamudu gharama za utumiaji wa nishati safi ya kupikia, ili kunusuru afya zao na maisha yao zisiathirike na mambo ya mikaa na moshi wa kuni, na kuifikia hii ajenda ya 2030 -2034 kufikia 80% kwa nchi yetu kwa wananchi kutumia nishati safi na salama ya kupikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira umekuwa mkubwa. Elimu zaidi inatakiwa itolewe. Pia ujenzi holela katika miji yetu na vijiji vyetu pia ni uharibifu wa mazingira. Nashauri pia katika kupanga miji badala ya kuwa na bustani za maua, basi sasa tuweke na bustani za miti, ili kusaidia uhifadhi wa mazingira na kupata hewa safi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutambua mchango mkubwa wa taasisi zisizo za kiserikali Tanzania ambapo zinatoa juhudi mbalimbali katika kuhakikisha uhifadhi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najielekeza mchango wangu kwenye sekta ya Muungano. Ni kesho tu nchi yetu tunafikia miaka 61 ya Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar. Tumetoka mbali, ni safari ndefu, tumepitia changamoto nyingi, lakini Taifa letu limesimama imara kuhakikisha huu Muungano unadumu na unakuwa faida kwa Watanzania. Wale wasiotutakia mema wamebaki kukodoa macho na wataendelea kukodoa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia pongezi hizi nazitoa kwa watangulizi wetu walioasisi Muungano huu na waliofuatia kushika Serikali zetu zote mbili ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa awamu zote tofauti mpaka kufikia hii awamu, kwa juhudi zao za makusudi kuhakikisha wanakuwa kifua mbele kuulinda na kuutetea Muungano kwa maslahi ya wananchi, nchi yetu ya Tanzania na ustawi wetu kwa jumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi kubwa sana zimechukuliwa na Serikali, inafaa kuwapongeza katika kutatua changamoto mbalimbali za Muungano zinazojitokeza mara kwa mara na kutatua changamoto hizo. Kazi hiyo iendelee kwa muda muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kama alivyosema Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amemkumbuka katika

wale wanne walioshiriki kuchanganya udongo wa Tanganyika na Zanzibar, ambaye amepoteza maisha hivi karibuni. Nami pia napenda kumwombea dua kwa Mwenyezi Mungu ampe malazi mema Mbunifu wa Jina la Tanzania, Bwana Mohamed Iqbal Dar aliyezaliwa Tanzania katika Jiji la Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtanzania huyu alishinda tuzo la kutunga Jina la Tanzania katika washindani 80 kwa wakati huo na alikuwa ni kijana wa miaka 18 tu, lakini ubunifu wake ulipelekea leo Watanzania tunajivunia jina zuri lenye haiba na ladha duniani, Jina la Tanzania. Huyu naye Mwenyezi Mungu ampe malazi mema na amlipe kwa wema wake aliotufanyia sisi Watanzania na vizazi vitakavyokuja, jina letu linazidi kupaa angani duniani kote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu napenda niseme machache ambayo mara kwa mara viongozi wetu wanayarudia na imefika wakati sasa, basi kuweko na sheria au kinga maalumu ya kuzilinda Tunu za Taifa letu ikiwemo Muungano wetu, kwa sababu sasa isiwe ndiyo sehemu ya watu kupatia umaarufu kwenye majukwaa na vyama vya kisiasa kutaka kuvuruga Muungano, amani na umoja wetu. Kusiwe na nafasi hiyo. Hizi Tunu za Taifa zinatakiwa kulindwa na kuenziwa kwa ustawi wa wananchi, na maisha ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuvuruga ustawi wa Muungano litakuwa ni janga kubwa kwa hapa tulipofikia. Muungano huu unatakiwa kutunzwa na kuenziwa kama nilivyosema hapo mwanzo. Sheria hizo madhubuti zitasaidia kulinda Muungano wetu usibughudhiwe, usichokonolewe na pia usidharauliwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi kubwa imefanyika na Mataifa mengi duniani wanaiga na wanatamani nao wawe kama nchi ya Tanzania kwa sababu kuna nchi nyingi zilijaribu kufanya kama sisi ikiwemo Gambia na Senegal, lakini wameshindwa; Tanzania tupo imara na tunaendelea. Taifa limekuwa moja, tunapendana na tunashikamana, udugu wetu na mshikamano wetu huu uendelee, tusichezee Tunu zetu za Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nami nashauri Wizara hii iongezewe fedha, kwa maana ya kudhibiti mabadiliko ya tabianchi, lakini pia, kudhibiti majanga na maafa yanayotokea, wakati wa mabadiliko ya tabianchi au uharibifu wa mazingira unapotokea. Ikiwemo kwenye bajeti hii, ujenzi wa majengo ya sekta za Muungano kwa upande wa Zanzibar. Zanzibar tuna majengo kidogo sana ya sekta za Muungano. Kuna haja ya kuimarisha kule kuwepo na majengo yenye heshima na hadhi kama ilivyo Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikimalizia, napenda kuwapongeza viongozi wote wa Serikali zetu mbili kwa juhudi kubwa wanazozifanya kuwaletea wananchi ustawi wao wa maisha, afya, na uchumi wao, waendelee na hizo juhudi zao, tunawapongeza na tunawatakia maisha mema. Tunawaombea ushindi mkubwa wa kishindo kwenye uchaguzi ujao wa mwaka huu Oktoba, 2025. Tunahakikisha Watanzania tutawarejesha tena na waendelee kututumikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nakushukuru kwa nafasi, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud. Nilimtaja Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia fursa hii muda huu wa jioni niweze kuchangia kwenye hoja hii iliyopo Mezani na nianze kwa kuiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru Mwanamazingira namba moja ambaye ni Rais wa Nchi, Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye amelichukua suala la mazingira akalipatia kipaumbele katika Serikali yake ya Awamu ya Sita. Pongezi kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za pili ziende kwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Isdor Mpango, yeye ndio msimamizi wa

mazingira. Nampongeza sana, amesimamia sana na amefanya kampeni hasa ile ambayo ameianzisha ya Soma na Mti. Watoto wetu wanaenda kukua wakiwa na *philosophy* ya kwenda kulinda mazingira yao kwa ajili ya maendeleo endelevu. Hongera sana Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wa tatu, ni Wizara, nianze na Waziri Mhandisi Hamad Masauni, ana muda mchache tangu aje kwenye Wizara hiyo, lakini sisi kama Kamati tumeona jitihada kubwa sana ambayo ameifanya kwa muda mfupi. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwa rafiki yangu Khamis Hamza Khamis, nimezoea jina la Chilo. Yeye tangu awali tulikuwa naye kama wanavyosema Wahenga, anayejua mihemko ya mgonjwa ni yule anayemuuguza. Basi Chilo katika maendeleo na michango mkubwa ya kusukuma mbele katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira, ametoa mchango mkubwa sana. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Katibu, Naibu Makatibu wote pamoja na watendaji wote katika hii Wizara ya Mazingira. Baada ya pongezi, nawapongeza kwa kazi kubwa ambayo wameifanya tangu Mhandisi Hamad Masauni, na sisi wenyewe kama Wajumbe wa Kamati. Amefanikiwa kuingiza Bungeni marekebisho madogo ya Sheria ya Mazingira Sura 191 ambayo yamekuja kuanzisha kisheria Kituo cha Taifa cha Kuratibu Kaboni. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara ya Kaboni ilikuwa ikifanyika kiholela holela lakini sasa ipo kisheria na tunaamini sana msimamizi wake mkuu Kaimu Mtendaji ambaye ni Prof. Eliakimu Zahabu ataendelea kufanya kazi kwa uweledi na kwa mafanikio makubwa sana. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu kwa hicho Kituo cha Kuratibu Biashara ya Kaboni, nchi yetu ina zaidi ya misitu kama 565 ikiwa ni misitu ya Serikali na ile inayomilikiwa na halmashauri. Misitu ambayo sasa imeshaingia kwenye hii biashara ya Kaboni

haijafika hata 60. Napo hapa ni chanzo na fursa mpya, ni chanzo kipya ambacho kinaweza kikaingiza fedha kwenye Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana sana, ifanyike jitihada ya usiku na mchana kuhakikisha ndani ya muda mfupi ujao angalau tuingize misitu isiyopungua 200, ili tuweze kufikia yale malengo ya biashara ya kaboni kuchangia kwenye pato la Taifa, ambalo halitapungua chini ya shilingi trilioni moja ya fedha ya Kitanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawapa hongera kwenye mabadiliko hayo madogo. Tumeona umeongeza majukumu ya usimamizi wa mabadiliko ya tabianchi kwa vitengo vya mazingira kwa Wizara za Kisekta. Hongera sana. Mmefanya kazi kwa muda mfupi na tunayaona mabadiliko. Mimi nimekuwepo kwenye hiyo Kamati kwa muda mrefu na nimeona mabadiliko makubwa, hongereni sana kama Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiu yetu sisi Wanakamati na Bunge ambalo tunaona, kama mmeweza kupiga hapa, mmeweza kupiga mwendo na mkafanya marekebisho haya, safari inayokwenda sasa ni hii na tunaiomba ingefanyika ndani ya Bunge hili la Kumi na Mbili, katika Kikao hiki cha Kumi na Tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiu ya Kamati ni kwenda sasa kuifanya *NEMC* (Baraza la Hifadhi la Mazingira) kubadilika. Tulipe nguvu zaidi iwe neema, na iwe mamlaka. Kwa nini iwe mamlaka? Nchi yetu watu wanaongezeka, lakini eneo la nchi haliongezeki. Misitu tuliyonayo na fursa tulizonazo, na ardhi tuliyonayo haiongezeki. Shughuli za kibinadamu zinaongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uchafuzi wa mazingira kila sehemu ndani ya miji. Kuna uharibifu wa mazingira wa ukataji miti, kuna uchafuzi wa mazingira kwenye mito, kwenye maziwa, kwenye bahari. Kuna changamoto nyingi ambazo ili ziweze kutatuliwa sasa hivi, zinahitaji chombo madhubuti chenye nguvu ambacho kitatambulika kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi hatutakuwa wa kwanza kutengeneza chombo hicho. Majirani zetu wanacho hicho chombo; Kenya wana mamlaka, Uganda wana mamlaka *(National Environmental Management Authority - NEMA)*. Namibia wana mamlaka, *South Africa* wana mamlaka. Ukiangalia maliasili, fursa walizonazo ukilinganisha na sisi, sisi ndiyo matajiri. Kwa nini sisi tusifike hapo? Tunalazimika, na sasa ni wakati ambao ni kamili. Wakati ndiyo huu wa kulifanya sasa Baraza la Mazingira kuwa mamlaka ili iweze kudhibiti, ili iweze kutatua changamoto ambazo sasa hivi zinayakumba mazingira yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye Uchumi wa Bluu. Nawapa pongezi. Tunayo Sera ya Uchumi wa Bluu ya Mwaka 2024, lakini bado. Kwa hiyo, tunahitaji katika Bunge hili kama ulivyoahidi, Serikali ilete Muswada wa Sheria ya Uchumi wa Bluu ili tuweze kufaidika na maliasili ya maji inayotuzunguka kote. Tukifanya hivyo, tutasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, kwenye bajeti hii inayoendelea, kule Kigoma tulikuwa na mradi. Tuna Mradi wa Uhimilivu wa Mabadiliko ya Tabianchi katika Mkoa wa Kigoma ambao thamani yake ni shilingi bilioni 17. Nimeona sasa hivi kwenye bajeti hii, zimezungumzwa nazo zimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, fedha hizo zishuke katika Mkoa wa Kigoma ili tuweze kuboresha mifumo ya Kiekolojia ambayo inazunguka Ziwa Tanganyika, na Ziwa Tanganyika liendelee kuwa zuri na liendelee kutoa mazao ya uvuvi kwa faida ya vizazi vya sasa na vizazi vijavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la uchafuzi wa mazingira, hasa taka zinazozunguka mijini. Tunazo changamoto, ukienda kwenye miji mbalimbali unakuta dampo zimewekwa kwenye makazi. Sasa huu ni wakati wa kuhakikisha yanaandaliwa maeneo ambayo ni mbali na makazi, ambapo tunaweza tukatupa hizo taka ngumu kwa ajili ya afya za watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nawapongeza Wanakamati wenzangu, Kamati ya Maji na Mazingira, na wadau wote ambao tumekuwa bega kwa bega kusukuma gurudumu hili la maendeleo kwa namna bora ya kuweza kulinda na kuhifadhi, na kuendeleza maliasili zetu kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo kwa maendeleo endelevu. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix. Nilimtaja Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Muungano na Mazingira. Nachukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa *Eng.* Masauni. Nampongeza na mkwe wangu Mheshimiwa Khamis Chilo na Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu. Kwa kweli sasa hivi Wizara ya Muungano imeshiba. Wizara ya Muungano imeshiba na kwa kweli wanafanya mambo makubwa sana. Wakati wa kipindi chote cha nyuma tulichopitia, mfupa huu ulikuwa ni mgumu sana. Kipindi kama hiki ilikuwa ni kelele, zogo, matusi, lakini leo tunasema *Alhamdulillah! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mheshimiwa Rais wetu Mama Samia Suluhu Hassan anastahili pongezi kubwa sana. Ni Mama msikivu, ni Mama mkarimu, ni Mama mcha Mungu. Waheshimiwa Wabunge, sote ni mashahidi, tunamsifu Mama Samia kwa mambo mazuri anayoyafanya na yanaonekana. Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Watanzania, tusichoke kumtetea, kumpambania, na kumpigania. Iwe jua, inyeshe mvua, lazima tumtetee Rais wetu, ni Rais wa mfano. Anafanya mambo makubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka yake hii minne alipopokea kijiti, Muungano wetu ulikuwa hauko vizuri. Kulikuwa na kero 25, leo Mama Samia ametatua kero 22. Kwa kweli amefanya mambo makubwa sana. Tumpongeze, tumshukuru, lakini tuwashukuru na Watendaji wa Wizara hii. Kwa kweli ni watu wazalendo, wakarimu, wachapakazi. Sisi tutawapongeza, lakini Mwenyezi Mungu ndio atawapa faraja zaidi ya duniani na kesho mbele ya Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawapongeza viongozi wetu Waasisi, waliounganisha Tanganyika na Zanzibar kuifanya nchi yetu iwe moja. Kwa kweli walifanya jambo kubwa sana, waliona mbali. Leo hata usalama wa nchi yetu hii tuna amani kwa Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, Mama Samia ameunganisha makundi mbalimbali, ameunganisha Wizara ambazo siyo za Muungano, leo wanafanya kazi pamoja. Sasa hivi unamwona Mheshimiwa Prof. Kabudi Zanzibar anafanya kazi na Mheshimiwa Tabia Mwita. Katibu Mkuu Msigwa anafanya kazi Zanzibar pamoja na Fatma. Kwa kweli ni jambo la faraja kubwa sana alilolifanya Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hatutachoka kumshukuru na kumwombea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapomzungumza amefanya, yamefanywa kwa sababu yanaonekana. Ndipo unapowasikia huko barabarani kuna wahuni wanamsema vibaya sana, kwa kuwa wanajua aliyoyafanya ni makubwa. Hakuna atakayepinga kama hakufanya. Kwa hiyo, hawana la kusema, wanakuwa wanamchafua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt Samia alizaliwa na baba yake na mama yake. Aliapiwa kwa jina lake akaitwa Samia Suluhu Hassan. Tunawaomba wale wahuni wamwite Samia Suluhu Hassan, wala hawatatukwaza sisi, lakini sisi bado tutaendelea kumpambania Rais wetu, Mama yetu, kipenzi chetu. Hii ni hazina yetu. Hii ni hazina yetu Watanzania; ni jambo kubwa sana kuwa na Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapoambiwa mitano tena, tuisimamie. Tumng'ang'anie, tumpambanie kwa nguvu zetu zote. Muda wote, *time* yote tukiwa barabarani, tukiwa baharini, au tukiwa nchi kavu, Kiongozi huyu ni wa kumpambania. Amefanya mambo makubwa, hususan sisi wanawake ametuweka kwenye *level* nzuri sana. Sasa hivi hakuna mwanamke anayepewa eneo kufanya ashindwe kufanya kazi. Anafanya kazi kwa sababu anamwona Rais anafanya kazi. Kwa hiyo, lazima naye afanye kazi. Lazima tumtetee, tumpambanie kwa nguvu zetu zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana wasanii wa *Bongo Flavour*. Kwa kweli vijana wale wanastahili sifa, wanastahili pongezi, ni mashujaa. Hawaogopi, wanamtetea Mama Samia kwa nguvu zao zote, na sisi tusimame twende na Mama Samia. Viongozi, sasa hivi sisi Zanzibar kwa kweli hujui huyu kazaliwa Makunduchi, huyu kazaliwa Mtambwe, huyu kazaliwa Micheweni, huyu kazaliwa Kojani, sote ni kitu kimoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi amejenga masoko, lakini masoko yale tuliopo Zanzibar na waliotoka Bara, nusu bin nusu. Huo ndiyo Muungano tuliokuwa tunautaka. Ushirikiano, umoja, mshikamano, na leo tumefikia sehemu ile tuliyoitaka. Kero hazitakwisha, zitakuwa zinazaliwa kila leo kwa sababu na sisi bado tunazaliwa. Hata hivyo, Mama Samia anaendelea kuzitatua na sisi tunayaona matunda yake. Jamani, mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muungano umefikia pale Waasisi waliounda walipokuwa wanataka ufikie, basi sasa hivi umefikia. Kuna mambo mengi yamefanywa Zanzibar, mambo mengi sana ya maendeleo yamefanyika na sote tunaona, kwa nguvu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hatufichi, hilo ni kweli; tumeona na yanaendelea kufanywa.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tumtetee Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, tumzungumze kwa yale aliyoyafanya, na ameyafanya. Yale aliyoyafanya ni mengi. Miaka minne tu, lakini amefanya mambo

mengi sana, yanaonekana. Barabara, bara zipo na Zanzibar zipo. Viwanja vya ndege vinajengwa, Bara vinajengwa na Zanzibar vinajengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli hilo hatufichi. Mawaziri wetu wanafanya kazi Bara na wanafanya kazi Zanzibar. Siyo Sekta za Muungano, lakini wameungana wanafanya kazi pamoja. Hilo ndilo tulikuwa tunalitaka lifanyike. Hilo tunalitaka lifanyike na sasa hivi limefikia lengo la Muungano wetu kuwa imara, kuwa mtulivu, lakini hata sisi wenyewe tumekuwa watulivu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tukipita bandarini *Alhamdulillah,* hakuna kero yoyote wala hakuna shida yoyote; unapita, unakwenda, unarudi, unakwenda unarudi; hicho ndicho Watanzania tulikuwa tunakitaka.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Kuna taarifa Mheshimiwa Mwanakhamis. Mheshimiwa Rashid Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mwanakhamis kwa mchango wake mzuri, lakini nataka tu nimwambie kwamba, siku hizi hakuna kero za Muungano, isipokuwa ziko changamoto za Muungano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanakhamis, unaipokea taarifa hiyo ya Mheshimiwa Rashid Shangazi?

**MHE. MWANAKHAMIS KASSIM SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea. Hilo alilolisema ni kweli. Ndiyo niliposema, sasa hivi tuko shwari kabisa. Hakuna kero, hakuna matatizo yoyote. Tunaendelea murua na tunakwenda. Hayo ndiyo tulikuwa tunayataka. Yote hayo ni Mama yetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ni kweli ni Mama mpenda maendeleo, ni Mama

mpenda watu, ni Mama msikivu, na mwelewa. Tunasema *Alhamdulillah. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wafanyabiashara wanatoka Zanzibar wanakuja Dar es Salaam kuchukua vitu, hakuna zogo wala tafrani. Hilo ndilo tulikuwa tunalitaka. Nawaomba Waheshimiwa tuendelee kumtetea Rais wetu, kumpambania, na kumpigania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said. Nilimtaja Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mheshimiwa Tamima Haji Abass ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika bajeti hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza hatuna budi kumshukuru *Allah Subhanahu wa Ta'ala* kwa kutujaalia uzima, afya, na uhai, kwa sababu wakati tunaanza Bunge hili mwaka 2020 tulikuwa tuna wenzetu ambao sasa hivi wameshaaga dunia, hawapo hapa. Kwa hiyo, sisi ambao tupo ni kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia kutumia huu muda wa ziada ambao tumepewa, basi kumwabudu Mwenyezi Mungu ili kutengeneza Akhera yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na timu yake. Kwa kweli Wizara hii inafanya kazi kubwa sana kuanzia mtangulizi wake Mheshimiwa Dkt. Jafo, sasa hivi tumekuja na Waziri Mheshimiwa *Eng.* Masauni. Kwa kweli wamefanya kazi kubwa sana katika kipindi kifupi, kwa sababu, katika kipindi hiki kifupi ambacho amekamata hii Wizara, basi tumeweza kuona *reforms* nyingi ambazo huko nyuma watangulizi wake walizianza na kutokana na pilika nyingi hawakuziendeleza, lakini yeye amezifanyia haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miaka mitano hii ya Bunge lako Tukufu, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwani nimepata bahati ya kuweza kuchangia bajeti hii kwa miaka mitano mfululizo. Katika miaka hii mitano katika Bunge hili la Kumi na Mbili, kwa kweli kuna *reforms* nyingi zimefanyika, za kisera pamoja na za kisheria, ambazo zimeweza kuongeza tija katika usimamizi wa mazingira pamoja na kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tuna sera mpya ya mazingira ambayo imetambua au imejumuisha masula mazima ya mabadiliko ya tabianchi, ambayo huko nyuma hayakuwa *mainstreamed* au hayakutambulika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, hivi karibuni tu mwaka 2024 tumeweza kuja na sera ya Uchumi wa Bluu kama alivyozungumza mwenzangu Mheshimiwa Kavejuru, sera ambayo imeweza kusimamia au kuweka mikakati ya vipi tutapata fursa za Uchumi wa Bluu ambazo wenzetu wamezitumia kwa kipindi kirefu lakini sasa na sisi tuna mwaka wa kuweza kujipanga vizuri na kuweza kupata zile fursa za Uchumi wa Bluu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Februari mwaka huu 2025 tumeweza kufanya mabadiliko ya sheria ambayo yameweza kutusaidia vilevile kujumuisha mabadiliko ya tabianchi kwa upana wake katika sheria. Hapo mwanzo ilikuwa masuala ya mazingira ndiyo yalikuwa yamekithiri zaidi katika sheria yetu, lakini hivi sasa angalau kuna mtiririko mzuri na kuna usimamizi mzuri wa mabadiliko ya tabianchi katika sheria yetu ambayo inakwenda kuongeza tija katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo mabadiliko, haya yasingewezekana kama Serikali na hasa kupitia Mheshimiwa Rais, hakuwa msikivu na kuweza kuyafanyia kazi yale ambayo Bunge lako Tukufu yamekuwa yakiyapitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namshukuru sana Mama Samia kwa kuwa msikivu, ambaye amekuwa ni mhifadhi na

mwana mazingira namba moja ambaye ametumia nguvu binafsi katika kuhakikisha kwamba masuala ya mabadiliko ya tabianchi na upambanaji wa athari za mazingira basi zinakuwa katika pahali pake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Mheshimiwa Rais, amekuwa yeye mwenyewe ni mwelimishaji, ameelimisha kupitia makongamano na mihadhara, hali kadhalika kwa kutumia filamu ya *Royal Tour* pamoja na *Amazing Tanzania* kuweza kuelimisha jamii na kuvinadi vivutio mbalimbali ambavyo vimo katika maeneo mbalimbali ya mazingira yetu ikiwemo mbuga za wanyama, misitu, maziwa, mito na kadhalika. Kwa hiyo, Mama Samia ameonesha wazi kwamba yeye ni mhifadhi namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika, Mama Samia ameonesha moja kwa moja kwamba yeye ni mpambanaji kwa sababu amesimamia mipango ya usimamizi wa mazingira kwa kutumia mikutano mbalimbali ya kikanda pamoja na ya Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumemwona Mheshimiwa Rais akishiriki katika mikutano mbalimbali ya mabadiliko ya tabia ya nchi, ameenda kule Sharm El Sheik, ameenda kule Uingereza na maeneo mbalimbali ili kuisaidia nchi kuweza kupata fursa za kifedha na rasilimali watu ili kuongeza tija katika upambanaji wa mabadiliko ya tabia ya nchi, pia kupambana na athari za mazingira ambazo zimesheheni katika maeneo mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa pamoja na *reforms* ambazo zimetokea, sisi kama wadau, sisi kama Bunge tulitamani sana kuona kwamba kuna baadhi ya mambo pia yangeweza kufanyika katika Bunge lako Tukufu hili katika kipindi hiki cha miaka mitano, katika hili Bunge la Kumi na Mbili. Hata hivyo, kutokana na sababu zisizoweza kuzuilika, tunakwenda kumaliza bajeti ya mara hii katika Bunge la Kumi na Mbili, haya mambo hayakuweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ni suala zima la kuwa na taasisi madhubuti ya kuweza kusimamia athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na masuala mazima ya usimamizi mahiri wa mabadiliko ya tabianchi. Sasa ningemwomba Mheshimiwa Waziri atusaidie hapa, kwamba ile ahadi ambayo amekuwa ameweka, kusema kwamba hata katika Bunge hili la mara hii katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa atakuja na hayo mabadiliko, lakini bahati mbaya Bunge hili linaenda kwisha lakini kwenye ratiba hatujaona hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri aje atueleze sababu ambazo zimepelekea kwa nini mabadiliko ya kuwa na taasisi mahiri yenye nguvu ambayo inakwenda kusimamia mabadiliko ya tabia ya nchi pamoja na usimamizi wa mazingira hatukuiona? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungetamani kama Wabunge kuona kwamba *NEMC* inakwenda kuwa mamlaka na hili tumelizungumza tangu siku ya mwanzo ya Bunge hili na tunaendelea kulizungumza, mpaka hivi sasa tunakwenda kumaliza Mkutano wa mwisho huu wa Bunge hili la Kumi na Mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali kadhalika tumelizungumza suala zima la Uchumi wa Bluu. Tungependa kuona kwamba suala la Uchumi wa Bluu ambalo tumelifanyia haki kwa kuweza kuweka sera ya mwaka 2024, tungeona kwamba kuna sheria nayo vilevile ya kuweza kuratibu masuala mazima ya Uchumi wa Bluu inakuja hapa katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulitegemea tuone, kwa sababu tunao huu mpango kabambe ambao tumeona kwamba taasisi mbalimbali kushiriki kwake siyo kuzuri sana, tungependa kuona kuna sheria ya kuratibu *mainstreaming* au ushiriki wa taasisi katika kupambana na athari za mabadiliko ya tabianchi na changamoto za mazingira. Tungependa pia tulione hili linatokea katika kuziratibu hizi taasisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ni ombi langu, katika Bunge hili, na niliwahi kuzungumza hapa kwamba kuna hii

*Basel Convention*, Mkataba wa Uteketezaji wa Taka Hatarishi. Tunajua kwamba kulingana na mkataba wa *Basel* ambao uliasisiwa kule Stockholm, tunatakiwa tuwe na taasisi ambayo ndiyo ina-*issue* vibali vya kuweza kusafirisha taka hatarishi kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuzungumza kwamba Zanzibar wanapata shida sana kusafiri kutoka Zanzibar kuja Dodoma kwa kufuata vibali vya kusafirisha hizi taka au vyuma chakavu. Naomba Mheshimiwa Waziri, hebu tu-*question* madaraka ya taasisi yako, kule Zanzibar, aidha tuka-*identify ZEMA* au Idara ya Mazingira ikawa kama ni wakala ambaye ataweza kutoa vibali vya usafirishaji wa vyuma chakavu bila kuathiri au kusumbua wananchi wa Zanzibar kusafiri na kupoteza gharama nyingi kuja Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, nashukuru sana Mheshimiwa Waziri umezungumza kwenye hotuba yake hapa kwamba anakwenda kufanya mapitio ya Mfuko wa Jimbo. Kwa kweli tangu tumeanza Bunge hili 2020 mpaka hii leo tumekuwa tukilalamikia kuhusu changamoto za Mfuko wa Jimbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunashukuru kwamba Mheshimiwa amelivalia njunga hili na tunaombea heri kama alivyo yeye ni *fighter,* yaani mpambanaji, tunajua na hili atalifanya kwa haraka ili katika Bunge hili, hatukufanikiwa sana kutumia hii fursa, lakini *we hope* na tunategemea kwamba kwa kibali cha Mwenyezi Mungu tutakuwa tupo hai na salama na wananchi wetu katika Majimbo yetu watuturejesha wote humu ndani tuje tushuhudie katika kipindi Bunge linalokuja, basi tunaweza kwenda kupata hizi *benefits* za mapitio mapya ya Mfuko wa Jimbo na kuweza kupata hizi faida ambazo sasa hivi tunazikosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah. Nilimtaja Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mheshimiwa Maryam Omar Said ajiandae.

**MHE. TAMIMA HAJI ABASS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii adhimu na muhimu katika nchi yetu. Namshukuru Mwenyezi Mungu mpaka muda huu kunipa uhai, nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuwapongeza sana Waziri wa Wizara hii, Mheshimiwa *Eng.* Masauni, Naibu Waziri Mheshimiwa Khamis, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya katika kutuletea maendeleo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutuongoza vema, na wewe pia Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kazi nzuri unazozifanya kila siku kutusimamia hapa Bungeni, na kwa miongozo yako tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye ametuonesha njia, sisi wanawake tunaonekana tunaweza duniani kote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai, Mheshimiwa Spika amekuwa ni Spika wa Mabunge ya Dunia, ametokea ndani ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Dunia imetuelewa kwamba wanawake tunaweza na ndiyo maana uongozi mkubwa mkubwa unakuja ndani ya nchi yetu kupitia uongozi wake Dkt. Samia. Tumeona viongozi mbalimbali wanachaguliwa duniani huko kuongoza taasisi mbalimbali za Kimataifa, kwa hiyo, tunazidi kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, naye kwa kuunganisha Muungano

pamoja na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Viongozi wetu hawa wameusimamia Muungano, wanauendeleza mpaka sasa hivi tunaonekana kama nchi imetulia na imetulia kweli, tunafanya kazi zetu na wananchi wote wanafanya shughuli zao bila wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Muungano na Mazingira, imeenea nchi nzima. Hapa Tanzania Bara inakwenda vizuri na kule kwetu Zanzibar inakwenda vizuri, kwa sababu tumeona miradi mingi ambayo inatekelezwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inakwenda hadi Zanzibar na wananchi wameona kwa macho yao.

Mheshimiwa Mweyekiti, nikisema hivyo, hivi sasa ndani ya Mkoa wangu wa Kaskazini Unguja kuna shule na hospitali za ghorofa ambapo hapo mwanzo hazikuwepo na zimekuja ndani ya uongozi wa viongozi hawa wawili kwa kuonesha dhamira ya dhati ya kutaka kuwaletea maendeleo wananchi wao ili kila mmoja awe sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee na mchango wangu, niungane na Kamati ya Katiba na Sheria. Wao walitoa mapendekezo yao hapa, walitoa ushauri, wamesema kwamba katika mambo wanayotaka yapewe kipaumbele kwa kipindi hiki ni ufanywe utafiti wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayohusu Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo muhimu, kwa sababu kama tutakuwa tunatekeleza, tunapanga mipango ambayo tunaiachia njiani, kwa kweli ufanisi wake utakuwa hauonekani na ile tija tunaitarajia haitapatikana. Kwa hiyo, ni muhimu Wizara hii ikaenda kulisimamia hili ili tuone zile nguvu tunazozitumia zinakwenda kama zilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Kamati hii imeshauri pia kuanzishwa Kituo cha Kumbukumbu na Nyaraka za Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Hili nalo ni muhimu, kwa sababu vizazi vinavyokuja kama hapatakuwa na kumbukumbu nzuri watakuwa hawaelewi kitu gani kilichotokea huko nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waasisi wetu walitengeneza Muungano au walisimamia Muungano kwa madhumuni ya vizazi vyote vya Tanzania. Kama utakuwa unaishia hapa hapa, hakuna kumbukumbu yoyote inayowekwa, sifikirii kama vizazi vinavyokuja watakuwa wanajua huu Muungano ni nini? Kwa hiyo, hili ni jambo muhimu waliloliwaza Kamati, nawapongeza sana, tuendelee kulisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, nataka kusema Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama angekuwa mchezaji wa mpira wa miguu, nafasi zote anaziweza. Tangu nimeingia ndani ya Bunge hili Tukufu mwezi wa Septemba 2022, nilikuwa nasikiliza michango ya Wabunge kila Mbunge aliyesimama hakuna hata mmoja aliyeacha kumsifu au kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye utalii unamkuta Dkt. Samia, ukienda kwenye Nishati unamkuta Dkt. Samia, ukienda kwenye michezo unamkuta Dkt. Samia, ukienda kwenye maji unamkuta Dkt. Samia, yaani ukisema shughuli zote. Kwa hiyo, kama tutazitafsiri zile kazi anazozifanya, basi tutasema huyu mchezaji anaweza namba zote, ukimpanga anaziweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema nini? Tumeona katika taasisi mbalimbali wanafanya mikutano na makongamano, baadaye wanampa tuzo Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Nashauri Bunge lako Tukufu na sisi tuone namna Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hili la Kumi na Mbili tuandae tuzo maalum kwa Mama huyu ili iweze kuwa chachu kwake kuona kitu gani nasi Wabunge wenzie tumemthamini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwamba Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge. Kama Mheshimiwa Rais ni sehemu ya Bunge ni wajibu wetu Wabunge tumpongeze. Tunampongeza kila siku, lakini bado, tumpe tuzo, na kubwa zaidi tutakapotoka hapa ikifika Oktoba, 2025 ndiyo basi tukampambanie, apate kura kwa wingi baadaye tumvike taji. Kwa hiyo, naomba sana kama litakuwa limetupendeza, basi tufikirie tuzo ya namna yoyote inamfaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiangalia kwenye mazingira, Mheshimiwa Dkt. Samia, kule Kaskazini siku ya tarehe 27/01/2024 siku yake ya kuzaliwa, badala ya kukaa nyumbani akala keki, basi aliona aende akapande miti, baadaye ndiyo ale keki na wananchi. Kile kitendo kiliwafurahisha watu na kuona huyu mama anapambania mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara, lile shamba ambalo amekwenda kupanda miti tarehe 27 ile siku yake ya kuzaliwa tulienzi na tuliwekee kumbukumbu kwamba ni moja ya alama na iingie katika kumbukumbu zile za Taifa kuwa Rais wetu huyu alifanya kitu kizuri ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea mbele kidogo vilevile kwenye Wizara hii, naiomba sana ile miradi ambayo wameipanga kuitekeleza kule Zanzibar, basi waisimamie na vilevile kuangalia zile fursa nyingine au zile changamoto nyingine zilizopo kule za mazingira au uharibifu wa mabadiliko ya tabianchi, basi yanashughulikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano, kule kwetu Kaskazini kuna kijiji kinaitwa Muwanda. Katika Kijiji cha Muwanda kulikuwa kuna mikoko kwa sababu pale kuna kitu wanaita sijui ghuba inaingia maji, maji yanatoka baharini yanaingia ndani. Sasa kulikuwa kuna mikoko, lakini ile mikoko mingi imekatwa, ukienda pale utasikitika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu ambayo hakuna mikoko kabisa. Basi tulione lile eneo kwa kushirikiana na Idara ya Mazingira ya Zanzibar tuone tukalipande miti na tuisimamie. Tukifanya hivyo, basi yale mambo mengi ambayo yanaleta changamoto ndani ya maeneo yetu, tutakuwa tunayashughulikia na tunayatatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, nalishukuru sana Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna ambavyo tunafanya kazi, kwa sababu tunafanya kazi hizi na tumeonekana tunafanya kazi, miradi mingi iliyopo ndani ya maeneo yetu inaendelea, hakuna miradi iliyosimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa usimamizi wa Wabunge pamoja na kuitii Serikali yao, tunakuta maendeleo mengi na mafanikio mengi, wananchi wetu wanatuelewa. Chama chetu cha Mapinduzi kimeshatuwekea njia, viongozi wetu wameshatuteulia tayari kuwa hawa ndio tunawasimamisha kwenye Uchaguzi Mkuu kwa ajili ya kuendelea kutupa maendeleo. Kwa hiyo, kilichobakia, kazi kubwa ambayo tuliyonayo hapo mbele yetu, sisi twende tukasimame kwa pamoja tuhakikishe tunawapa ushindi mkubwa viongozi wetu hawa ili tuendelee kushika dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Tamima Haji Abass. Nilimtaja Mheshimiwa Maryam Omar Said, na Mheshimiwa Anatropia Theonest ajiandae.

**MHE. MARYAM OMAR SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja iliyopo Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mdau wa mazingira na ni Balozi wa Mazingira pia. Haijawahi kupita hoja ya Muungano na Mazingira nisiisemee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nawashukuru kwa dhati viongozi wangu wa Taifa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan pamoja na Rais wa Zanzibar Mheshimiwa Dkt. Hussein Ally Mwinyi, wamenitendea haki katika Jimbo langu, hata kama ukizingatia lile jimbo asilimia kubwa niseme nusu na robo ni wapinzani kwa sababu mimi nimetokea Chama cha Wananchi *CUF* nikiwa mwanamke pekee ninayeongoza Jimbo kule Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia mwenzangu mwakilishi ni wa *ACT* Wazalendo lakini pia yupo Diwani mmoja ni wa *ACT* na CCM wana Diwani mmoja tu. Kwa kweli hawakufanya ubaguzi, wameleta maendeleo sawa na Majimbo yaliyo na wawakilishi

wao. Hivi nisiache, niwashukuru kwa dhati, nami niwaambie, nina deni, ila nitalilipa *Inshallah* kwa uwezo wa Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali, mwaka 2024 nilizungumzia bajeti ya mazingira, na katika ushauri wangu niliwaambia fedha hazitoshi, lakini pia nilisema tusitegemee fedha kutoka nje. Tuanze na cha kwetu kwanza, halafu hiki ambacho tuna ki-*engage* kutoka huku, tutakiangalia baadaye. Naishukuru Serikali imelifanyia kazi, bajeti imepanda mpaka 41%, lakini pia, fedha ya ndani imeongezeka kwa asilimia kubwa. Hilo niwashukuru Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nijielekeze katika suala la Muungano. Nimeona hapa mmejipanga vizuri katika kuhakikisha elimu ya Muungano inafika kwa makundi mengi, lakini kadiri ambavyo tunajipanga na huku nyuma wapo waliokuwa hawataki maslahi kwenye Muungano wetu huu, kitu ambacho ikiwa tuliungana kwa mchanga sasa hivi tujue ni Muungano wa damu. Wapo waliotoka Zanzibar wameolewa huku Tanzania Bara, hatuwezi kubagua tena na wapo Watanzania Bara wameoa kule kwetu Zanzibar, ni lazima tuwe makini na hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi ushauri wangu hapa ni, Serikali tushuke chini zaidi. Nakumbuka elimu ya Muungano nilisoma nikiwa Darasa la Tatu. Kule tulikuwa tunafundishwa mambo ya ukoloni, kulikuwa kuna sura inaitwa Ukoloni Mamboleo, baadaye tena inakuja biashara ya utumwa *then* tunaingia kwenye Muungano. Sifikirii kama hivi bado vipo kwa sababu, tunakumbana na masuala mengi ya watoto wetu wadogo ambao wanataka kufahamu huu Muungano ni nini? Hebu turudi tena kule chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mmesema kwamba kuna kipindi ambacho kinarushwa kwenye Redio Zanzibar, kwenye *TBC,* lakini mimi niwaambie vipo vijiji mpaka leo mawasiliano ni ya shida, hizo redio hazifiki. Pia vipo vijiji mpaka leo umeme haujafika, hakuna *television.* Hebu tushuke chini zaidi tuandae hata kama ni majarida kila baada ya muda tuwe na magazeti kwamba, hili gazeti kila lini litakuwa na mwendelezo wa mambo ya Muungano,

ilimradi tuweze kuwafikia wananchi wetu wote, hususani watoto wetu wadogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nafahamu Muungano, ukija kuniuliza hakuna ambacho utanidanganya, lakini namhofia huyu mwanangu huku chini, yeye atakuja kuufahamu Muungano kama mimi ninavyoufahamu! Hebu turudi tena, tushuke chini shuleni, tushuke zaidi vijijini ambako haya tunayoyasema bado hayajafika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili, nitajiwekeza kwenye mazingira. Nimejitambulisha hapa, mimi ni Balozi wa Mazingira, na sio mimi tu, tuliteuliwa mabalozi wa mazingira wengi, nakumbuka Wabunge kama watatu, wanne hivi. Wengine waliacha kamba njiani baada ya kuona sasa hii kazi ya ubalozi haina hata chochote, sisi bado tunaendelea pamoja na dada yangu kule, Mheshimiwa Esther Matiko, tupo kwenye *group* la Mabolozi wa Mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri, mnaona jinsi Mabalozi wa Mazingira wanavyojitolea na kutuma kazi zao, wanakwenda kwenye shughuli, hawasubiri mialiko, wanakwenda kwenye shughuli, hata kama hamtawatambua, wanawafuata kila sehemu, lakini kiukweli mmewasahau hawa vijana ni vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi kile Mheshimiwa Dkt. Jafo, alipowateua alikuwa anaendelea na kuna vitu alikuwa anavifanya, ilifika mpaka akatoa tuzo kwa Mabalozi wa Mazingira. Mbona sasa haya hayaendelei! Mbona hawa vijana ni kama hatuwajui! Basi kama tumeshindwa, hatuna haja nao tena, twende tukawaambie, tuwape hata shukurani kwa pale walipofika. Kwa nini, hamjibu hoja zao na mpo pale kwenye ma-*group*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katibu Mkuu yupo, Naibu Katibu Mkuu yupo, Waziri upo, Naibu Waziri upo, hebu jitokezeni siku moja kwenye lile *group* muwaweke sawa. Wanaona kama wamesahauliwa, wanaona kwamba, labda ni Mheshimiwa Dkt.

Jafo ndio alikuwa akilitaka hili jambo. Wanafanya kazi, wanajitolea sana, hebu twendeni tukawaone. Siyo mara moja au mara mbili, mimi kila siku nikisimama hapa nawasemea, lakini siridhiki, kwa sababu hakuna hatua iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi cha Naibu Waziri, Mheshimiwa Chande, pamoja na Mheshimiwa Dkt. Jafo, walifanya vizuri kwenye Balozi wa Mazingira. Mheshimiwa Chilo, kaka yangu, unaona lawama ya kwenye ma-*group,* hebu rudi tukawaweke sawa hawa vijana. Wapo kila sehemu na wanafanya kazi kwa kujitolea, wanasafisha fukwe, wanafanya mambo mengine. Sisemi kwamba, nami ni lazima niingizwe huko, mimi nawasemea wao ambao hawawezi kusema hapa ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nijielekeze moja kwa moja kwenye hili suala la mazingira. Kwa tulipofikia sasa, nadhani Mheshimiwa Waziri utaona hapa ndani inapokuja hoja ya mazingira Wazanzibari wengi ndio tunanyanyuka kusema, ni kwa sababu sisi tunaathirika zaidi. Zanzibar ni visiwa, ulifika muda ikaja habari hapa kwamba miamba ya visiwa imeanza kumomonyoka, watu wakaanza kupata taharuki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wakati sasa, hebu twendeni tutafute fedha kwa hali yoyote tufanye upembuzi yakinifu nchi nzima halafu tuweze kubaini yale maeneo, yapewe kipaumbele, twendenayo Zanzibar jamani, hali ni mbaya. Kuna visiwa kama Ntambwe Kuu, kiukweli hiki kisiwa kimeanza kupotea. Kwa asilimia kubwak imebaki theluthi ndogo tu, hebu nendeni mkaangalie hali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, mwisho, nimalizie kwa kusema, nashukuru, pamoja na yote ambayo nimeyasema hapa, lakini nina la kwangu moja ambalo naomba aidha Naibu Waziri ama Waziri, baada ya yote tuambatane twende jimboni mkaniangalie hali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli kuna daraja ambalo maji yanapita yanayokwenda baharini, kwa kipindi hiki cha msimu wa

mvua hakuna mwanafunzi hata mmoja anayetoka kwenye kijiji hicho au kwenda kijiji jirani ambacho shule ipo kwa sababu, mimi mwenyewe nimeshawekeza karibu mara mbili. Pesa ya Mfuko wa Jimbo haijakidhi, na ushahidi wa picha ninao hapa, nikimaliza kuchangia nitawatumia. Hebu twendeni mkaangalie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni mwanamke pekee niliyetoka kwenye Jimbo kule Pemba, nisipofanya vizuri nitakosa hamasa za wanawake wenzangu. Nataka nifanye vizuri, hata kama nisitarudi, lakini warudi wanawake wengine zaidi ili kampeni ya mama, ile ya 50% au zaidi iweze kufikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo machache, nashukuru sana, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Maryam Omar Said. Nilimtaja Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mheshimiwa Reuben Kwagilwa na Mheshimiwa Abubakari Asenga, ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mara nyingi sana huwa napenda kuisemea hii Wizara. Siisemei kwa sababu nyingine yoyote, ni kwa sababu ninaamini ni moja kati ya Wizara ambazo kipaumbele chake kimekuwa ni kidogo. Huwa tunapimaje kipaumbele kutoka kwenye bajeti husika? Ukiangalia kwanza matumizi na fedha za maendeleo zinatoa majibu yote kwamba, tunatoa kipaumbele gani kwa Wizara halisi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasahau, na ninarudia, nimesema mwaka jana, 2024, tukiharibu mazingira athari za mazingira haziwezi kuturuhusu kufanya kitu kingine mbadala. Kwa hiyo, kupanga ni kuchangua. Nilitamani baada ya majadiliano ya Wabunge ya mwaka 2024 kuona *positive improvement*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeeleza hapa wakati inawasilisha, imesema hata bajeti ya fedha za maendeleo, fedha za ndani kwa mwaka 2024 tulipanga shilingi bilioni 700 tu, fedha za maendeleo na fedha za matumizi ya kawaida. Katika hiyo

fedha imeenda 53%. Nilikuwa nasoma randama hapa, sasa ni kwa kiwango gani sisi tunataka kuleta mabadiliko kwenye maendeleo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila siku bajeti zetu tunategemea Wazungu ndio watuendeshee masuala ya mazingira. Tunapaswa sisi wenyewe kujua *impact* ya mabadiliko ya tabianchi yanayotukumba sisi, yanayoikumba jamii na kusababisha hata mipango mingine ambayo Serikali imekuwa inaipanga isitekeleze kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi. Kwa hiyo, naendelea kulia na hii Wizara na nitaendelea kuisema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nitoe pongezi, ameeleza mchangiaji wa mwisho, michango ambayo wamekuwa wakiifanya mabalozi mbalimbali wa mazingira, mimi pia ni mpenzi wa mazingira. Sasa wengine mmewateua, mimi nimejiteua, sihitaji uteuzi kuwa Balozi wa Mazingira. Unapaswa kuguswa na mazingira, kusimamia, kuchukua juhudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimekuwa *champion* katika kuhakikisha ninapambana, ninapanda miti, ninahakikisha mazingira ni safi na huo ndiyo wito ambao ninautoa kwa kila mtu. *It has to come from us.* Kama tunataka mabadiliko, yaanze na sisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawapongeza vijana, akina Chage Alex Chage, wanachapa kazi, lakini pia kuna rafiki yangu anaitwa Emmanuel Likuda, nimemtambulisha asubuhi hapa. Huyu ni mmoja kati ya waandaaji wa Tuzo za *Tanzania Mazingira Award,* anatumia gharama zake, anatafuta wafadhili kwa shida kwa ajili yaku-*recognize* Wizara, taasisi, wadau, wanamazingira ambao wameweka *positive contribution*. Sio hao tu, wapo wengi, siwezi kutaja *list* yote. Tutambue hizo jitihada siyo ndogo, lakini zina-*make impact* katika kuhakikisha mazingira yetu yanaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya mtu ambaye napaswa pia ku-*recognize* mchango wake kwenye mazingira ni Mheshimiwa Rais, *with due respect*. *She has done a big deal*

kwenye suala la mazingira na ninadhani amepata tuzo mbalimbali za nishati safi. Kwa hiyo, juhudi za hivyo siwezi kuzi-*compromise* kwa mtu aliyefanya hivi, ameonekana anafanya *clip,* anapika kwa kutumia gesi na huo ndiyo mfano ambao kila Mtanzania hiyo ni *modal,* kwamba, kila Mtanzania anapaswa kupika kwa kutumia gesi, ina maana hapa tunaondoa matumizi ya kuni na mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu linakuja. Pamoja na jitihada za kupika kwa kutumia gesi, tumejiandaaje kuhakikisha gesi inakuwa *affordable*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama nchi, tumebarikiwa kuwa na gesi asilia. Ni kwa kiwango gani Serikali imejipanga? Narudia hii na nimeleta maswali kadhaa, kuhakikisha inaweka miundombinu ya gesi asilia, *at least* kwenye majiji. Leo mmekuja na tamko, na mmelirudia kwamba, mnaandaa sera ya kuzuia taasisi zinazopika au zinazohudumia watu zaidi ya 100 kutumia mkaa na kuni, lakini mnajua gharama ya kutumia gesi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua hiyo *LPG* gesi ni biashara! Kwa nini? Tunataka kuongeza gharama za uzalishaji kwenye taasisi, na mkijua kwamba, tuna uwezo wa kusogeza gesi asilia karibu kwenye maeneo ya wananchi, tukapunguza hiyo gharama. Tunasubiri nini kwenye haya matumizi ya gesi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anapokuja kuhitimisha, nitataka Serikali ieleze mkakati wa kuhakikisha tunaanza na Majiji kama Dodoma, tuje Arusha, tuje Mwanza halafu na hizo ndiyo ziwe *modal* na *case study* kuhakikisha taasisi zote, majumba, yanaunganishiwa gesi. Shida ni nini? Gesi zinapatikana nchini, kwa nini, tunaendelea kutumia dola kuwapa wawekezaji, kwa maana ya wafanyabiashara, kuagiza gesi ya *LPG* nje wakati ni gharama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifanya kampeni ya kuwagawia akina mama mitungi. Ninyi mmeona, baada ya kumaliza huo mtungi anapata wapi hela ya kuujaza tena au ilikuwa ni *showoff?* Wabunge tunashukuru, mlitupatia mitungi 200. Baada ya hiyo

mitungi, mwenzenu huwa napigiwa simu, sasa Mheshimiwa tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni lazima tuwe na mpango mkakati wa kufanya habari za gesi ya kupikia ni *sustainable*. Mmeeleza kwenye taarifa yenu kwamba, *NMB* imetenga zaidi ya shilingi milioni 100 kwa ajili ya ku-*finance* wale wanaoanzisha biashara mbadala, kwa maana ya nishati ya kupikia, kama gesi na vitu vingine. Nilichosikia, riba yao ni asilimia moja kwa mwezi. Ina maana ukifanya kwa *twelve months* ni 12% *that is big money*. Kwa nini hiyo gharama inakuwa kubwa kama lengo letu ni kupunguza gharama za watu kutumia kuni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hiyo mkae vizuri na *NMB* wasiwalaghai wananchi wapungeze bei, kama kweli wanataka kumsaidia mama kuhakikisha suala la nishati mbadala linakuwa endelevu. Kwa hiyo, naomba niiweke wazi kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tuanze kutumia *CNG*. Tumeongea mara nyingi kuhusu gesi za kwenye magari. Haya magari tunaweza kutumia gharama kwa kutumia gesi hiyo ina-*cutdown cost,* lakini pia ni *environment friendly*. Hiyo tunaionaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla hatujaanza kuwaza kubana watu na kuwaumiza kwenye kuhakikisha wanaacha kutumia kuni, tuanze kuwaza sasa kuanzisha vituo ambavyo vina gesi tunayozalisha sisi hapa nchini na hatu-*import* nje. Kwa hiyo, hilo la kupiga vita au la kupiga marufuku mkaa na kuni kwenye taasisi, naomba viongozi mliangalie vizuri, kama hamjaanda mazingira msikurupuke kuwaumiza wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine ambacho nilitaka nikiseme hapa ni suala la taka. Kuna mzungumzaji hapa ameeleza vizuri uchafu uliojaa kila sehemu na hapa nidadavue vizuri, Mheshimiwa Waziri leo wakati unasoma hotuba yako, katika Kifungu Na. 66 nimeona ghafla umegeuka Waziri Mkuu, unaagiza Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Yaani unawaagiza TAMISEMI, Halmashauri za Miji na nini, kuhakikisha usafi na mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nashauri Maafisa Mazingira waondolewe TAMISEMI, ili muweze kuwasimamia, lakini kwa sasa kazi wanayoifanya huko TAMISEMI ninyi nyote ni mashahidi kwamba, Halmashauri zetu hazijafanya vizuri kwenye utunzaji wa mazingira. Mmekuwa na wiki za upandaji wa miti, nami huwa nashiriki, ni mdau sana wa upandaji wa miti, lakini ni kwa kiwango gani hizo Halmashauri zinahakikisha zinavyopanda hiyo miti ambayo mmesema ni 1,000,000 inakua?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnaweza mkawa-*task* maafisa wenu badala ya kutoa agizo hapa. Yaani wewe mwenyewe umekiri, tena nime-*quote* hapa, ukasema nakiri kwamba; naomba nitafute hicho kikaratasi nikusomee. Ukasema, "Fungu la 66, bado hali ya usafi wa miji na majiji yetu siyo ya kuridhisha." Mheshimiwa Waziri ukisema hayo, nani atafanya? Yaani wewe ukituambia sisi Wabunge, twende kusimamia! Kwa hiyo, ninachoshauri ni kwamba wale maafisa uwarudishe kwenye ofisi yako, ili uweze kuwasimamia. Itakuwa ni rahisi kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, niende kwenye suala lingine la mazingira, lakini linalowagusa zaidi akina mama. Tunatambua kwamba, wapikaji wakubwa ni akina mama na wanaohangaika wengi ni akina mama. Iwapo tunaweza kuhakikisha upatikanaji wa nishati mbadala, na hasa kwa kupitia mikaa ya mawe na hapa ninaongelea makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tuna Mgodi wa Kiwira na kwa sasa unazalisha makaa ya mawe na vizuri sana ni kama kamati tulitembelea na tumeona inaweza ikawa ni nishati ambayo ni *affordable*. Sasa nitoe wito kwa Serikali kuhakikisha inaongeza fedha ya kutosha kuhakikisha kile kiwanda kinazalisha makaa ya mawe na yasambazwe maeneo mengi, ili yaweze kupunguza hizo gharama za utumiaji au upikaji wa kutumia kuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kabisa, kwa uchache niongelee masuala ya Muungano. Wamesema watu wa bara wengi hawachangii Muungano; hatuchangii kwa sababu, sisi Muungano, *it is part and parcel of our life*. Sisi tumezaliwa tumeukuta Muungano kwa hiyo, hatujui kitu kingine nje ya

Muungano, *we are comfortable* na tunafurahi, tunaona mambo yanayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imani yangu ni uimara wa Muungano unatokana na uimara wa Tanganyika na Zanzibar. Tumia nafasi yako umwagize Waziri wa Mambo ya Ndani atueleze kuna kosa gani la watu kwenda Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana CHADEMA wameenda Mahakamani kuhudhuria kesi ya Mwenyekiti wa Chama, lakini wamezuiwa, wamepigwa, wameumizwa. Kuna kosa gani la kisheria la watu kwenda Mahakamani? Kwa sababu, tunachokitaka ni kuhakikisha Muungano upo salama. Watu kwenda Mahakamani wamekosea wapi? Ni kifungu gani cha sheria kinazuia watu kwenda Mahakamani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo kama hayo, ambayo yanakuwa na ukakasi tukiyaruhusu yakajitengeneza kwenye maeneo yetu ya Muungano, ndio Mwalimu Nyerere aliwahi kusema ukianza mimi Mzanzibara na huyu Mzanzibari, baadaye utasema mimi Mkerewe na huyu nini. Kwa hiyo, tukitoka kwenye Muungano, tukaanza kupambana humu ndani CCM, CHADEMA, itakuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, kuna wimbo unasambaa mtaani na ninyi mmeusikia kwenye *social media*. Kuna mtu alikuwa anaimba, sijui "wapinzani wakifa, mimi siwezi kulia." Hii nchi hatujafikia hapo. "Nitamtupa Kagera awe chakula cha mamba," *Come on!* Naomba msitufikishe hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mama yetu, Mheshimiwa Rais, ambaye ametusimamia na anatuongoza vizuri. Muda wote ameruhusu demokrasia. Wapinzani walifanya mikutano, walifanya maandamano, kulikuwa na shida? Kwa hiyo, leo ndiyo tunaanza kukimbiana, huyu akifa mimi siwezi kulia! Tusiruhusu nchi yetu iende hivyo. Nchi yetu tunaipenda, tumezaliwa na hatuna nchi nyingine zaidi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Anatropia Theonest. Nilimtaja Mheshimiwa Reuben Kwagilwa, Mheshimiwa Abubakari Asenga, ajiandae.

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii nami nipate kuchangia hoja iliyopo mbele yetu. Hoja ya Ofisi ya Makamu wa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii nami niungane na wenzangu nimpongeze sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa *champion* wa utunzaji wa mazingira ndani ya nchi yetu, nje ya mipaka ya nchi yetu, nje ya mipaka ya Afrika na ndani ya dunia. Hoja ya *NEMC* kuwa Mamlaka kamili ni hoja ya kumsaidia *champion* huyu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kutekeleza majukumu yake ya kuendelea kuitumikia nchi yetu katika kuyatunza mazingira, ili nayo yatutunze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 1983 nchi yetu ilikuwa na chombo cha ushauri kwa Serikali na wadau kuhusu masuala ya mazingira. Ilipofika mwaka 1997 tulitunga sera ya mazingira nchini na tukatunga Sheria ya Usimamizi wa Mazingira nchini mwaka huo huo 1997. Vilevile Sheria hiyo ya Usimamizi wa Mazingira Nchini ilitunga pia, uwepo wa Taasisi hii ambayo leo tunayo *NEMC* kwenye Kifungu kidogo cha 16 (1). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Sheria ile ya Mwaka 1997 imeipa *NEMC* majukumu yafuatayo: Jukumu la kwanza ni kufanya ukaguzi wa mazingira kwenye ardhi na jengo lolote. La pili ni kufanya uchunguzi wa kimazingira katika maeneo mbalimbali. La tatu ni kufanya na kuratibu tafiti za kimazingira, kukusanya taarifa na kuzisambaza, na vilevile kupitia taarifa ya tathmini ya athari za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho hapo chini, ukisoma hiyo sheria kuna kubainisha miradi au *program* gani ziingie katika kukaguliwa masuala ya kimazingira. Sasa ukiangalia *nature* ya majukumu haya ya sheria ile ya mwaka 1997 utagundua kwamba changamoto za leo za kimazingira ni nyingi sana na zina wigo

mpana sana kuliko majukumu haya ambayo tumeipatia *NEMC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ile ya mwaka 1997 imegatua mamlaka ya kiutendaji na usimamizi wa mazingira katika makundi yafuatayo; imemtambua Mkurugenzi wa Mazingira wa *NEMC* kama sehemu ya wasimamizi wa mazingira, imetambua Mamlaka za Serikali za Mitaa kama sehemu ya wasimamizi wa mazingira, na ikatambua wizara za kisekta kama wasimamizi wa mambo ya kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hizi wizara za kisekta kuna taasisi kama vile *TASAC, TPA, Deep Fishing Authority, DSFA* pamoja na mamlaka za bonde ambazo zipo chini ya Wizara ya Maji. Wote hao wamepewa dhamana na sheria hiyo ya kusimamia mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa sheria ile ya mwaka 1997 ni kwamba, sheria hii haikutoa mamlaka kwa chombo chochote kuwa msimamizi wa jumla wa masuala ya mazingira nchini. Hapo ndipo shida inapoanzia, kwamba una sheria ambayo imetapanya mamlaka ya usimamizi wa mazingira halafu imeacha hivyo hivyo, haijatoa mamlaka ya kwa chombo kimoja cha kuwa-*supervise* wengine wote ambao wana-*deal* na mazingira. Hiyo *gap* ni kubwa…

*(Hapa kulikuwa na tatizo la vipaza sauti)*

**MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona mitambo imegoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, katika dunia ya leo, jambo linalosumbua uchumi wa nchi zote duniani kwa sasa, iwe ni Ulaya, iwe ni Asia, iwe ni Afrika, yapo mambo mawili tu makubwa ambayo yanaumiza vichwa vya wachumi. Jambo la kwanza ni mabadiliko ya tabianchi na jambo la pili ni mitaji yenye gharama kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la mabadiliko ya tabianchi sisi tusipofika mahali tukalichukulia kwa u-*serious* wake kama nchi, litakuja kuturudisha nyuma sana. Fikiria kwa mfano leo tuna mtandao wa barabara wenye thamani zaidi ya shilingi trilioni 35; mafuriko yakipita tu upande mmoja yamebeba barabara zote. Kama Taifa tunaingia hasara. Hii ni kwa sababu hatujaweka namna nzuri ya usimamizi wa kuyatunza mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa anazozifanya Mheshimiwa Rais, lakini *with this disorganized arrangement* za kisheria, kwa kweli tutakuwa hatumtendei haki Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *weakness* nyingine ya sheria hiyo ya mwaka 1997 ni kwamba haimtenganishi Waziri na shughuli za kila siku za utendaji za usimamizi wa mazingira. Kwa hiyo, unakuta ana dhamana ya kutoa vibali, anatoa leseni, na anatoa vyeti. Waziri kwenye mazingira anatakiwa awe ni ngazi ya mamlaka ya rufaa, kwamba *NEMC* wakifanya mambo, wakitofautiana na wananchi huko, wakitofautiana na taasisi nyingine, wakate rufaa kwa Waziri. Sio kwamba Waziri awe katikati ya utendaji. Kwa hiyo huo ni upungufu wa sheria hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka 2021 tuliamua kama nchi kufanya mapitio, na tukatunga sera mpya tofauti na ile ya mwaka 1997. Kwa nini tulitunga sera mpya? Ni kwa sababu ile ambayo nimetangulia kuitaja, kwamba kulikuwa na ongezeko kubwa la changamoto katika uhifadhi wa mazingira ndani ya nchi na nje ya nchi, lakini kama nchi tulikuwa tume-*ratify,* tulikuwa tumeridhia mikataba mbalimbali ya Kimataifa ya utunzaji wa mazingira, ikatusababisha sasa tutunge sera mpya ambapo sera ile imeelekeza mambo yafuatayo yafanyike:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ikatazame mabadiliko ya tabianchi, kama nilivyosema; ya pili, tukatazame taka za kielekroniki; la tatu, tukatazame uchafuzi wa mazingira unaotokana na uchimbaji wa mafuta na gesi; la nne, tukaangalie usimamizi wa kemikali katika masuala ya mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo haya yote *serious* ambayo tumeyatunga kwenye sera ya mwaka 2021, hatujayatungia sheria. Tunayo sheria ya mwaka 1997, sera tunayo ya mwaka 2021*, it is a contradiction.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yaani unawezaje kuwa na sheria ya mwaka wa zamani sana halafu una sera ya sasa ambayo hujaitungia sheria, lakini mambo yaliyotajwa kwenye hiyo sera bado unayatekeleza kwa sheria ya zamani? Hiyo ni kupapasapapasa mambo na tunaweka reheni usalama wa mazingira ya nchi yetu na kesho ya Watanzania wanaofuata baada ya sisi kupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nafikiri ni muhimu sana, ndiyo maana tunajenga hoja kwamba, ni lazima tuwe na mamlaka ambayo tumeipa dhamana ya kusimamia mazingira, siyo baraza. Baraza lipo kwa sheria ile ya zamani ambayo majukumu yake ndiyo yale nimewasomea ambayo hayaendani kabisa na changamoto za sasa za kimazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka hiyo ya 1997 tulipoitunga hii sheria haikuongelea hata uchimbaji tu, hata madhara ya mazingira kwenye uchimbaji wa madini. Leo tuna migodi mingi, leo tuna athari za mazingira katika maeneo mengi sana. Kwa hiyo ni muhimu sana kutokana na sera hii ya mwaka 2021 tutunge sasa sheria ambayo ita-*accommodate* matakwa ya hii sera. Sheria ambayo itaifanya *NEMC* iwe mamlaka kamili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitawaeleza ni kwa nini tunataka *NEMC* iwe mamlaka kamili? Sababu hizi hapa ninawapa. Sababu ya kwanza, tutaipa nguvu na utekelezaji bora zaidi wa sera mpya, hiyo ninayoiongelea, na kanuni pamoja na sheria tutakayokuwa tumeitunga. Pili, ni kufanya maamuzi kwa urahisi na kutekeleza matakwa ya sheria na kanuni kwa ufanisi zaidi. Vilevile ni kuruhusu matumizi bora ya rasilimali fedha na rasilimali watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti na ndugu zangu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti ya Bunge hili. Nafahamu namna ambavyo *NEMC* hawana fedha wala ubavu wa kuweza kutekeleza

changamoto zilizo mbele yao. Sasa tukiifanya hii kuwa mamlaka kamili, maana yake tuta-*consolidate* vyanzo vyote vya kazi wanazozisimamia ili zirudi kwao wakatekeleze majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huwezi ukawa unakusanya senti zinazotokana na uharibifu wa mazingira, halafu hurudishi kufanya ile *restoration* ya mazingira. Hatuwezi kwenda hivyo. Ikiwa mamlaka maana yake ni kwamba tutaainisha na *sources* zake kwenye sheria itakayoanzisha hiyo mamlaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kwamba, *NEMC* ikiwa mamlaka, tutaipa mtazamo wa kuaminika kwa umma. Mniwie radhi sana niseme, katika taasisi ambazo jamii yetu ina mashaka nazo sana ni pamoja na *NEMC*. Yaani ukiona jambo lako *NEMC* ni shida, kibali kitachukuwa muda mrefu sana, kila kitu kitachukuwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu kwa kuwa sheria imegawanya gawanya majukumu, unakuta hapa Afisa wa Serikali za Mitaa anayehusika na Mazingira aliyetajwa hapa amepita na amechukuwa tozo, halafu tena *NEMC* naye anapita hapo hapo tena anatoa maelekezo mengine. Kwa hiyo, ni *contradiction, a total of contradictions! (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanyeni hivyo kuanzisha mamlaka mpya ili tuongeze ushirikiano wa Kimataifa kwa nchi nyingi duniani, kwa sababu nchi zote nyingine zilizo nyingi zinatumia mamlaka za mazingira badala ya Baraza la Mazingira. Kwa hiyo, unakuta hata kiutendaji nchi zikikutana kukaa kuongelea mazingira, wakiitwa watendaji wa mamlaka, sisi hapa unaweza ukashangaa akalazimika kwenda Waziri. Huyu hawezi kuongea lugha moja na wale ambao ni watendaji *typical* kutoka kwenye mamlaka hizo nyingine za nchi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nashauri tufanye hivyo ili pia mamlaka iongeze wigo mpana zaidi wa majukumu ikijumuisha uangalizi na tathmini ya kina ya athari za mazingira, lakini vilevile uthibiti wa uchafuzi wa mazingira na utekelezaji wa mipango endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuifanya *NEMC* kuwa mamlaka, ni suala ambalo haliepukiki kama kweli tuna nia ya dhati ya kumsaidia Mheshimiwa Rais kuendelea kuwa *champion* wa kutuhudumia Watanzania na dunia nzima kwenye suala la utunzaji wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kwagilwa Reuben. Nilimtaja Mheshimiwa Abubakari Asenga, na Mheshimiwa Pauline Gekul ajiandae na baadae Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ajiandae.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Kwa Kiswahili tunasema ni saada na sudi na bahati iliyo njema kupata nafasi nami ya kuchangia katika Wizara hii nyeti katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema mambo mawili tu makubwa ambayo, moja ni mazingira na la pili ni la Muungano. Kwa kuanza na mazingira, tumeona takwimu nyingi sana zikirudiwa kuhusu namna kila mwaka nchi yetu inavyoteketeza hekta za misitu kwa ajili tu ya mkaa. Kutokana na hali hiyo, ndipo tunapompongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona hatari hiyo na kuanza kutoa gesi, na kuhakikisha uwekezaji mkubwa unafanyika katika gesi kiasi kwamba gesi ifikie kununuliwa kwa bei rahisi kwa kila Mtanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naipongeza Wizara chini ya Mheshimiwa Makamu wa Rais na Waziri kaka yetu Mheshimiwa Masauni, Katibu Mkuu na viongozi wote ambao wameweza kushirikiana na Wizara ya Nishati ili kuhakikisha jambo hili la gesi linakwenda vizuri, na ni jambo la msingi sana. Kwa hiyo, nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba ukifikiri hekta laki moja tunateketeza kwa mwaka; na nimemsikia Mheshimiwa Waziri Jafo wakati fulani akizungumza akitaka kuweka mpango wa

kuzuia Dar es Salaam; kuna wakati watazuia mkaa; nikawa nazunguka kule Kilombero Jimboni, napima hekta moja, mbili yaani nione hekta kumi ukubwa wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hekta laki moja, siyo ndogo. Katika mambo ambayo tunatakiwa tuwekeze kwa nguvu, basi ni kuzuia kuteketea kwa misitu yetu, kwenda kutengeneza mkaa. Tuache kabisa habari hiyo na tusahau habari ya mkaa. Mtu akikamatwa amekata mti uliokaa miaka 100, mti ambao umekaa miaka 60, mti ambao umekaa miaka 50, anakata anachoma mkaa, hiyo iwe ni jinai na ni kosa la jinai kabisa, tufikie wakati huo; lakini huwezi kumhukumu Mtanzania kwa sababu hujamfikishia nishati mbadala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maonesho tuliona hapa Bungeni wakati fulani, tulipewa majiko hata ya umeme, ambapo kumbe unaweza kuwa na jiko la kisasa la umeme linalotumia umeme chini zaidi kuliko hiyo gesi, na wengine tukayanunua hapa yanachemsha maharage kwa *unit* ndogo kabisa. Hiyo pia ni njia mbadala ya kupelekea watu. Tuna umeme wa megawati 2,115, tupeleke umeme huu watu wanunue, yale majiko pia yasambazwe bila kodi, watu waache kupikia mkaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ningelikuwa na mamlaka Dar es Salaam ingekuwa ya kwanza kuacha kutumia mkaa. Nenda Dar es Salaam, pishana na malori kwenye foleni yaliyobeba mkaa, ukiangalia ukisema hii ndiyo miti ya nchi yangu na miaka 50, miti ina miaka 100 ni hatari. Siyo jambo la kuleta masihara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama viongozi wetu, Mheshimiwa Waziri, na hii ni sekta mtambuka, wanaweza wakaamua jambo hilo, majiji yetu yaache kutumia mkaa ili tunusuru miti ndani ya nchi hii. Hakuna miti itayopandwa ama hii inayopandwa pandwa huku itakayolingana na hii miti tunayokata ya miaka 100, hadi miaka 50, hakuna kitu kama hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kuwa kiongozi Rombo pale kwa Prof. Mkenda, Moshi, Kilimanjaro. Kukata mti ni kama umeiba, umevunja nyumba ya mtu. Mimi nilikuwa *DAS*, ilikuwa

unatuonesha miti minne uliyopanda ndiyo tunakupa kibali cha kukata mti mmoja, na kibali hicho kinatolewa na *DC,* anajua kuna mti unakatwa Kata fulani leo chini ya uangalizi wa mgambo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini baadhi ya maeneo katika nchi hii tunakata miti tunavyotaka. Nafikiri hili siyo jambo zuri. Kwa hiyo, nataka kusisitiza hapo. Nimeongea sana kwa sababu takwimu zinavyotolewa hivyo zinaonekana kama ni takwimu rahisi rahisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kwenye mazingira, waweke nguvu kwenye maeneo yenye misitu ambayo haijaguswa, kama vile Kilombero kule kwetu. Ukifika kule unaona giza la miti ya Udzugwa na Hifadhi ya Nyerere. Walinde na wahakikishe kuwa wanawapa wananchi gesi hata bure ili wasivamie misitu na kukata miti na kuokota kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, waelekeze nguvu kama Kilombero kule ambako tuna mradi wa kuzalisha umeme wa Kidatu unaotokana na maporomoko ya maji ambayo hayakauki kwa sababu tunatunza miti; tuna Kihansi, haikauki kwa sababu tunatunza miti. Kwa hiyo, watusaidie kutuletea gesi ili tusiendelee kukata miti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kumalizia upande wa Muungano. Sisi tuliopata bahati ya kusoma Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere pale na kusikiliza hotuba za Mwalimu Nyerere, katika maisha yake, unaweza kusema aligusia sana suala la Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inataka kusema hapa, sidhani kama ninazikumbuka zile hotuba, lakini Mwalimu amezungumza mambo mengi sana kuhusu Muungano. Kuna hotuba maarufu ya Mwalimu Nyerere anazungumzia nyufa tano za nchi hii. Anasema "nyumba yetu ilipotikisika tuliona nyufa. Nyingine katika paa, nyingine katika dari na nyingine katika sakafu." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, akataja ufa wa rushwa, akataja watu kupuuza sheria, ukabila, udini, lakini akachukua muda mrefu

kuzungumzia Muungano. Akasema "kumbukeni kinachowafanya mseme sisi Wazanzibar, wao Watanganyika ni dhambi ya ubaguzi na huu Muungano uliopo, kwa sababu sisi leo tuna Muungano wa Tanzania tunawaona Wazanzibar; kwa sababu tuna Muungano wa Zanzibar, wanawaona Watanganyika."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ndiyo ilikuwa sababu ya kwanza Mwalimu Nyerere anasisitiza *East Africa* iungane, akiwaambia, Kenya kuna makabila, Uganda kuna makabila, tukiungana katika East Africa hamtatazamana ndani ukabila wenu, mtaangalia Tanzania, mtaiangalia Uganda na mtaiangalia Kenya, kwamba tukichelewa wenzetu watatupita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa leo tunazungumza habari za ubaguzi. Kuna viongozi wachache wanaozungumza mambo ya ubaguzi. Tunajua kuna siasa ndani yake, nikupe siri. Mimi najua, vipo vyama vya siasa vilikaa vikasema hii CCM kwa Muungano huu huwezi kuing'oa kwa sababu inakubalika huku, inakubalika huku. Tupambane, tupate sehemu ya Tanganyika, tuwe na Serikali ya Tanganyika. Tukifanya Serikali ya Tanganyika kuna siku tutaongoza nchi hii. Wanajidanganya, kuna watu waliozaliwa baada ya Muungano hawawezi kukubali hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mwalimu Nyerere anasemaje? "Dhambi ya ubaguzi mkishaitenda mtaendelea, ni sawasawa na kula nyama ya mtu. Mkila nyama ya mtu mtaendelea tu kula, hamtaacha, mtatengana na Wazanzibar." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu anasema kwamba, "wale watakaowashangaa wenzao wakiwatenga watabaki salama." Hotuba maarufu kabisa anasema, "Wazanzibar wakiwakataa Watanganyika kwa dhambi ile ile ya ubaguzi, wao wana Rais, sisi hatuna Rais, kwa nini?"

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu ni zile zile za kitoto ambazo viongozi leo wanazirudia kwenye vyama vya siasa. Wanaona wivu Rais wa Zanzibar. Mwalimu alishasema, mtawakataa Wazanzibar mtasema wao Wazanzibar, wao wana Rais, sisi

hatuna Rais, kwa nini? Akatoa mfano mpaka wa Rais Einstein. Mtawafukuza Wazanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu alizungumza hilo kwa upande wa Tanganyika pia; mtakuta kumbe mlijidanganya tu. Hapa kuna Wazaramo, kuna Wachanga, kuna Wapare, mtamaliza kuchoma nyumba za Wapemba mtakuta kumbe hamjabaki wamoja kama Watanganyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu akarudia tena, Wazanzibar wakiwakataa Watanganyika, Watanganyika watabaki wanawashangaa Wazanzibar watasema, wenzetu wanatuacha kwa nini? Kwa dhambi ile ile ya ubaguzi, Wazanzibar nao hawatabaki salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo hiyo hotuba maarufu utakuta kuna Wazanzibar na Wazanzibara. Sasa leo tunauliza, kama Mwalimu alizungumza miaka hiyo jambo hilo na Mheshimiwa Shangazi ametuambia sasa hivi tuna changamoto, hatuna tena zile kero za Muungano, tukiacha siasa Muungano wetu ni jambo la msingi kuliko kitu kingine chochote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napendekeza Mezani hapa kwamba lazima tuwe *very serious* kwenye jambo la Muungano. Vyama visajiliwe, endapo vinaamini Muungano; na sisi hatuna shida na aina ya Muungano, tukienda kwenye uchaguzi mkuu Oktoba, *ACT* nenda kaseme nataka Serikali 10, CCM sema nataka Serikali mbili, CHADEMA nenda sema nataka Serikali tatu, na nani na nani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweke sheria hapa, tukishachaguliwa na wananchi wanaochagua CCM, wamekubaliana na aina ya Muungano wa Chama cha Mapinduzi, hakuna mjadala mpaka uchaguzi mkuu ujao, hakuna kuruhusiwa kusema baada ya uchaguzi kama sera zako zilikataliwa, unazungumza kwa watu kuhusu kubagua nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yupo kiongozi mmoja wa siasa anaongea kuhusu Muungano kama anaongea kuhusu takataka fulani hivi, watu wanamwangalia, vyombo vinamwangalia. Mimi namwombea mema atoke kule alipo, lakini vyombo vinamwangalia yeye na watu wanamwangalia, anachezea Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo suala hata la Mahakamani kuweka hiyo kesi kwenye *TV,* kwani ni suala la kimuungano? Siyo suala la kimuungano, lakini ninachozungumza, sisi Watanzania leo tunaona suala la kutengana kuwa na Serikali ya Tanganyika ni kitu rahisi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato ulifanyika, viongozi wetu waliona busara, mapendekezo ya katiba yalikuja, watu wakayapinga, wakasema subiri kwanza twende kwanza kutoa elimu…

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga, kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Dkt. Joseph Mhagama.

**TAARIFA**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba nimpe taarifa mzungumzaji, anaongea vizuri kaka yangu, lakini kwa lengo la kuulinda Muungano huu, naomba ikiwezekana Muungano huu upewe kinga ya kikatiba, asiruhusiwe mwanasiasa yeyote kuugusa Muungano wetu, kwani ndiyo heshima, ndiyo tunu na ndiyo utambulisho wa Utanzania wetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asenga, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikukumbushe, wakati wa Bunge la Katiba yupo kiongozi mmoja wa vyama vya siasa alisema “Muungano huu hauna mkataba, ni feki.” Mimi nilikuwa pale Umoja wa Vijana. Sisi tuliiomba Serikali wakaenda kufungua sanduku la chuma kutuletea mkataba ule wa Muungano, tukau-*print* kwenye *t-shirt,* tukauvaa kwa maandamano katika nchi hii. Akasema, na huo mkataba wenyewe siyo saini ya Nyerere wala Karume. Huyu mtu anatumika na nani? Kwa nini tunaacha mambo kama haya? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kupendekeza, kwamba jambo la msingi msicheze nalo. Sisi CCM tunasema kuwa ni aina hii ya Muungano mpaka tutakapokuja kubadilisha Katiba. Kama kuna chama kingine kinaamini aina ya Muungano, ukishachaguliwa, kama hujachaguliwa hauna haja ya kuendekeza hii *slogan* yako ya kubagua nchi hii kwa chuki ambazo hazina maana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Abubakari Asenga. Nilimtaja Mheshimiwa Pauline Gekul, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano ajiandae.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi. Najua muda wangu ni mchache dakika tano, nakushukuru sana. Pia, namshukuru Mungu kwa kutupa nafasi ya kutekeleza majukumu yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwa kinara wa nishati safi na salama. Pia, nampongeza Naibu Waziri Mkuu na Wizara yake kwa kufanikisha hili ambalo Mheshimiwa Rais wetu, mama yetu ametamani, gesi kupatikana kwa Watanzania kwa bei ya ruzuku. Nawapongeza sana, sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nakupongeza kwa kazi kubwa unayofanya. Ninaamini pia na Wizara yako ni sehemu ya jambo hili la Mama ambalo limegusa maisha ya

Watanzania wengi, kupata mitungi ya gesi kwa bei nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri tu kwa ile mikoa ambayo bado programu hii haijafika, iweze kufika mapema. Hii itasaidia kuokoa misitu yetu na itasaidia akina mama wale ambao walikuwa wanasubiri kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa nishati safi, nashauri tu kwamba tumefanikiwa sana kwenye masuala la haya mapishi. Sasa hivi hakuna nyumba ambayo haina mtungi wa gesi ule mdogo. Naomba watafiti wetu waangalie ni jinsi gani ya kuboresha ile mitungi ipatikane kwa *package* ya Mtanzania. Kama ni shilingi 2,000 wakati anafanya *refilling,* wakati anakwenda kujaza. Hiyo *package* iweze kupatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunaweza tukatoa mitungi hii sasa kwa bei ya ruzuku halafu ukashangaa watu wanapeleka kwenye vyuma chakavu au wakatumia kwa matumizi mengine. Kwa hiyo, naomba watafiti wetu watusaidie zile *packages* za gesi ziweze kum-*fit* kila mmoja wetu. Mwenye shilingi 10,000 na mwenye shilingi 5,000. Hii itasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunaboresha *packages* kupitia utafiti, waangalie pia katika *packages* hizo pawepo na sehemu ya kuoka au kuchoma, kwa sababu kinachomaliza misitu yetu kwa sasa siyo kupika vyakula hivi ambavyo watu wanapika, labda wali, ugali au vile vya kuchemsha. Vyakula vya kuchoma ndiyo vinamaliza sasa mkaa na unaona kila siku magunia ya mkaa yanavunwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba katika kuboresha kwenye utafiti, zile *packages* za gesi pawepo na sehemu ndogo ya kuchomea hata kama ni ule mtungi mdogo, ili anayetaka kuchoma chochote pale nyumbani, basi atumie. Kwa sababu matumizi mengi ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Waweze kuwa na *package* hiyo na wakati huo iweze kusoma pia ile gesi inayotumika. Mtu ajue, yaani iwe kama mita ya umeme tu, mtu afahamu kwamba gesi yangu imebaki kiasi gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais kwa kweli amelisukuma hili na tunaona Serikali inafanya vizuri. Sasa wafanye utafiti kuboresha hili ili liwafae watu wote ambao wanatumia hii nishati safi na salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *TFS*, wanatusaidia sana kulinda misitu yetu. Nilikuwa nadhani wao kuendelea kuwepo Maliasili, kwa mawazo yangu wangehamia Mazingira kwa sababu wanatupatia miti. Nawapongeza sana, kwani tunapanda miti ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishauri pia aina ipi ya miti ambayo tunaweza tukapanda kwa ajili ya mazingira yetu. Wao wanapambana pia; na adui yao mkubwa ni watu wa mkaa ambao wanahusiana na Ofisi ya Mazingira. Nadhani ikipendeza sasa, waweze kuhamia upande wa mazingira ili washirikiane kwa pamoja badala ya kubaki na *component* ndogo ya utalii wakati wao kazi zao kubwa ni uhifadhi na kulinda misitu yetu kwa ajili ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ikiwapendeza *TFS* washirikiane na Wizara ya Mazingira. Siyo kwamba hawashirikiani, lakini wakiwa pamoja wanaweza waka-*plan* pamoja na ku-*implement* pamoja, ikapendeza zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la pili ni kuhusu vyanzo vya maji. Natamani nione kwenye Wizara hii kuwe na bajeti ya kusafisha na kutunza maziwa yale madogo madogo ambayo yamekuwa yakitusaidia sana kwenye vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natolea mfano kwenye Jimbo langu. Sisi Wanababati vyanzo vyetu vyote vya maji vinatokana na Ziwa Babati. Yaani visima vyote vya Wizara ya Maji vimechimbwa pembeni ya Ziwa Babati, lakini ziwa hili liko upande wa mazingira na wenzetu wa uvuvi pia wana samaki wao mle. Je, ni nani anasafisha lile ziwa sasa? Sisi kama halmashauri tumejitahidi, tumesafisha. Tulitumia shilingi milioni 30, tukachukua vijana wetu tukawapeleka pale wakaenda *manually* kuvuta yale magugumaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini haya matatizo Mheshimiwa Waziri wetu wa Mazingira na Muungano hayako Babati tu, na bahati nzuri Naibu wake aliwahi kufika kule. Nadhani kwenye *components* za bajeti yao waweze kuweka *item* ya kusafisha haya maziwa, magugumaji yatolewe. Tutenge fedha, siyo kwa Ziwa Babati tu, tuna... *(Makofi)*

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, kuna Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Ni kwamba haya magugumaji anayozungumza Mheshimiwa, yako katika Ziwa Victoria kwa kiwango kikubwa. Imefikia mpaka *ferry* zetu sasa zinaharibika, lakini Mheshimiwa Waziri hajaja hata kuyaangalia hayo magugumaji yaliyoko pale Sengerema na Kigongo. Nakushukuru sana, endelea Mheshimiwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, unaopokea hiyo Taarifa?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa ya Mheshimiwa mwenzangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani kwa kuwa suala la matumizi ya ziwa ni suala mtambuka; wavuvi, maji, na mazingira nawaomba watenge bajeti. Basi tukubaliane kama Serikali, bajeti hiyo inakaa wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi sisi Wanababati baada ya kutenga shilingi milioni 30 kuwapeleka vijana kutoa yale magugumaji, kuna wakati walifika kwenye kina kirefu hawawezi kuendelea tena na wakafurahia lile zoezi kabisa. Halafu pia baada ya kusafisha na kuondoa yale magugumaji tukaanza kupata samaki wakubwa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwenye maziwa yetu kote nchini, iwe Ziwa Tanganyika, Ziwa Victoria, Ziwa Basotu au ziwa lolote tu, Wizara ya Mazingira wapewe fedha...

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Taarifa inatoka wapi? Mheshimiwa Issaay.

**TAARIFA**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mchango mzuri wa dada yetu Mheshimiwa Gekul, Wizara imetuma wataalamu miaka mitatu kutembelea Ziwa Babati na Ziwa Tlawi katika Halmashauri ya Babati na Halmashauri ya Mji wa Mbulu, lakini taarifa hiyo mpaka leo haijarudi katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul, unaipokea hiyo Taarifa?

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea Taarifa ya Kaka yangu Mheshimiwa Issaay wa Mbulu. Mheshimiwa Waziri, ninakuomba kaka yangu, wewe ni mchapakazi, Naibu wako na Serikali yetu. Nakuomba basi mtenge *vote* kwa ajili ya kusafisha haya maziwa na mje na teknolojia, siyo *manually* tena kama tunavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imebidi sisi tutenge *1.8 billion* sasa hivi kwenye bajeti hii, tumeomba Hazina, na kwa kuwa Serikali iko hapa, na wote mnafanya kazi kwa pamoja, mtupitishie na hizo fedha, mje mwone tunavyoondoa *manually* na vijana wetu, lakini mtuletee teknolojia sasa ili kuondoa haya magugumaji, inaweza ikasaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, muda wangu umeisha. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Pauline Gekul.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais. Nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge, na Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Waziri Mheshimiwa *Eng.* Hamad Yussuf Masauni, Mbunge, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ushindani wa Kimataifa *(National competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni: "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimamizi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno ikiwemo kuimarisha Muungano na usimamizi thabiti wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi tisa, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, imesimamia kwa ufanisi utekelezaji wa kulinda na kuimarisha Muungano wetu. Pia, naipongeza Serikali kwa mwendelezo mzuri wa kusimamia mikakati ya kulinda mazingira na kupambana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi hiki wakati dunia inapambana na athari za majanga ya mabadiliko ya tabianchi, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, imetekeleza kwa ubunifu mkubwa mikakati ya kulinda mazingira yetu, ikiwemo matumizi ya nishati mbadala na biashara ya hewa ukaa *(carbon credit)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua ya kuweka ruzuku kwenye gesi ya kupikia ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya matumizi ya nishati mbadala kwa wananchi. Matumizi ya gesi kwa kupikia imeongezeka kwa kiasi kikubwa na hii ni ishara ya kupunguza matumizi ya kuni na kulinda misitu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekit, kuna ongezeko kubwa la biashara ya hewa ukaa *(carbon credit)* na kutokana na fursa za biashara hii kuinua uchumi wetu, napendekeza Serikali iongeze msukumo

wa elimu ya biashara hii kwa halmashauri zote na hata taasisi zinazosimamia misitu na hata rasilimali nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iweke mkakati wa kuhakikisha mapato ya fedha za kigeni yanaongezeka kupitia mazao ya biashara ya hewa ukaa. Kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni yatasaidia kuimarisha uhimilivu wa Deni la Taifa na pia kuendeleza utulivu wa shilingi yetu dhidi ya sarafu kuu za kigeni na hata kuhakikisha utulivu wa mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali naomba ihakikishe kipaumbele cha kuwekeza kwenye sekta zinazolinda mazingira, ikiwa ni pamoja na mwendelezo wa *SGR* kutokana na kutumia umeme unaotokana na vyanzo vya maji na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza pia maboresho ya *TAZARA* yalenge kuwa ya treni za kutumia umeme na hata msisitizo wa matumizi ya umeme au gesi kwa vyombo vya usafiri. Serikali inashauriwa kuchukua hatua zaidi za kuimarisha usimamizi wa kuhifadhi mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kidunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na athari za kiuchumi uliokumba dunia nzima ikiwemo changamoto za upatikanaji wa fedha za kigeni, hatua za kuimarisha sekta hizo hapo juu, inaweza kuwa fursa kwa Serikali kupunguza matumizi ya fedha za kigeni kununua mafuta na wakati huo huo kuwa na ongezeko la fedha za kigeni kupitia biashara ya kaboni *(carbon credit)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza sana Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa *Eng.* Hamad Yussuf Masauni, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Khamis Hamza Khamis, Mbunge na wataalamu na wadau wa Wizara hiyo kwa kazi kubwa wanayofanya. Pia nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu leo utahusu suala la waokota taka hapa Tanzania. Uchafu ni kitu chochote kilichopo katika mazingira ambacho husababisha kero na uchafuzi. Mifano ya uchafu tunaoishi nao kwenye mazingira yetu ni taka za kutoka kwenye majumba yetu, vyuma chakavu na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchafu huu wa mazingira una madhara makubwa kwenye udongo, hewa na maji. Kwa ujumla uchafu siyo rafiki kwa binadamu na viumbe wengine. Waokota taka wamekuwa na mchango mkubwa sana wa kuziondoa taka hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kundi la waokota taka limekuwa na mchango mkubwa kwenye utunzaji wa mazingira hapa nchini. Kundi hili hubeba jukumu muhimu katika kupambana na uchafuzi wa mazingira. Pia hutoa mchango mkubwa kwenye kuokota taka kama chupa za plastiki, vyuma au mabati ambavyo hurudishwa kwenye mfumo na kuchakatwa na kutengeneza bidhaa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa mchango wa kundi hili hapa nchini ni mkubwa sana, lakini bado hawajatambuliwa kisheria hapa nchini Tanzania. Hivyo basi, ni vyema Serikali ikachukua hatua madhubuti za kusaidia na kulitambua kundi hili ikiwa ni pamoja na kuwalinda kisheria na kisera ili mchango wao katika usimamizi wa taka nchini Tanzania uimarike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo linahitaji umakini, kwani waokota taka ni sehemu muhimu ya mfumo wa utunzaji wa mazingira hapa nchini. Hawa wasingekuwepo, taka zingesababisha kero kubwa kwenye mazingira na mifumo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na umuhimu wa waokota taka hapa nchini Tanzania, wamekuwa wanakutana na changamoto mbalimbali, kama vile:-

(i) Kuwepo mtazamo mbaya kutoka kwa jamii kwa kundi hili. Huko mitaani waokota taka hukutana na unyanyapaa wa

kijamii ambapo jamii inawaona kama watu wasio na hadhi kwa kuona kwamba kazi wanayofanya ni duni; na

(ii) Waokota taka hawana vifaa vya kuwalinda kiafya. Kwa ujumla, waokota taka wana ukosefu mkubwa wa vifaa vya kujikinga na madhara mbalimbali. Hivyo basi, ni vyema Serikali ikahakikisha kwamba waokota taka wanapatiwa vifaa vya kujilinda dhidi ya hatari za afya zinazotokana na mazingira ya kazi yao.

Mheshimiwa Spika, kutokana na unyeti wa jukumu lao hili, ni vyema Serikali ya Tanzania ikachukua hatua za haraka kutambua mchango wao na kuboresha mazingira ya kazi yao. Hivyo basi, napendekeza Serikali ichukue hatua za kutambua rasmi waokota taka wa Kitanzania kwa kuweka sheria na sera zinazowatambua, kwani wao ni sehemu muhimu ya mfumo wa usimamizi wa taka.

Mheshimiwa Spika, naomba hapa nitofautishe wazo langu la waokota taka na Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni zake ambayo imetoa mamlaka katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa nchini kusimamia Sheria ya Taka Ngumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MHE. BAHATI KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikupongeze wewe binafsi kwa kazi nzuri unayoifanya katika kutuongoza vyema katika Bunge hili, pia nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Masauni, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Naibu Waziri wake pamoja na Watendaji wote wa Wizara hii wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu ya Muungano ni jambo muhimu hasa ukilinganisha kuwa Watanzania wengi waliopo sasa ni kizazi kipya na hawana kumbukumbu sahihi

kuhusu Muungano wetu. Hivyo, nawapongeza na kuiomba Wizara hii iendelee kutoa elimu hasa kwa vijana, lakini pia kushusha elimu hii hadi mashuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza Serikali kwa kuratibu vizuri masuala ya kiuchumi na kijamii baina ya Tanzania Bara na Zanzibar na kuiwezesha Zanzibar kupata mgawanyo wake wa zaidi ya shilingi bilioni 49.2. Fedha hizi zimeiwezesha Zanzibar kutekeleza miradi yake na kutatua changamoto mbalimbali za wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuwatendea haki wananchi wa Taifa hili. Kwa kweli tunasema Mama ahsante sana kwa kazi kubwa unayoendelea kututendea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunapenda kumpogeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika miaka hii minne ya Mheshimiwa Rais imekuwa ya neema na baraka kubwa katika nchi yetu kwa sababu ameleta miradi mingi mno ambayo toka Taifa hili lipate Uhuru haijawahi kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa kufanikisha ujenzi wa kuta mbili yenye urefu wa jumla ya wastani wa 325 katika eneo la Sipwese, Mkoa wa Kusini, Pemba. Hakika jambo hili ni jema sana na linafaa kupongezwa kwa kuwa limesaidia sana kuzuia maji ya bahari yasilete athari kwa mashamba ya wakulima wa eneo hilo na kuwawezesha wananchi hasa wanafunzi kupita vizuri katika eneo hilo wakati wote bila kujali na kujaa kwa maji ya bahari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, naomba sana Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na kuangalia vyema ukuta mmoja kwa kuwa unazuia na kusababisha maji ya mvua kubaki jambo ambalo linaleta athari nyingine za mafuriko katika eneo hilo. Aidha, naomba Ofisi hiyo pia iendelee kujenga kuta na matuta katika maeneo mengine kwa kuwa kwa maumbile yake, Zanzibar inapata athari kubwa za maeneo mengi kuingia maji ya chumvi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza sana Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwezesha Tanzania kuwa Mwenyekiti wa Kundi la Majadiliano la Afrika la Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kipindi cha miezi tisa ijayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ushauri kwa Serikali kutumia fursa hiyo ipasavyo ili kuhakikisha Tanzania inapata fursa za kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha, teknolojia, utaalamu katika masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya hewa ya Kaboni; pia nazishukuru sana Serikali zote mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kutayarisha Kanuni za Usimamizi wa Biashara ya Hewa ya Kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa biashara hii ni mpya, naomba Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuendelea kujenga uwezo stahiki na wadau wote wa Bara na Zanzibar wakiwemo Waheshimiwa Wawakilishi, Madiwani na Masheha na watendaji mbalimbali wa ngazi za Serikali Kuu na Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira pamoja na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuendelea na ushirikiano mzuri kwenye sekta ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. Kwa hakika ushirikiano mzuri uliopo baina ya Ofisi hizo, *NEMC* na *ZEMA* unafaa kuigwa, kupongezwa na kuendelezwa. Maoni yangu ni kuwa ushirikiano huo uendelee kudumu ili kuhakikisha athari za kimazingira na mabadiliko ya tabianchi yanapungua siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana.

**MHE. ZULFA MMAKA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uhai na uzima wake. Pia, tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa jinsi ambavyo anaendelea kutuongoza vizuri na utu juu yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie kuhusu suala la mazingira na tabianchi. Kwa upande huu napenda kugusia suala la mmomonyoko wa ardhi katika eneo la Kijiji cha Tibirinzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Tibirinzi linasumbuliwa na shida ya kuingiliwa na maji ya Bahari. Suala hili tumeshalizungumzia sana ila bado halijapatiwa Suluhu. Naomba sana Serikali au Wizara waliangalie suala hili kiupekee, kwani eneo hili wananchi wanalitumia kwa shughuli za kilimo. Naomba sana suala hili lipatiwe suluhu ili wananchi waendelee na shughuli zao za kujipatia riziki hususan akina mama wanaofanya kilimo eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake na kampeni kabambe ya kutunza mazingira hasa hasa pale alipoamua kugawa gesi nchi nzima ili wananchi waweze kuachana na uchafuzi wa mazingira hasa ukataji wa kuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gesi hizi zimekuja kumtua mama kuni kichwani. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa jambo hili na uwekezaji mkubwa kwenye suala zima la upatikanaji wa gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanazozifanya ya kumsaidia Mheshimiwa Rais, *Allah* atawalipa kwa ujira wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishie kwa kusema naunga mkono hoja hii.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Naibu Waziri, nina tangazo dogo la wageni ambao wapo Bungeni jioni hii. Tuna wageni wa Waheshimiwa Wabunge.

Tunao wageni 45 wa Mheshimiwa Nashon William Bidyanguze, Mbunge, ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM)*. Karibuni sana wanafunzi wetu kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM*. *(Makofi)*

Pia, tuna taarifa pia kutoka kwa Meneja wa Bunge *Sports,* anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote, kesho saa moja kamili asubuhi kwenye Uwanja wa Jamhuri hapa Dodoma kutakuwa na mechi baina ya *Bunge Sports* na *Kunduchi Veterans*. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa na wanamichezo wote mnaombwa kuhudhuria bila kukosa. Vigezo, masharti na utaratibu utazingatiwa. *(Makofi)*

Baada ya tangazo hilo, sasa namkaribisha Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Khamis.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nachukua fursa hii kumshukuru Mungu kwa kuwa ametujalia kukutana hapa tukiwa wazima wa afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nachukua fursa hii kukushukuru wewe, na kwa haraka haraka nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wote kwa ujumla ambao wamechangia ama wametoa michango yao kwenye bajeti hii. Kwa hakika michango yao ilikuwa iko *very constructive* na yale yote ambayo wametushauri, tumetelekeza na wamependekeza, tutaona namna ambavyo tunaenda kuyafanyia kazi kwa maslahi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana wananchi wangu wa Jimbo la Uzini kutoka Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Kati Unguja kwa kuniamini na ninawaomba sana waendelee kuniamini. Kwa

sababu kazi tunayoifanya ni kubwa, na ninyi Waheshimiwa Wabunge, Chama na Serikali inaona mchango wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nataka niseme maneno mawili ambayo yatakuwa yana mambo mengi ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hakika ni kinara wa mazingira, na amekuwa kinara wa mazingira wa Tanzania, Afrika na Duniani kote. Hii ni kwa sababu kabla ya kuwa Rais tayari ilikuwa ameshaanzisha kampeni mbalimbali za mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alikuja na Kampeni ya Kusoma na Mti. Kama ambavyo mnaelewa tuliwataka wanafunzi wote wa chuo, sekondari na msingi, wote tuhakikishe kwamba wanapanda miti. Pia, alikuja na kampeni ya nishati safi ya kupikia ambayo sasa imekuwa ndiyo ajenda ya dunia. Vilevile, alikuja na kampeni kubwa ya utunzaji wa vyanzo vya maji. Kwa mnasaba huo tunasema, Daktari ni kinara wa mazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Rais amekuwa akishiriki katika mikutano mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa, ambayo ilikuwa ina mnasaba na masuala ya mazingira. Ninyi ni mashahidi, tumekuwa tukimwona kwenye *Cops* mbalimbali na mikutano mingine inayogusa masuala ya mazingira na mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kadiri ambavyo tunakutana na nchi hizo na Mataifa hayo, huwa tunajaribu kuwaeleza namna ambavyo nchi zilizoendelea ziendelee kusaidia nchi zinazoendelea katika suala zima la kusaidia kutatua changamoto ya mazingira na athari kubwa ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amekuwa kinara wa mazingira kwa sababu ametoa fedha nyingi sana ambazo zimekuja kutengeneza miradi ambayo imekuja kusaidia kwa namna moja ama nyingine katika suala

zima la mabadiliko ya tabianchi katika nchi yetu. Iko miradi iliyokuja, ile ya *EBA*, kuna miradi iliyokuja kwa sababu ya ku-*control* changamoto ya uharibifu wa tabaka la *ozone*. Pia, iko miradi mingine ambayo moja kwa moja ilikuja ikaleta sura ya kimazingira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndiyo muumini wa kweli wa Muungano wa Tanganyika na Zanzibar na katika hili ameonesha kwa vitendo. Leo Muungano tulionao una umri wa miaka 61 na kesho ndiyo tunakwenda kuadhimisha miaka 61 ya Muungano wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Samia Suluhu Hassan aliuchukua Muungano huu kama Kiongozi wa Kitaifa katika nchi hii. Wakati ule Muungano huu una jumla ya miaka 56. Maana yake kitendo cha kuuchukua na kuuendeleza Muungano huu kutoka miaka 56 na leo una umri wa miaka 61, maana yake Daktari amefanya kazi kubwa na kwa kweli tunakiri ni muumini wa Muungano huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kaendesha Muungano huu kwa busara. Muungano huu umekuwa una changamoto nyingi na sisi tunafahamu na wengine tumesema hapa, lakini pamoja na changamoto zote hizo, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameuendesha Muungano huu kwa busara na leo unaendelea kudumu na utadumu kwa kadiri ambavyo Mwenyezi Mungu ataujalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kupunguza changamoto. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa busara zake changamoto hizi zimepungua. Ndani ya kipindi chake kuna Mbunge mmoja hapa amesema, zaidi ya changamoto 15 zimetatuliwa ndani ya kipindi kidogo cha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni muumini wa kweli wa Muungano huu na anafanya kazi kubwa katika kuhakikisha kwamba Watanzania

hasa katika Muungano huu, basi wanaishi katika mazingira mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka niendelee kusema kwamba, hapa kuna jambo limezungumzwa, suala la mabalozi wa mazingira. Suala hili kweli tulilitengeneza sisi wenyewe na mabalozi hawa tuliwatengeneza na kuwateua na tukawapa mamlaka ya kutusaidia hali ya kimazingira katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nasema, tunawapa ushirikiano wa hali ya juu. Wao wenyewe wanaandaa mambo yao ya kimazingira, wanatualika tunakwenda, na sisi tukiandaa mambo yetu huwa tunawaalika. Pia, kwenye Sherehe zetu za Muungano na za Mazingira tunawaalika na tunawasaidia pale ambapo tunahisi hapa tunayo nafasi ya kusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaambia tu Waheshimiwa Wabunge, tunatambua uwepo wa Mabalozi wa Mazingira na tutaendelea kushirikiana nao kwa sababu wanatusaidia katika kufichua changamoto mbalimbali za kimazingira katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, imetajwa hapa changamoto nyingine ya mmomonyoko na kuliwa kwa visiwa na maeneo ya bahari. Hii kweli ni changamoto, lakini sisi kama Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, tulitafuta fedha na fedha zilipatikana. Mama Samia Suluhu Hassan alitoa fedha nyingi za kutosha na tukaanza ujenzi wa baadhi ya matuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetengeneza Sikwese, tumeanza kushughulikia suala lile la Mikindani na ninataka niwaambie baadhi ya Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mbunge wa Mtambwe kwa upande wa Mtambwe Mkuu, namwambia rafiki yangu Mheshimiwa Simai wa Nungwi, niwaambie watu wa Gando, Lindi, Mtwara na maeneo mengine yote yenye changamoto hii, Serikali inaendelea kutafuta fedha. Tutakapozipata fedha hizo tutahakikisha tunakwenda kutatua changamoto hii kwa sababu tumeiona ni kubwa na kwa kweli

maji sasa yamekuwa yanaingia kwenye mitaa na mengine yanaingia kwenye vipando ambavyo havihimili maji ya chumvi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Hamza Khamis. Sasa namkaribisha mtoa hoja, Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa *Eng.* Hamad Yussuf Masauni.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii ya uweza kuhitimisha hoja. Naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana na kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niorodheshe majina ya waliochangia kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wengine ambao hawakupata nafasi. Waliochangia ni Waheshimiwa Wabunge 16 ambao ni Mheshimiwa Jackson Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Kalenga; Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, Mbunge wa Jimbo la Jang'ombe; Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Mbunge wa Jimbo la Nungwi; na Mheshimiwa Juma Usonge Hamad, Mbunge wa Jimbo la Chaani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Ali Juma Mohamed, Mbunge wa Jimbo la Shaurimoyo; Mheshimiwa Kasalali Emmanuel Mageni, Mbunge wa Jimbo la Sumve; Mheshimiwa Saada Monsour Hussein, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Kaskazini Unguja; Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mbunge wa Viti Maalum *(NGO's)*; Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, Mbunge wa Jimbo la Buhigwe; na Mheshimiwa Mwanakhamis Kassim Said, Mbunge wa Jimbo la Magomeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah, Mbunge wa Jimbo la Donge; Mheshimiwa Tamima Haji Abass, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa

Maryam Omar Said, Mbunge wa Jimbo la Pandani; Mheshimiwa Anatropia Theonest, Mbunge wa Viti Maalum; Mheshimiwa Abubakari Asenga, Mbunge wa Jimbo la Kilombero; na Mheshimiwa Pauline Gekul, Mbunge wa Jimbo la Babati Mjini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuorodhesha naomba nichukue fursa hii kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote ambao wamechangia na wako ambao pia wamechangia kwa maandishi kwamba tumepokea maoni yao yote na tutayafanyia kazi. Yale ambayo tutapata fursa ya kuyatolea ufafanuzi sasa hivi, tutatoa ufafanuzi na yale ambayo hatutapata fursa kwa sababu ni mengi, tunaahidi kuyachukua na kwenda kuyafanyia kazi. Pia, tutayatolea majibu kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niigawe michango yangu katika maeneo matatu. Kwanza, nitazungumzia hoja za Muungano, baadaye nitazungumzia hoja za masuala ya mazingira na kumalizia na hoja za masuala ya Uchumi wa Buluu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, katika suala la Muungano, naomba kuchukua fursa hii kwanza kumpongeza kwa dhati kabisa ya moyo wangu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa nini nampongeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa sababu katika mijadala ya Bajeti ya Wizara ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, mimi nimekuwa Bungeni sasa huu ni mwaka wangu wa 15. Miaka yote bajeti hii ilipokuwa ikiwasilishwa hoja zilizokuwa zikizungumzwa hapa na Waheshimiwa Wabunge ilikuwa ni kero, kero, kero; lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameigeuza Wizara hii kutoka kuwa Wizara ya kero za Muungano na sasa kuwa ni Wizara yenye fursa za Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi wa hayo ni jinsi ambavyo katika kipindi cha miaka minne ameweza kutatua kero 15 kwa

mpigo, katika kero 25 ambazo zilikuwa zinasumbua sana. Hatuziiti tena kero, sasa hivi tunaziita ni hoja ama ni fursa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kuthibitisha haya ninayozungumza, naomba nizitaje haraka haraka kwa sababu ya muda. Jambo la kwanza ambalo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanikiwa kulipatia ufumbuzi ni ile hoja iliyokuwa inahusu uvuvi wa Bahari Kuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo unafahamu kwamba, Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi katika ukanda wa uchumi wa Bahari Kuu, ilikuwa haitekelezwi Zanzibar, lakini kuanzia hiyo sheria ilipofanyiwa marekebisho, Februari, 2007 sasa hivi imeweza kuzitambua taasisi zinazohusika na matumizi ya Bahari Kuu kwa upande wa Zanzibar na kuzijumuisha katika Kamati Tendaji ya Mamlaka ya Uvuvi ya Bahari Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ndilo lililopelekea sasa kuwa na Mamlaka ambayo Makao Makuu yake yako Fumbo kule Zanzibar na mgawanyo wa mapato kutokana na uanzishwaji wa taasisi hii ni 50% inakwenda katika uendeshaji, 30% inakuja upande wa Tanzania Bara na 20% inakwenda Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, hata kuna uwiano wa muda wa wale watendaji wakuu wa taasisi hii kuweza kukaa, jambo ambalo limesaidia sana katika kuunganisha nguvu za pamoja katika kusaidia kuzitumia fursa nzuri za uchumi wa Bahari Kuu kwa maslahi mapana ya nchi yetu kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amelishughulikia, ni uingizaji wa maziwa kutoka Zanzibar. Utakumbuka kwamba kulikuwa kuna changamoto ya maziwa kutoka katika Kiwanda cha Azam kilichopo Zanzibar kwa muda mrefu, lakini kutokana na umahiri wake Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameweza kuikabili changamoto hiyo na sasa hivi tozo ile imepunguzwa na hivyo sasa baada ya marekebisho ya Kanuni ya Tozo kufanyika na kupunguzwa kutoka shilingi 2,000/= kuja shilingi 250/=, sasa jambo hilo siyo hoja tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amelifanyia kazi ni hoja ya ajira kwa Watumishi wa Zanzibar kwenye Muungano. Kulikuwa kuna changamoto ya muda mrefu ambayo ilisababisha upungufu mkubwa sana wa uwakilishi wa Watanzania wenye asili ya Zanzibar kwenye Taasisi za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo na lenyewe limepatiwa ufumbuzi katika kipindi cha miaka minne ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Hatua zimechukuliwa ikiwemo, kwanza, kuhamasisha Wazanzibar kuomba ajira zinazotangazwa katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na vilevile, Taasisi za Muungano kufungua Ofisi zake Zanzibar ikiwa ni pamoja na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, sasa hivi uwiano wa 21% kwa 79 ndiyo ambao unatumika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa haraka haraka ni suala la mgawanyo wa mapato, ambalo na lenyewe kama ambavyo mnafahamu kwa sasa hivi mgawanyo wa mapato ni 4.5% kwa upande wa Zanzibar. Ingawa jambo hili nitalizungumza kwa mapana yake baadaye, halijakamilika lote, lakini kimsingi 4.5% ambayo Zanzibar inastahili kupata, inapata bila changamoto yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni ukarabati wa Hospitali ya Mnazi mmoja. Hili lenyewe lilikuwa ni changamoto ya muda mrefu. Mkopo huu wa ukarabati wa Hospitali kongwe kabisa ya Mnazi mmoja, ulikuwa umechukua muda mrefu, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amelimaliza hili baada ya kufanya marekebisho na wale wafadhili ambao ni *Saudi Fund* kukubali kuondoa kipengele kilichokuwa kina utata katika makubaliano hayo ambacho kilihitaji kuweka dhamana baadhi ya mali za nchi. Jambo hilo limekamilika na tayari huo mkataba umeshasainiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusu mkopo wa Bandari ya Mpigaduri, lilikuwa na lenyewe linafanana  na hili la mkopo wa hospitali na changamoto na tatizo lilikuwa ni hilo hilo na lenyewe limepata ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine lilikuwa ni suala la usimamizi, ukokotoaji na ukusanyaji wa mapato yatokanayo na simu. Hili nalo limefanyiwa ufumbuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni suala la mapato ya Uhamiaji. Kama ambavyo mnafahamu kwamba, katika hiki kipindi ambacho bado katika zile kero tatu; moja inayohusu uanzishaji wa Mfuko wa Pamoja wa Fedha ikiwa bado haijafanyiwa kazi ni lazima Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo inatakiwa ipate fedha kwa ajili ya kujiendesha iweze kupata vyanzo vya pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ilikubalika kwamba tozo zinazotokana na huduma mbalimbali ikiwemo *VISA* ziweze kubakia Zanzibar, na hilo jambo limeweza kupatiwa ufumbuzi na sasa zinabaki kwa ajili ya matumizi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni kuhusiana na Uwakilishi wa Makamu Mwenyekiti kwenye Baraza la Rufaa, halikadhalika kwenye Bodi ya Bima ya Amana. Hoja hii ilisababishwa na kutokucheleweshwa na kuwasilishwa mapendekezo ya jina, na lenyewe limekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia suala la kodi itokanayo na kodi ya zuio pamoja na kodi ya mapato, ambapo kulikuwa kuna fedha nilizungumza katika hotuba yangu kiasi cha shilingi bilioni 21.7 zimelipwa Zanzibar. Kwa hiyo, changamoto hii na yenyewe imekwisha, ingawa kwenye eneo la kodi ya mashirika bado kuna mambo mengine madogo yamekamilishwa ili liweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nimalizie hoja nyingine tatu nazo ni hoja ya ongezeko la umeme, hoja ya mkopo wa ujenzi wa *Terminal Three* ya Uwanja wa Ndege, na hoja ya ujenzi wa barabara ya Chake – Wete, zote hizi zimekamilika.

Mheshimwia Mwenyekiti, kwa hiyo, ninapozungumza kwamba sasa ni lazima tumpongeze Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuweza kuzikamilisha hoja zilizokuwa zinasumbua kwa miaka mingi kwa kipindi kifupi, ninamaanisha. Naomba niwapongeze

sana Waheshimiwa Wabunge kwa kumuunga mkono, na leo mchango wenu unathibitisha uweledi na uimara wa Mheshimiwa Rais wetu katika kuhakikisha amezikabili hizo hoja na kugeuza Muungano wetu kuwa ni fursa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili la utatuzi wa hizi hoja ni jambo la muhimu sana, kwa sababu kama kuna kitu ambacho kinasababisha Muungano utetereke, mojawapo ni hili. Huu Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar umekuwa ni Muungano wa mfano, umedumu kwa miaka mingi, sasa ni mwaka wa 61 na Muungano huu umepita katika changamoto nyingi, lakini mpaka leo umeendelea kuwa imara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanataka kujiuliza kwa nini Muungano wa Tanzania umekuwa imara? Kwa uzoefu wa Miungano ya nchi nyingine duniani ambayo haikuweza kufanikiwa na uzoefu wa Muungano wetu sisi ambao umeweza kufanikiwa, kuna mambo kadhaa ambayo sisi tunaona yametusaidia sana. Moja, ni ujirani na ukaribu kati ya Visiwa vya Zanzibar pamoja na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu angeweza kuvichukua visiwa vya Zanzibar akaviweka kwenye Bara la Asia, akaviweka Bara la Amerika, Bara la Ulaya, lakini ameviweka karibu na Tanzania Bara, kwa hiyo, huu ukaribu hauepukiki, hilo ni moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukaribu huu ndiyo umesababisha historia yetu sisi ya hizi pande mbili kuwa zinafanana sana. Moja, uasili wa historia hiyo ni mapambano ya ukombozi wa nchi zetu, ushirikiano wa wananchi wa hizi pande mbili ukiachilia mbali uasili na udugu wao wa damu wa kihistoria, lakini historia haiwatenganishi watu wa hizi pande mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni utashi na matarajio yanayofanana, kwamba wananchi wa hii nchi hasa kipindi kile cha ukombozi walikuwa na matarajio ya kupata amani. Nichukue fursa hii kupongeza sana viongozi wote waliopita kuanzia Viongozi Waasisi wa hili Taifa mpaka viongozi waliopita na viongozi

waliopo. Sasa hivi, kwa kuweza kusimamia Muungano wetu pamoja na amani ya hii nchi na hivyo kutimiza matarajio ya wananchi wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo nilitaka kulizungumza ni suala la uwiano katika madaraka. Jambo hili na lenyewe limekuwa ni jambo ambalo limeleta faida kubwa na kusaidia katika kuimarisha Muungano wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ndiyo linafananna na yale niliyoyazungumza ni utaratibu wa kushughulikia hoja za Muungano. Bila hili kufanyika Muungano wetu lazima utayumba, kwa sababu wabaya ambao wanatafuta fursa ya kuutetereshа huu Muungano wanapita kule kule kuwapotosha wananchi kwamba Muungano huu hauna faida, una matatizo haya na matatizo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ambazo Serikali imezichukua katika kuweka njia mbalimbali tokea kipindi cha Serikali zilizopita mpaka hiki kipindi ambapo nimempongeza Dkt. Samia kwa kazi nzuri aliyoifanya, zimesaidia sana kuufanya Muungano wetu uwe imara tofauti na Miungano ya nchi nyingine nyingi zilizojaribu kuungana ikiwemo Ethiopia na Eritrea, walijaribu kuungana katika Afrika; Senegal na Gambia, walijaribu kuungana wakashindwa; Ghana, Guinea na Mali, walijaribu kuungana wameshindwa; nchi nyingi sana, Zambia na Zimbabwe; na kadhalika na kadhalika. Kwa hiyo, niliona hilo nilizungumze kwa sababu ni jambo ambalo ni la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tukiri kwamba tuna changamoto. Changamoto kubwa ya Muungano wetu kama ambavyo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wamezungumza ni kwamba, Muungano huu wa miaka 61 na *generation* ya akina Mwalimu Nyerere na Mzee Karume iliyobaki sasa hivi ni wachache sana. Asilimia kubwa ya wananchi wanaoishi sasa hivi ni watu ambao wamezaliwa baada ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ni dhahiri lazima tukubaliane na ukweli kwamba, vijana wengi bado wanakosa

uelewa mpana wa misingi ya Muungano wetu. Changamoto hiyo lazima kama Serikali tukiri na tuifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linasababisha kwamba wakati mwingine unakuta baadhi ya watu wanakosa ile *spirit* ya Waasisi wa hili Taifa. Waasisi wa hili Taifa wakati wanaunganisha hizi nchi hawakuangalia ni nani atapata nini? Waliangalia udugu wa asili na namna gani ambavyo pande hizi mbili zitashirikiana pamoja na wananchi wa hizi pande, watasaidiana kwa maslahi mapana na kuweza kuboresha maisha ya wananchi wa nchi hizi na haikuwa kuangalia yule ni nani, huyu ni nani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana sasa hivi ile *spirit* ya Waasisi wetu kwa baadhi ya wananchi na wengine hata viongozi imeonekana kupungua. *Spirit* yao ilikuwa inaangalia katika kusaidiana zaidi kidugu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mfano mmoja. Jana Mheshimiwa Prof. Kabudi aliniambia wakati Kiwanda cha Mahonda kinatengenezwa Zanzibar, ambayo ni moja kati ya zile hoja tatu ninazotaka nizizungumzie baadaye, kwamba tumezungumza, kuna hoja tatu ambazo hazijapata ufumbuzi: Hoja ya kwanza, ni ile hoja ambayo inahusu sukari ya Mahonda kuweza kuuzwa katika soko la Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa ambazo Profesa na mwenyewe yuko pale ananiangalia, jana wakati tunabadilishana Mawazo, alinieleza akaniambia kwamba, kipindi cha Mwalimu, wakati Kiwanda cha Mahonda kinajengwa, ilikuwa kuna sera ya kuwezesha viwanda vya ndani, na Mwalimu akasema "hakikisheni ule mvinyo ambao unazalishwa katika Kiwanda cha Mahonda, wote unamalizika kuuzwa Tanzania Bara, kabla ya kutafuta sehemu nyingine."

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo *spirit* ya Waasisi. Kuna mambo mengi ambayo Waasisi wa hili Taifa wamefanyiana kwa maslahi mapana ya nchi hizi mbili, hiyo lazima irudi. Katika kuirudisha hiyo, tumeamua kujipanga Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kuhakikisha tunakuja

na mpango kabambe wa elimu ambao utaanza kuanzia kesho ambapo tunaadhimisha Maadhimisho ya Miaka 61 ya Muungano mpaka yatakapokuja Maadhimisho mengine ya Miaka 62 ya Muungano. Hatutasubiri programu za elimu kwa umma zifanyike katika kipindi cha Maadhimisho. Kuanzia sasa zitakuwa ni programu endelevu na zitalenga katika kuangalia maeneo mbalimbali hususan katika maeneo ambayo yanagusa vijana wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika hoja zile mbili ambazo nimezungumza kwamba bado hazijapata ufumbuzi, nyingine ilikuwa ni ile hoja ya *Joint Finance Committee* (Mfuko wa Pamoja wa Fedha). Katika kulikabili hilo na kutimiza yale malengo ya Waasisi wetu, umefika wakati kwanza lazima wananchi watambue kwamba uchumi wa Zanzibar na Uchumi wa Tanzania Bara siyo uchumi shindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna haja ya kuangalia fursa ambazo zinaweza zikasaidia sehemu moja na nyingine badala ya kusaidia sehemu moja huku zikileta athari sehemu nyingine. Hivyo basi, tutafanya jitihada zinazowezekana pale ambapo *Joint Finance Committee* itakapoundwa tuipe kazi na maelekezo ya kuja na mkakati kabambe na kufanya stadi ya kina kabisa kuangalia maeneo ya fursa ambazo yatasaidia kama ni maeneo ya upande mmoja yasiwe na madhara kwa eneo lingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kulikuwa kuna hoja hapa ilikuwa inazungumzwa kama ni kero, kwamba watu walikuwa wanaleta bidhaa kutoka Zanzibar, lakini wanazuiliwa Bandarini. Katika hali ya kawaida kilichokuwa kinafanyika siyo kuzuiliwa, lakini ni kuangalia kama kuna utofauti wa kodi ili isiweze kuathiri Mifumo ya Kodi ya Tanzania Bara; lakini ukiangalia kwa makini, unaweza ukahisi kwamba jambo hilo lilikuwa linafanyika kwa nia mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, yapo mambo ambayo yanaweza yakafanyika na mifano iko mingi, kwa mfano kuna nchi ambazo zimepiga hatua kubwa sana na kwa haraka na

mazingira yake hayatofautiani sana na Zanzibar. Kwa mfano, nchi nne ambazo zinasifika sana kwa kupiga hatua kimaendeleo katika hii karne. Moja, ni nchi ya Dubai, ambayo mazingira yake yanafanana sana na Zanzibar kwa namna moja, kwa maana Dubai ni nchi ambayo ipo katika Muungano wa *UAE* kama ilivyokuwa Zanzibar kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi nyingine ni Panama, inafanana na Zanzibar kwa sababu ni kisiwa vilevile chenye udogo kama Zanzibar. Nyingine ni Singapore pamoja na Ireland, mazingira yote hayatofautiani sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mara nyingine tena na Dkt. Hussein Mwinyi kwa kuanza kufanyia kazi haya, kwa sababu misingi ya kufanikiwa katika hizi nchi nilizozitaja kubwa ni maeneo matatu: moja, kuna umiminikaji mkubwa sana wa uwekezaji. Fedha nyingi sana zinatoka kuingia katika nchi zao kuwekeza. Vilevile kuna utaalamu pamoja na teknolojia za kutosha kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hilo kwa upande wa Zanzibar kipindi hiki cha Uongozi wa Dkt. Hussein Mwinyi na Mheshimiwa Dkt. Samia kama Rais wa Muungano tunaona mwelekeo, kwamba sasa Zanzibar inabadilika, na Zanzibar inaelekea kuwa ni kivutio cha Wawekezaji pamoja na watu wenye mitaji mbalimbali kuja kuwekeza, jambo ambalo likifanikiwa, litaweza kuwa chachu ya mafanikio vilevile kwa upande wa Tanzania Bara ambapo ndiyo sehemu ambayo kuna soko kubwa la bidhaa kwa upande wa ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niliona hilo nilizungumze kwamba ni moja katika kipaumbele chetu cha Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, kuhakikisha kwamba, kwanza, tunasimamia utoaji wa elimu wa kimkakati; pili, tunaweza kuhakikisha kwamba hizi hoja tatu ambazo zimebakia zinakamilika ili tuweze kui-*pass Joint Finance Committee,* kuweza kutusaidia kutimiza haya malengo niliyoyaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilizungumzwa ni suala la Mfuko wa Jimbo. Kwenye Muungano nimalizie na hili la Mfuko wa Jimbo, ambalo ni kweli kwamba imekuwa ni changamoto kwa Wabunge wengi kwa jinsi ambavyo sheria hii ilivyokaa. Sheria hizi siyo Msahafu, siyo Biblia, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeshaanza mchakato wa kupitia hii sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo niliwahi kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge kwenye semina, ni kwamba tutakutana nao kuweza kuwapa semina na kupata maoni yao ili changamoto zote zinazowasumbua katika huu mfuko ziweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba niende kwenye eneo la Mazingira. Katika mazingira kuna mambo makubwa matatu ambayo ninataka niyazungumze. Moja, ni suala ambalo lilizungumzwa kwa hisia kali na Waheshimiwa Wabunge na wako ambao waliniambia kwamba nilitoa ahadi katika Bunge lililopita wakati tukipitisha mabadiliko ya sheria ndogo ya kuingiza pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ile ilikitambua kituo chetu cha kuratibu biashara ya Kaboni kisheria. Nataka niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuweza kupitisha yale mabadiliko ambayo kwa muda mfupi yameweza kuleta tija kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi tunavyozungumza kama ambavyo lengo letu lilivyokuwa limekusudiwa la mabadiliko yale ya kukifanya kituo cha kuratibu biashara ya Kaboni iwe ya kisheria, tulikuwa tuna dhamira ya kuhakikisha nchi yetu inapata faida inayostahili katika hii biashara. Moja katika faida ambazo zinastahili ni kuhakikisha maeneo yote yenye fursa ya biashara ya kaboni tunayatumia ipasavyo na kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo tumeanza kufanikiwa katika kipindi kifupi tokea mwezi wa Pili mpaka sasa hivi tupo

katika makubaliano ambapo tayari tumeshapa fedha kupitia *WFP* kwa ajili ya Mradi wa Nishati Safi ambao unakwenda kufungamanishwa na biashara ya Kaboni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tayari tupo katika hatua za mwisho za kusaini makubaliano na Taasisi ya Korea pamoja na Serikali ya Japan kuweza kuhusisha mahusiano ya biashara ya Kaboni baina ya nchi na nchi. Kwa muda mrefu biashara hii imekuwa ikifanyika kwa kutegemea watu wengine wakifanya biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna miradi ambayo haivutii wafanyabiashara binafsi, hivyo ni lazima tujenge mahusiano na nchi nyingine ili tuweze kuwa na mahusiano ya moja kwa moja na kuweza kuingiza miradi ambayo hata siyo kivutio kwa watu binafsi iweze kufaidika. Miradi hiyo ni mingi sana katika sekta takribani nyingi katika nchi yetu ambazo bado hatujazitumia vizuri, kwa hiyo ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi ambacho tunapitisha hiyo sheria ni kweli niliahidi hapa mbele ya Bunge hili Tukufu kwamba, tutaleta mabadiliko mengine makubwa ya sheria katika hili Bunge, lakini niliwaeleza kwamba lengo na dhamira ya Serikali ni kufanya hivyo. Sikuahidi moja kwa moja, niliwaeleza kwamba lengo na dhamira ya Serikali ni hiyo na bado lengo na dhamira ya Serikali iko vilevile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge hili bado halijaisha, nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba hatua tulizozifikia siyo mbaya, michakato yote migumu iliyokuwa inahitaji kuandaa huu Muswada katika ngazi ya Wizara imekamilika. Kama mnafahamu kwamba utaratibu wa kisheria hasa kwa jambo ambalo linataka kuja kwa huu utaratibu nilioueleza, lina mlolongo wake wa Kiserikali ambao ni lazima ufuatwe. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani tumwombe Mungu kwamba tuweze kukamilisha kama ambavyo dhamira yetu iko pale pale na tuweze kutimiza hilo lengo, lakini dhamira ya Serikali inatambua umuhimu wa jambo hili, tunatambua kwamba

kuna changamoto nyingi sana za mazingira sasa hivi. Sisemi kwamba kufanya *NEMC* kuwa *NEMA* ndiyo mwarobaini pekee, kuna mambo mengi ambayo tumeshayafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kuna watu hapa walizungumza kuhusiana na wale Maafisa Mazingira waliokuwa TAMISEMI. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba, tayari tumeshafanya jitihada za kufanya vikao, semina, na tumetoa elimu mbalimbali na kuanza kuwa *activate* hawa Maafisa Mazingira wa ngazi za Mikoa na Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulitekeleza hilo, tumeteua Maafisa wa Mazingira kutoka Ofisi ya Makamu wa Rais ambao watakuwa wanafanya kazi moja kwa moja na Wakurugenzi wa Mazingira kwenye TAMISEMI ili kuweza kutengeneza muunganiko na mahusiano mazuri kati ya Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira; Wizara ya TAMISEMI; pamoja na Halmashauri. Hilo ni jambo ambalo tayari tumeanza kulifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tunaamini kwamba *NEMC* itakapokuwa *NEMA*, itaweza kuipa meno kuweza kuwa na udhibiti wa kisheria kudhibiti ukiukwaji wa sheria unaoendelea nchini. Itaweza kuchukua hatua na kuzuia kwa kiasi kikubwa sana kwa kuendelea pamoja na kushirikisha hatua nyingine ambazo nimezieleza na nyingine ambazo sijazieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, nataka mwendelee kutuamini kwamba dhamira yetu ilikuwa ni njema na dhamira ile ipo pale pale na tunaendelea kufanya kila linalowezekana kuhakikisha dhamira hiyo inatimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo nataka nilizungumze ni suala la Uchumi wa Buluu. Hili la mabalozi nadhani naungana mkono na Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba tunaendelea kuwapa moyo, tuponao na tunathamini jitihada zao na kazi ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la nishati safi kama ambavyo mnafahamu, kuna kazi kubwa na nzuri sana ya uratibu wa suala hili chini ya Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa akizishirikisha Wizara zote mtambuka katika kuhakikisha Mkakati wa Serikali wa Miaka 10 wa Nishati Safi unaweza kuleta mafanikio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wetu kama nilivyoeleza katika hotuba kwamba tumefanikiwa, taasisi 903 ambazo zinalisha zaidi ya watu 100 kuweza kuacha kutumia nishati chafu. Naendelea kusisitiza katazo ambalo nimelitoa na hivyo taasisi zote nchini ambazo zinalisha zaidi watu 100 zitumie nishati safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la mwisho kwenye mazingira ni suala la magugumaji. Nataka niungane na Waheshimiwa Wabunge waliosimama kuhusiana na changamoto hii na jinsi ambavyo inaleta usumbufu sana. Hata hivyo nataka niwahakikishie, jambo hili Serikali imelichukua kwa uzito mkubwa sana na kwa mara nyingine tena nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ni mtambuka, linagusa sekta nyingi sana. Tulishafanya kikao chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu na tumeandaa mkakati kabambe wa kukabiliana na jambo hili na mkakati huu unakwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa jambo hili lipo chini ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba nisiende sana; ni kazi ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu anaisimamia vizuri na mwenyewe itakapompendeza anaweza akaitolea taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa suala la Uchumi wa Buluu. Jambo hili nilizungumze kwa kifupi kwamba tupo katika hatua nzuri za kuanzisha mifumo ya kitaasisi pamoja na mifumo ya kisheria. Kama ambavyo nilieleza katika Bunge lililopita kwamba, mabadiliko ya Sheria ya Mazingira yanakwenda sambamba na uanzishwaji ama kama siyo uanzishwaji, ni utambuaji wa masuala ya uratibu wa Uchumi wa Buluu kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari jambo hili na lenyewe lipo katika hatua nzuri na ninaamini kabisa muda siyo mrefu sana litaweza kukamilika. Baada ya kusema hayo, nadhani zile hoja ambazo zilikuwa zimezungumzwa, nyingi sana nimezitolea ufafanuzi. Nilijaribu kuangalia hoja za mmoja mmoja hapa, najua sekunde zangu zimebaki chache, kwa hiyo, labda nizisome baadhi yao ambazo sikuzitolea maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ni hoja ya miradi kutopelekewa fedha. Kwa mfano, kuna mradi ambao umezungumzwa wa kujenga ustahimilivu wa mabadiliko ya tabianchi katika Mkoa wa Kigoma. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge wa Mkoa wa Kigoma kwamba tayari fedha hizi zilishapokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hiyo na mradi huu upo katika hatua za mwisho kukamilika. Tunatarajia mwezi Mei mradi huu utaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine ambalo lilizungumzwa ni kuhusiana na Hoja ya Kamati ya Bunge kuhusu utekelezaji wa baadhi ya miradi ya maendeleo kama vile Mradi wa Bwawa la Sigiri na josho la mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika. Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Halmahauri ya Wilaya ya Tanganyika, inaendelea kukamilisha kuweka miundombinu ya maji katika josho lililopo Kijiji cha Kapanga na shughuli ya uimarishaji wa Bwawa la Sigiri unaendelea kufanyika kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Nzega. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kulikuwa na hoja ya kwamba utafiti ufanyike kuhusiana na miradi kabla haijatekelezwa na ishirikishe Wizara za Kisekta. Nataka niwahakikishie kwamba ushauri huo tumeupokea na kwamba tutaendelea kufanya tafiti na tathmini kabla ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ili kufikia malengo yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, tumepokea ushauri kwamba Ofisi ya Makamu wa Rais imekuwa ikishirikiana na Wizara za Kisekta na itaendelea kushirikiana na Wizara za Kisekta na wadau

wengine katika hatua zote za uibuaji, uandaaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuongeza tija na manufaa kwa jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni suala la kutenga fedha za kutosha katika miradi na kwamba fedha hizi zionekane kidogo na miradi hii ina muhimu na kutanua wigo ili iweze kunufaisha wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ushauri huu tumeupokea na tutaendelea kutenga fedha za ndani na kutafuta fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza miradi ya mazingira itakayoleta manufaa ya jamii na kutunza mazingira. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya tathmini katika maeneo yote nchini kwa lengo la kuibua miradi itakayonufaisha wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hoja zote nimezikamilisha. Naomba sasa nikushukuru kwa nafasi hii uliyonipa ya kuweza kuchangia na ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Hoja imeungwa mkono.

Katibu.

**NDG. RUTH MAKUNGU – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi.

**MWENYEKITI:** Kamati ya Matumizi.

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:**

**KITABU CHA PILI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 31 – Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*....................................Sh. 5,691,861,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tabasam.

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka ufafanuzi wa Serikali kuhusiana na suala la magugumaji katika Ziwa Victoria na hasa katika eneo la Kigongo – Busisi. Pale kuna vivuko vya Serikali vya mabilioni ya shilingi, na vyote vimeharibika kwa sababu ya magugumaji, na hili jambo limezuia mpaka usafiri wa maji katika ya Sengerema na Wilaya ya Misungwi upande wa Kigongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hali hii Mheshimiwa Waziri anamaliza kutoa ufafanuzi katika bajeti hii hajazungumzia mkakati wa Serikali kutoa magugumaji katika Ziwa Victoria. Hili jambo halikubaliki. Kwa hiyo, naomba ufafanuzi wa Serikali kuhusiana na hili jambo, na asiponiridhisha nitakamata shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, umesema unaomba ufafanuzi, hujasema unashika shilingi.

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilieleza jambo hili, lakini nilishindwa kulieleza kwa marefu kwa sababu kama nilivyoeleza mwanzo kwamba jambo hili Serikali imelichukua kwa uzito

mkubwa na kutokana na uzito wake, Kiongozi wetu Mkuu wa Shughuli za Serikali ambaye ni Mheshimiwa Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa ameamua kulibeba yeye kwa sababu linahusisha Wizara mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano kama ulivyozungumza kuna Wizara inahusu masuala ya ujenzi ambayo ndiyo yenye dhamana ya vivuko inahusika, kuna Wizara ya Uvuvi na Mifugo inahusika, kuna Wizara ya Mazingira inahusika, kuna Wizara ya Fedha inahusika, kwa sababu tunahitaji fedha ili kufanya hayo, na kuna Wizara ya Maji Mheshimiwa Aweso inahusika pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika kutekeleza mkakati huo wa Kitaifa wa Serikali, kwanza ilitumwa timu ya wataalamu kwenda katika eneo lile la kule karibu na lile Daraja la Kigongo – Busisi kutembelea na wakawasilisha ripoti hiyo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu na Naibu Mawaziri pamoja na Makatibu Wakuu sote tulikuwepo, tukajadili mkakati huo wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna hatua ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu amezielekeza. Sasa kwa kuwa jambo hili linasimamiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, siyo heshima kwangu mimi kusimama kueleza, lakini nimtoe wasiwasi na kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba jambo hili Serikali imelichukulia katika ngazi ya juu kwa uzito wake. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi, wakati utakapofika ataona hatua ambazo zinachukuliwa ambazo Mheshimiwa Waziri Mkuu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Tulikuwa tunataka ufafanuzi kwa sababu hilo suala ni la kisera na fungu lilishaafikiwa.

Katibu.

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:**

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.................Sh. 762,634,000
Kifungu 1003 - *Policy and Planning Division*.............Sh. 2,631,317,000
Kifungu 1004 - *Government Communication Unit*........................................................Sh. 578,039,000
Kifungu 1005 - *Internal Audit Unit* ..........................Sh. 621,460,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*................................Sh. 779,183,000
Kifungu 1007 - *Information and Communication Technology Unit*....................................Sh. 578,231,000
Kifungu 1008 - *Legal Services Unit* ..............................Sh. 760,626,000
Kifungu 1009 - *Monitoring and Evaluation Unit*......................................Sh. 676,918,000
Kifungu 2001- *Union Secretariat*................................Sh. 3,379,921,000
Kifungu 5001 – *Environment*....................................Sh. 12,398,024,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 026 – Ofisi Binafsi ya Makamu wa Rais**

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management*..................................Sh. 19,946,399,000

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE - MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 31 - Ofisi ya Makamu wa Rais,Muungano na Mazingira**

Kifungu 1001- *Administration and Human Resources Division*..............................Sh. 1,700,000,000
Kifungu 5001 – *Environment*....................................Sh. 31,359,578,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. AZIZA MAKWAI – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoka taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imemaliza kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae. Namwita mtoa hoja aje kutoa hoja yake.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 123 (3) (a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Februari, 2023 naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi zake, hivyo naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kwa mujibu wa Kanuni, nitalihoji Bunge. Wanaokubaliana na hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. *(Makofi)*

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Ahsanteni sana. Kwa hiyo, sasa natangaza rasmi kwamba Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yamepitishwa na Bunge hili na sasa yanaenda kufanyiwa kazi na baadaye tuweze kufikia malengo yetu.

Nitumie fursa hii kuwapongeza Kamati zote mbili kwa uchanganuzi wao na kuchanganua bajeti na baadaye kuleta mashauri kwenye Wizara. Pia, naishukuru Wizara ya Muungano na Mazingira, na wote ambao wamehusika katika Wizara hii kipindi cha Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, nawapongeza sana, na sasa hivi tunaye Mheshimiwa *Eng.* Hamad Yussuf Masauni na Mheshimiwa Naibu Waziri wake, ndugu yetu Mheshimiwa Hamza, nawashukuru wote kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Pia, nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote, tokea asubuhi michango yenu ni mizuri sana ya kuboresha Muungano wetu na kwa bahati nzuri kesho ndiyo tunahitimisha ama tunaadhimisha miaka 61 ya Muungano wetu tukiwa imara, na tukiwa salama. Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano, Muungano wetu upo imara kwa misingi yake iliyoundwa na Waasisi wetu. *(Makofi)*

Niwatoe hofu Watanzania wote na Waheshimiwa Wabunge tukumbushane tu kwamba mwaka 2018 tulifanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa, mliopo mtakumbuka. Kuna kifungu cha 6(a)(5) kinataka au kinalazimisha kila chama cha siasa nchini Tanzania kulinda na kudumisha Muungano wetu wa Tanganyika na Zanzibar, Mapinduzi ya Zaznibar, *democracy*, utawala bora, kupinga rushwa, maadili, uzalendo, Mwenge wa Uhuru, amani na utulivu katika kutunga sera za vyama vya siasa, uteuzi wa viongozi wake, na uchaguzi wa viongozi wa chama cha siasa. *(Makofi)*

Nakumbusha hili kwa sababu Mungu akipenda mwaka huu, mwezi Oktoba tutakuwa na uchaguzi, na hapa tunashukuru kwamba kesho kwenye maadhimisho yetu ya Muungano tunasema Muungano ni dhamana, heshima na tunu ya Taifa. Kwa hiyo, tushiriki Uchaguzi Mkuu 2025 kwa maana ya kwamba

nikikumbusha hivyo tujue tu kwamba Muungano wetu unaheshimika kisheria na kila kitu.

Kwa hiyo, wanasiasa wote wa Tanzania wakiwemo wanachama wetu wa Chama Cha Mapinduzi ni muhimu kuheshimu kifungu hiki cha Sheria ili tuingie kwenye uchaguzi kwa amani na utulivu.

Baada ya kusema hayo niwatakie Maadhimisho mema ya miaka 61 ya Muungano wetu na ninawaombea kila la heri Waasisi wetu huko walipo, pamoja na viongozi wetu waliopo, Mwenyezi Mungu awajalie afya njema, uzima na maisha marefu pamoja na sisi Waheshimiwa Wabunge ili tuweze kuendelea kurudi na kudumisha Muungano wetu. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, naahirisha Shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.37 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 28 Aprili, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*